

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 4 Juni, 2014

(Mkutano Ulianiza Saa Tatuhuji)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE: MWIGULU L. M. MCHEMBA):

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. ESTHER L. M. MIDIMU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. CHRISTINA M. LISSU (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa Wizara ya Fedha Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Swali letu la kwanza kama ilivyo ada linalelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini. Kwa niaba yake Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

Na. 182

Uwekezaji Kwenye Pori la Makere Kusini

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA) aliuliza:-

Nakala ya Mlando (Online Document)

Licha ya kwamba kuna uwekezaji unaoendelea kwenye Pori la Makere Kusini (Kagera Nkanda) katika Jimbo la Kasulu Vijiji; bado kuna mambo ya kuhoji:-

(a) Ushirikishwaji wa wananchi na wawakishi wao ukoje, hasa ikizingatiwa kuwa hata Mbunge wao hana taarifa sahihi juu ya uwekezaji huo?

(b) Je, Halmashauri na Wananchi wanaozunguka eneo hilo la uwekezaji wananaufaika vipi na eneo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijiji, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna uwekezaji unaoendelea katika Pori la Makere Kusini. Wananchi wanashirikishwa kutoka mwanzo na mazungumzo kati ya mwekezaji (Mawalla Trust Ltd.) na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa njia ya vikao vya Kijiji, Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira na kwa kupitia Baraza la Madiwani.

Kupitia vikao hivyo Serikali ya Kijiji na Wananchi waliridhia kutoa eneo hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ili litumike kwa uwekezaji kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Kagerankanda uliofanyika tarehe 25 Julai, 2011. Mkataba kati ya Mwekezaji, Mawala Trust Ltd. na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ulisainiwa mbele ye Baraza la Madiwani tarehe 5 Juni, 2012.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mkataba uliowekwa kati ya Halmashauri ya Wilaya na Mwekezaji, Halmashauri na Wananchi wanaozunguka eneo hilo watanufaika kwa kupata mapato ya shilingi milioni 440 kwa mwaka kama kodi ya pango la ardhi kwa matumizi ya uhifadhi wa maliasili na kuendesha shughuli za utalii.

Aidha, wananchi kupitia Serikali zao za vijiji watanufaika kwa kulipwa asilimia 25 ya kiasi kilicholipwa na Mwekezaji kwa Halmashauri ya Wilaya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwekezaji amewezesha wananchi kwa kuwapa mafunzo ya ufugaji bora wa Nyuki na kuwapatia zana bora za ufugaji nyuki kwa ajili ya kuyatunza mazingira na kuwaongezaa kipato.

Aidha, Mwekezaji alitaa fedha kiasi cha shilingi milioni 32 kwa ajili ya upimaji wa Vijiji na kuandaa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji viwili vya Kagerankanda na Mvinza ambavyo vinapakana na eneo la uwekezaji na wananchi wamepata ajira kwa kushirikishwa katika ngazi za doria na kulinda kambi za Watalii.(Makofii)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wizara kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ina jukumu la kuzilea na kuzilinda Halmashauri zetu. Sasa ninataka kufahamu maoni ya Wizara kuhusiana na mkataba huu ambaa Halmashauri hii imeingia na huyu Mwekezaji.

Je, wao kama Wizara waliridhia?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba tunapokuwa na shughuli za Uwekezaji popote katika ngazi zetu za vijiji kwa kupitia maeneo yaliyopo, hatua ya kwanza ni kuwashirikisha wananchi wenyewe, lakini mbili ni lazima Kamati zinazohusika ikiwemo Ward DC - Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo inamiliiki kimoja kati ya vijiji hivyo. Pia Baraza la Madiwani likiisharidhia sasa Wizara tunakuwa tumeridhika kwa sababu hatua za msingi za kushirikisha wananchi zinakuwa zimepitiwa.

Kwa hiyo, kwa hatua waliyofikia na kwa kuwa pia tumeona kampuni inayowekeza imetoa tija kwa wananchi wa maeneo yale kwa kuwapeleka mafunzioni. Lakini pia kuwapa vifaa bora vya ufugaji unaopelekea pia kulinda msitu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, mwekezaji yule ametoa mchango mkubwa sana; amejenga madarasa mawili pamoja na jengo la utawala kwenye Shule ya Sekondari ya Kimanya. Pia amejenga bweni la Wasichana katika shule ya Sekondari ya Makere, jambo ambalo kwa kweli na sisi tunaona kwamba, wananchi wanapata tija. Kwa hiyo, sisi Wizara tumeridhia kwa uendeshaji huo, unless Wananchi sasa wanaleta malalamiko kwenye maeneo ambayo hayajakamilika.

MHE. MOSES J. MACHALI:- Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nimwulize Waziri swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu iliingia mkataba na Kampuni ya Mawalla Trust Ltd., lakini bahati mbaya aliyekuwa Mkurugenzi au Mmiliki wa Kampuni hii alifariki dunia na hatunaye. Ikatokea taarifa kwamba, mkataba waliokuwa wameingia Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu pamoja na Kampuni hii, ni kwamba kampuni ile ilipaswa kuwa inalipa zaidi ya shilingi milioni 440. Halmashauri ilipata kueleza kwamba, fedha hizo hazitalipwa kwa sababu mmiliki wa Kampuni hayupo.

Nilikuwa naomba kupata kauli ya Serikali. Je, itakuwa tayari kufuatilia ili kubaini kama fedha hizi zililipwa au hazijalipwa kwa sababu kuna utata au misingi ya kifisadi ambayo imekuwa inafanywa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu? Je, Naibu Waziri yuko tayari kuweza kufuatilia na hatimaye aweze kutupa jibu ambalo pengine ni sahihi juu ya fedha hizi ziko wapi?

NAIBU SPIKA: Majibu ya ombi hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkoo, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitsaa (TAMISEMI).

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameeleza jambo ambalo linaendelea na sasa jambo hili kwetu ni jipyaa na kwa kuwa ameomba kufuatilia, ninataka nimuhidi kwamba, tutafuatilia na tutampatia taarifa Mheshimiwa Mbunge ili aweze pia kuwa na ufuatiliaji wa karibu katika jambo hili. Ahsante sana. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho Mheshimiwa Keissy nilikuona.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mashamba mengi ya Wawekezaji ambao hawalipi kodi ya ardhi kwenye Vijiji husika au Halmashauri.

Je, Serikali ina mpango gani kufuutilia wawekezaji ambao inawapa vibali wasilipe kodi ya ardhi kuzifidia Halmashauri zetu badala ya hao Wawekezaji ambao Serikali inawalea kisiasa? Mfano katika Wilaya ya Nkasi? (Makof)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Keissy kama ifuatavyo:-

Suala lolote la uwekezaji mahali popote kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi ni jambo ambalo kwanza ni lazima liridhiwe na eneo hilo. Lakini katika kuridhia kunakuwa na makubaliano, yale makubaliano ndiyo msingi wa uwepo wake. Kama jamii husika haikubaliani kati ya mambo ambayo wanataka yafanyike,hakuna nafasi ya Mwekezaji kuendelea kwenye eneo hilo, na sisi Serikali kazi yetu ni kulinda makubaliano yaliyowekwa kati ya Mwekezaji na Wananchi.

Pale ambapo inaonekana wananchi hawajardhia Serikali hatuvezi kuruhusu kuendelea tu kama Wananchi wa eneo hilo hawajardhia. Tumeendelea kuhakikisha kwamba, maeneo yote ya uwekezaji yanatoa tija kwa wananchi wetu. (Makof)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Sasa tuhamie swalii la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijiji.

Na. 183

Kujenga Upya Shule ya Msingi Kabungu

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Shule ya Msingi Kabungu ni ya muda mrefu toka enzi za mkoloni; shule hii ambayo ni chakavu sana iko pemberi sana na maeneo wanayoishi wananchi wa kijiji cha Kabungu.

Je, Serikali iko tayari kujenga shule hii ili iendane na mazingira ya sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Msingi Kabungu ilijengwa tangu enzi za mkoloni mwaka 1949 katika eneo ambalo mwanzoni lilikuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Mpanda. Aidha, baadhi ya wakazi walihama kutoka katika makazi yao ya asili kwenda katika makazi mapya ambayo ni mbali na shule hiyo. Halmashauri imeshauriwa kusimamia sheria inayodhibiti uanzishaji wa makazi holela ili kuondoa tatizo la watu kuishi mbali na miundombinu ya jamii kama vile shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Shule ya Msingi Kabungu ina wanafunzi 309 wakiwemo wavulana 147 na wasichana 162. Kwa upande wa miundombinu shule ina mahitaji

ya madarasa Kumi (10), yaliyopo ni madarasa matano(5), ikiwa bado kuna upungufu wa madarasa matano(5).

Aidha, madarasa matatu (3) yalijengwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Shule inazo nyumba za Walimu tano (5) ambapo moja ilijengwa katika mradi wa MMEM, shule ina ofisi tatu ambazo ambazo zinatosheleza mahitaji na ina matundu ya vyoo 16 ambayo yanakidhi mahitaji ya Walimu na Wanafunzi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya majengo ya shule hiyo ni chakavu, kutokana na majengo hayo kuwa ya muda mrefu. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika shule hiyo kama nilivyoeleza awali kuwa baadhi ya majengo yalijengwa kupitia MMEM I na II.

Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, inaendelea na mikakati ya uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo ili ilingane na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Bajeti wa mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imekusudia kuongeza idadi ya madarasa, lakini pia Serikali imeishauri Halmashauri hii kuendelea kukarabati miundombinu ya shule hii kwa kupitia mapato yake ya ndani. (Makofii)

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimeuliza kwenye swalii la msingi, shule hii ya Kabungu ni ya muda mrefu na Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba, ilianza kujengwa toka mwaka 1949. Mazingira yake hayafai na hayana mvuto hata kwa watumishi wanaofanya kazi katika shule hiyo.

Shule hii sambamba tu na shule nyingine zote ambazo zilijengwa enzi za ukoloni, miundombinu yake ilishachakaa na zimezeeka. Kuna shule za Mwese, Milala na Ikola zinafanana na mazingira ya shule ya Kabungu sambamba na shule zingine ambazo zipo katika maeneo mengine nchini.

Je, Serikali imejipanga vipi kuweza kutatua matatizo haya ambayo yanazikabili shule chakavu kama hizo? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; pamoja na kuwa kuna uchakavu, shule nyingi zimekuwa hazina Walimu wa kutosha na kuna baadhi ya Wanafunzi waliomaliza kwenye vyuo mbalimbali ajira zao zimekuwa ni tata.

Serikali ina kauli gani kuweza kumaliza tatizo la Walimu hasa katika shule za Sekondari, kwenye jimbo langu, shule za Mishamo, Mwese, Katuma, Ikola, Karema na Mpanda Ndogo ambako kuna uhaba mkubwa sana wa Walimu ambao wanahitajika kuweza kutatua tatizo la ufundishaji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Swali la kwanza kuhusiana nauchakavu wa miundombinu ya shule za Msingi. Kwa ngazi ya shule za msingi bado tumeendelea kufanya mawasiliano na Halmashauri husika kubaini shule zote chakavu na kuzishauri kutenga mapato yao ya ndani kwa ajili ya ukarabati kama ambavyo shule hii ya Kabungu ilivyoanza. Nina amini zile shule nyngine zote kama zimeishabainiwa tayari zinaweza sasa kupata ukarabati kwa maeneo yao.

Eneo ambalo tumeanza kulipa fedha shilingi milioni hamsini, hamsini ni shule za Sekondari kongwe ambazo tayari tumeishaanza kuzipeleke. Sasa hivi shule ambazo tumezibaini zimepata zaidi ya shilingi milioni 250. Kwa hiyo, tutaendelea na zoezi hilo kwa shule za Sekondari, tukiishamaliza tutaweza kuja kuungana na jitihada sasa za Halmashauri kwa shule za msingi ili kuweza kuboresha miundombinu ya shule za msingi pia.

NAIBU SPIKA: Tuendelee na swali linalofuata la Mheshimiwa Goodluck Ole - Medeye.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):
Naam!

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika....

NAIBU SPIKA: Samahani kidogo, kuna nyongeza ya jibu! Malizia Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):
Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni muhimu sana na ninaomba Watanzania wanisikilize na hasa wale vijana waliomaliza vyuo vikuu kwa kozi za Ualimu na hawajapata ajira mpaka leo.

Mwaka huu sisi tumepata kibali cha kuajiri Walimu 36,186. Tulichofanya tumeendelea kuwapa muda wa kuripoti ili tujue exactly ni wangapi wameenda kuripoti na wangapi hawajaripoti ili tuweze sasa kuweka mpango wa kuongeza wengine kusheheneza kibali tulichokipata. Mpaka tarehe 30 Mei, 2014 ni Walimu 33, 894 pekee ndiyo wameripoti na huo ndiyo mwisho wetu. Kazi ambayo sasa tunafanya ni kutambua yale mapengo 2219 ili tuwezekuwachukua wale ambao hawakupata ajira waingie hapa.

Lakini kwa sasa ambapo Halmashauri nyngi zinaendelea kutuandikia kwamba, Walimu wa Masomo ya Sanaa (Arts) wametosheleza. Kwa hiyo, nafasi ya kwanza tunayowapa ni ya masomo ya Sayansi. Hata hivyo, bado tunaendelea na jambo hili, tutapanga vituo, tutaoa kwenye mtandao kwa wale ambao wamekosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye eneo hili ni muhimu tukalieleza kwamba, tuna Walimu ambao wanaendelea kutuandikia messages waliosoma kozi ambazo zinatamkwa kama Bachelor of Education (Psychology), Bachelor of Education (Administration). Hawa ajira yao haitakuwa kwenye Kurugenzi ya Msingi na Sekondari.

Hawa wataajiriwa na Wizara ya Elimu kwenda kufundisha Vyuo vya Walimu kwa sababu mahitaji ya Kurugenzi ya Msingi na Sekondari, lazima Mwalimu wanaeweza kumwajiri ni yule mwenye teaching subjects (masomo) ambayo ameyasomea kwa ngazi ya chuo kikuu. Kwa hiyo, hili ndiyo ambalo pia tutalifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili wapo Wanachuo ambao wamesoma degree za kozi nyngine kama vile Sheria na maeneo mengine, nje ya Ualimu na baada ya kumaliza degree hizo wamekuja kusoma Post Graduate in Education. Hawa nafasi yao ya ajira

Nakala ya Mlango (Online Document)

kwenye Kurugenzi ya Sekondari ni ndogo kwa sababu sisi tunahitaji Mwalimu aliyesomea masomo ya kufundishia darasani kwa ngazi ya degree. Sasa kama alisomea sheria sisi Sekondari hatufundishi sheria.

Kwa hiyo, ni vyema sasa kwa vijana waliomaliza kidato cha Sita wanaokwenda vyuo vikuu sasa wakawa makini katika kuchagua kozi ambazo zitakuja ku-fit kwenye mahitaji yetu sisi kwa Kurugenzi za Sekondari ili kufundisha kwenye Secondary schools zetu.

Kwa hiyo, huu ndiyo wito wangu kwa wale wote ambao wamekosa ajira, na sasa tunaanza kutoa majina. Tutatoa kwenye website hivi karibuni ili tuone tume-fit kiasi gani. Pia tulioomba kibali cha zaidi ya Walimu 36,000 tukiishapata kibali tutaongeza pia ajira hiyo kwa sekta ya elimu.

Na. 184

Tatizo Sugu la Maji – Halmashauri ya Wilaya ya Arusha

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE aliuliza:-

Tarehe 17 Septemba, 2010 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu kwenye Uwanja wa Emaoi, Wilayani Arumeru aliahidi kwamba Serikali itaandaa *District Water Master Plan* kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na kwamba Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huo ili ifikapo mwaka 2015 kero ya maji katika Wilaya hiyo iwe historia, lakini hadi leo hakuna kilichofanyika licha ya jitihada za mbunge wa eneo hilo kufuatilia sana suala hilo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 323,198 ambapo kati yao wakazi 186,162 sawa na asilimia 57.6 wanapata huduma ya maji safi na salama. Katika kuboresha huduma ya maji kwa Halmashauri ya Arusha, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo kazi mojawapo inahusu uandaaji wa *District Water and Sanitation Master Plan*. Programu hii ni ya miaka 20 na inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2005/2006 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa *District Water Master Plan* imeshakamilisha ambapo katika awamu ya kwanza ya utekelezaji inahusisha ujenzi wa miradi ya Ikirevi, Oloigeruno, Loovilukuny, Nduruma, Ngaramtoni, Bwawani, Likamba, Losikito, Oloitushula, na Nengun'g yenye jumla ya vituo vya kuchotea maji 168 ambayo inatarajwa kuhudumia wananchi wapatao 42,000 ikiwa ni sawa na asilimia 13. Aidha, miradi wa kijiji cha Ilkirevi umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi katika vijiji vya Oloigeruno, Loovilukuny, Nduruma, Ngaramtoni, Bwawani, Likamba, Losikito, Oloitushula na Nengun'g ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kiasi cha fedha kilichotengwa shilingi milioni 762.9 zimetengwa kwa ajili ya

Nakala ya Mlango (Online Document)

utekelezaji wa mpango kwa awamu ya kwanza na mwaka 2013/2014, shilingi bilioni 1.06 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa awamu ya pili ya utekelezaji wa program hii ambayo inatarajiwa kuanza 2014/2015 hadi 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 32.1 zinakadiriwa kugharimu ujenzi wa miradi ya maji kwa vijiji 37. Jumla ya vituo vya kuchotea maji 759 vitajengwa na wananchi wapatao 189,907 wanaotarajiwa kunufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015, Halmashauri ya Arusha imetenga jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Master Plan kwa miradi ya Ilkerin, Oloovolos, Likiushin, Lesiraa, Olchorovos.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majina hayo ni ya Tanzania hapa hapa au (Makofi/Kicheko)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Haya majina haya tunaanza kupata uzoefu sasa na Imibia ikiwa ni sehemu ya awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu, miradi hii inatarajiwa kunufaisha wananchi 17,924 mara itakapokamilika. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mpango huo kwa kadri rasilimali fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu ya swali hilo lakini nisikitike kwamba yana mapungufu. Naamini jambo moja mtaalamu aliyeandaa majibu haya pengine ameshindwa kutofautisha Master Plan na Program. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha haina Master Plan ya maji. Master Plan huandaliwa kwa kushirikisha wadau kuanzia wanufaika kwa maana ya Vijiji, Kata, hadi wilaya. Mbunge ni mdau muhimu katika hilo na mimi sijawahi kushiriki na wala kuona hiyo rasimu ya Master Plan ya maji ingawa nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba ni vizuri Serikali ikatusaidia kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni ya kuandaa Master Plan ya maji na kutenga fedha na kutekeleza. Kwa sababu tumebakiza mwaka mmoja kabla hatujafika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambacho ndio kipindi kile ambacho Mheshimiwa Rais alisema kwamba ifikapo kipindi hicho kero ya maji kwenye Halmashauri ya Wilaya Arusha itakuwa historia.

Ningeomba kujulishwa ni mkakati upi utakaotumika katika kipindi hiki cha mwaka mmoja uliobakia ili kutuwezesha kwanza sio kutengeneza Master Plan kwa sababu hata ikielezwa sasa hivi hatutaweza kutekeleza kwa kipindi hikilichobakia kifupi kupata fedha za kutekeleza mpango wa dharura ambao nilikwishawasilisha kwa Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye nafikiri makofi hayo yanakuelekeza wewe.

MHE.DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi huo ni utovu wa nidhamu ndani ya Bunge Mheshimiwa Naibu Spika. Haiwezekani Mbunge anauliza swali halafu watu wanampigia kelele, nina uchungu na wananchi wangu mimi walionichagua.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa malizia tafadhali.

MHE.DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndio nauliza swali sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichoomba naomba kujua ni mkakati gani utakaotumika katika kipindi hiki kifupi cha mwaka mmoja ili kutuwezesha kupata fedha za kutuwezesha kupata fedha za kutekeleza mpango wa dharura amba Mheshimiwa Rais alipotembelea wilaya hiyo tarehe 1 Novemba, 2012 nilimjulisha juu ya hali hiyo na akaniagiza nimpelekee na nilikwisha mpelekea mahitaji hayo ya fedha ili walau tuweze kuendeleza vyanzo vya maji mtiririko na pili kuweza kujenga malambo pastel ambapo maji ya mtiririko hayapo?

Pili, naomba kujua Waziri wa Maji atakuja lini wilayani kwetu ili aone hali halisi ya upungufu wa maji katika wilaya hiyo?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Medeye. Waheshimiwa Wabunge ni msisitizo kwa sababu suala hili la maji Mheshimiwa Ole-Medeye kwa kweli limekuwa likimgusa kipekee kabisa.

Sasa naomba tu majibu yawe mafupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tu niseme kwamba Rais alichokisema ni kuandaliwa kwa District Water Master Plan kama ambavyo alikuwa amesema.

Lakini tu niseme kwamba amekiri kwamba yeye ni mdau kwa hiyo mimi naamini kabisa Serikali inaanzia katika wilaya yake ambaye ni Diwani na ni Mjumbe katika Halmashauri hiyo. Kwa hiyo, aendelee na sisi tuko tayari kuipokea hiyo na kuifanya kazi. Kwa hiyo tushirikiane naye kwa hilo.

La pili, ni kwamba Waziri yuko tayari hata mimi mwenyewe kufika Arumeru, lakini pia yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa hiyo tutaendelea kushirikiana naye wakati wowote kuona kwamba tunatatua tatizo la maji katika wilaya yake.

NAIBU SPIKA: Tuhamie Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, swali la Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa, Mbunge wa Namtumbo.

Na. 185

Ununuzi wa Mazao ya Wakulima

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Wilaya ya Namtumbo na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wake ni moja kati ya maeneo yanayochangia sana uzalishaji wa chakula kwa Taifa.

(a) Je, Serikali inatambua kuwa msimu uliopita imewasababishia Wakulima hao kuharibikiwa na mazao yao walipopeleka katika Vituo vya NFRA na kununua mazao machache na kuacha mengine kunyaeshewa na mvud?

(b) Je, ni hatua gani za makusudi zinazochukuliwa dhidi ya hali hiyo na kuwasaidia wakulima walioathiriwa na hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto za ununuzi wa mahindi kuitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) zilizojitokeza katika msimu wa mwaka 2011/2012 zilizotokana na upatikanaji wa fedha za ununuzi wa mahindi kwa wakati pamoja na upungufu wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao. Aidha, utaratibu wa wafanyabiashara binafsi kununua mazao kwa bei ndogo kuliko bei ya NFRA ilipelekea wakulima wengi kupeleka mahindi katika vituo vya NFRA kuliko uwezo wa uhifadhi na Bajeti ya ununuzi wa Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2011/2012 NFRA ilipanga kununua mahindi tani 50,000 mkoani Ruvuma. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi Wakala ulifanikiwa kununua jumla ya tani 52,268.977 ambapo tani 4,688.975 ziliunuliwa Wilayani Namtumbo, tani 9,744.541 Wilayani Mbinga, tani 26,635.461 Songea Vijiji na tani 11,200 Songea Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji wa masoko endelevu ya mazao ya kilimo ikiwemo mazao ya mahindi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuruhusu uuzwaji wa mazao nje ya nchi kwa utaratibu. Kuimarisha miundombinu ya masoko ili kurahisisha usafirishaji na uhifadhi wa mazao na kuboresha mfumo wa kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa mbalimbali za masoko kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeendelea kujenga uwezo wa NFRA kwa kuongeza bajeti ya ununuzi wa nafaka hadi kufikia shilingi bilioni 109 na kuwezesha kununua tani 219,377 mwaka 2013/2014 pamoja na kukamilisha ujenzi wa maghala mawili mjini Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, NFRA, imepanga kuanzisha Kanda mpya ya Kigoma itakayohudumia mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita na Tabora na hivyo kupunguza majukumu kwa Kanda ya Shinyanga, ambayo kwa sasa inahudumia mikoa minane ya Kanda ya Ziwa.

Aidha, utaratibu wa Mkutano wa Bunge la Bajeti kuanza mwezi Aprili, hadi Juni umewezesha kuharakisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa nafaka wakati wa msimu wa ununuzi unaoanza tarehe 1 Julai na kumaliza Disemba kila mwaka.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa msimu huo wa mwaka 2011/2012 wakulima hawa waliharibikiwa mazao yao yakiwa katika vituo vya NFRA kabla hayajapokelewa kwa sababu kama Serikali ilivyozieleza katika jibu lake la msingi. Lakini pia msimu wa mwaka 2013/2014 Serikali ilichelewa sana kuwalipa wakulima fedha zao na huku ikijua uchumi wa kuendesha maisha yao kusomesha watoto wao, tiba zao unategemea sana mapato yanayotokana na kilimo.

Je, sasa Serikali kwa kutambua hayo imejjipangaje mwaka huu 2015 kununua mapema mahindi na kuwalipa mapema na kwa wakati ili wao nao wanufaikie na uchumi unaokua wa asilimia saba?

(b) Kwa kuwa Halmashauri zetu pia zinategemea mapato ya ndani kutokana na kodi za mazao na NFRA inaponunua inatakiwa ilipe kodi hiyo Halmashauri zetu na kwa kuwa Halmashauri ya Namtumbo inaidai NFRA shilingi 105,000,000 za msimu wa mwaka 2013/2014.

Je, Serikali sasa inaweza kuielekeza NFRA iweze kuwalipa ili tuepukwe hoja za ukaguzi lakini pia tuweze kugharamia shughuli tulizozipanga Halmashauri ya Namtumbo?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama tumejipangaje kulipa madeni. Kwanza naomba niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge ndio tunaopitisha Bajeti ya Serikali humu ndani, sasa tatizo la kulipa kimsingi linatokana tu na upatikanaji wa fedha Hazina. Lakini sisi kama Wizara ya Kilimo na kwa maana kupitia NFRA kama tungekuwa tunapata fedha kwa wakati kusingekuwa na tatizo lolote la kulipa wakulima wanapouza mahindi yao.

Kwa hiyo, kwa kipindi cha mwaka huu anachosema kwamba tumejipangaje kulipa mapema sisi tunasema hatuna tatizo kama Wizara na Hazina watatupa fedha mapema wananchi watalipwa mapema inawezekanavyo. Kwa hiyo ni suala la Wabunge wote na kuhakikisha kwamba Hazina wanatoa fedha mapema ili wananchi hao wanaouza mazao yao waweze kulipwa mapema.

Mheshimiwa anataka kujua kwamba hii produce cessy tutalipa namna gani. Kwanza naomba niweke kumbukumbu vizuri kwake kwamba kwa kumbukumbu tulizonazo za NFRA Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo inatudai cess 100,671,055 hiyo ndiyo figure tuliyonayo sisi. Sasa suala hili kama nilivyosema produce cess ambayo kwa ujumla kwa wilaya zote ambazo zinadai ni karibu shilingi bilioni 5 ndio zinazodaiwa ili tuweeze kulipa cess kwa Halmashauri zote ambazo zinauza mahindi na sisi deni hili tumeshapeleka Hazina kama Hazina wakitoa fedha basi Halmashauri zote zinaweza zikalipwa mapema inavyowezekana. (Makofii)

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, Waweja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jimbo la Kishapu ni mionganii mwa wilaya zilizotekeleza mpango wa kulima mazao yanayoendana na hali ya ukame. Na kwa kuwa wananchi wangu wa Kishapu wameitikia wito wa kulima mtama kwa wingi sana kuliko wilaya yoyote katika mkoa wa Shinyanga na kwa kuwa mtama huo sasa umekuwa ni mwingi na wananchi baada ya kuitikia kwao wamelima mtama mwingi kufuatia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa mwaka huu na mwaka wa jana atanunua mtama na kuweka katika hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je naomba kujua Wizara ni lini itaanza kuununua mtama huo ili wananchi hawa wanufaika na zao la mtama walilolima na mwakani waweze kulima kwa wingi zaidi? (Makofii)

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuwahamasisha wakulima kulima zaidi mimi nadhani ni jambo jema, kwa sababu kwa kufanya hivyo tunawaepusha pia na suala la njaa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si sahihi kwamba wananchi wote watakoalima mazao basi Serikali itakuwa na uwezo wa kuyanunua mazao yote. Haitawezekana ndiyo sababu sasa tumeruhusu wananchi kuweza kutafuta masoko nje ya nchi kwa ajili ya kuuza, lakini wakifuata utaratibu.

Hata hivyo niseme kwamba utaratibu tulio nao sasa kwa sababu tumeona suala la soko ni changamoto kubwa tunafikiria kuanzisha soko la bidhaa pamoja na masoko ya mazao au Commodity Exchange na tunadhani tukianzisha utaratibu huu itakuwa ni vizuri zaidi kwa ajili ya wananchi hawa kupata soko kuliko lilivyo sasa.

Kwa bahati nzuri Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji ilishaenda Ethiopia kule kwa ajili ya kujifunza utaratibu wa hii Commodity Exchange. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika tunaandaa Paper ambayo itaenda kwenye vikao vya juu ili kuweza kuridhia. Tukishafanya utaratibu wa Commodity Exchange suala la ukosefu wa soko kwa bidhaa halitakuwepo.

Sasa suala la kwanza Serikali itanunua mtama lini. Niseme tu kwamba bado hatuna fedha za kutosha kwa ajili ya kuweza kununua mazao ya wananchi wote na kwa kweli niseme bado hatuna mpango kabisa wa kununua mtama wa wananchi, kwa sababu kama nilivyosema ya ukosefu wa fedha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda swali linalofuata la Mheshimiwa Aliko Nikosuma Kibona, Mbunge wa lleje. Mheshimiwa Aliko Nikosuma Kibona.

Na. 186

Motisha Kwa Wakulima wa Zao la Pareto

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Wilaya ya lleje hususan Ukanda wa Umalila, Kata za Ibaba, Itale, Ngulilo na Ndola ni mojawapo ya wazalishaji wakuu wa zao la Pareto katika Nyanda za Juu Kusini:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na wanunuzi ina mpango gani wa kuwapa motisha Wakulima hao wa zao la Pareto kwa kuwajengea Barabara na visima vya maji kama ilivyo kwa Wakulima wa mazao mengine kama Kahawa?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikosuma Kibona, Mbunge wa Jimbo la lleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua juhudzi za wakulima wa Wilaya ya lleje katika uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini ikiwemo zao la pareto. Aidha, Wilaya ya lleje ni kati ya maeneo muhimu katika mkakati wa kuongeza uzalishaji zao la pareto nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Pareto ya mwaka 1997 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2009 inatoa fursa kwa wadau wa sekta ya pareto wakiwemo wanunuzi, wakulima, Halmashauri za Wilaya zinazolima pareto na Serikali kukubaliana kutekeleza majukumu ya pamoja (Shared Functions) katika uendelezaji wa zao la pareto nchini. Aidha, mionganini mwa majukumu hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuendeleza zao la pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Makampuni yanayonunu pareto yamekuwa yakifanya shughuli mbalimbali za kuendeleza zao la pareto kwa kushirikiana na wadau kama sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Pareto na Utoaji wa Huduma kwa Jamii (Corporate Social Responsibility (CSR) ikiwemo usambazaji wa pembejeo na utoaji wa elimu ya kilimo bora cha pareto kwa wakulima. Aidha, Serikali itaendelea kuhimiza Makampuni ya ununuzi wa pareto kuangalia uwezekano wa kujenga miundombinu kama visima vya maji na barabara ili kuimarisha mahusiano kati yao na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Halmashauri za Wilaya katika maeneo yanayolimwa pareto upata fedha zinazotokana na ushuru wa mazao (Produce Cess), hivyo nitoe wito kwa viongozi katika wilaya hizo kwa kushirikiana na wadau ikiwemo wanunuzi wa pareto kutenga kiasi cha fedha zinazotokana na mapato ya pareto kwa ajili ya kujenga miundombinu ya barabara na maji kama sehemu ya utekelezaji wa sera na sheria za kilimo nchini, ikiwemo sheria ya pareto na kanuni zake. (Makof)

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ninakushukuru kunipa nafasi nina maswali mawili ya nyongeza swal la kwanza Serikali imeruhusu soko huria katika mazao karibu yote hapa nchini na kwa kufanya hivyo humfanya mkulima kuchagua mnunuzi wa zao lake na kupata faida, Kwa nini katika eneo hili inaoekana mnunuzi wa pareto wa lleje katika Ukanda niliousema yuko mmoja hakuna ushindani?

Lakini swal la pili ni kwamba ninapenda kujua pale ambapo mnunuzi wa mazao haya haonyeshi nia ya kushirikiana na wananchi katika aspect ya social responsibility.

Je, Serikali inatushauri nini kwa mnunuzi ambaye kabisa haonyeshi nia ya kusaidia wananchi anakanunua mazao hayo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa lleje, kama ifuatavyo:-

Suala la ununuzi kwamba ni soko huria tunakubali lakini soko huria hili ni lazima liwe na utaratibu. Lakini pia nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli mnunuzi kwa Wilaya ya lleje yuko mmoja. Utaratibu wa ununuzi wa zao la pareto ni tofauti kidogo na mazao mengine, kwa sababu mnunuzi wa zao la pareto ni lazima awe na maabara pamoja na Processing Plant maeneo ya jirani.

Kwa hiyo, kama mnunuzi huyo hawezi kukamilisha masharti hayo hawezi kupata leseni ya ununuzi wa zao la pareto. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama anawafahamu wanunuzi wengine na sisi tunawaalika wanunuzi wengine ili mradi wana maabara pamoja na Processing Plant watapewa leseni kwa ajili ya kununua pareto bila ya kizuizi chochote. (Makof)

Lakini swal la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba mnunuzi huyu hayuko tayari kushirikiana hasa katika aspect ya Corporate Social Responsibility ninaomba niseme kuwa kimsingi suala la kujitolea kwa mnunuzi au mtu mwingine yoyote anapofanya shughuli katika jamii ni suala la utashi wake yeye mwenyewe.

Huvezi kumlazimisha kwamba kwa sababu unanunua mazao katika eneo letu au unafanya shughuli katika eneo letu basi ni lazima utuchangie katika masuala fulani. Kwa hiyo, hili ninaomba niseme kwamba ni suala la hiari lakini pia na mahusiano yenyewe kati ya jamii ile na wanunuzi ambaao wanafanya kazi katika maeneo haya. (Makof)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swal la Mheshimiwa Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini.

Waheshimiwa Wabunge, leo mniwie radhi sana kwa sababu ya muda.

Na. 187

Gharama ya Kiwanda cha Korosho cha Lindi

MHE. SALUM K. BARWANY aliuliza

Serikali ilijenga zaidi ya Viwanda kumi na mbili (12) vya korosho katika Mikoa ya Kusini ukiwemo Mkoa wa Lindi:-

- (a) Je, kiwanda cha Lindi kilijengwa kwa gaharama gani?
- (b) Je, kiwanda hicho kiliuzwa kwa gaharama gani?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho kwa miaka ya 1970 ambapo uzalishaji ulifika tani 145,000 kwa mwaka Serikali ilitekeleza mpango wa ujenzi wa viwanda 12 vya kubangua korosho kikiwemo kiwanda cha kubangua korosho Lindi kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia. Aidha uendeshaji wa viwanda hivyo ulisimamiwa na Mamlaka ya Korosho Tanzania mpaka vilipobinafsishwa mwaka 2004 na 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha korosho Lindi kilijengwa mwaka 1977 kwa kutumia teknolojia ya kitaliano ni mojawapo ya viwanda 8 vya kubangua korosho vilijengwa 1977 na 1980 kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia wenyewe thamani ya shilingi 93,211,985.8. Mkopo huo ultumika kujenga viwanda vya korosho vya Lindi, Mtama, Nachingwea, Masasi, Newala 1, Newala II, Likombe na Kibaha, pamoja na kujenga jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya korosho.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto mbalimbali kikiwemo ukosefu wa mtaji na matatizo ya uendeshaji wa viwanda vya korosho kikiwemo kiwanda cha korosho Lindi vilisimama kufanya kazi ambapo mwaka 1996, viliwekwa chini ya iliyokuwa Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRS*) kwa ajili ya kubinafishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ubinafsishaji mwaka 2004 kiwanda cha korosho Lindi kiliuzwa kwa kampuni ya Bucco Investment Holdings Limited kwa thamani ya shilingi milioni 50. (*Makofii*)

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa lengo la Serikali ilikuwa ni kutoa ajira kwa wananchi wa Lindi na maeneo ambako viwanda hivi vilijengwa na pia azma ilikuwa ni kutokana na kuuza korosho ghafi ili tuuze korosho ambazo tayari zimebanguliwa.

Je, Serikali ina mpango gani kwa sasa wa kuwasaidia hao wamiliki wapya ambao wamekwama katika kuvifanya viwanda hivyo vifanye kazi?

Kuna taratibu gani za Kisheria kupitia uuzaji huo ambao mpaka leo viwanda hivyo bado havijafanya kazi.

Je, Serikali inaweza kubatilisha umiliki wa viwanda hivyo ili wapatikane wamiliki wapya ili wananchi wa Lindi wapate ajira hususanii akina Mama?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba viwanda hivyo vilianzishwa kwa ajili ya kukuza ajira lakini pia na pia tubangue korosho hapa nchini badala ya kuza ghafi.

Sasa anasema tuna mpango gani wa kuvisaidia viwanda hivi. Ninaomba niseme kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisimamia sana jambo hili na bahati nzuri mimi nilipewa nafasi ya kusimamia Kamati ndogo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda kwa ajili ya kupitia utaratibu wa viwanda hivi ili viweze kuzalisha zaidi.

Taarifa ya awali tulishiwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tayari kuna viwanda karibia vinne ambavyo tumnekwisha vi-identify ambavyo tunataka vianze uzalishaji mapema iwezekanavyo, kwa maana ya kwamba viweze kufanyiwa ukarabati wa kutosha lakini pia wote tunajua pia kule Mtware kuna mpango wa kujenga viwanda vingine.

Kwa mfano TANECU wana mpango wa kujenga kiwanda ambapo pia wameshapata mkopo kutoka Benki ya TIB. Kwa hiyo, ukianzia na hilo ni kwamba bado Serikali ina nia ya dhati kabisa kwamba badala ya kupeleka korosho ghafi nje ya nchi, basi korosho hizi zinabanguliwe hapa nchini lakini pia kwa maana ya kukuza ajira.

Suala la kubatilisha umiliki ninaomba niseme kwamba ukishamwuzia mtu kitu anakuwa na ownership kubatilisha umiliki ni suala lingine ambalo mpaka ujue kwamba ameshindwa ndipo Rais anaweza kuchukua hatua hiyo.

Lakini nimhakikishie kwamba wamiliki wote wa viwanda hivi wameshatuhakikishia sisi Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwamba sasa wako na mipango mbalimbali ambayo kimsingi tumeshaiona yenye nia kabisa ya dhati ya kuona kuwa viwanda hivi vinaweza kufufuliwa na kufanya kazi kikamilifu. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Asante sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda ninawaona kabisa lakini tukubaliane tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria suala la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy.

Na. 188

Hukumu ya Makosa ya Ubakaji

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

Je, ni kwa sababu gani hukumu ya makosa ya ubakaji hutolewa tofauti ambapo wengine huhukumiwa kifungo cha maisha wakati wengine hufungwa kifungo cha miaka 15-30?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kubaka ni kosa la jinai ambalo linatyendeka katika mazingira yaliyoelezwa chini ya kifungu cha 130 (1) na (2) cha Sheria ya Kanuni za adhabu, sura ya 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu ya kosa la kubaka imetamkwa wazi na Sheria ya Kanuni za Adhabu chini ya Kifungu cha 131 (1).

Adhabu ya kosa hili chini ya Sheria ni kifungo cha miaka 30 au kifungo cha maisha, pamoja na kuchapwa viboko na kulipa faini. Vilevile Mahakama inaweza kutoa amri kwa mbakaji kumlipa fidia muathirika wa ubakaji kulingana na maumivu aliyoyapata. Pamoja na adhabu inayotolewa chini ya kifungu 131 (1) kifungu cha 131 (3) kinabainisha endapo mwathirika wa ubakaji ni mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 10, adhabu kwa mbakaji atakapopatikana na hatia ni kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mkosaji mwenye umri wa miaka 18 au chini ya hapo kifungu cha 131 (2) kinaeleza kwamba adhabu yake itakuwa ni kuchapwa viboko endapo kosa alilolitenda ni kosa la kwanza; kifungo cha miezi kumi na mbili na kuchapwa viboko kama kosa la pili na endapo atarudia kosa hilo kwa mara ya tatu na kuonekana ni mzoefu atafungwa kifungo cha maisha. Kwa mantiki hiyo nipende kumueleza Mheshimiwa Moza kwamba hakuna hukumu ya kifungo cha miaka 15 kwa makosa ya ubakaji.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa adhabu hii ya kifungo cha maisha au miaka thethini bado ubakaji unaendelea kwa kasi. Kwa nini adhabu isiwe ni ya kifo na liwe fundisho kwa wengine?

Swali la pili, kwa kuwa, matukio mengi ya ubakaji huchukua muda mrefu sana kutatuliwa yanapofikishwa kwenye vyombo vya Sheria huku watoto wakiendelea wakiendelea kuathirika kiakili.

Je, Serikali ina mpango gani kuweka muda maalum kwa kesi za ubakaji kuamuliwa kwa haraka?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Moza kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia masuala mbalimbali ya Jinai na amekuwa akifanya jithada sana ya kutembelea magereza yetu nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wengine nao kufanya ufuatiliaji kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa bado ubakaji unaendelea kwa kasi lakini hata kama tutababilisha adhabu kuwa kifo tumekuwa tukiona makosa ya mauaji pia yanajitokeza na bado watu wanapewa adhabu ya kifo na bado mauaji yanaendelea. Tunaamini kuwa kifongo cha maisha bado kinatosha kwa hiyo nitoe wito kwa wale amba ni wazoefu au wana utaratibu wa ubakaji basi wakome mara moja.

Lakini vilevile nitoe wito kwa wazazi kuwa karibu zaidi na familia zao na watoto wao ili watoto wao wasiweze kufanyiwa vitendo hivi maana kwa mujibu wa takwimu na tafiti inaonekana kuwa makosa mengi ya namna hii yamekuwa yakifanywa na ndugu au watu wa karibu sana na familia husika.

Kuhusiana na swali la pili kwamba Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba makosa haya ya ubakaji Mahakamani yanasilizwa mapema. Kama ambavyo nilijibu katika swali la msingi wili iliyopita kuhusiana na masuala ya ukatili wa kijinsia. Mahakama inao mpango hivi sasa kwa kushirikiana na polisi upeletelezi umekuwa ukijitahidi sana kufanya upeletelezi ndani ya miezi mitatu, lakini kwa masuala ya uendeshaji wa mashtaka pia tumekuwa tukijitahidi kuhakikisha nayo tunayafanya ndani ya miezi mitatu ili kwa ujumla wake basi mwathirika aweze kuwa amepata hukumu ile ndani ya miezi ya sita.

Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na Mahakama za Mwanzo Kalambo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo yaliyopo Mji Mdogo wa Matai hayana jengo lenye hadhi na nyumba za Watumishi wa Mahakama.

(a) Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo lenye hadhi ya Mahakama ya Wilaya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kukarabati Mahakama za Mwanzo katika Vijiji vya Kisanga, Mwimbi, Mwanzye, na Matai ili wananchi wapatiwe haki zao kwa wakati?

(c) Je, Serikali haioni haja ya kujenga Mahakama katika Tarafa ya Mwambenenkoswe ili kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta haki?

NABU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kujenga majengo ya Mahakama yenye hadhi katika Wilaya zote mpya hapa nchini.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu kupitia Mahakama itajenga jengo lenye hadhi ya Mahakama ya Wilaya ya Kalambo ili kusogea huduma karibu na wananchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia Mahakama itakarabati majengo ya Mahakama za mwanzo katika vijiji vya Kasanga na Mwanzye ili wananchi wapate haki zao kwa wakati. Mahakama za Mwanzo katika vijiji vya Mwimbi na Matai zitakarabatiwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kujenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa zote mpya. Hivyo basi katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 Serikali kupitia Mahakama itajenga eneo la Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Nambwenkose.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri sana ambayo yametolewa na Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Wilaya ya Kalambo ina jumla squire kilomita elfu nne na kumi na saba na ina idadi ya wananchi wasiopungua laki mbili na elfu saba.

Nilitaka kujua katika hali ya kwaida chochote kile ambacho huwezi kukipima huwezi huwezi ukakiboresha ni utaratibu upi ambao Serikali kwa kupitia Wizara hii inao kila idadi ya wananchi wangapi wanapata huduma ya Mahakama.

Swali la pili, kwa kuwa suala la ukarabati litachukua muda mrefu na Mahakama za mwanzo kwa maana ya Mwimbi, Mweannzye zipo tayari, Wizara hii imeshapitishiwa Bajeti.

Je, itakuwa tayari kuhakikisha kuwa inawapeleka Mahakimu ili wananchi waanze kupata huduma Kisheria wakati wakisubiri ukarabati?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa maswali yako. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angela Kairuki, japo swali la kwanza ni la takwimu, sijui kama utaliweza!

NABU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusiana na utaratibu gani ambayo Mahakama inautumia kupanga eneo lipi lipeleke Mahakama kwa kulingana na idadi ya wananchi nipende tu kusema kwamba sisi tunaangalia mipango ya Serikali inavyokwenda katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, katika kila Kata tuna hakikisha kwamba kunakuwa na Mahakama ya Mwanzo na katika kila Wilaya kunakuwa na Mahakama ya Wilaya lakini vilevile katika Mkoa tunaweka Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa na baadaye Mahama Kuu na juu kabisa Mahakama ya Rufaa.

Kuhusiana na suala la pili endapo tutakuwa tayari kupeleka Mahakimu katika Mahakama mbalimbali za Wilaya hiyo, niseme tu kwamba tuko tayari na katika mwaka huu wa fedha, tumeomba kibali cha kuajiri takribani Mahakimumia tatu (300) na Watumishi wengine mia nane. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutapeleka Mahakaimu hao. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Mwisho kwa siku ya leo ni Wizara ya Nishati na Madini na swali linaulizwa na Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita.

Na. 190

Miradi ya Umeme Vijiji vya Kondoa

MHE. ZABEIN M. MHITA aliuliza:-

Serikali iliteua Vijiji kumi na tatu (13) ili vipatiwe umeme katika Wilaya ya Kondoa, kazi ya upimaji imeshafanyika.

Je, ni lini kazi ya uwekaji wa nguzo za kufunga umeme itatekelezwa ili wananchi wa vijiji hivyo wanufaikie na nishati hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itapeleka umeme katika vijiji vya Wilaya ya Kondoa na Chemba kuititia mpango Kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili chini ya wakala wa Nishati Vijijini (REA). Madi huu utatekelezwa na Mkandarasi DERM Electric Tanzania Limited aliyeanza kazi mwezi Oktoba 2013.

Kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenyе urefu wa kilomita 487.2, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenyе urefu wa kilomita 368.2, ufugaji wa transfoma kumi na sita na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 2,615 mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015 mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015 na utagharimu shilingi bilioni 13.99.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi ni kukamilika kwa kazi ya upimaji (survey) kuweka mambo, pamoja na michoro kwa ajili ya ujenzi wa njia za umeme, kazi ya uchimbaji wa mashimo pamoja na usimikaji wa nguzo inaendelea.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuishukuru Wizara kwa dhati kabisa kwa sababu baada ya kufuatilia Wizarani kwa muda mrefu kwa lengo la kuogezewa vijiji kutoka vijiji kumi na tatu nimeongezewa hadi kufikia vijiji hamsini na moja na taasisi kumi na mbili ninashukuru sana.

Sasa kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini wamehamasika sana kwa hatua iliyofikiwa ninaomba Wizara sasa kwa vijiji ambavyo vimebaki navyo vipatiwe umeme katika awamu inayofuata ili wananchi wake waweze kunufaika na upatikanaji wa umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikijibu Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba Vijiji vyote katika nchi yetu vinapata umeme na nimpongeze sana Mheshimiwa Zaiben ambaye amekuwa akifuatilia kwa karibu sana, mara kwa mara akinigongea mlango na mimi namwambia karibu akiomba Vijiji mbali mbali.

Nimhakikishie tu kwamba kwa jinsi pesa zitakavyopatikana na katika mpango wetu unavyoendelea Vijiji vyote katika maeneo yote vitapatiwa umeme.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana bado tupo Wizara hiyo hiyo Swalil la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, kwa niaba yake, Mheshimiwa tafadhal!

Na. 191

Kufunga Umeme Kułoka Karatu Hadi Endamararie

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO K.n.y. MHE. ISRAEL YOHANNA NATSE) aliuliza:-

Je, ni lini kazi ya kufunga umeme toka Karatu hadi Endamararie itakamilika baada ya nguzo kuwekwa kwa muda mrefu sasa na ahadi zinatolewa na TANESCO kutotimizwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Swalil la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kufunga umeme kutoka Karatu hadi kijiji cha Endamararie uliotekelzwa na Serikali kupitia TANESCO umekamilika kwa asilimia 100 mnamo tarehe 29 Mei, 2014. Kazi ya Mradi zilijumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenyе urefu wa kilomita 6.4; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, yenyе urefu wa kilomita 2.5; na kufunga transfoma mbili ili kuwapatia umeme wananchi wa Kijiji cha Endamararie na Shule ya Sekondari Florian. Gharama za Mradi hii ni Shilingi 229,663,503.56.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, Swalil la mwisho la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nishukuru kwa majibu yaliyotolewa na nitoe wito sasa kwa wananchi wa maeneo husika waweze kipeleka maombi ili wapatie umeme. Nina Swalil moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna tarafa mbili, tarafa ya Mbulumbulu na tarafa ya Mang'ola na ni tarafa zenyé idadi kubwa sana ya watu lakini hawana umeme.

Je, wananchi hawa wa Mang'ola na Mbulumbulu lini watapatiwa umeme?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu Swalil la msingi nilizungumzia REA awamu ya kwanza, tarafa alizozisema zipo katika mpango wa REA namba mbili na hivyo wananchi wawe na subira tukiendelea kutekeleza Miradi hii awamu kwa awamu.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, muda ukitazama hauko upande wetu naomba moja kwa moja nitambue wageni waliofika kututembelea katika siku ya leo.

Wageni 44 wa Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Waziri wa Fedha, ambaa ni viongozi wa Wizara ya Fedha, Makamishna Wakuu, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wenyeviti wa Bodi na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Dkt. Servacius Likwelile - Katibu Mkuu, Ndugu Dorothy Mwanyika - Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Elizabeth Nyambibo - Naibu Katibu Mkuu na Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu (BOT). Naomba wasimame! Karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma. Ahsanteni sana mnaweza kukaa. (Makofii)

Wageni wengine watano (5) wa Mheshimiwa Waziri Saada Mkuya Salum, wanatoka Benki ya Posta Tanzania wakiongozwa na Profesa Leticia Rutashobya, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi. Wale wa kutoka Posta, karibuni sana, karibuni sana!

Wageni 14 wa Mheshimiwa Mwigulu Mchomba, Naibu Waziri Fedha ambaa ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Iramba CCM wakiongozwa na Ndugu Charles Makala, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM - Wilaya ya Iramba. Karibuni sana, wageni wote kutoka Iramba kule Kilomboi, Mbunge wenu Mheshimiwa Mwigulu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. (Makofii)

Mheshimiwa Gosbert Blandes ana mgeni ambaye ni Ndugu Rashid Kasumuni, Diwani wa Kata ya Nyakasimbi. Karibu Mheshimiwa Diwani pale ulipo, karibu sana. Kuna wageni wa Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Rosemary Kirigini kutoka Meatu, ni Madiwani 40 wakiongozwa na Mheshimiwa Pius Machungwa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Meatu. Madiwani Meatu pale mlipo msimame! Inaelekea hawajafika tutawatambulisha baadaye basi kundi hili la Meatu.

Wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu, wanafunzi mia moja (100) na walimu sita (6) kutoka Shule ya Sekondari ya Pallotti - Singida. Wanafunzi kutoka Pallotti - Singida, Karibuni sana. Mnapendeza kabisa inaonekana shule yenu ni moja ya Shule nzuri sana kule Singida. Karibuni sana. Naona Mbunge wenu hapa Christowaja amepiga makofii kwelikweli. (Makofii)

Wageni wa Mheshimiwa Zabein Mhita ambao ni wanafunzi 56 na walimu tisa (9) kutoka Shule ya Msingi Ubembeni wakiongozwa na Mwalimu Amina Masanga ambaye ni Mwalimu Mkuu. Wageni kutoka Ubembeni kule Kondoa. Karibuni sana walimu na wanafunzi mmeona Mbunge wenu Mheshimiwa Zabein anavyoizula Serikali kuhusu kufanikisha masuala ya umeme huko Kondoa. Ahsanteni sana walimu na wanafunzi kutoka Ubembeni.

Wageni wa Mheshimiwa Augustino Masele wa Jimbo la Mbogwe ambao ni Philip Kamili ambaye ni Katibu Kata wa CCM Kata ya Ilolangulu, Ndugu Abdallah Hassan - Afisa Mtendaji Kata Ilolangulu na Ndugu Patrick Joseph - Katibu Kata wa CCM Kata ya Ikobe. Karibuni sana pale mlipo, karibuni sana!

Wageni wa Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, ambaye ni Mheshimiwa Mzee Polycarp Shayo, kutoka Rombo. Karibu sana Mzee Shayo pale ulipo!

Wageni tisa (9) wa Mheshimiwa Mary Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Mji wa Korongwe. Madiwani kutoka Halmashauri ya Mji wa Korogwe! Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, Mheshimiwa Chatanda anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. Miiongoni mwa watu hao yupo Salma Stephen Ngonyani, Mariam Stephen Ngonyani na Mama Hawa. Karibuni sana, wote hawa ni kutoka Korogwe. Karibuni sana. (Makofij)

Wageni watano (5) wa Mheshimiwa Meshack Opulukwa - Mbunge, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka CHADEMA na UDP. Wageni watano (5) wa Mheshimiwa Opulukwa! Karibuni sana. (Makofij)

Wageni wa Mheshimiwa Gregory Teu, Mbunge wa Mpwapwa, ambao ni wanafunzi 39 na waalimu wane (4) kutoka Shule ya Msingi Kikombo Mpwapwa. Walimu na Wanafunzi kutoka Mpwapwa! Ahsante sana. Wanafunzi wa Kikombo.

Waheshimiwa Wabunge Shule hii ya Kikombo ya Msingi ni moja ya Shule bora kabisa katika Mkoa wa Dodoma na ina milikiwa na Kituo cha *Tanzania Livestock Research Institute* na wamekuja hapa Dodoma kwa ajili ya kufanya mitihani ya kujipima na wenyeji wao Shule ya Msingi ya Chadulu, karibuni sana muendelee kufanya vizuri. Mbunge wenu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni Mheshimiwa Teu.

Wageni wanane (8) kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya CAG, wageni wake karibuni sana.

Wageni sota (6) wa Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mbunge wa Tarime, wakiongozwa na Mheshimiwa Peter M. Chacha, Diwani wa Kata ya Nyandoto kutoka Tarime. Karibuni sana.

Mwisho ni Ndugu Zainab Abdallah na Ndugu Olivia Sanare, ambao wapo kwa ajili ya kutembelea Bunge.

Tangazo la Mwisho Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa wale waumini wa Kanisa Katoliki miiongoni mwa Wabunge na Wafanyakazi wa Bunge kwamba Wanajumuiya hiyo ya Kikatoliki kuwa kutakuwa na ibada ya misa saa saba mchana. Tangazo hili limeletwa na Sista Cecilia Pareoso na Flateri Joseph Selasini. (Makofij/Kicheko)

Ahsanteni sana. Katibu tuendelee!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Fedha

MWONGOZO WA SERIKALI

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa na Mheshimiwa Moses Joseph Machali! Ni hao wawili?

Tuanze na Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman kwa kifupi sana.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako lipo tatizo kubwa sana linaloendelea katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na tatizo hili lina athari kubwa takribani Watanzania milioni 16, hivi sasa ninavyoongea wanalia na nimepokea meseji nydingi sana katika email yangu baada ya jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri la kuwakosesha matumaini Watanzania waliopo huko baada ya kulima mtama kwa wingi na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kununua.

Sasa kwa kuwa tatizo kama hilo lipo katika Zao la Pamba na zao hili limeajiri Watanzania milioni 16 asilimia 33 ya Watanzania. Leo hii wanaathirika baada ya kuivuna Pamba yao na hawaoni mwelekeo wa Serikali kuwasimamia juu ya ununuzi na bei ya Pamba. Watanzania hawa wanaathirika sana, nilikuwa naomba mwongozo wako na utaratibu Serikali kwanini isitoe tamko.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suleimn Nchambi Suleiman, nusu dakika nimewona Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kumpa taarifa mwongeaji kwamba anasema amepata meseji na wakati kipindi kilichopita walisema humu ndani simu haziingii, yeye amepataje hiyo meseji wakati humu simu haziruhusiwi?

MHE. SELEMAN M. N. SELEMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani aliyotoa utaratibu hakufuatilia mwongozo wangu. Yeye ni memweleza mimi nimepata meseji kwa njia ya mtandao yaani email, tatizo vichwa vyetu hivi vinabebwa katika mwili vingine havifikiri vinaona tu nakutafuna. Kazi ya kichwa katika mwili pia ni kufikiri kwa hiyo, nadhani yupo nyuma tu ya mtandao, mimi taarifa yangu ilikuwa nimepokea meseji nydingi kwa Watanzania shilingi milioni 16, sasa hii milioni 16 wataleta sasa hivi kwa dakika moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali sasa itusaidie, Watanzania milioni 16 wa zao la Pamba wanalia, wanahitaji kujua zao lao la Pamba walilolihangaikia kwa miezi minne mpaka mitano, mpaka hivi sasa Pamba wanayo ndani, wanahitaji kwenda kuiiza sasa Serikali itutelee tamko inawasaidiaje Watanzania hawa wa Zao la Pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu ni huo tu waweja sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Nchambi. Kwa kuwa leo ni Wizara ya Fedha, jioni katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anaweza akapitia vilevile katika kuona namna gani Mazao kama haya yanaweza yakanunuliwa.

Mheshimiwa Moses Machali!

MJUMBE FULANI: Kafulila Mheshimiwa Naibu Spika!

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa. Mheshimiwa Kafulila!

MHE. DAVID Z. KUFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wa kiti chako kufuatia mgongano wa kauli za Serikali hasa kutokana na kauli ambayo iliokea hapa Bungeni ambapo Naibu Waziri aliyeungwa mkono na Waziri pamoja na Waziri Mkuu kwa maana ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alitoa shutuma nzito dhidi ya Uingereza na akashtumu Ubalozi wa Uingereza kuhusiana na suala zima la ESCROW Account.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ile ilikuwa ni zito, Watanzania na Wabunge tulisikia, Waziri akaungamkono na Waziri Mkuu akaungamkono lakini siku moja baadae Ikulu ambayo ambayo ni Ofisi Kuu ya nchi iliofa taarifa kukana kauli ile. Dola ambayo inaongozwa na Bunge, Mahakama na Serikali, Watanzania na Wabunge tunashindwa kuelewa, msimamo wa Serikali katika jambo hili, katika kauli ambazo zimetolewa Bungeni humu ni upi, ni kauli ya Ikulu au ni kauli ya Serikali ambayo imetolewa hapa Bungeni?

Naomba mwongozo kiti chako kiniambie, kwa sababu kauli ile ilitolewa kufuatia utetezi wa Serikali kulinda ufisadi wa ESCROW Account ambao nimeutaja hapa ndani ya Bunge. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako Watanzania washike kauli ipi. Kauli ya Ikulu au ya Serikali hapa Bungeni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uvezeshaji, Mheshimiwa Mary Michael Nagu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa utaratibu Serikali ina sauti moja na ina ngazi mbalimbali. Kwa hivyo, kama Naibu Waziri ameongea hapa Bungeni na hatimaye Ikulu ikasimama na ninyi mnajua kwamba Ikulu ndiyo inayoongoza.

Kwa hiyo, sauti ambayo inaelekeza sauti moja ni hiyo ya Ikulu na kwa hivyo, tamko la Ikulu ndilo ambalo linasimama na sisi Wabunge pamoja na Balozi wa Uingereza ndiyo ambayo wataichukua kama sauti ya Serikali. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa!

MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako, mara nyingi Mwenyekiti, tumekuwa na utaratibu wa Bunge kuleta wageni hapa lakini mara nyingi Mwenyekiti, Wabunge wa CCM wakija na wageni hapa wanasifiwa kwamba wanafanya kazi vizuri kama ambavyo umefanya leo kumtaja Mwigulu Nchemba pamoja na Mary Chitanda.

Wakati huo huo Bwana Opulukwa na Wabunge wa CHADEMA au upinzani CUF au NCCR wakileta Wageni wao hapa hatujaona kiti chako kikisema kwamba Wabunge hawa wanafanya kazi nzuri sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka kujuu. Ningombaa unilinde Mheshimiwa Naibu Spika.

Nakala ya Mlando (Online Document)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa naomba ukae, kuna taarifa unataka kupewa halafu utaendelea.

MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, nimekuona kwa taarifa.

TAARIFA

MHE. SELEIMAN M. N. SELEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri Watanzania wanafuatilia sana Bunge, taarifa niliyotaka kumpa Mchungaji wangu na naamini yeye ni mchungaji na anapitia vitabu vya Mungu.

Maombi ni silaha kuliko silaha yoyote iliyoko duniani na kwa sababu ni dhahiri wenzetu wanaposimama ni kunungunika, nikulalamika na kukataa Bajeti na kutoka nje. Sasa utawapongeza kwa kukataa Bajeti na kutoka nje hawatetei Majimbo? (Makofi)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa taarifa yake. Lakini naomba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mwenye floor ni Mchungaji Msigwa, sasa mkisimama wengi kwa namna hiyo mnachanganya Mchungaji hapa. Naomba tumpe nafasi Mheshimiwa Peter Msigwa amalizie. Mheshimiwa Peter Msigwa, malizia tu Mwongozo wako.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu taarifa yake naipuuza kama ninavyompuza kwa sababu Jimbo lake analotoka ni kat i ya Majimbo maskini sana katika Tanzania. Kwa hiyo, hana cha kuniambia hawezikulinganisha na Jimbo la Iringa Mjini.

Lakini nirudi kwenye hoja yangu kwamba sisi sote tunakuja na wageni hapa Bungeni. Lakini kiti chako kimekuwa na tabia kwa mfano kimekuwa kikiwasifu sana Wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Sasa nataka useme ni kipimo gani unachotumia kwa Wabunge wa CCM wanaonekana wanafanya kazi vizuri na Wabunge wa Upinzani hawafanyi kazi.

MBUNGE FULANI: Kipimo cha kukaa Bungeni siyo kutoka nje. Hawatoki nje ya Bunge kama Upinzani.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Sasa nataka njue kiti chako kinafanya namna gani. Lakini yule nampuuza kwa sababu Jimbo lake ni mionganoni mwa Majimbo maskini sana Tanzania. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Msigwa nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane. Kiti hakina upendeleo Waheshimiwa Wabunge mkiendelea kufanya kazi nzuri tutaendelea kuwa tunawasifu bila tatizo lolote.

Katibu tuendele!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Fedha

NAIBU SPIKA: Naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salim. Mheshimiwa Waziri karibu sana tafadhalii.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2014/2015. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka 2014/2015. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunitrea kuwa Waziri wa Fedha. Ninaahidi nitatekeleza jukumu hili kwa weledi na uadilifu. (Makofii)

Vilevile nawapongeza Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima - Mbunge na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mcemba - Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Fedha. Kadhalika nachukua fursa hii kumshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene kwa utendaji kazi wake mahiri na sote tunamuombea Mwenyezi Mungu ampe nguvu na afya njema katika kazi zake mpya Wizara ya Viwanda na Biashara. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Bwana Rished Bade kwa kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe, kumpongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza vema majadiliano ya Bunge la Bajeti. (Makofii)

Naomba nitumie nafasi hii kuishukuru kwa namna ya kipekee Kamati ya Kudumu ya Uchumi, Viwanda na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisasa na Makamu wake Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge wa Mkinga kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyotoa kwa Wizara wakati wa kuchambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Fedha. (Makofii)

Nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, pamoja na Kamati nzima kwa ushauri wao. (Makofii)

Katika uandaaji wa hotuba hii, Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati hizo, pamoja na ushauri na maoni ya hoja mbalimbali zilizotolewa wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Wizara ilipata pigo kwa kuondokewa na kiongozi wetu mkuu, Marehemu Dkt. William Augustao Mgimwa, tunawashukuru viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, washirika wa maendeleo, taasisi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ushirikiano waliotupa kipindi chote cha msiba. Tumeendelea kuenzi misingi imara aliyojenjea marehemu katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Aidha, tunapenda kutoa pole kwa ndugu na jamaa kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Chalinze Marehemu Said Ramadhani Bwanamdogo, tunapenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe kwa msiba wa mama yake mzazi na vilevile Mheshimiwa Martha

Mlata kwa kufiwa na baba yake, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 Mei, 2014, Wizara ya Fedha ilipata pigo tena baada ya kifo cha mke wa Katibu Mkuu Hazina. Kwa namna ya kipekee naomba nitumie tena fursa hii kutoa pole kwa Dkt. Servacius Likwalile kwa kufikiwa na mkewe. Hata hivyo, Dkt. Likwilile ameendelea kutekeleza majukumu yake ya kikazi katika kipindi chote cha msiba. Wizara inatoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki na familia yake kwa msiba wa mpPENDWA wao. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Yussuph Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete Mbunge wa Chalinze kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee vilevile napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2014/2015. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu nitaanza kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mipango ya Wizara katika mwaka 2013/2014, nitaelezea pia mikakati mbalimbali ambayo Wizara imeweka kwa mwaka 2014/2015 ili kuendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi yakiwemo usimamizi wa Bajeti, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, usimamizi wa misaada na mikopo, ulipaji wa deni la Taifa, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma, usimamizi wa utekelezaji wa MKUKUTA na usimamizi wa mashirika na taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitawasilisha bajeti ya mwaka 2014/2015 kwa mafungu saba ya Wizara ya Fedha ambayo ni Fungu 7, Fungu 10, Fungu 13, Fungu 21, Fungu 22, Fungu 23 na Fungu 50 pamoja na Fungu 45 la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba uniruhusu nisome maelezo haya kwa muhtasari na hotuba yote kama inavyoonekana kwenye vitabu vya hotuba iingie kwenye Hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Malengo yaliyozingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na utekelezaji wake kwa mwaka 2013/2014 ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa nne na ukurasa wa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, katika mwaka 2013/2014 kuititia Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, Wizara ya Fedha katika maabara ya utafutaji wa rasilimali fedha iliwekewa malengo yafuatayo:-

- (i) Kuongeza mapato mapya ya kodi ya shilingi triliuni 1.16;
- (ii) Kuongeza mapato mapya ysiyo ya kodi ya shilingi bilioni 96.7; na
- (iii) Kudhibiti matumizi na kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa katika sekta zinazotekeliza miradi hiyo.

Nakala ya Mlango (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Aprili, 2014 ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vilivyoibuliwa chini ya BRN umefikia shilingi bilioni 338 sawa na asilimia 29.14 ya lengo la kukusanya shilingi trillioni 1.16. Matokeo yasiyoridhisha yalisababishwa na baadhi ya mapendekezo ya BRN kutotekelezwa katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo ni kubadilisha mfumo wa ushuru wa bidhaa zisizo za petroli kutoka specific kwenda *ad valorem*, makisio yake yalikuwa shilingi bilioni 386 na kuanzisha kodi ya zuio asilimia tano kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambapo makisio yalikuwa ni shilingi bilioni 225.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ukusanyaji wa mapato ndiyo msingi wa kufanikiwa kwa BRN, Serikali inachambua vyanzo mbadala vyta kufidia mapato haya ili kuhakikisha lengo kuu la kuongeza mapato kwa shilingi trillioni 3.48 linafikiwa ifikapo mwaka 2015/2016. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze mwenendo wa uchumi. Katika mwaka 2013/2014 Wizara kupitia Benki Kuu iliendelea na jukumu la kuandaa, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya kuhakikisha gharama za maisha hazongezeki. Kutokana na juhud hizi mfumuko wa bei umeshuka kutoka wastani wa asilimia 16 mwaka 2012 hadi kufikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki uchumi umeendelea kuimarika huku ukuaji halisi wa Pato la Taifa ukiongezeka kwa asilimia saba katika kipindi cha mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.9 katika mwaka 2012. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kiasi kikubwa ni pamoja na mawasiliano asilimia 22.8, huduma za kifedha asilimia 12.2, ujenzi asilimia 8.6 na uuzaaji bidhaa wa jumla na rejareja asilimia 8.3. Katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha kwamba lengo la msingi la utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi linadumishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeratibu uandaaji wa mwongozo wa mpango na bajeti kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017 kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusambaza kwa wadau mwezi Disemba kama ilivyopangwa. Aidha, Wizara imeandaa na kuchapisha vitabu vya bajeti ya Serikali vya mwaka 2014/2015 *Volume I, Volume II, Volume III* na *Volume IV* kama ilivyowasilishwa Bungeni kwa ajili ya mjadala wa Bunge la Bajeti la mwaka 2014/15 unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha tafsiri rahisi ya bajeti ya Serikali (*Citizen's Budget*) kwa mwaka 2013/2014 na kitabu cha *Budget Background and Medium Term framework* 2013/2014 hadi mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa saba mpaka ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kwa ufupi usimamizi wa misaada na mikopo. Katika mwaka 2013/2014, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mikataba 18 kwa ajili ya misaada na mikopo nafuu yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 958.027 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Aidha, Wizara imeendelea kuratibu ukamilishaji wa Mwongozo mpya wa Ushirikiano wa Maendeleo yaani *Development Cooperation Framework (DCF)* ambao utachukua nafasi ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo huu una lengo la kusimamia ushirikiano wa maendeleo baina ya Serikali na wadau wa maendeleo na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa MPAMITA.

Lengo la ujumla ni kupatikana ufanisi katika misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo na kubainisha wajibu wa kila mdau wa maendeleo wakiwemo raia, Waheshimiwa Wabunge, asasi zisizo za Kiserikali na sekta ya habari. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara imepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kuzindua Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo na kuandaa mpango kazi wake pamoja na kuhamasisha matumizi yake kwa washirika wa maendeleo, Wizara, Idara zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, taasisi binafsi na Waheshimiwa Wabunge;

(ii) Kutathmini utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali inayotekelzwa kwa fedha toka Washirika wa Maendeleo kwa nia ya kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inapatikana katika miradi hiyo;

(iii) Kushiriki kwenye majadiliano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; na

(iv) Kuendelea kutafuta fedha za misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na misaada ya kiufundi kutoka kwa mashirika ya Kimataifa na nchi wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa limeendelea kusimamiwa na Sheria ya Madeni ya mwaka 1974 na marekebisho yake ya mwaka 2004. Wizara imeendelea kutoa kipaumbe katika ulipaji wa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 malipo ya deni la ndani yalifkia shilingi trilioni 1.694 ambapo kati ya malipo hayo riba ni shilingi bilioni 581.20 na mtaji (*principal rollover*) ni shilingi bilioni 1,113.33. Aidha, deni la nje limelipwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 340.22 kati ya kiasi hicho malipo ya riba ni shilingi bilioni 201.52 na deni halisi *principal* ni shilingi bilioni 138.70.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati ikiwa ni pamoja na kulipa kwa wakati madeni mbalimbali ambayo Serikali imeingia mikataba (*contractual liabilities*) na madai ya dharura (*contingent liabilities*) pindi pale yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 313 wa kada ya uhasibu, ugavi na kompyuta kutoka kwenye Wizara, Idara za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Manispaa, Halmashauri za Miji na Wilaya waliopo vyuoni na watumishi 218 walipewa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Aidha, Wizara imeendelea kusambaza Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki -*TISS*. Mikoa hiyo ipo katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji zaidi na malengo ya mwaka 2014/2015 upo katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 12 na 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuongelea kidogo kuhusiana na Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management Reform Programme - PFMRP). Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma imekamilisha utafiti wa mfumo wa kupeleka fedha kwenye Serikali za Mitaa, mpango wa utekelezaji wa utafiti huo umeandaliwa na utekelezaji wake utaanza mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti juu ya mifumo ya fedha inayotumiwa na Serikali kwa lengo la kuiunganisha mifumo hiyo ili kuboresha usimamizi wake umekamilika.

Vilevile wahasibu 522 kutoka Wizara mbalimbali, Hazina Ndogo na Sekretarieti za Mikoa walipata mafunzo juu ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za hesabu katika sekta ya umma na watumishi wengine 34 ambao wanasimamia programu hii kutoka katika Wizara na taasisi walipata mafunzo ya kusimamia mabadiliko na Kuandaa Mipango Mkakati yaani *Change Management and Strategic Planning*. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wa kuandaa mipango na bajeti inayolenga katika kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwa kuendelea na utekelezaji wa awamu ya nne ya programu ya PFMRP kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kupitia na kuboresha mifumo ya kifedha na kuangalia njia bora ya kuiunganisha baada ya utafiti kukamilika;

(ii) Kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani katika Wizara, Idara, Wakala za Serikali na Halmashauri za Serikali za Mitaa juu ya ukaguzi wa mifumo ya fedha, usimamizi na ukaguzi wa vihatarishi, ukaguzi wa bajeti na mishahara na ukaguzi wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya ununuvi wa umma. Utekelezaji wa sera na udhibiti wa ununuvi wa umma, rufaa za zabuni za umma na huduma ya ununuvi Serikalini ni kama unavyooneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 14 hadi ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mali za Serikali. Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kuandaa Sera ya Mali ya Umma. Lengo la sera hii ni kusimamia na kutoa miongozo ya udhibiti wa mali ya umma. Aidha, Wizara ilifanya uthamini wa mali ya Serikali katika Mikoa mitano na Wizara mbili, hivyo kufanya Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali zilizofanyiwa uthamini kufikia 42. Katika kipindi hicho, usimikaji wa mfumo wa uhakiki wa mali ya umma ulikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara iliendelea na zoezi la kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.58 zilikusanywa kutokana na mauzo ya vifaa hivyo na shilingi milioni 12.83 kutokana na utoaji wa leseni za udalali. Utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Millennium Challenge Account Tanzania (MCA-T). Programu ya Millennium Challenge Account Tanzania iliendelea na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, nishati ya umeme na maji. Miradi yote ya barabara imekamilika isipokuwa sehemu ya Laela hadi Sumbawanga katika barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga ambayo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2014. Miradi ya umeme na maji imekamilika na ipo katika kipindi cha uangalizi.

Nakala ya Mlando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na utekelezaji wa kuridhisha, Tanzania imekidhi vigezo na hivyo itanufaika na awamu ya pili ya msaada wa Serikali ya Marekani kuitia Shirika lake la Changamoto za Milenia (MCC). Katika awamu ya pili, miradi itakayofadhiliwa ni ile ya umeme na barabara za vijiji Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa ndani. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imetekeliza yafuatayo:-

- (i) Kutoa mwongozo wa Kamati za Ukaguzi katika sekta ya umma kwa lengo la kuhakikisha utendaji wenyewe tija kwa Kamati zote za Ukaguzi;
- (ii) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani 458, Wajumbe wa Kamati za Ukaguzi na wadau wa Ukaguzi wa Ndani wapatao 567;
- (iii) Kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo 11;
- (iv) Ukaguzi wa orodha ya malipo ya mishahara; na
- (v) Kuhakiki madai mbalimbali yaliyowasilishwa Wizarani kabla ya kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za Serikali itaendelea kuimarisha ofisi za Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa lengo la kusimamia matumizi ya fedha za umma. Utekelezaji zaidi na malengo ya mwaka 2014/2015 upo ukurasa wa 20 na 21 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa hesabu za Serikali. Katika mwaka 2013/2014 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imetekeliza kazi zake kwa mujibu wa sheria. Ofisi imeendelea kuwa mshirika katika Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa katika kukagua taasisi za Umoja wa Mataifa. Aidha, Ofisi imeendesha mafunzo kwa Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali na Kamati ya Bajeti kwa lengo la kuzijengea uwezo wa kuimarisha uwajibikaji na utawala bora. Vilevile ukaguzi wa mapato na matumizi ya Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu nao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Ofisi ya Taifa Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2014/2015 yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 21 na 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuelezea kwa kifupi uratibu wa Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya II kwa kufanya ufuatiliaji, tafiti na tathmini na kuandaa taarifa ya utekelezaji na hali ya umaskini nchini ili kuwezesha maamuzi ya kisera, kibajeti na kiutekelezaji. Kazi ya uandaaji wa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya II imekamilika na kuwekwa katika tovuti ya Wizara.

Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha Taarifa ya Maendeleo ya Malengo ya Milenia. Taarifa ya awali inaonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara ni asilimia 28.2 ambapo kwa Dar es Salaam ni asilimia 4.2, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 21.7 na maeneo ya vijiji ni asilimia 33.3. Umaskini wa chakula ni asilimia 9.7 ambapo kwa Dar es Salaam ni asilimia 1.0, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 8.7 na maeneo ya vijiji ni asilimia 11.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukusanya na kuchambua taarifa mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali ili kuandaa Taarifa ya mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA II;
- (ii) Kuandaa taarifa ya mwisho ya kutathimini utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia;
- (iii) Kufanya mapitio ya MKUKUTA II;
- (iv) Kukamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Kinga ya Jamii pamoja na kuainisha viashiria vya upimaji juhudzi za kinga ya jamii; na
- (v) Kuratibu mkutano wa kitaifa wa kujadili sera za kupambana na umaskini nchini.

Pia Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaandaa mapendekezo ya hatua zitakazofuata baada ya MKUKUTA Awamu ya II kufikia kikomo mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuititia Mradi wa SELF II imeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Aprili, 2014 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 8.6 ilikopeshwa kwa wajasiriamali 4,943 kuititia Asasi ndogo 103. Kati ya walikopeshwa wanawake ni 2,040 sawa na asilimia 41 na wanaume ni 2,903 sawa na asilimia 59. Kwa wastani urejeshwaji wa Mikopo ya Mradi wa SELF umeendelea kuwa wa ufanisi mzuri katika kiwango cha asilimia 90 hivyo kuwezesha fedha za mkopo kuzunguka na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji zaidi wa Mradi wa SELF II pamoja na malengo ya mradi huu kwa mwaka 2014/2015 yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria na Miswaada ya Fedha. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha kuititia Sheria ya Fedha ya mwaka 2013 - *The Finance Act, 2013*. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka usimamizi mzuri wa kodi na fedha za umma. Aidha, sheria mbalimbali zilizopitishwa na Bunge ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaifu ya mwaka 2013 yaani *The GEPF Retirement Benefit Fund Act, 2013* na Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya mwaka 2013 yaani *The Excise (Management and Tariff) (Amendment) Act, 2013* yaliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa 13 mwezi Desemba, 2013 yalilenga kuondoa kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye sim card.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji zaidi wa Sheria na Miswada ya Fedha pamoja na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni kama unavyooneshwaa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 25 hadi ukurasa wa 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani PPP. Wizara imeendelea kupokea na kuchambua maandiko ya miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa mwaka 2013/2014, Wizara imepokea na kuchambua miradi minne ya PPP. Katika uchambuzi wa miradi imebainika kwamba kuna upungufu katika upembuzi yakinifu pamoja na ukosefu wa wataalam wa kufanya upembuzi huo. Aidha, Wizara imeshiriki kutoa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ubia Na. 18 ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake kwa lengo la kuweka usimamizi mzuri wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015 Wizara imetenga fedha za kuanzisha Mfuko wa Kuwezesha Utekelezaji wa Miradi ya Ubia yaani PPP Facilitation Fund.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kuitia Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu imepokea na kuchambua taarifa 46 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi na taarifa 14 za kiintelijensia zimevasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria.

Aidha, mafunzo ya kudhibiti fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi yametolewa kwa watoa taarifa 135 na washiriki 86 kutoka katika vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhhibiti wa Fedha Haramu na Mali Athirika. Vilevile mafunzo hayo yametolewa kwa washiriki 49 kutoka Mamlaka za Udhhibiti. Kadhalika masuala yanayohusiana na utoroshaji wa fedha nje ya nchi yanaratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitia Kamati iliyoundwa na Serikali na taarifa ya Kamati hiyo itapatikana baada ya kazi hiyo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara kuitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu itatekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku inayohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi.

Pili, kutoa mafunzo kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na kwa watoa taarifa.

Tatu, kutoa miongozo ya kudhibiti fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi kwa watoa taarifa.

Nne, kuratibu zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi katika sekta mbalimbali nchini.

Na tano, kuendelea na hatua za kuijunga na Umoja wa Kupambana na Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi Duniani yaani EGMONT Group of Financial Intelligence Units.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kuitia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Stadi ya Kubainisha Mfumo Bora wa Kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuendelea na uchambuzi wa uhusiano wa mwenendo wa uchumi na mapato ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara kuitia Tume ya Pamoja ya Fedha inatarajia kukamilisha Stadi ya Kubainisha Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano wa Tanzania na kufanya Stadi ya Uwekezaji katika mambo ya Muungano.

Aidha, Tume inatarajia kuhuisha takwimu mbalimbali za stadi zilizofanywa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari, elimu na mawasiliano kwa umma. Utekelezaji wa Wizara juu ya habari, elimu na mawasiliano kwa umma pamoja na masuala ya watumishi yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mashirika na taasisi za umma. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kuitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imechambua na kutangaza katika Gazeti la Serikali mashirika 10 ambayo yanatakiwa kuchangia asilimia 10 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2014 kiasi cha shilingi bilioni 25 kimekusanya ikiwa ni sawa na asilimia 69.4 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 36 kwa mwaka 2013/2014.

Aidha, katika kutekeleza zoezi la kuingia mikataba ya utendaji na Bodi za Mashirika ya Umma, Wizara inakamilisha majadiliano na Bodi za Mashirika ya Umma. Vilevile zoezi la kumpata Msajili wa Hazina limefikia hatua za mwisho. Matarajio ni kwamba uteuzi utafanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kwanza kusimamia utendaji wa Bodi za Wakurugenzi wa mashirika na taasisi za umma na kuingia mikataba ya utendaji na Bodi za mashirika ya umma.

Pili, kusimamia mikakati ya kurekebisha mashirika ya umma na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa.

Na tatu, kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Shirika Hodhi la Mali za Umma (CHC) imeendelea na zoezi la ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika ya umma. Wizara inaendelea na zoezi la tathmini ya utendaji wa mashirika mengine yaliyobinafsishwa kwa lengo la kufahamu kama makubaliano ya mikataba ya mauzo yanazingatiwa na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya wastaifu na mirathi. Wizara imeendelea kuboresha kumbukumbu za wastaifu, kulipa mafao na michango ya kisheria kwa wakati.

Hadi Aprili, 2014 kumbukumbu za wastaifu 142,014 zimehifadhiwa kwenye mfumo wa kompyuta (SAPERION) na shilingi bilioni 220.79 sawa na asilimia 87 ya makadirio kimelipwa kama mafao ya wastaifu wanaolipwa pensheni na Hazina.

Aidha, Wizara imefanya uhakiki wa wastaifu walio kwenye daftari la Hazina katika mikoa tisa. Vilevile shilingi bilioni 522.86 sawa na asilimia 76 ya makadirio ya mwaka kimelipwa kama michango ya mwajiri kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wanaochangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na michango ya Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni wa PPF na Mfuko wa Mafao ya Kustaifu (GEPF). Utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania yaani TRA, hadi kufikia Aprili 2014, mapato halisi ya kodi yalifikia shilingi trilioni 7 bilioni 771.5 sawa na asilimia 75 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 10 bilioni 395.4. Aidha, kodi zilizochangia zaidi ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kodi ya Kampuni na Kodi ya Mapato ya Ajira ambazo kwa pamoja zilichangia zaidi ya asilimia 80 ya mapato hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hatua mbali mbali ambazo zimechukuliwa katika kipindi cha mwaka 2013/2014, kumekuwa na changamoto katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato. Sababu zilizochangia kutofikia malengo ni pamoja na mapato pungufu ya kodi ya kampuni kuliko iliyotarajiwa kutoka kwenye baadhi ya kampuni za madini na kushuka kwa makusanyo hususan kodi ya zuio kutokana na kupungua kwa makusanyo kwenye shughuli za utafiti wa gesi na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ni pamoja na kufutwa kwa tozo ya kadi za simu yaani *sim card levy* na makusanyo hafifu kutoka kwenye ushuru wa bidhaa wa huduma za uhawilisho wa fedha yaani *money transfers*.

Kwa upande wa forodha sababu zilizochangia kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ni ukuaji mdogo wa uingizwaji wa bidhaa kutoka nje na ongezeko la kuingiza bidhaa kupitia njia zisizo rasmi (*panya roads*) na bandari bubi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kudhibiti ukwepajji kodi, Wizara kupitia TRA inachukua hatua kadhaa za kudhibiti upotevu wa mapato kupitia bandari bubi na panya roads, kwa kufanya upelelezzi ili kuzigundua njia hizo na kuzidhibiti kwa kutumia Kikosi Kazi cha Kuzuia Magendo (*Flexible Anti-Smuggling Team*). Aidha, elimu kwa wafanyabiashara na wananchi wanaozunguka eneo la Pwani imeendelea kutolewa, ushirikiano na vyombo vingine vya udhibiti yaani Polisi, Uhamiaji na Usalama wa Taifa umeanzishwa na kufanya doria katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuimarisha makusanyo ya kodi, Mamlaka imeendelea kufanya yafuatayo:

(i) Kuimarisha matumizi ya Mashine za Kieletroniki za kutoa Risiti yaani *Electronic Fiscal Devices (EFDs)* ambapo kwa sasa inakamilisha zoezi la kuwaingiza wafanyabiashara wote wanaostahili kuanza kutumia mashine hizo;

(ii) Kuanzisha Mfumo wa Uthamini wa Mizigo ya Forodha yaani *Tanzania Customs Integrated System (TANCIS)* ambao umeanza kutumika mwezi Aprili, 2014 pamoja matumizi ya mfumo wa kuthamini magari chakavu; na

(iii) Kuanzisha Kitengo cha Kodi ya Kampuni za Kimataifa - *International Tax Unit* kwa lengo la kubaini na kudhibiti mianya ya kupotea kwa kodi inayolipwa na kampuni za kimataifa zilizowekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania umeanza kutekeleza makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuweka mazingira ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha (*Single Customs Territory - SCT*) kuanzia Januari, 2014. Ili kuhakikisha kwamba mizigo ya nchi jirani haiuzwi nchini kinyume na utaratibu wa forodha, mfumo wa kieletroniki wa ufuatilaji wa mizigo inayosafirishwa utatumika. Kupitia mfumo huu mizigo na ama vyombo vya usafirishaji hufungwa lakili ya kieletroniki (*electronic seal*) na kifaa cha mawasiliano ambavyo huunganishwa na mfumo mkuu ili kuonesha mwenendo mzima wa usafiri hadi mizigo husika utakapovuka mpaka wa nchi. Aidha, mbinu nyingine za udhibiti saidizi kama doria, usuluhishi wa taarifa (*reconciliation*) na ukaguzi zitatumika ili kuongeza udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, rufaa za kodi. Utekelezaji wa rufaa za kodi ni kama unavyooneshwa katika kitabu chetu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kibenki Benki Kuu ya Tanzania. Wizara kupitia Benki Kuu imeendelea kusimamia Sekta ya Kibenki ambapo kati ya kipindi cha Machi 2013 na Machi 2014, idadi ya benki na taasisi za fedha imeongezeka kutoka 51 na matawi 585 hadi 53 na matawi 625 kote nchini. Jumla ya mali ya sekta ya kibenki imekua kutoka shilingi trilioni 17.9 hadi shilingi trilioni 21.1. Kiwango cha mitaji kilifikia wastani wa asilimia 18.5 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 10 kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Mfumo wa Taarifa za Wakopaji yaani *Credit Reference Bureau* unaendelea vyema ambapo hadi sasa kampuni mbili zimepewa leseni ambazo ni Kampuni ya Creditinfo

Tanzania Limited iliyoanza kazi Juni, 2013 na Kampuni ya Dun & Bradstreet Credit Bureau (T) Limited iliyoanza kazi Septemba 2013. Kampuni nyingine kwa jina la Transunion, nayo hivi karibuni imepewa leseni ya muda na inajiaanda kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hizi kwa sasa zinaandaa taarifa za wateja kutoka kwenye kumbukumbu ambazo zinahifadhiwa Benki Kuu. Taarifa hizi bado zinafanyiwa uhakiki kabla ya kuanza kutumika rasmi ma mara baada ya data bank hiyo kukamilika, makampuni haya ya Credit Reference yataanza kufanya kazi hiyo kikamilifu na kwa usahihi. Benki Kuu inaendelea kuyahimiza mabenki ambayo bado hayajawasilisha taarifa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 30 Novemba, 2013 Marais wa Afrika Mashariki walitia sahihi Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Afrika Mashariki. Tukio hili ndilo limeanzisha safari yetu ya kwenda kwenye hatua ya kuwa na sarafu moja ifikapo mwaka 2024. Chini ya Itifaki hii, tumekubaliana vigezo ambavyo tutatakiwa tufikie kabla ya kuingia kwenye umoja huo na road map ya miaka 10 ambayo itaanza kutekelezwa mara tu baada ya nchi zote kuridhia utekelezaji wake.

Katika mpango huo, mambo muhimu ni kukamilisha utekelezaji wa Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja, kuoanisha mifumo ya kifedha, sera za ubadilishaji wa fedha za kigeni, sera za bajeti na mifumo ya malipo, uhuisho wa mifumo ya takwimu na kuhuisha sheria zote zinazohusiana na uanzishwaji wa umoja wa kifedha

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nielezee kwa ufupi kuhusiana maendeleo ya Benki ya Maendeleo yaani TIB. Kwa mwaka 2013/2014 TIB Development Bank ambayo zamani Benki ya Rasilimali iliendelea na marekebisho ya ndani ambapo shughuli za Benki zimegawanywa katika kampuni mbili ambazo ni TIB Development Bank Limited inayohusika na shughuli za maendeleo na TIB Corporate Finance Limited inayohusika na shughuli za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Benki ya Maendeleo TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Twiga Bancorp na Benki ya Posta kwa mwaka 2013 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 45 hadi ukurasa wa 37 hadi ukurasa wa 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kwa ufupi kuhusiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Kufuatia uamuzi wa Serikali kuanzisha Benki ya Kilimo, Wizara imetekeliza yafuatayo:-

- (i) Kuzindua Bodi ya Wakurugenzi wa Benki;
- (ii) Kukamilisha zoezi la upatikanaji wa Mtendaji Mkuu na Wakuu wa Idara;
- (iii) Kuandaa Muundo wa Benki na Muundo wa Utumishi;
- (iv) Kuandaa majukumu ya wafanyakazi;
- (v) Kuandaa rasimu ya Mpango wa Biashara; na
- (vi) Kupatikana kwa ofisi za Benki.

Mwaka 2014/2015, Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatarajia kupata leseni ya biashara, kuajiri wafanyakazi na kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na sera ya taifa ya huduma ndogo za kifedha, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha (*National Microfinance Policy*) ya mwaka 2000 ili kuondoa mapungufu ya kisheria yaliyojiteze katika utekelezaji wake kwa lengo la kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuweka mazingira mazuri katika ukuaji wa sekta hiyo.

Aidha, katika mwaka 2014/2015, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Taasisi Ndogo za Huduma za Fedha pamoja na kutunga Sheria ya Taasisi Ndogo za Huduma za Kifedha yaani *Microfinance Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za bima. Kwanza tutaanza na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima yaani *TIRA*. Katika mwaka 2013/2014 Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imekamilisha na kutoa Mkakati wa Kuendeleza Bima ya Watu wa Kipato cha Chini yaani *National Micro Insurance Strategy 2014 to 2017*. Aidha, hadi kufikia Aprili 2014, kampuni 30, madalali 100 na mawakala 500 wa bima walisajiliwa. Vilevile mauzo ya bima yaliongezeka kwa asilimia 18.5 hadi kufikia shilingi bilioni 481.7 ukilinganisha na shilingi bilioni 406.7 ambazo ni mauzo ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015 *TIRA* inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuendelea na maandalizi ya kufungua ofisi nyingine za kanda;
- (ii) Kuendelea na utaratibu wa uoanishaji (*harmonise*) sheria na kanuni za soko la bima katika eneo la Afrika Mashariki na lile la nchi za SADC;
- (iii) Kuendelea na tafiti za bima ya kilimo, mifugo, pamoja na bima za watu wa kipato cha chini (*micro – insurance*); na
- (iv) Kukamilisha taratibu za kuanzisha bima ya *Takaful*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Bima la Taifa yaani NIC, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilikamilisha urekebishaji wa Shirika la Bima la Taifa na usimikaji wa mfumo wa TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi. Utendaji wa Shirika kibiashara uliendelea kuimarka ambapo mapato ya bima yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 27.38 mwaka 2012 hadi kufikia shilingi bilioni 31.53 mwaka 2013, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 15. Mapato haya yalitokana na makusanyo ya bima za mtawanyo, vitega uchumi na mapato mengine. Utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/2015 yapo katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya mitaji na dhamana. Utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Soko la Hisa Dar es Salaam na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania pamoja na malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kama inavyooneshwa katika kitabu chetu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *credit rating*, Wizara iko katika hatua za mwisho za kupata taasisi mbili zitakaoendesha zoezi la tathmini ya kupima uwezo wa Tanzania wa kukopa na kulipa madeni yake. Mwezi Februari, 2014 Wizara ilizandikia kampuni za Fitch, Moody's *Investment Services* na Standard and Poor's kuwasilisha fomu zao za mikataba kwa hatua za uchambuzi. Tayari kampuni za Fitch na Moody's zimewasilisha fomu za mikataba kupitia kwa mshauri mwelekezi wa zoezi la *Credit Rating* yaani Citi Group.

Aidha, kuchelewa kwa zoezi hili kulitokana na kampuni hizi za upimaji (*rating agencies*) kutokukubaliana na aina ya fomu za mikataba zinazoandaliwa na Serikali pamoja na kuleta nyongeza ya gharama nje ya makubaliano yaliyosainiwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na taasisi za kitaalam na huduma nyingine, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2013/2014 pamoja na mipango kwa mwaka 2014/2015 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha pamaja na Taasisi za Mafunzo za Taasisi ya Uhasibu Arusha, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika ni kama inavyooneshwaa katika kitabu cha hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuelezee changamoto zilizopo. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Kwanza, Kuongeza mapato ya ndani ya Serikali ili kukidhi mahitaji ya matumizi ya maendeleo na ya kawaida.

Pili, mabadiliko ya hali ya uchumi na uongozi katika nchi za washirika wa maendeleo ambapo zimepelekea kushindwa kutimiza kwa baadhi ya miadi tuliyokubaliana.

Tatu, uwezo wa kusimamia mikataba katika kutekeleza baadhi ya miradi na programu za maendeleo.

Na nne, upatikanaji wa mikopo ya kibiashara kwa wakati kunakotokana na kubadilika kwa masharti kutoka kwa wakopeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kubuni vyanzo vipyaa ya mapato na kudhibiti matumizi pamoja na kupunguza upotevu wa mapato;

(ii) Kuboresha ushirikiano na washirika wa maendeleo yenyeh lengo la kuwa na uelewa sawa kuhusu masuala mbalimbali katika ushirikiano wetu;

(iii) Kuendelea kuzijengea uwezo Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia na kutekeleza mikataba ya miradi na programu za maendeleo.

(iv) Kuendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(v) Kushauri Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia vipaumbele wakati wa kupanga na utekelezaji kulingana na bajeti iliyotengwa na kuanza mazungumzo mapema na wakopeshaji wa mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya mapato na matumizi ya mafungu ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014. Mapitio ya mapato na matumizi ya mwaka 2013/2014 ya Mafungu ya Wizara ya fedha ambayo ni Fungu 7, Fungu 10, Fungu 13, Fungu 21, Fungu 22, Fungu 23 na Fungu 50 na Fungu 45 ni kama inavyooneshwaa katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ufupi nielezee Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mapato, katika mwaka 2014/15, Wizara ya Fedha Fungu 50 inakadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi yapatayo shilingi bilioni 126.19.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa upande wa Fungu 50 - Wizara ya Fedha, kwa fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Kwanza Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 66.23. Kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 5.62 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 60.61.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 29.8; kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 19.35 na fedha za nje ni shilingi bilioni 10.45.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, katika Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Kwanza Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 82.17; kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 5.01 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 77.15. Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 7.95 kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 4.80 na fedha za nje ni shilingi bilioni 3.15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 4,354.86, kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 10,341, Deni la Taifa ni shilingi bilioni 3,650 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni bilioni 693.91.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 21 – Hazina, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Kwanza, Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 790.32. kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 4.01 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 786.31 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara na taasisi zilizo chini ya fungu hili, nyongeza ya mishahara ya watumishi wa Serikali pamoja na matumizi maalum.

Pili, Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 57.42, kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 17. fedha za nje ni shilingi bilioni 40.42.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Udhhibitii wa Fedha Haramu. Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni mbili na Miradi ya Maendeleo, fedha za nje ni shilingi bilioni 0.19.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 2.32 kwa matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo, shilingi 318,661,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni mbili ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo, Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 88.45, kati ya fedha hizo shilingi 670,328,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 87.78 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 1.94 kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi milioni 650,000,000 na fedha za nje ni shilingi bilioni 1.29.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 69.84. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 10.41 na Matumizi Mengineyo ni shilingi bilioni 59.43. Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 13.01, kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 8 na fedha za nje ni shilingi bilioni 5.01.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakuu wa Idara na Vitengo, wafanyakazi wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius Likwelile na Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Elizabeth Nyambibo, Profesa Adolf Mkenda na Ndugu Doroth Mwanyika kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vilevile nawashukuru Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali chini ya Wizara kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu mazito ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii vilevile inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha, kwenye www.mof.go.tz

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na sasa naomba kutoa hoja. (Makofi)
(Hoja ilitolewa iamuliwe)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA SAADA MKUYA SALUM (MB) AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2014/15**

UTANGULIZI:

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2014/15.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka 2014/15. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunitfea kuwa Waziri wa Fedha. Ninaahidi kwamba nitatekeleza jukumu hili kwa weledi na uadilifu.

Vile vile, nawapongeza Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) na Mhe. Adam Kighoma Ali Malima (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha. Kadhalika, namshukuru pia aliyejewa Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Janeth Zebedayo Mbene (Mb) kwa utendaji kazi wake mahiri na tunamuombea Mwenyezi Mungu ampe nguvu na afya njema katika kazi zake mpya Wizara ya Viwanda na Biashara. Nichukue pia fursa hii kumpongeza Bw. Rished M. Bade kwa kuteuliwa kuwa Kamishna Mkoo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bunge la Bajeti.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru kwa namna ya pekee Kamati ya Kudumu ya Uchumi, Viwanda na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mbunge wa Kisera) na Makamu wake Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mbunge wa Mkinga) kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatao kwa Wizara wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti Mhe. Andrew John Chenge (Mbunge wa Bariadi Magharibi) pamoja na Kamati nzima kwa ushauri wao. Katika uandaaji wa hotuba hii, Wizara imizingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati hizo pamoja na ushauri na maoni ya hoja mbalimbali zilizotolewa wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/14.

5. **Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu, Wizara ilipata pigo kwa kuondokewa na kiongozi wetu mkuu Marehemu Dkt. William Augustao Mgimwa. Tunawashukuru Viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, Washirika wa Maendeleo, Taasisi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ushirikiano waliotupa kipindi chote cha msiba. Tumeendelea kuenzi misingi imara aliyojenyea marehemu katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Aidha, tunapenda kutoa pole kwa ndugu na jamaa kufuatia kifo cha aliyejewa Mbunge wa Chalinze Marehemu Saidi Ramadhani Bwanamdogo. Vile vile, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe kwa msiba wa mama yake mzazi aliyesariki tarehe 01 mwezi Juni, 2014. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

6. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 27 mwezi Mei 2014, Wizara ya Fedha ilipata pigo tena baada ya kifo cha mke wa Katibu Mkuu - Hazina. Kwa namna ya kipekee naomba nitumie tena fursa hii kutoa pole kwa Dkt. Servacius Likwelile kwa kufiwa na mkewe. Hata hivyo Dr. Likwelile ameendelea kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote cha msiba. Wizara inatoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa familia yake kwa msiba wa mpendwa wao. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza, Mhe. Yusuf Salim Hussein Mbunge wa Chambani, Mhe. Godfrey William Mgimwa (Mbunge wa Kalenga) na Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mbunge wa Chalinze) kwa kuchaguliwa kwao.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2014/15.

9. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu nitaanza kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mipango ya Wizara katika mwaka 2013/14. Nitaelezea pia mikakati mbalimbali ambayo Wizara imeweka kwa mwaka 2014/15 ili kuendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi yakiwemo: usimamizi wa Bajeti ya Serikali; ukusanyaji mapato ya Serikali; usimamizi wa misaada na mikopo; ulipaji wa Deni la Taifa; usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma; usimamizi wa utekelezaji wa MKUKUTA; na usimamizi wa mashirika na taasisi za umma.

10. **Mheshimiwa Spika**, mwisho nitawasilisha bajeti ya mwaka 2014/15 kwa mafungu saba ya wizara ya fedha ambayo ni fungu 7, 10, 13, 21, 22, 23 na fungu 50 pamoja na fungu 45 la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

11. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa uniruhusu nisome maelezo haya kwa muhtasari na hotuba yote kama inavyoonekana kwenye vitabu vya hotuba iingie kwenye Hansard.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2013/14 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015

12. **Mheshimiwa Spika**, malengo yaliyozingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya wizara pamoja na utekelezaji wake kwa mwaka 2013/14 ni kama unavyooneshwu katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa tano na wa sita.

Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa

13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, kupitia Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, Wizara ya Fedha katika maabara ya utafutaji wa rasilimali fedha iliwekewa malengo yafuatayo: kuongeza mapato mapya ya kodi ya shilingi trillioni 1.16; kuongeza mapato mapya yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 96.7; kudhibiti matumizi; na kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa katika sekta zinazotekeliza miradi hiyo.

14. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2014, ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vilivyoibuliwa chini ya BRN umefikia shilingi bilioni 338 sawa na asilimia 29.14 ya lengo la kukusanya shilingi trillioni 1.16. Matokeo yasiyordhisha yalisababishwa na baadhi ya mapendekezo ya BRN kutokutekelezwa katika mwaka 2013/14. Mapendekezo hayo ni kubadilisha mfumo wa ushuru wa bidhaa zisizo za petroli kutoka specific kwenda advalorem (makisio shilingi bilioni 386) na kuanzisha kodi ya zuio ya asilimia tano kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi (makisio shilingi bilioni 225.6). Kwa vile ukusanyaji wa mapato ndio msingi wa kufanikiwa kwa BRN, Serikali inachambua vyanzo mbadala vya kufidia mapato haya ili kuhakikisha lengo kuu la kuongeza mapato kwa shilingi trillioni 3.48 linafikiwa ifikapo mwaka 2015/16.

Mwenendo wa Uchumi

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kupitia Benki Kuu iliendelea na jukumu la kuandaa, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya kuhakikisha ghamama za maisha hazongezeki. Kutokana na juhudhi hizi, mfumuko wa bei umeshuka kutoka wastani wa asilimia 16 mwaka 2012 hadi kufikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2013. Katika kipindi hiki uchumi umeendelea kuimarika huku ukuaji halisi wa Pato la Taifa ukiongezeza kwa asilimia 7.0 katika kipindi cha mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.9 katika mwaka 2012. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kiasi kikubwa ni pamoja na mawasiliano asilimia 22.8, huduma za kifedha asilimia 12.2, ujenzi asilimia 8.6, na uuzaaji bidhaa wa jumla na rejareja asilimia 8.3. Katika mwaka 2014/15, Wizara kupitia Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha kwamba lengo la msingi la utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi linadumishwa.

Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha 2014/2015 – 2016/2017 kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusambaza kwa wadau mwezi Desemba kama ilivyopangwa. Aidha, Wizara imeandaa na kuchapisha vitabu vya bajeti ya Serikali vya mwaka 2014/15 (Volume I, II, III na IV) kama vilivyowasilishwa Bungeni kwa ajili ya mjadala wa Bunge la Bajeti la mwaka 2014/15 unaoendelea; kitabu cha tafsiri rahisi ya bajeti ya Serikali (Citizen's Budget) kwa mwaka 2013/2014; na Kitabu cha Budget Background and Medium Term Framework – 2013/2014 – 2015/2016.

17. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/15 ni kama unavyooneshwaa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa tisa mpaka ukurasa wa 11.

Usimamizi wa Misaada na Mikopo

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mikataba 18 kwa ajili ya misaada na mikopo nafuu yenyeye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 958.027 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu ukamilishaji wa Mwongozo mpya wa Ushirikiano wa Maendeleo - Development Cooperation Framework ambaa utachukua nafasi ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA). Mwongozo huu una lengo la kusimamia ushirikiano wa maendeleo baina ya Serikali na Wadau wa Maendeleo na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa MPAMITA. Lengo la ujumla ni kupatikana ufanisi katika misaada kutoka kwa Washirika wa maendeleo na kubainisha wajibu wa kila mdau wa maendeleo wakiwemo raia, wabunge, asasi zisizo za kiserikali na sekta ya habari.

19. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kuzindua Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo na kuandaa mpango kazi wake pamoja na kuhamasisha matumizi yake kwa Washirika wa Maendeleo, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Taasisi Binafsi na Waheshimiwa Wabunge; kutathmini utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali inayotekelawa kwa fedha toka Washirika wa Maendeleo kwa nia ya kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inapatikana katika miradi hiyo; kushiriki kwenye majadiliano na Jumuia za kikanda na kimataifa; na kuendelea kutafuta fedha za misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na Misaada ya Kiufundi kutoka kwa Mashirika ya Kimataifa na nchi wahisani.

Ulipaji wa Deni la Taifa

20. **Mheshimiwa Spika**, Deni la Taifa limeendelea kusimamiwa na Sheria ya Madeni ya mwaka 1974 na marekebisho yake ya mwaka 2004. Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika ulipaji wa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 malipo ya deni la ndani yalifikia shilingi bilioni 1,694.53 ambapo kati ya malipo hayo riba ni shilingi bilioni 581.20 na Mtaji (principal rollover) ni shilingi bilioni 1,113.33.

Aidha, deni la nje limelipwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 340.22, kati ya kiasi hicho malipo ya riba ni shilingi bilioni 201.52 na deni halisi *principal* ni shilingi bilioni 138.70.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati ikiwa ni pamoja na kulipa kwa wakati madeni mbalimbali ambayo serikali imeingia mikataba (Contractual Liabilities) na madai ya dharura (Contingent Liabilities) pindi yanapotokea.

Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma

22. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 313 wa kada ya uhasibu, ugavi na kompyuta kutoka kwenye wizara, idara za serikali, sekretariati za mikoa, manispaa, halmashauri za miji na wilaya walipo vyuoni na watumishi 218 walipewa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Aidha, Wizara imeendelea kusambaza Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki -TISS. Mikoa hiyo ipo katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 14.

23. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji zaidi na malengo ya mwaka 2014/15 upo katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 14 na 15.

Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma - Public Finance Management Reform Programme (PFMRP)

24. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma imekamilisha utafiti wa mfumo wa kupeleka fedha kwenye Serikali za Mitaa, mpango wa utekelezaji wa utafiti huo umeandaliwa na utekelezaji wake utaanza mwaka wa fedha 2014/15. Aidha, utafiti juu ya mifumo ya fedha inayotumiwa na Serikali kwa lengo la kuiunganisha mifumo hiyo ili kuboresha usimamizi wake umekamilika. Vile vile, Wahasibu 522 kutoka Wizara mbalimbali, hazina ndogo na sekretarieti za mikoa walipata mafunzo juu ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Hesabu katika Sekta ya Umma na watumishi wengine 34 ambaao wanasmamia programu hii kutoka katika wizara na taasisi walipata mafunzo ya kusimamia Mabadiliko na Kuandaa Mipango Mkakati -Change Management and Strategic Planning. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wa kuandaa mipango na bajeti inayolenga katika kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwa kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Programu ya PFMRP kwa kufanya yafuatayo: kupitia na kuboresha mifumo ya kifedha na kuangalia njia bora ya kuiunganisha baada ya utafiti kukamilika; na kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani katika wizara, idara, wakala za Serikali na halmashauri za Serikali za Mitaa juu ya ukaguzi wa mifumo ya fedha, usimamizi na ukaguzi wa vihatarishi, ukaguzi wa bajeti na mishahara, na ukaguzi wa miradi.

Sera ya Ununuzi wa Umma

26. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa sera na udhibiti wa ununuzi wa umma, rufaa za zabuni za umma na huduma ya ununuzi serikalini ni kama inavyooneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 17 hadi ukurasa wa 21.

Usimamizi wa Mali ya Serikali

27. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara iliendelea Sera ya Mali ya Umma. Lengo la sera hii ni kusimamia na kutoa miongozo ya udhibiti wa mali ya umma. Aidha, Wizara ilifanya uthamini wa mali ya Serikali katika mikoa mitano na wizara mbili, hivyo kufanya wizara, idara zinazojitegemea na wakala wa Serikali zilizofanyiwa uthamini kufikia 42. Katika kipindi hicho, usimikaji wa mfumo wa uhakiki wa mali ya umma ulikamilika.

Vile vile, Wizara iliendelea na zoezi la kuondosha mali chakavu katika wizara na idara za Serikali ambapo jumla ya shilingi biliioni 1.58 zilikusanywa kutokana na mauzo ya vifaa hivyo na shilingi milioni 12.83 kutokana na utoaji wa leseni za udalali. Utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/15 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 22 na 23.

Mpango wa Millenium Challenge Account – Tanzania (MCA-T)

28. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Millenium Challenge Account Tanzania iliendelea na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, nishati ya umeme na maji. Miradi yote ya barabara imekamilika isipokuwa sehemu ya Laela- Sumbawanga katika barabara ya Tunduma- Sumbawanga ambayo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2014. Miradi ya umeme na maji imekamilika na ipo katika kipindi cha uangalizi.

Aidha, kutokana na utekelezaji wa kuridhisha, Tanzania imekidhi vigezo na hivyo itanufaika na awamu ya pili ya msaada wa Serikali ya Marekani kuititia Shirika lake la Changamoto za Milenia (MCC). Katika awamu ya pili, miradi itakayofadhiliwa ni ya umeme na barabara za vijijini Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Ukaguzi wa Ndani

29. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara imetekeleza yafuatayo: kutoa Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi katika Sekta ya Umma kwa lengo la kuhakikisha utendaji wenyе tija kwa Kamati zote za Ukaguzi; kutoa mafunzo ya kuwajenjea uwezo wakaguzi wa ndani 458, wajumbe wa Kamati za Ukaguzi na wadau wa ukaguzi wa ndani wapatao 567; kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo 11; ukaguzi wa orodha ya malipo ya mishahara; na kuhakiki madai mbalimbali yaliyowasilishwa wizarani kabla ya kulipwa.

30. **Mheshimiwa Spika**, wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali itaendelea kuimarisha ofisi za Mkaguzi Mkuu wa ndani kwa lengo la kusimamia matumizi ya fedha. Utekelezaji zaidi na malengo ya mwaka 2014/15 upo ukurasa wa 24 na 25 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

31. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imetekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria. Ofisi imeendelea kuwa mshirika katika Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa katika kukagua taasisi za Umoja wa Mataifa. Aidha, Ofisi imeendesha mafunzo kwa Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali na Kamati ya Bajeti kwa lengo la kuzijenjea uwezo wa kuimarisha uwajibikaji na utawala bora. Vile vile, ukaguzi wa mapato na matumizi ya vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu unaendelea.

32. **Mheshimiwa Spika**, malengo ya Ofisi ya Taifa Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2014/15 yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 26 na 27

Uratibu wa Utekelezaji wa MKUKUTA

33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA II kwa kufanya ufuatiliaji, tafiti, na tathmini na kuandaa taarifa ya utekelezaji na hali ya Umaskini nchini ili kuwezesha maamuzi ya kisera, kibajeti na kiutekelezaji. Kazi ya uandaaji wa Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA II imekamilika na kuwekwa katika tovuti ya Wizara. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha Taarifa ya Maendeleo ya Malengo ya Milenia. Taarifa ya awali inaonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara ni asilimia 28.2 ambapo kwa Dar es Salaam ni asilimia 4.2, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 21.7 na maeneo ya vijijini ni asilimia 33.3. Umaskini wa chakula ni asilimia 9.7 ambapo kwa Dar es Salaam ni asilimia 1.0, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 8.7 na maeneo ya vijijini ni asilimia 11.3.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kukusanya na kuchambua taarifa mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali ili kuandaa Taarifa ya mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA II; kuandaa taarifa ya mwisho ya kutathimini utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia; kufanya mapitio ya MKUKUTA II; kukamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Kinga ya Jamii pamoja na kuainisha viashiria vya upimaji juhudii za kinga ya jamii; na kuratibu mkutano wa kitaifa wa kujadili sera za kupambana na umaskini nchini. Pia Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaandaa mapendekezo ya hatua zitakazofuata baada ya MKUKUTA II kufikia kikomo mwezi Juni, 2015.

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa SELF II imeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Aprili 2014, mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 8.6 ilikopeshwa kwa wajasiriamali 4,943 kupitia Asasi ndogo 103. Kati ya walokopeshwa, wanawake ni 2,040 sawa na asilimia 41 na wanaume ni 2,903 sawa na asilimia 59. Kwa wastani, urejeshwaji wa Mikopo ya Mraidi wa SELF umeendelea kuwa wa ufanisi mzuri katika kiwango cha asilimia 90 hivyo kuwezesha fedha za mkopo kuzunguka na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

36. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji zaidi kwa mraidi wa SELF pamoja na malengo ya mraidi huu kwa mwaka 2014/15 yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 29.

Sheria na Miswada ya Fedha

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria mbalimbali za Fedha kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2013 - *The Finance Act, 2013*. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka usimamizi mzuri wa kodi na fedha za umma.

Aidha, Sheria mbalimbali zilizopitishwa na Bunge ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaifu ya mwaka 2013 - *The GEPF Retirement Benefit Fund Act, 2013* na marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya mwaka 2013 - *The Excise (Management and Tariff) (Amendment) Act, 2013* yaliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa 13 mwezi Desemba, 2013 yaliyolenga kuondoa kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye Sim Card.

38. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji zaidi wa sheria na miswada ya fedha pamoja na Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 30 hadi ukurasa wa 31.

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi – PPP

39. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kupokea na kuchambua maandiko ya miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Katika mwaka 2013/14, Wizara imepokea na kuchambua miradi minne ya PPP. Katika uchambuzi wa miradi imebainika kwamba kuna upungufu katika upembuzi yakinifu pamoja na ukosefu wa Wataalam wa kufanya upembuzi huo.

Aidha, Wizara imeshiriki kutoa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ubia Na. 18 ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake kwa lengo la kuweka usimamizi mzuri wa ubia.

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Wizara imetenga fedha za kuanzisha Mfuko wa Kuwezesha Utekelezaji wa Miradi ya Ubia -*PPP Facilitation Fund*.

Udhiliti wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi

41. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kupitia Kitengo cha Udhiliti wa Fedha Haramu imepokea na kuchambua taarifa 46 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi na taarifa 14 za kiintelijensia zimewasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria. Aidha, mafunzo ya kudhibiti fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi yametolewa kwa watoa taarifa 135 na washiriki 86 kutoka katika vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhiliti wa Fedha Haramu na Mali Athirika.

Vile vile, mafunzo hayo yametolewa kwa washiriki 49 kutoka Mamlaka za Udhiliti. Kadhalika, masuala yanayohusiana na utoroshaji wa fedha nje ya nchi yanaratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Kamati ilioundwa na Serikali, na taarifa ya Kamati hiyo itapatikana baada ya kazi hiyo kukamilika.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara kuitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu itatekeleza yafuatayo: kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku inayohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kutoa mafunzo kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na kwa watoa taarifa; kutoa miongozo ya kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kwa watoa taarifa; kuratibu zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi katika sekta mbalimbali nchini; na kuendelea na hatua za kujunga na Umoja wa Kupambana na Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi Duniani - EGMONT Group of Financial Intelligence Units.

Tume ya Pamoja ya Fedha

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kuitia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Stadi ya Kubainisha Mfumo Bora wa Kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuendelea na Uchambuzi wa Uhusiano wa Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara kuitia Tume ya Pamoja ya Fedha inatarajia kukamilisha Stadi ya Kubainisha Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano wa Tanzania, na kufanya Stadi ya Uwekezaji katika Mambo ya Muungano. Aidha, Tume inatarajia kuhuisha Takwimu mbalimbali za Stadi zilizofanywa na Tume.

Habari, Elimu na Mawasiliano kwa Umma

45. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa wizara juu ya habari, elimu na mawasiliano kwa umma pamoja na masuala ya watumishi yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa 33 hadi ukurasa wa 35.

Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kuitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imechambua na kutangaza katika Gazeti la Serikali mashirika 10 ambayo yanatakiwa kuchangia asilimia 10 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Aprili 2014, kiasi cha shilingi bilioni 25.0 kimekusanywa ikiwa ni asilimia 69.4 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 36 kwa mwaka 2013/14.

Aidha, katika kutekeleza zoezi la kuingia mikataba ya utendaji na Bodi za Mashirika ya Umma, Wizara inakamilisha majadiliano na Bodi za Mashirika ya Umma.

Vile vile, zoezi la kumpata Msajili wa Hazina limefikia hatua za mwisho. Matarajio ni kwamba uteuzi utafanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

47. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo: kusimamia utendaji wa Bodi za Wakurugenzi wa mashirika na taasisi za umma na kuingia mikataba ya utendaji na Bodi za mashirika ya umma; kusimamia mikakati ya kurekebisha mashirika ya umma na kufanya tathmini na ufuutiliaji wa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa; na kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma ili kuongeza mapato ya Serikali.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kuitia Shirika Hodhi la Mali za Umma (CHC) imeendelea na zoezi la ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika ya Umma. Wizara inaendelea na zoezi la tathmini ya utendaji wa mashirika mengine yaliyobinafsishwa kwa lengo la kufahamu kama makubaliano ya mikataba ya mauzo yanazingatiwa na kuchukua hatua stahiki.

Mafao ya Wastaafu na Mirathi

49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha kumbukumbu za Wastaafu, kulipa mafao na michango ya kisheria kwa wakati. Hadi Aprili 2014, kumbukumbu za wastaafu 142,014 zimehifadhiwa kwenye mfumo wa kompyuta (SAPERION) na shilingi bilioni 220.79 sawa na asilimia 87 ya makadirio kimelipwa kama mafao ya wastaafu wanaolipwa pensheni na Hazina. Aidha, Wizara imefanya uhakiki wa wastaafu walio kwenye daftari la Hazina katika mikoa tisa. Vile vile, shilingi bilioni 522.86 sawa na asilimia 76 ya makadirio ya mwaka kimelipwa kama michango ya mwajiri kwa Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wanaochangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na michango ya Bima ya Afya.

50. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni wa PPF na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF). Utekelezaji kwa mwaka 2013/14 ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 37 hadi ukurasa wa 39.

Mamlaka ya Mapato Tanzania

51. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2014, mapato halisi ya kodi yalifikia shilingi bilioni 7,771.5 sawa na asilimia 75 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 10,395.4. Kodi zilizochangia zaidi ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kodi ya Kampuni na Kodi ya Mapato ya Ajira ambazo kwa pamoja zilichangia zaidi ya asilimia 80 ya mapato hayo.

52. **Mheshimiwa Spika**, licha ya hatua mbali mbali ambazo zimechukuliwa katika kipindi cha mwaka 2013/14, kumekuwa na changamoto katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato. Sababu zilizochangia kutofikia malengo ni pamoja na: mapato pungufu ya Kodi ya Kampuni kuliko ilivyotarajiwa kutoka kwenye baadhi ya kampuni za madini; na kushuka kwa makusanyo hususan Kodi ya Zui Kutokana na kupungua kwa makusanyo kwenye shughuli za utafiti wa gesi na mafuta. Sababu nyingine ni pamoja na kufutwa kwa Tozo ya Kadi za Simu - SIMcard levy na makusanyo hafifu kutoka kwenye Ushuru wa Bidhaa wa Huduma za Uhawilisho wa Fedha - Money Transfers. Kwa upande wa Forodha sababu zilizochangia kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ni ukuaji mdogo wa uingizwaji wa bidhaa kutoka nje, na ongezeko la kuingiza bidhaa kupitia njia zisizo rasmi (panya roads) na bandari bubu..

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kudhibiti ukwepaji kodi, wizara kupitia TRA inachukua hatua kadhaa za kudhibiti upotevu wa mapato kupitia bandari bubu na panya roads, kwa kufanya upelelezi ili kuzigundua njia hizo na kuzidhibiti kwa kutumia Kikosi Kazi cha Kuzuia Magendo (Flexible Anti-Smuggling Team).

Aidha, elimu kwa wafanyabiashara na wananchi wanaozunguka eneo la Pwani imeendelea kutolewa, ushirikiano na vyombo vingine vya udhibiti yaani Polisi Uhamiaji na Usalama wa Taifa umeanzishwa; na kufanya doria katika maeneo hayo.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudzi za kuimarisha makusanyo ya kodi, Mamlaka imeendelea kufanya yafuatayo: kuimarisha matumizi ya Mashine za Kieletroniki za kutoa Risiti - *Electronic Fiscal Devices (EFDs)* ambapo kwa sasa inakamilisha zoezi la kuwaingiza wafanyabiashara wote wanaostahili kuanza kutumia mashine hizo; kuanzisha Mfumo wa Uthamini wa Mizigo ya Forodha - *Tanzania Customs Integrated System (TANCIS)* ambao umeanza kutumika mwezi Aprili 2014 pamoja matumizi ya mfumo wa kuthamini magari chakavu; na kuanzisha Kitengo cha Kodi ya Kampuni za Kimataifa - *International Tax Unit* kwa lengo la kubaini na kudhibiti mianya ya kupotea kwa kodi inayolipwa na kampuni za kimataifa zilizowekeza nchini.

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kutekeleza makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuweka mazingira ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha (Single Customs Territory - SCT) kuanzia Januari, 2014. Ili kuhakikisha kwamba mizigo ya nchi jirani haiuzwi nchini kinyume na utaratibu wa forodha, mfumo wa ki-elektroniki wa ufuatilaji wa mizigo inayosafirishwa utatumika. Kupitia mfumo huu, mizigo na ama vyombo vya usafirishaji hufungwa lakili ya ki-elektroniki (electronic seal) na kifaa cha mawasilaino ambavyo huunganishwa na mfumo mkuu ili kuonesha mwenendo mzima wa usafiri hadi mizigo husika utakapovuka mpaka wa nchi.

Aidha, mbinu nyine za udhibiti saidizi kama doria, usuluhishi wa taarifa (reconciliation) na ukaguzi zitatumika ili kuongeza udhibiti.

Rufaa za Kodi

55. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa rufaa za kodi ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 42 na 43.

Huduma za Kibenki

Benki Kuu ya Tanzania

56. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Benki Kuu imeendelea kusimamia Sekta ya Kibenki ambapo kati ya kipindi cha Machi 2013 na Machi 2014, idadi ya benki na taasisi za fedha imeongezeka kutoka 51 na matawi 585 hadi 53 na matawi 625 kote nchini. Jumla ya mali ya sekta ya kibenki imekua kutoka shilingi trillioni 17.9 hadi shilingi trillioni 21.1. Kiwango cha mitaji kilifika wastani wa asilimia 18.5 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 10 kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Mfumo wa Taarifa za Wakopaji - Credit Reference Bureau unaendelea vyema, ambapo hadi sasa kampuni mbili zimepewa leseni ambazo ni: kampuni ya Creditinfo Tanzania Limited ilioanza kazi Juni 2013 na kampuni ya Dun & Bradstreet Credit Bureau (T) Limited ilioanza kazi Septemba 2013. Kampuni nyine kwa jina la Transunion, nayo hivi karibuni imepewa leseni ya muda na inajiandaa kuanza kufanya kazi.

57. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni hizi kwa sasazinaandaa taarifa za wateja kutoka kwenye kumbukumbu ambazo zinahifadhiwa Benki Kuu. Taarifa hizi bado zinafanyiwa uhakiki kabla ya kuanza kutumika raski. Mara baada ya data bank hiyo kukamilika, makampuni haya ya Credit Reference yataanza kufanya kazi hiyo kikamilifu na kwa usahihi. Benki Kuu inaendelea kuyahimiza mabenki ambayo bado hayajawasilisha taarifa kufanya hivyo.

58. **Mheshimiwa Spika**, Tarehe 30 Novemba 2013, Marais wa Afrika Mashariki walitia sahihi Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Afrika Mashariki. Tukio hili, ndilo limeanzisha safari yetu ya kwenda kwenye hatua ya kuwa na sarafu moja ifikapo mwaka 2024. Chini ya Itifaki hii, tumekubaliana vigezo ambavyo tutatakiwa tufikie kabla ya kuingia kwenye umoja huo na road map ya miaka 10 ambayo itaanza kutekelezwa mara tu baada ya nchi zote kuridhia utekelezaji wake. Katika mpango huo, mambo muhimu ni; kukamilisha utekelezaji wa Umoja wa forodha na Itifaki ya soko la pamoja; kuoanisha mifumo ya kifedh, sera za ubadilishaji wa fedha za kigeni, sera za bajeti, na mifumo ya malipo; uhuisha mifumo ya takwimu na; kuhuisha sheria zote zinazohusiana na uanzishwaji wa umoja wa kifedha

Benki ya Maendeleo TIB

59. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, TIB Development Bank (zamani Benki ya Rasilimali) iliedelea na marekebisho ya ndani ambapo shughuli za Benki zimegawanywa katika kampuni mbili ambazo ni TIB Development Bank Limited inayohusika na shughuli za maendeleo na TIB Corporate Finance Limited inayohusika na shughuli za biashara.

60. **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Benki ya Maendeleo TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Twiga Bancorp na Benki ya Posta kwa mwaka 2013/14 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 45 hadi ukurasa 48.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo - TADB

61. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia uamuji wa Serikali kuanzisha Benki ya Kilimo, Wizara imetekeleza yafuatayo: kuzindua Bodi ya Wakurugenzi wa Benki; kukamilisha zoezi la upatikanaji wa Mtendaji Mkuu na Wakuu wa Idara; kuandaa Muundo wa Benki na Muundo wa Utumishi; kuandaa majukumu ya wafanyakazi; kuandaa rasimu ya Mpango wa Biashara; na kupatikana kwa ofisi za Benki. Mwaka 2014/15, Benki ya Maendeleo ya Kilimo **inatarajia** kupata leseni ya biashara, kuajiri wafanyakazi na kuanza kutoa huduma.

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha

62. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha - National Microfinance Policy, 2000 ili kuondoa mapungufu ya kisheria yaliyojitezea katika utekelezaji wake kwa lengo la kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuweka mazingira mazuri katika ukuaji wa sekta hiyo.

Aidha, katika mwaka 2014/15, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Taasisi Ndogo za Huduma za fedha pamoja na kutunga Sheria ya Taasisi ndogo za huduma za kifedha - Microfinance Act.

Huduma za Bima

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imekamilisha na kutoa Mkakati wa Kuendeleza Bima ya Watu wa Kipato cha Chini - National Micro Insurance Strategy 2014-2017. Aidha, hadi kufikia Aprili 2014, kampuni 30, madalali 100 na mawakala 500 wa bima walisajiliwa.

Vile vile, mauzo ya bima yaliongezeka kwa asilimia 18.5 hadi kufikia shilingi bilioni 481.7 ukilinganisha na shilingi bilioni 406.7 ambazo ni mauzo ya mwaka uliopita.

64. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, TIRA inatarajia kutekeleza yafuatayo: kuendelea na maandalizi ya kufungua ofisi nyingine za kanda; kuendelea na utaratibu wa uoanishaji (harmonise) sheria na kanuni za soko la bima katika eneo la Afrika Mashariki na lile la nchi za SADC; kuendelea na tafiti za bima ya kilimo, mifugo, pamoja na bima za watu wa kipato cha chini (micro – insurance); na kukamilisha taratibu za kuanzisha bima ya Takaful.

Shirika la Bima la Taifa – NIC

65. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Wizara ilikamilisha urekebishihi wa Shirika la Bima la Taifa na usimikaji wa mfumo wa TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi. Utendaji wa Shirika kibashara uliedelea kuimarika ambapo mapato ya bima yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 27.38 mwaka 2012, hadi kufikia shilingi bilioni 31.53 mwaka 2013, ongezeko hilo ni sawa na

asilimia 15. Mapato haya yalitokana na makusanyo ya bima za mtawanyo, vitega uchumi na mapato mengine. Utekelezaji zaidi na malengo kwa mwaka 2014/15 yapo ukurasa wa 50 na 51 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Masoko ya Mitaji na Dhamana

66. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Soko la Hisa Dar es Salaam na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania pamoja na malengo kwa mwaka 2014/15 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 42 hadi ukurasa wa 46.

67. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu credit rating, wizara iko katika hatua za mwisho za kupata taasisi mbili zitakazoendesha zoezi la tathmini ya kupima uwezo wa nchi wa kukopa na kulipa madeni yake. Mwezi Februari 2014, Wizara ilizandikia kampuni za Fitch, Moody's Investment Services na Standard and Poors kuwasilisha fomu zao za mikataba kwa hatua za uchambuzi. Tayari kampuni ya Fitch na Moody's zimewasilisha fomu za mikataba kuitia kwa mshauri mwelekezi Citi Group.

Aidha, kuchelewa kwa zoezi hili kulitokana na kampuni hizi za upimaji (Rating Agencies) kutokukubaliana na aina ya fomu za mikataba zinazoandalishi na serikali pamoja na kuleta nyongeza ya gharama nje ya makubaliano yaliyosainiwa awali.

Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

68. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2013/14 pamoja na mipango kwa mwaka 2014/15 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha pamoja na taasisi za mafunzo za Taasisi ya Uhaisbu Arusha, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Taasisi ya Uhaisbu Tanzania, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 56 hadi ukurasa wa 62.

CHANGAMOTO

69. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

- i. Kuongeza mapato ya ndani ya Serikali ili kukidhi mahitaji ya matumizi ya maendeleo na ya kawaida;
- ii. Mabadiliko ya hali ya uchumi na uongozi katika nchi za washirika wa maendeleo ambapo zimepelekea kushindwa kutimizwa kwa baadhi ya miadi;
- iii. Uwezo wa kusimamia mikataba katika kutekeleza baadhi ya miradi na programu za maendeleo; na
- iv. Upatikanaji wa mikopo ya kibashara kwa wakati kunakotokana na kubadilika kwa masharti kutoka kwa wakopeshaji.

70. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- i. Kubuni vyanzo vipya vya mapato na kudhibiti matumizi pamoja na kupunguza upotevu wa mapato;
- ii. Kuboresha ushirikiano na washirika wa maendeleo yenyen lengo la kuwa na uelewa sawa kuhusu masuala mbali mbali katika ushirikiano wetu;
- iii. Kuendelea kuzijengea uwezo Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia na kutekeleza mikataba ya miradi na programu za maendeleo;
- iv. Kuendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma - "Public Financial Management Reform Programme (PFMRP)"; na
- v. Kushauri Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia vipaumbele wakati wa kupanga na utekelezaji kulingana na bajeti iliyotengwa.
- vi. Kuanza mazungumzo mapema na wakopeshaji wa mikopo ya kibashara.

Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu ya Wizara kwa Mwaka 2013/14

71. **Mheshimiwa Spika**, mapitio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/14 ya mafungu ya wizara ya fedha ambayo ni fungu 7,10,13,21,22,23 na 50 pamoja na fungu 45 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 64 hadi ukurasa wa 68.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

Mapato

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara ya Fedha Fungu 50 inakadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi yapatayo shilingi **126,188,104,000 (bilioni 126.19)**

Maombi ya Fedha

Fungu 50 - Wizara ya Fedha.

73. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida Shilingi **66,239,790,000 (bilioni 66.23)**. Kati ya hizo mishahara ni shilingi shilingi **5,620,668,000 (bilioni 5.62)** na matumizi mengineyo shilingi **60,619,122,000 (bilioni 60.61)**.

(b) Miradi ya Maendeleo Shilingi **29,803,232,000 (bilioni 29.71)**. Kati ya hizo:

- (i) Fedha za Ndani - Shilingi **19,350,000,000 (bilioni 19.35)**.
- (ii) Fedha za Nje - Shilingi **10,453,232,000 (bilioni 10.45)**.

Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali:

74. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida - Shilingi **82,170,024,000 (bilioni 82.17)**. Kati ya hizo mishahara shilingi **5,012,762,000 (bilioni 5.01)** na matumizi mengineyo shilingi **77,157,262,000 (bilioni 77.16)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – Shilingi **7,950,000,000 (bilioni 7.95)** Kati ya hizo:

- (i) Fedha za Ndani -Shilingi **4,800,000,000 (bilioni 4.80)**.
- (ii) Fedha za Nje -Shilingi **3,150,000,000 (bilioni 3.15)**.

Fungu 22- Deni la Taifa

75. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **4,354,865,076,000 (bilioni 4,354.86)**. Kati ya hizo mishahara ni shilingi **10,341,136,000 (bilioni 10.34)**, Deni la Taifa shilingi **3,650,612,000,000 (bilioni 3,650.61)** na matumizi mengineyo ni shilingi **693,911,940,000 (bilioni 693.91)**.

Fungu 21 - HAZINA

76. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida Shilingi **790,325,216,000 (bilioni 790.32)**. Kati ya hizo mishahara ni shilingi **4,015,511,000 (bilioni 4.01)** na matumizi mengineyo shilingi **786,309,705,000 (bilioni 786.31)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya Idara na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili, nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Serikali na matumizi maalum.

(b) Miradi ya maendeleo ni shilingi **57,417,015,000 (bilioni 57.42)**. Kati ya hizo;

- (i) Fedha za Ndani- Shilingi **17,000,000,000 (bilioni 17.0)**
- (ii) Fedha za Nje- Shilingi **40,417,015,000 (bilioni 40.42)**

Fungu 13 – Kitengo cha Udhibili wa Fedha Haramu:

77. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - Shilingi **2,000,000,000 (bilioni 2.0)**.

(b) Miradi ya Maendeleo, fedha za nje Shilingi **195,000,000 (bilioni 0.19)**.

Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha:

78. **Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **2,318,661,000 (bilioni 2.32)** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi **318,661,000 (bilioni 0.32)** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **2,000,000,000 (bilioni 2.0)** ni matumizi mengineyo.

Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina:

Nakala ya Mtandao (Online Document)

79. **Mhesimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - Shilingi **88,455,278,000** (**bilioni 88.45**). Kati ya hizo shilingi **670,328,000** (**bilioni 0.67**) ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **87,784,950,000** (**bilioni 87.78**) ni matumizi mengineyo.

- (b) Miradi ya Maendeleo – Shilingi **1,943,000,000 (bilioni 1.94)** Kati ya hizo:

 - (i) Fedha za Ndani –Shilingi **650,000,000 (bilioni 0.65).**
 - (ii) Fedha za Nie -Shilingi **1,293,000,000 (bilioni 1.29).**

Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

80. **Mhesimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/14, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida shilingi **69,843,825,000 (billioni 69.84)**. Kati ya hizo mishahara ni shilingi **10,408,402,000 (billioni 10.41)** na matumizi mengineyo shilingi **59,435,423,000 (billioni 59.43)**.

(b) Miradi ya maendeleo shilingi **13,011,432,000 (bilioni 13.01)**, kati ya hiso:

- (i) Fedha za ndani shilingi **8,000,000,000 (bilioni 8.0)**.
 - (ii) Fedha za nje shilingi **5,011,432,000 (bilioni 5.01)**.

HITIMISHO

81. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Idara na Vitengo, Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius B. Likwelile na Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Elizabeth J. Nyambibo, Prof. Adolf F. Mkenda na Ndugu Doroth S. Mwanyika kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Vile vile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali chini ya Wizara kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

82. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz)

83. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Saada Mkuya Salum kwa kusoma hotuba yako. Tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Esther bado unataka kusimama au tuendelee?

MBUNGE FULANI: (*Hakutumia kipaza sauti*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea wale wageni wa kutoka Meatu wamefika, naomba pale mlipo msimame. Wageni kutoka kule Mwanhuzi.

Wageni hawa ni wageni wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, ambaye ni DC wa Meatu na mionganini mwao ni Madiwani 27 wakiongozwa na Ndugu Pius Machungwa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, karibuni sana.

Lakini pia mionganini mwao kuna watendaji 28 wakiongozwa na Kaimu Mkurugenzi, Ndugu John Aloyce, lakini pia mionganini mwao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi saba wakiongozwa na Dada Pendo ambaye ni Katibu wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Meatu. (Makofii)

Karibuni sana, sana. Wabunge wenu wote wawili hapa Mheshimiwa DC na Mheshimiwa Mpina wanafanya kazi nzuri sana humu ndani ya Bunge. Karibuni sana. (Makofii)

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mpina. (Makofii)

MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA

BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba nami niongeze sauti yangu kwa namna ya pekee kabisa kutoa pole kwa misiba ambayo imewafika Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Zitto Kabwe pamoja na Mheshimiwa Martha Mlata kwa kufiwa na wazazi wetu, tunamwomba Mungu aendelee kuwatia nguvu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea katika hotuba yangu ukurasa wa 8 kile kipengele cha 3.3 Mashine za Risiti (*EFD*), huo ukurasa wa 8 wote ufutwe. Halafu ukurasa wa 9, paragraph ya kwanza, ya pili, ya tatu, ifutwe na kuanza na paragraph ile inayosema "Katika Awamu ya Pili."

Mheshimiwa Naibu Spika, na baada ya kusema hayo naomba hotuba yangu yote iingizwe kwenye kumbukumbu za *Hansard* kama ambavyo imewasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kabisa kwa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Meatu ambao wapo hapa na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisasa kwa jinsi ambavyo wananiunga mkono katika harakati za kuleta maendeleo katika Wilaya ya Meatu na Jimbo langu la Kisasa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naendelea kusema kwamba hakika sitapumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisasa. Na hii ni sahihi tu kwani heri punda aumie, lakini mzigo wa tajiri ufile salama na ninyi mnajua huko kwetu ndama jeuri hakatwi pembe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nianze na utangulizi, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya wizara katika mwaka wa fedha 2013/2014 - Deni la Taifa. Katika muda mfupi tumeshuhudia ongezeko kubwa la Deni la Taifa kutoka shilingi trilioni 21.2 Juni, 2013, hadi shilingi trilioni 29.477, Januari, 2014, hili ni ongezeko la shilingi trilioni 8.277 kwa kipindi cha miezi saba tu.

Ongezeko hili la deni haliendi sambamba na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ujenzi wa miundombinu ya uchumi, hali hii inapelekea kujengeka hofu kwa kuwa huenda deni hili likawa uchochoro na ubadhirifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza kuona kuwa deni linaongezeka kila mwaka licha ya Serikali kulipa zaidi ya shilingi trilioni tatu kila mwaka wa fedha, pia kwa upande wa fedha zinazopokelewa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miundombinu ya uchumi zipo chini ya 50% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika kila mwaka wa fedha. Kwa upande makusanyo ya mapato ya ndani yanaendelea kuripotiwa kuwa yana wastani wa 90% ya malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya Serikali kuendelea kusema kuwa deni hili ni himilivu, lakini viashiria (*financial indicators*) vinaonesha kuelmewa kwa Taifa na mzigoto mkubwa wa madeni, mfano mapato ya ndani yamezidiwa na matumizi ya kawaida hivyo kuipelekea Serikali kukopa hata kwa ajili ya warsha, semina, safari, mafunzo na matengenezo ya magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa hivi sasa limefikia 47% ya Pato la Taifa (*nominal value*), lakini kwa kipimo cha bei ya sasa (*pv of debt-to-GDP*) Deni la Taifa limefikia 24%. Huku deni la nje pekee likiwa ni 13.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya CAG kuahidi kwa muda mrefu kufanya ukaguzi maalum wa Deni la Taifa hili ili kuweza kujua uhalali wa madeni haya, lakini hadi sasa taarifa yake haijawasilishwa. Kamati inahoji ni lini taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni ili kuwawezesha wananchi kufahamu undani wa jambo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji wa fedha za maendeleo (*funds disbursement*) katika Wizara mpaka Machi na Aprili, 2014. Ukiangalia hapo chati ambapo ni mwezi wa nne, tulikuwa tumebakiza miezi miwili tu kumaliza bajeti hii tunayoendelea nayo, lakini Wizara zote utaona nyiningine katika lile jedwali ambalo nimeliwasilisha pale, zipo chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, Wizara kama ya maendeleo ya mifugo na uvuvi licha ya umuhimu wake hadi mwezi wa nne, 2014 ilikuwa imepokea 13% tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa ushahidi huu ni dhahili kuwa Wizara nydingi hadi mwisho wa mwaka wa fedha zitakuwa chini ya 50% ya fedha zitakazopokea za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini Serikali/Hazina haipeleki fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge? Na kwa nini uhamisho wa fedha katika mafungu mbalimbali ni mkubwa kinyume na sheria na taratibu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - *Transfer pricing*. Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi sana katika eneo hili hususan katika makampuni makubwa yenye makampuni tanzu hapa nchini (*Multinational Companies*), mfano katika maeneo ya madini, simu, mabenki, gesi na kadhalika. Aidha, eneo hili limekuwa likihusishwa na rushwa kubwa kati ya makampuni na watumishi wa Serikali. Pia tafiti zinaonyesha kuwa utoroshaji wa fedha nje ya nchi unachangiwa sana na *transfer pricing* na *mis-pricing*. Serikali itilie mkazo katika usimamizi na udhibiti wa TP ili kuhakikisha kuwa bei zinazotumika katika kampuni mama na kampuni tanzu ni bei halisi ya soko, *I mean Arm's length price*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha kanuni na miongozo usimamizi wa *Transfer Pricing (regulations and guidelines)* jambo ambalo lilipiganiwa

sana na Kamati yangu. Kwa siku za nyuma tulikuwa tunatumia kanuni na miongozo ya UN pamoja na ya OECD ambayo haikuwa na nguvu ya kutosha kisheria kudhibiti TP. Licha ya kwamba Sheria ya Kodi (*The Income Tax Act, 2004*) Section 33(1) na (2), iliweka kipengele cha kusimamia TP, lakini haikuwa na kanuni na miongozo ya kusimamia sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kitengo cha Kodi cha Kimataifa (*International Taxation Unit - ITU*) katika Mamlaka ya Mapato (TRA) ambapo endapo kitengo hiki kitawezeshwa kikamilifu kitasaidia sana kupambana na *Transfer Pricing* na *Mis-Pricing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa kushughulikia hoja za kesi za *Transfer Pricing* hivi sasa ni miaka mitatu tu, muda ambao ni mfupi sana, inapendekezwa muda huo uongezwe hadi miaka sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa tiketi wa kielektroniki (*Electronic Ticketing System - ETS*). Ni kwa muda mrefu Serikali imekuwa haipati mapato ya kutosha kutoka sekta ya michezo hususan mpira wa miguu ulio chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania. Hii inatokana na mfumo dhaifu wa ukusanyaji fedha kipindi cha kuuza tiketi, mfano tiketi bandia kuendelea kutumika, kukosekana kwa uwazi katika mapato halisi, uwezo mdogo wa kusambaza tiketi nchi nzima, rushwa katika mageti. Hali hii inaifanya TRA ishindwe kusanya mapato halisi katika sekta hii na hata katika upande wa vilabu na wachezaji hawanufaiki ipasavyo, kwani fedha nyingi hubaki mifukoni mwa wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, TFF iliona changamoto hizi na kuamua kutangaza zabuni ya electronic ticketing mwaka 2012, CRDB Bank ilishinda zabuni hiyo na tayari imekwisha tayarisha na kuweka mfumo wa system design and hardware acquisition and installation kwa gharama ya shilingi bilioni tatu toka mwaka 2013, na katika viwanja sasa hivi tayari wameweka vya Kaitaba, Mkwakkani, Azam Complex, Sokoine, Jamhuri, CCM Kirumba, Sheikh Amri Abeid, zote hizi zimekamilika katika mwaka huu wa 2014 na sasa shughuli ya kusimika mfumo huo katika Uwanja wa Taifa wa Dar es salaam unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu mpya utaongeza mapato kwa Serikali kwa kiwango kikubwa, TFF, vilabu na wachezaji watanufaika pia. Aidha tunashuhudia mfumo huu ulipotumika katika maeneo ya TANAPA, KCMC, TRA wenyewe ambapo mapato yalipanda kutoka 200% mpaka 300%; ukiangalia jedwali pale mfano tu wa KCMC mapato yao yalipanda kutoka milioni mbili kwa siku na kupanda mpaka milioni 12 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maoni na ushauri wa Kamati yangu TRA iweke sharti la lazima la kuitaka TFF kutumia mfumo wa *Electronic Ticketing* katika kuuza tiketi zake ikiwa ni jitihada za kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine za risiti (*EFD*). Katika awamu ya pili ya lengo la kuwaunganisha wafanyakishara wa mashine za *EFD*, walipa kodi 200,000 wasio kwenye mfumo wa VAT katika mwaka wa fedha 2013/2014 hadi kufikia tarehe 31 Machi walikuwa ni walipa kodi 23,534 tu ndio waliounganishwa katika mfumo wa *EFD*, kati walipa kodi 17,916 ni wale walio katika mfumo wa VAT na 5,618 ni wale ambao hawapo katika mfumo wa VAT.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwaunganisha walipa kodi 200,000 ambao hawamo katika mfumo wa VAT na wenye mzunguko wa fedha wa chini ya shilingi milioni 40 umekuwa wa kusuasua na wenye lawama nyingi, kwani wamekuwa wakidai kuwa moja, EFDs zinagharama kubwa za kuzinunua ambapo gharama yake ni shilingi 60,000/= mpaka 700,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zinaonyesha kuwa mzunguko wa biashara wenyewe thamani ya shilingi milioni 14 mpaka milioni 40 kwa mwaka mtaji wake hauzidi shilingi milioni tano, hivyo kumlazimisha mtu mwenye mzunguko mdogo huu wa fedha anunue kifaa cha EFDs ni kuyumbisha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, gharama za matengenezo ni kubwa mno na mashine hizi huharibika mara kwa mara. Tafiti zilizofanywa na TCCIA zinaonyesha kuwa watumiaji wa mashine hizi hutumia siku 54 kwa mwaka kuzipeleka kwenye matengenezo na sharti la matengezo ya mashine hizi hufanywa na wakala aliyeuza mashine hiyo ambayo amekuwa akijipangia bei anayotaka yeye. Mbaya zaidi mawakala hawa hawapo kila sehemu, hivyo wafanyabiashara hulazimika kusafiri umbali mrefu kuwafuata. Hali hii imekuwa ikiongeza gharama kubwa sana kwa uendeshaji wa biashara ukizingatia kuwa mitaji yao hii ni midogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mashine za EFDs zinatumia lugha ya kiingereza ambayo wafanyabiashara na Watanzania wengi hawaifahamu, na hivyo kushidwa kuziendesha mashine na kusababisha matumizi yasiyo ya lazima kwa kuongeza gharama za biashara kwa maana ya kuajiri mtu wa kuweza kuwasomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, makosa katika kubonyeza hayarekebishiki kiurahisi na wakati mwininge husababisha malipo makubwa ambayo huchukua muda na mlongo mrefu kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini Serikali isitoe mashine hizi bure kwa wafanyabiashara hususan wale wa kipato cha chini cha shilingi milioni 40 kwani EFDs ni kifaa cha TRA katika kukusanya kodi. Mfano, baadhi ya makampuni ya huduma za simu yamekuwa hata yakitoa vifaa pamoja na mitaji kwa mawakala wao, iweje Serikali ishindwe kufanya hivyo kwa wafanyabiashara wake hawa wadogo? (makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini EFDs ziuzwe na wazabuni badala ya TRA wenyewe? Kwa upande wa TANESCO mita za LUKU huuzwa na shirika lenyewe na siyo wazabuni, pia matengenezo ya LUKU hufanywa na Shirika. Ikumbukwe kwamba EFDs ni chombo muhimu chenye taarifa muhimu ya mapato ya Serikali iweje kiuzwe na kufanyiwa matengenezo na mtu binafsi yaani mzabuni?

Kamati inashauri kuwa upatikanaji wa huduma za matengenezo zipatikane kila Wilaya na kwa umbali usiozidi kilomita 40 ili kuwarahisishia wafanyabiashara kuendesha biashara hizo na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza ari na uhiari kwa walipa kodi. Ili kutambua na kujenga morali kwa walipa kodi nchini kila mwaka, naliomba Bunge lako liweke azimio la kuwapongeza walipa kodi bora nchini. Aidha, Kamati yangu inaomba na inatumia fursa hii kuwashimiza wananchi wote kujua umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari, kwani maendeleo ya Taifa hili tutayaleta sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu (*dollarization*). Katika uchumi *dollarization* ni matumizi ya fedha za kigeni kama vile dola ya Kimarekani katika kuhifadhi akiba yaani *store of value*, kupitia thamani yaani *the unit of account* na kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani yaani *medium of exchange*. Kwa mujibu wa Sheria ya *Foreign Exchange Act of 1992*, fedha halali ya malipo ni shilingi ya Tanzania. Katika siku za hivi karibuni shilingi imekuwa ikitumika sambamba na dola ya Kimarekani *unofficial dollarization*. Pia wananchi na makampuni ya ndani kuendelea kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za

kigeni transaction dollarization. Amana ya fedha za kigeni katika mabenki imeongezeka na kufikia 26% ikiwa na maana kwamba katika kila mwaka shilingi milioni 100 iliyopo katika mabenki, shilingi 26 ziko katika fedha za kigeni. Sheria ya mwaka 1992 ilichakachuliwa na tamko la Serikali la mwaka 2008 ambalo liliruhusu matumizi holela ya dola nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kutumia sarafu ya Tanzania sambamba na ile ya kigeni, kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za kigeni kunaiondolea sarafu ya Tanzania ushindani katika soko (*International market Competitiveness*), Bureau de Change za ndani kukosa soko na kupelekea Serikali kukosa mapato, sarafu ya Tanzania kutokujulikana kimataifa kwa kuwa mgeni huja na dola yake na kuondoka na dola yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaitaka Serikali ifute tamko lake la mwaka 2008 linaloruhusu matumizi holela ya fedha za kigeni dollarization na kuitaka Benki Kuu kusimamia Sheria ya Foreign Exchange Act, 1992 kuwa sarafu ya Tanzania itatumika kwa malipo halali ya ndani na nukuu za bei zote kufanyika kwa shilingi ya Tanzania.

Vilevile kufanya marekebisho ya Sheria kwa kutoza kodi, malipo yanayofanywa kwa fedha za kigeni kama nchi nyingine zinavyo kama Afrika Kusini pamoja na Peru na Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka ya kubadilishga fedha za kigeni. Imegundulika kuwa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hapa nchini hayasimamwi kikamilifu na Benki Kuu, kwani ubadilishaji holela wa fedha umetawala nchini. Sheria inatamka mtu ye yeyote anaetaka kubadilisha fedha kuwa na kitambulisho, tiketi na shughuli anayofanya lakini hivi sasa tunashuhidia watu wanakwenda kubadilisha fedha bila kitambulisho na wala hakuna risiti zinazotolewa kwa huduma hiyo. Hii ni hatari kwa Taifa kwani inaweza kutumika kama uchochoro mkubwa wa utorosha wa fedha nje ya nchi yaani *illicit financial outflow* na ukwepajji mkubwa wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati katika eneo hili. Kamati inashauri Benki Kuu kusimamia kikamilifu biashara ya maduka ya kubadilisha fedha (*Bureaux de Change*) kwa kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaotenda makosa katika biashara hii sambamba na kufanya marekebisho Sheria ya Fedha za Kigeni yaani *The Foreign Exchange Act of 1992*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Maendeleo ya TIB (*TIB Development Bank*). Kwa kuzingatia umuhimu wa benki hii katika uharakishaji wa maendeleo, uchumi na ukuaji wa sekta binafsi tulikubaliana katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano yaani mwaka 2010/2011 hadi 2015/2016 benki hii ingeweza kuwa imepewa shilingi bilioni 500 yaani kila mwaka shilingi bilioni 100. Lakini cha kusikitisha hadi sasa ni shilingi bilioni 110 tu zimepelekwa ikiwa umebakili mwaka mmoja tu wa mpango huu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuwa Serikali imeshindwa kutimiza azma yake hiyo ya kuiongezea benki hii mtaji kama ambavyo ilikubalika katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano hivyo ikubali ombi la TIB kuiruhusu kukopa shilingi bilioni 300 kutoka katika Mfuko wa Jamii ya PPF na NSSF na kwamba Serikali ikubali kutenga fedha shilingi bilioni 30 kila mwaka kulipa riba ya mkopo huo kwa mfululizo wa kipindi cha miaka 10 yaani kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Posta. Benki hii imekuwa ikifanya vizuri na mtaji wake umekuwa ukukua sana, ili Benki hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi inahitaji mtaji wa shilingi bilioni 7.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inashauri Serikali kuiptatia Benki ya TPB mtaji wa shilingi bilioni 7.5 kama walivyoomba ambapo Kamati imejiridhisha na uwezo mzuri wa kiutendaji ambayo faida inaonekana ya wazi na Kamati yangu inawapongeza sana Mkurugenzi wa TIB Development Bank pamoja na Benki ya Posta kwa kazi nzuri sana wanayoifanya na kuzifanya hizi benki kupaa kimaendeleo na zinakuwa kila siku. Kamati inawapongeza sana Wakurugenzi hao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Twiga Bancorp Limited. Benki hii haifanyi vizuri sana, thamani ya amana zinapungua kila mwaka na kumejitokeza na wizi wa Tanzania shillings bilioni 3.3 katika benki hiyo uliofanywa na watumishi wa benki makao makuu wakishirikiana na wafanyakazi wa benki wa tawi la Mlimani City na wateja. Licha ya kamati kuomba kuletewa taarifa na hatua stahiki zilizochukuliwa na uongozi wa benki imekuwa ikiletewa taarifa nusu nusu na zisizokamilika na kupelekea mashaka kuwa uongozi umekuwa hauna nia ya dhati ya kurejesha fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inauliza ni kwa nini wizi ulioanza kufanyika mwaka 2007 uje kugundulika mwaka 2012 wakati ukaguzi ulikuwa ukifanyika kila mwaka? Kwa nini hadi sasa kesi iliyopo mahakamani ni ya shilingi milioni 704 tu? Kamati haikubaliani kuwa eti wizi wa shilingi bilioni 5.596 bado unafanyiwa uchunguzi chini ya DCI. Ni uchunguzi gani unaofanywa zaidi ya taarifa ya ukaguzi iliyobaini mpango mzima wa jinsi fedha hizo zilivyoibowiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeamua kuunda Kamati ndogo kufuatilia hatua mahususi zilizochukuliwa kuhusiana na wizi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zingine za sekta ya mabenki pamoja na fedha nchini. Kiwango kikubwa cha lazima cha sehemu ya amana (*statutory minimum reserve – SMR*) za sekta binafsi (*private sector deposits*) 10% kwa maana ya private sector, lakini kwa maana ya Serikali ni 40% ambacho ni kiwango kinachohifadhiwa na Benki Kuu ikiwa ni amana isiyo na faida yoyote wakati mabenki hulipa riba kwa kutunza fedha hizo. Kiwango hiki cha SMR ni kikubwa na kwamba utaratibu huu hauzingatii uwezo wa benki na hivyo unaathiri uwezo wa utoaji mikopo nafuu na hivyo kuchangia mabenki kutoza riba kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu kuweka kiwango kikubwa sana cha riba inayotozwa kwa mabenki na Serikali zinapokopa kutoka Benki Kuu yaani *Treasury Bill Rate*. Benki Kuu imepandisha kiwango cha riba kutoka 7.58% hadi 12.58%. Kiwango hiki cha riba cha takribani 13% kimekuwa ni kichocheo kikubwa cha mabenki kutoza riba kubwa na kumesababisha wananchi kushindwa kukopa, kurejesha mikopo yao na pia hata kufilisika na kushindwa kurejesha riba kubwa.

Mheshimiwa Naibi Spika, mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge Serikali imekuwa ikisema kwamba watu wanaopandisha riba ni mabenki lakini ukweli ni kwamba Benki Kuu ndiyo ambao wamesababisha kiwango cha riba nchini kupanda baada ya kuwa wanaongeza kila siku *interest rate* yao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kukosekana kwa sovereign rating ambayo ingesaidia mabenki na taasisi za fedha kukopa fedha kutoka katika soko la kimataifa (*International market*) kwa riba nafuu. Kukosekana kwa utaratibu huu ambapo Serikali imekuwa ikisema ipo kwenye mchakato sasa ni zaidi ya miaka 10 na hivyo huwalazimu kulipa kiwango kikubwa cha kinga ya hasara yaani *the high risk premium*.

Kwa hiyo kwa kufanya hivyo benki zetu haziwezi kupata mkopo ambao ni wa bei nafuu hata tunapokopa kwenye mabenki ya kimataifa kama hazitakuwa na huo mpango wa sovereign rating.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati katika eneo hili. Kamati inashauri kwamba Serikali kuitia Benki Kuu ipunguze kiwango cha riba kwa mabenki kutoka 12.58% hadi 7.58%, mpango wa sovereign rating ukamilike haraka, kiwango cha statutory minimum reserve kishuke hadi 5% kwa sekta binafsi na 20% kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipe dhamana zake (*Government guarantee*) na madeni ya wazabuni na wakandarasi ambayo yamefikia shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi na mafunzo. Kamati iligundua kwamba katika Chuo cha Uhasibu cha Arusha Kamati haikuridhishwa na ongezeko kubwa la gharama za ujenzi wa maktaba ya kisasa ulioongezeka kutoka shilingi 2.8 hadi bilioni 6.8 na kwamba sababu zilizotolewa juu ya ongezeko la fedha hizo Kamati yangu haikubaliani nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sintofahamu hiyo kamati imeiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuvi (PPRA) kufanya ukaguzi wa mradi huu na kujiridhisha kama ongezeko hilo ni halali na kama liliufuata sheria na taratibu za manunuvi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu CHC, utakumbuka kwamba tuliweka Azimio la Bunge kwamba CHC itakoma kufikia tarehe 30 Juni, 2014. Kutekeleza Azimio hilo, Wizara kwa kuzingatia Sheria ya Ununuvi wa Umma ilitangaza kwenye vyombo vya habari kumpata mshauri mwelekezi wa kufanya tathmini ya utendaji wa CHC mwezi Septemba, 2013. Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kimepata zabuni hiyo na baada ya taratibu zote kukamilika.

Kamati inashangazwa na Wizara kushindwa kutekeleza Azimio la Bunge kwa miaka mitatu na kutangaza kumpata mzabuni katika mwezi wa Mei, 2014 ikiwa ni mwezi mmoja tu kabla ya Shirika hili kufika ukomo. Hata hivyo Kamati illiagiza Wizara kuleta taarifa ya tathmini mbele ya Kamati tarehe 2 Juni, 2014 lakini hadi nasoma taarifa ya leo agizo la Kamati halijatekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliarifiwa kuwa shughuli za CHC zitarithiwa na ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo haijaandalowiwa kuweza kukabiliana na majukumu hayo ambayo yamesalia:-

- (i) Ni madeni bilioni 116.88;
- (ii) Usimamizi wa kesi 432 zenye thamani ya fedha bilioni 656; na
- (iii) Ufilisi wa mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuwa majukumu yaliyosalia ni mazito na kwa kuwa Serikali imeshindwa kufanya tathmini kwa wakati kama Azimio la Bunge liliyyotaka na kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina haijaandalowiwa kikamilifu kushika majukumu haya hivyo Kamati inashauri kuwa CHC iongezwe muda wa miaka mitatu mingine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la manunuvi, Sheria ya Manunuvi ya mwaka 2004 iliwaondoa Waheshimiwa Madiwani katika uidhinishaji wa zabuni lakini sheria ya leo imewarejeshwa Waheshimiwa Madiwani na ninatoa wito kote nchini mliko Waheshimiwa Madiwani mjue sasa mmerejeshwa katika kuhakikisha kwamba zile zabuni mnazi-approve ninyi. Laikini Sheria ya Manunuvi pia ya mwaka 2011 iliwarejeshwa Madiwani ikashindwa kutambua kwamba hata Wabunge hawa wanalo jukumu la kurejeshewa sheria ya wao waweze kupitia

mikataba ya Serikali. Kwa hiyo Kamati inaona kabisa kwamba mikataba ya Serikali yote iletwe hapa Bungeni kwa ajili ya kuhakikiwa kabla utekelezaji haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa madini ya gesi na mafuta. Kamati ilifanya ziara nchini Norway na kujifunza mambo mengi na vilevile imeona baadhi ya mikataba ambavyo haifanyi vizuri. Katika mkataba mmoja ambaao nimeuonyesha humo kwenye ripoti yangu, moja ushiriki wa Watanzania katika uchumi wa gesi katika utangulizi uliopo ukurasa wa tatu na ibara ya 8(1) katika mkataba huo ukurasa wa 11 wa nyongeza imewekwa wazi kwamba hapo kama nilivyoandika hivyo inaonyesha wazi kabisa kwamba ushiriki wa Watanzania katika uchumi ambapo kipengele hicho kimeshafunga kwamba hawa jamaa wataamua wao wenye ni jinsi gani watakavyowashirikisha Watanzania. Sasa haitakuwa na nguvu yoyote ya kisheria kwa sababu tayari mkataba umeshaingiwa ambaao unasisitiza kuwa kampuni za nje zitakuwa na uamuvi wa mwisho kuhusiana na mnyororo ya thamani na ugavi. Sisi leo tunapitia *local content* lakini mkataba tayari tulioingia umewapa madaraka haya makampuni ya nje kwamba yenye ndiyo yenyewe uamuvi wa namna gani watakavyotumia mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii ni kwamba je, sera yetu ya ikishirikishwa kwa wazawa ambayo ipo katika mchakato wa kutayarishwa na Wizara ya Nishati na Madini itakuwa na nguvu za kisheria juu ya vipengele vya mikataba ambayo imeshaingiwa huko nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao wa gesi ambaao Tanzania itaupata kupitia TPDC, kanuni iliyowekwa katika mkataba wa nyongeza kwa ajili ya kufikia malengo ya gesi zinazostahili kupata kampuni za nje na TPDC ni kama ifuatavyo; baada ya gesi kuchimbwa, zinafanyika hesabu kutambua kiwango cha gesi kilichopatikana, ukiondoa ilivyotumika katika uzalishaji. Hii inaitwa *adjusted gas quantity* ikiwa ni kwa mujibu wa ibara ya 11.1 ya mkataba wa nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *adjusted gas quantity* ikishajulikana kampuni za kigeni zitakuwa na haki ya kuchukua gesi kiasi kinacholingana na gharama wanazostahili kurudishiwa kimkataba (*recoverable contract expenses*). Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 11.1 (a),(b) na (C) iliyopo katika ukurasa za 11 na 12 katika mkataba wa nyongeza. Hizi gharama zote hizi za *recoverable contract expenses* ambayo ni *operating expenses* pamoja na *exploration expenses* pamoja na *development expenses*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa ibara ya 11.1 (a) iliyopo ukurasa wa 11 katika mkataba wa nyongeza, kampuni za nje zimeruhusiwa kutumia 70% ya gesi iliyozaalishwa ili kujilipa gharama zilizotumika kimkataba. Hii ina maana kwamba hadi hapo watakapomiliza kujilipa kila kitu, gesi itakayobaki kwa ajili ya kugawana ni 30% ya gesi yote inayozalishwa. Gesi iliyoobaki kwa ajili ya kugawana *profit gas* itagawanywa kwa utaratibu huo niliouonyesha kwenye jedwali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako umeisha.

MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kama nilivyoarifiwa kwamba muda wangu umekwisha, hotuba yangu imekuwa ndefu, nimejaribu hata kufanya summary imeshindikana, sasa niombe kwamba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa tuliofanya hadi leo hii tunahitimisha hotuba yetu.

Niendelee kuwashukuru sana na kuwapongeza sana Wajumbe, pia niwashukuru sana kwa namna ya pekee kabisa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na biashara. (Makofii)

Mimi Mwenyekiti wenu najivunia sana kuwa Wajumbe waliomahiri, waliobobea katika masuala ya uchumi na fedha, michango yenu na ushauri wenu utalisaidia Taifa hili, nawashukuru sana na naomba nimiratajwa kwa majina kama nilivyoyaorodhesha kwa sababu muda haunitoshi.

Nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na Spika wa Bunge letu kwa jinsi ambavyo mnatusaidia kufanya kazi zetu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwisho maombi ya fedha katika mwaka wa fedha, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha ya Uchumi kama Waziri wangu alivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na nakushukuru sana Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa hotuba yako nzuri kwa niaba ya Kamati yako.

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Kamati ilichambua kwa kina taarifa hizo na hatimaye kuishauri Wizara hiyo ipasavyo.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

2.1 WIZARA

2.1.1 Mapato yatokanayo na kodi

Mheshimiwa Naibu Spika, Hadi kufikia Machi 2014 serikali ilikuwa imekusanya mapato ya 69.2% badala ya 75% katika kipindi hicho ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 10.4. Kamati haikubaliani na sababu za kutokufikia malengo zinazotolewa na Wizara kwa kuwa ina amini kuwa TRA wanauwezo wa kukusanya mapato zaidi ya malengo yanayotolewa kila mwaka ambayo yako chini sana ikilinganishwa na wingi wa raslimali na ukuaji wa uchumi.

2.1.2 Mapato yasiyo ya kodi (Maduhuli)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi (Maduhuli) nao umekuwa wa kususua ambapo hadi kufikia Machi 2014 yalikuwa shilingi bilioni 326.3 sawa na 44.1% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 740.8. Vilevile sababu zinazotolewa kutokufikia malengo haziridhishi kwani hata michango ya 10% kutoka katika mashirika na Taasisi ya serikali hazikusanywi kikamilifu bila sababu za msingi.

2.1.3 Matumizi ya fedha za umma

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kupunguza matumizi mengineyo (OC) kwa kiasi cha shilingi bilioni 283 katika mwaka wa fedha 2013/2014. Ahadi hii ilitolewa kwa maandishi na Waziri wa fedha lakini hadi mwaka huu wa fedha unaelekea mwisho hakuna mchanganuo wowote uonao onyesha kupunguzwa kwa matumizi hayo, Bunge lilihakikishiwa kuwa kuhamishwa kwa fedha hizi na kupelekwa katika miradi ya maendeleo hakuta athiri utendaji wa serikali. Lakini cha kushangaza bajeti iliyowasirishwa matumizi mengineyo (OC) yameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inauliza kwa nini kwa kipindi kirefu serikali imeendelea kutetea matumizi ya aina hii kuwa ni muhimu lakini serikali haijawahi kuleta mchanganuo wa matumizi hayo (matrix) ili kuthibitisha umuhimu unaosisitizwa? Licha ya kamati na Bunge kuomba mchanganuo huo mara kwa mara.

2.1.4 Misamaha ya kodi

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa za Mapato kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2013 zimeonyesha kuwa misamaha ya kodi ilifikia kiasi cha Shilingi trilioni 1.51 ikiwa ni 3.1% ya pato la Taifa. Kiasi hiki ni kikubwa sana ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika mashariki, mfano Kenya (1%) na Uganda (0.4%).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa serikali imeahidi mara kwa mara kupunguza misamaha ya kodi na kwa kuwa tulikubaliana katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano (FYDP) kuwa misamaha ya kodi ishuke hadi kufikia 1% ya pato la taifa ifikapo mwaka 2015/2016. **Serikali iezeze katika mwaka huu wa fedha imepunguza misamaha ya kodi kwa kiasi gani (figure)?**

2.1.5 Deni la Taifa

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muda mfupi tumeshuhudia ongezeko kubwa la deni la Taifa kutoka Shilingi trilioni 21.2 (June, 2013) hadi shilingi trilioni 29.477 (Januari, 2014) hili ni ongezeko la shilingi trilioni 8.277 kwa kipindi cha miezi 7 tu, katika mchaganuo ufuatao: ikiwa trilioni 24.18 ni deni la serikali (Public debts), shilingi trilioni 3.75 ni deni la sekta binafsi na shilingi trilioni 1.15 ni deni la BOT kwa ajili ya kuondoa ukwasi kwenye uchumi.

Ongezeko hili la deni haliendi sambamba na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ujenzi wa miundombinu ya uchumi, hali inayopelekea kujengeka hofu kwa kuwa huenda deni hili limekuwa ni uchochoro wa ubadhilifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Inashangaza kuona kuwa deni linaongezeka kila mwaka licha ya serikali kulipa zaidi ya shilingi trilioni 3 kila mwaka wa fedha, pia kwa upande wa fedha zinazopokelewa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miundombinu ya uchumi zipo chini ya 50% fedha zilizoidhinishwa na bunge katika kila mwaka wa fedha, kwa upande makusanyo ya mapato ya ndani yakiripotiwa kukusanywa kwa wastani wa zaidi ya 90% ya malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Licha ya serikali kuendelea kusema kuwa deni hili ni himiliu lakini vipo viashiria (Financial Indicators) vinavyoonyesha kuelemewa kwa Taifa na mzigo mkubwa wa madeni, mfano mapato ya ndani yamezidiwa na matumizi ya kawaida hivyo kuipelekea serikali kukopa hata kwa ajili ya warsha, semina, safari, mafunzo, matengenezo ya magari, n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la taifa hivi sasa limefikia 47% ya pato la Taifa (Nominal value) na kwa kipimo cha bei ya sasa (Pv of debt-to-GDP) deni la taifa limefikia 24%. Huku deni la nje pekee likiwa ni 19.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Licha ya CAG kuahidi kwa muda mrefu kufanya ukaguzi maalumu wa Deni la Taifa ili kuweza kujua uhalali wa madeni haya lakini hadi sasa taarifa yake haijawasirishwa. Kamati inahoji ni lini taarifa hiyo itawasirishwa bungeni ili kuwawezesha wananchi kufahamu undani wa jambo hili?

2.1.6 Misaada na Mikopo

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa limekuwa tegemezi kibajeti kwa misaada na mikopo kwa zaidi ya 40% licha ya kuwa na rasilimali nyngi kama, gesi, Mafuta, ardhi kubwa yenye rutuba, madini ya kila aina, mito, misitu, bahari, maziwa, mbuga za wanyama, mifugo n.k ikilinganishwa na nchi jirani ambazo utegemezi wao wa bajeti ni kidogo, mfano Kenya 2% na Ethiopia 20.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kuwa Taifa linaendelea kuweka rehani mapato ya usoni kwa matumizi ambayo baadhi yanaweza kuahirishwa au kupunguzwa, mzigo mkubwa wa riba kwa matumizi ambayo tungeweza kuyagharamia kwa fedha zetu za ndani.

2.1.7 Upelekaji wa Fedha za maendeleo (Funds Disbursement) katika Wizara mpaka Machi na April, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, Wizara kama ya maendeleo ya mifugo na uvuvi licha ya umuhimu wake hadi April, 2014 ilikuwa imepokea 13.4% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa ushahidi huu ni dhahili kuwa wizara nyingi hadi mwisho wa mwaka wa fedha zitakuwa chini ya 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini serikali/hazina haipeleki fedha kama zilivyoidhinishwa na bunge? Na kwanini uhamisho wa fedha katika mafungu mbalimbali ni mkubwa kinyume cha sheria na taratibu?

3.0 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)

3.1 Transfer pricing

Mheshimiwa Naibu Spika, Bei za kugushi au kuhamisha mitaji (Transfer Pricing) zinatumwa na makampuni ya kimataifa yanayohusiana kwa madhumuni ya kupunguza kiwango cha kodi kwa nchi mbali mbali duniani kwa njia za ujanja. Mara nyingi makampuni makubwa ya kimataifa yanatoa bei za chini au za juu kwenye Ankara za biashara za nje (export under-invoicing and import over-invoicing).

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi sana katika eneo hili hususani katika makampuni ya kigeni yenye makampuni tanzu hapa nchini (Multinational companies-MNEs), mfano katika eneo la madini, simu, mabenki, gesi n.k. Aidha eneo hili limekuwa likihusishwa na rushwa kubwa kati ya makampuni na watumishi wa serikali, pia tafiti zinaonyesha kuwa utoroshaji wa fedha nje unachangiwa sana na Transfer pricing na Mis-pricing. Serikali itilie mkazo katika usimamizi na udhibiti wa TP ili kuhakikisha kuwa bei zinazotumika katika kampuni mama na kampuni tanzu ni bei halisi za soko (Arm's length price).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza serikali kwa kukamilisha kanuni na miongozo kusimamia TP (regulations and guidelines) jambo ambalo lilipiganiwa na kamati kwa muda mrefu. Kwa siku za nyuma tulikuwa tunatumia kanuni na miongozo za UN na OECD ambazo hazikuwa na nguvu ya kutosha kisheria kudhibiti TP. Licha ya kwamba sheria ya kodi (The Income Tax Act, 2004) section 33(1 & 2) iliweka kipengere cha TP lakini haikuwa na kanuni na miongozo ya kusimamia sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha kitengo cha kodi za kimataifa (International Taxation Unit-ITU) katika mamlaka ya mapato TRA, endapo kitengo hiki kitawezeshwa kikamilifu kitasaidia sana kupambana na TP na Mis-Pricing.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muda wa kushughulikia hoja na kesi za TP hivi sasa ni miaka 3 tu muda ambaao ni mfupi sana inapendekezwa muda huo uongezwe hadi miaka 6.

3.2 Mfumo wa Tiketi wa Kielektroniki (Electronic Ticketing System-ETS)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kwa muda mrefu serikali imekuwa haipati mapato ya kutosha kutoka katika sekta ya michezo hususani mpira wa miguu ulio chini ya shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (Tanzania Football Federation-TFF). Hii inatokana na mfumo dhaifu wa ukusanyaji fedha kipindi cha kuuza tiketi, mfano tiketi bandia kuendelea kutumika, kukosekana kwa uwazi katika mapato halisi, uwezo mdogo wa kusambaza tiketi nchi nzima, rushwa katika mageti, n.k. hali hii inaifanya TRA ishindwe kukusanya mapato halisi katika sekta hii na hata katika upande wa vilabu na wachezaji hawanufaiki ipasavyo, kwani fedha nyangi hubaki mifukoni mwa wajanja wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, TFF iliona changamoto hizi na kuamua kutangaza zabuni ya "electronic ticketing" mwaka 2012 na CRDB BANK ilishinda zabuni hiyo na tayari imekwisha tayarisha na kuweka mfumo huo (system design and hardware acquisition and installation) kwa gharama ya shilingi bilioni 3 toka mwaka 2013, na katika viwanja vya Kaitaba, Mkwakwani, Azam complex, Sokoine, Jamhuri, CCM kirumba and Sheikh Amri Abeid zimekamilika katika mwaka huu wa 2014 na sasa shughuli ya kusimika mfumo huo katika Uwanja wa Taifa wa Dar es salaam unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo huu mpya utaongeza mapato kwa serikali kwa kiwango kikubwa, TFF, vilabu na wachezaji watanufaika pia. Aidha tumeshuhudia mfumo huu ulipotumika katika maeneo kama TANAPA, KCMC, TRA (Holili, mtukula, sirari, horohoro, namanga, tunduma) ambapo Benki hii imeweka mfumo huu na umesaidia kuongeza mapato kwa 200% hadi 300%. Tazama jedwari hapo chini likionyesha jinsi mapato yalivyoongezeka katika taasisi ambazo tayari zinatumia mfumo wa ETS:

Idara/ Shirika mapato/malipo	Makusanyo kabla ya kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki kukusanya Baada ya ETS installation and use
------------------------------	--

Source: CRDB Bank, 2014

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA iweke sharti la lazima la kuitaka TFF kutumia mfumo wa "Electronic Ticketing" katika kuuza tiketi zake ikiwa ni jitihada za kuongeza mapato ya serikali.

3.3 Mashine za risiti (EFD)

Lalamiko kubwa la wafanyabiashara ni bei kubwa mashine hizo kwani kwa maelezo yao bei halali ni shilingi laki moja lakini mawakala ambao wamepewa kazi ya kuuza wanaziuza kwa shilingi laki 7 na kuzusha malalamiko ya wafanyabishara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja nyininge ya wafanyabiashara hao ni kuwa mashine hiyo inapoharibika haitengezwi sehemu yoyote isipokuwa kwa wakala anayeuzwa mashine na gharama ya matengenezo anatamka yeye mwenyewe na kwamba ukikataa kulipa bei ya matengenezo wanaithwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato TRA na analazimishwa kulipa faini ya milioni 2 kwa kosa la kukataa kutumia mashine hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wafanyabiashara hao wanahoji kuwa mashine hizo za EFD zina laini ya simu ndani ambayo inatoa ishara ya taarifa za biashara hivyo kwa nini mita za Tanesco zinakuwa ni mali ya Tanesco huku mita za maji nazo zikiwa ni mali ya Mamlaka za maji hivyo kwa nini mashine hizo za EFD zisimiliwi na TRA wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hata hivyo mita hizo za Tanesco zinapoharibika zinatengezwa na wao wenyewe hivyo kwa vipi mashine za EFD zikiharibika anatengeza wakala ambaye sio TRA mwenyewe liko jambo gani liliojificha hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha mashine hiyo ikizima ghafla na kama barua ya kuijulisha TRA hajafika mfanyabiashara analazimika kulipishwa faini ya shilingi milioni 2 bila kujali mfanyabiashara huyo mapato yake yakoje katika mtaji wake hivyo hujikuta akiingia kwenye maumivu makubwa.

Pia faini hizo zinazotozwa haziambatani na mapato ya mfanyabiashara husika hivyo kuchangia kuwafanya watumiaji hao waichukie Serikali na kuchukia pia kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunaamini kuwa mashine hizo zimeletwa kwa nia njema ya kuwezesha kuboresha ukusanyaji mapato na kuhifadhi taarifa za mfanyabiashara husika lakini kwanini mashine hiyo inaonekana imeletwa kumnufaisha msambazaji aliyepewa zabuni na maofisa wachache wa TRA walioshiriki kumleta na sio kuinufasha Serikali moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika awamu ya pili ya lengo la kuwaunganisha wafanyabiashara na mashine za EFD, walipa kodi 200,000 wasio kwenye mfumo wa VAT katika mwaka wa fedha 2013/2014, hadi kufikia machi 31 walikuwa ni walipa kodi 23,534 tu ndio walionganishwa katika mfumo wa EFD. Kati yao walipa kodi 17,916 ni wale walio katika mfumo wa VAT na 5,618 ni wale ambao hawapo katika mfumo wa VAT.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwa unganisha walipa kodi 200,000 ambao hawamo katika mfumo wa VAT na wenyewe mzunguko wa fedha wa chini ya shilingi milioni 40 umekuwa wa kusuasua na wenyewe lawama nydingi, kwani wamekuwa wakidai:

Moja, EFDs zinagharama kubwa za kuzinunua ambapo gharama yake ni shilingi 650,000 mpaka 700,000, tafiti zinaonyesha kuwa mzunguko wa biashara wenyewe thamani ya shilingi milioni 14-40 kwa mwaka mtaji wake hauzidi shilingi milioni tano, hivyo kumlazimisha mtu mwenye mzunguko mdogo aliipe kiasi hicho cha fedha kununua EFDs ni kumyumbisha kibiashara.

Pili, gharama za matengenezo ni kubwa mno na mashine hizi huharibika mara kwa mara, tafiti zilizofanywa na TCCIA zinaonyesha kuwa watumiaji wa mashine hizi hutumia siku 54 kwa mwaka kuzipeleka kwenye matengenezo, na sharti la matengezo ya mashine hizi hufanywa na

mawakala aliyeuza mashine hiyo ambao wamekuwa wakijipangia bei wanayotaka, na mbaya zaidi mawakala hawa hawapo kila sehemu hivyo wafanyabiashara hulazimika kusafiri umbali mrefu kuwafuata. Hali hii imekuwa ikiongeza gharama kubwa sana za kuendesha biashara ukizingatia kuwa mitaji yao ni midogo.

Tatu, Mashine za EFDs zinatumia lugha ya kiingereza ambayo wafanya biashara na watanzania wengi hawaifahamu, na hivyo kushidwa kuziendesha mashine na kusababisha matumizi yasiyo ya lazima na kuongeza gharama za biashara.

Nne, makosa katika kubonyeza hayarekebishiki kiurahisi na wakati mwengine husababisha malipo makubwa ambayo huchukua muda na mrongo mrefu kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini serikali isitoe mashine hizi bure kwa wafanya biashara hususani wale wa kipato cha chini ya milioni 40 kwani EFDs ni kifaa cha TRA katika kukusanya kodi? Mfano, baadhi ya makampuni ya huduma za simu yamekuwa hata yakitoa vifaa pamoja na mitaji kwa mawakala wao iweje serikali ishindwe kufanya hivyo kwa wafanya biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini EFDs ziuzwe na wazabuni badala ya TRA wenyewe? Kwa upande wa Tanesco mita za Luku huuzwa na shirika lenyewe na siyo wazabuni, pia matengenezo ya Luku hufanywa na shirika. Ikumbukwe kwamba EFDs ni chombo muhimu chenye taarifa muhimu ya mapato ya serikali iweje kiuze na kufanyiwa matengenezo na mtu binafsi yaani mzabuni? Kamati inashauri kuwa upatikanaji wa huduma za matengenezo zipatikane kila Wilaya na kwa umbali usiozidi kilomita 40 ili kuwarahisishia wafanya biashara kuendesha biashara kwa ufanisi zaidi.

3.4 Ukwepaji wa Kodi katika Bandari na changamoto ya ukusanyaji mapato

Mheshimiwa Naibu Spika, Baadhi ya wafanya biashara wanaotumia bandari ya nchini aidha kwa makusudi au kwa wakishirikiana na watumishi wa serikali kudanganya kwa kutokuonyesha thamani halisi ya bidhaa (under invoice), kuonyesha idadi ndogo ya bidhaa wanazoingiza nchini (Under declaration), pia hudanganya bidhaa zilizomo katika makontena kuwa ni zile zenye misamaha ya kodi kama vyandarua kumbe ni; aidha vitenge, nguo, khanga, na bidhaa za elektroniki n.k na hivyo kukwepa kulipa kodi. Hali ambayo imesababisha serikali kupoteza kiasi kikubwa cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usio na mashaka kuwa ongezeko la bidhaa za khanga na vitenge kutoka nje katika maduka mbalimbali nchini, nakukosekana kwa kumbukumbu kutoka mamlaka ya mapato (TRA) zinazoonyesha kulipiwa kwa bidhaa za aina hiyo ni uthibitisho unaojitosheleza kuonyesha ukwepaji mkubwa wa kodi katika bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na kuwa na ukanda mpana katika bahari ya hindi suala la bandari buba limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Katika ukanda wote wa pwani zipo bandari buba takribani 26 ambazo ndiyo kwanza mamlaka inafanya jitihada kudhibiti magendo hayo pia ikumbukwe kwamba licha ya kupoteza mapato mengi lakini njia hizi zimekuwa zikiingiza nchini vyakula vibovu, bidhaa zisizo na viwango, madawa ya kulevyta na hata silaha.

3.5 Kuongeza Ari ya Uhari kwa walipa kodi

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutambua na kujenga morali kwa walipa kodi nchini kila mwaka, naliomba Bunge lako kuweka azimio la kuwapongeza walipa kodi bora nchini. Aidha kamati inaomba na inatumia fursa hii kuwahimiza wananchi kuhusu umuhimu wa kodi na kulipa kwa hiar, kwani maendeleo ya taifa letu tutayaleta wenyewe.

4.0 Benki kuu, Benki na Taasisi za Fedha Nchini

4.1 Benki Kuu ya Tanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ya Tanzania imepewa mamlaka ya kutoa leseni kusimamia na kudhibiti mabenki na taasisi za fedha kupitia, sheria ya benki kuu ya mwaka 2006, sheria ya mabenki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, Sheria ya fedha za kigeni ya mwaka 1992 na kanuni, miongozo na sekula mbalimbali zilizotolewa kwa mujibu wa sheria hizi. Mtaji wa benki kuu ni shilingi bilioni 100, vilevile mtaji na “reserves” za benki kuu zilifika shilingi triliioni 1.12 katika mwaka wa fedha 2012/2013.

4.1.1 Dollarization

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika uchumi Dollarization ni matumizi ya fedha za kigeni kama vile dola ya kimarekani katika kuhifadhi akiba (Store of value), kupimia thamani (unit of account), na kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani (medium of exchange). Kwa mujibu wa sheria ya Foreign Exchange Act, 1992, fedha halali ya malipo ni Shilingi ya Tanzania, katika siku za karibuni Tanzania shilingi imekuwa ikitumika sambamba na Dolla ya kimarekani (unofficial dollarization) pia wananchi na makampuni ya ndani kupendelea kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za kigeni (Transaction dollarization). Amana ya fedha za kigeni katika mabenki imeongezeka na kufikia 26% ikiwa na maana kwamba katika kila shilingi 100 iliyopo katika mabenki nchini shilingi 26 ziko katika fedha za kigeni. Sheria ya mwaka 1992 ilichakachuliwa na tamko la serikali la mwaka 2008 ambalo liliruhusu matumizi holela ya dolla nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhara ya kutumia sarafu ya Tanzania sambamba na ile ya kigeni, kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za kigeni kunaiondolea sarafu ya Tanzania ushindani katika soko (International market Competitiveness), bureau de change za ndani kukosa soko na kupelekea serikali kukosa mapato, sarafu ya Tanzania kutokjulikana kimataifa kwa kuwa mgeni huja na sarafu yake na kuondoka na sarafu yake.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaitaka serikali ifute tamko lake la mwaka 2008 linaloruhusu matumizi holela ya fedha za kigeni (Dollarization) na kuitaka Benki kuu kusimamia sheria ya Foreign Exchange Act, 1992 kuwa sarafu ya Tanzania itatumika kwa malipo halali ya ndani na nukuu za bei zote zifanyike kwa shilingi ya Tanzania. Vilevile kufanya marekebisho ya sheria kwa kutoza kodi malipo yanayofanyika kwa fedha za kigeni kama nchi nyingine zinavyo fanya mfano Afrika Kusini, Peru, Ethiopia n.k.

4.1.2 Maduka ya kubadili Fedha (Bureaux de Change)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduka ya kubadili fedha za kigeni nchini yamefikia 233, ambapo 206 yalikuwa yanafanya biashara Tanzania bara na 27 Tanzania Zanzibar. Kamati imegundua kuwa maduka ya kubadili fedha hapa nchini yamekuwa hayasimamiwi kikamilifu na Benki Kuu, kwani ubadilishaji holela wa fedha umetawala nchini. Sheria inamtaka mtu yeyote anaetaka kubadili fedha kuwa na kitambulisho, ticket na shughuli anayofanya lakini hivi sasa tunashuhidia watu wanakwenda kubadili fedha bila vitambulisho na wala hakuna risiti zinazotolewa kwa huduma hiyo. Hii ni hatari kwa Taifa kwani inaweza kutumika kama uchochoro mkubwa wa kutorosha fedha nje ya nchi (Illicit Financial Outflows) na ukwepaji mkubwa wa mapato ya Serikali.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Benki Kuu kusimamia kikamilifu biashara ya maduka ya kubadiri fedha (Bureaux de change) na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaotenda makosa katika biashara hii sambamba na kuifanyia marekebisho sheria ya Fedha za kigeni (The Foreign Exchange Act, 1992).

4.1.3 Utoroshaji wa Fedha nje ya nchi (Illicit Financial flows)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa hivi karibuni na mtandao wa kimataifa wa Global Financial Integrity (GFI) umebaini kuwa Tanzania imepoteza zaidi ya dolla bilioni 1.87 za kimarekani sawa na shilingi trilioni 3.13 kila mwaka kutokana na mzunguko wa fedha haramu. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa baadhi ya wawekezaji wamekuwa wakitoa taarifa zisizo sahihi za kupanda au kushuka bei halisi ya bidhaa wanazonunua au kuuza (Mispricing-Over invoicing/under invoicing), mfano makampuni ya madini ambapo unakuta bei ya madini nchi za nje ni kubwa lakini wao wanataja bei ndogo hapa nchini, Makampuni ya mafuta yamekuwa yakinunua kwa bei ya chini lakini yakirudi hapa nchini yanataja bei kubwa kwa lengo la kukwepa kodi hali ambayo inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati baada ya kukutana na Benki kuu na Financial Intelligence Unit (FIU) kutaka kujua namna inavyo kabiliana, kuzuia na kurejesha fedha zilizo toroshwa lakini hapakuwa na taarifa zozote isipokuwa ndo kwanza tume imeundwa kuchunguza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inajua ni kazi ya kudumu ya FIU, kamati inajua ni kazi ya kudumu ya Benki kuu kusimamia, kudhibiti uhamishaji na utoroshaji wa fedha ndani na nje ya nchi. Na hivyo kamati inahoji tumefikia vipi hatua hii bila taasisi hizi muhimu kuchukua hatua stahiki? Kamati inahoji ni kwanini taarifa ya fedha za uswiss haijawasirishwa hadi leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kwamba taarifa ya Uswiss iwasirishwe mapema kabla ya Bunge hili kuisha ili kuwawezesha waheshimiwa wabunge na wananchi kujua ukweli wa jambo hili.

4.1.4 Escrow account

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inatambua hatua zilizochukuliwa na serikali za kumuagiza CAG na PCCB kufanya ukaguzi katika malipo haya kama ilivyoagizwa na Bunge. Kamati indiomba serikali ilete ripoti hiyo ya ukaguzi mapema kabla ya Bunge hili kuisha ili kuwesheha wananchi kuujua ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inasisitiza kuwa umuhimu wa uchunguzi kufanyika na taarifa kuleta bungeni haraka kwani jambo hili limevuta hisia nzito kwa watanzania na hamu ya kutaka kujua ukweli juu ya jambo hili.

4.2 Benki na taasisi za fedha

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya fedha nchini imekuwa ikitawaliwa zaidi na sekta ya benki, kwa takribani 75% ya raslimali zote. Kutoka 1992 mpaka April 2014, mabenki na taasisi za fedha zimeongezeka kutoka 5 mpaka 53, ikiwa ni mabenki 35 na taasisi za fedha 18 ambapo mabenki 23 toka nje ya nchi kama kampuni tanzu za mabenki mama. Ni mabenki 4 tu yaani NMB, CRDB bank, DCB commercial bank na maendeleo zimesajiriwa katika soko la hisa la Dar es salaam, huku benki za nje zote zikiwa hazijasajiriwa. Hadi Desemba 2013 zaidi ya matawi 622 ya mabenki

na taasisi za fedha yamefunguliwa nchi nzima. Hadi kufikia Desemba 2013 sekta ya kibenki ilikuwa na mtaji wa TZS 2.5 trilioni, rasilimali za TZS 20.2 trilioni, amana TZS 15.3 trilioni, mikopo ya shilingi trilioni 10.3, mikopo kwenye sekta binafsi ilifikia 21.9% ya pato la Taifa, ukwasi ulikuwa 36.5% na mikopo chechefu ilikuwa 6.5% ya mikopo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Benki zinazomilikiwa na serikali na zile za binafsi kama TPB, TIB, Twiga Bacorp na CRDB Benki ili kupokea taarifa za fursa na changamoto katika maendeleo ya sekta ya benki/fedha nchini.

4.2.1 Benki ya maendeleo ya Kilimo Tanzania (Tanzania Agricultural Development Bank- TADB)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashangazwa na serikali kuendelea kuimba wimbo ule ule wa kwamba uanzishwaji wa Benki hii umefikia hatua za mwisho lakini benki haianzi ikiwa ni miaka miwili sasa tangu tuelezwe taratibu zimekamilika. Kamati inauliza tatizo la kutokuanza kwa Benki hii ni nini? Kwa sababu kama kila kitu kimekamilika je ni nini hasa kinasubiriwa?

4.2.2 Benki ya Maendeleo (TIB Development Bank)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza maamuzi ya marekebisho ya TIB kuwa benki ya maendeleo ikiwa na lengo la kuziba pengo la kuwa na benki inayotoa mikopo ya kati na muda mrefu. TIB mpya itafanya kazi katika mfumo wa makampuni mawili yanayotegemeana, kampuni ya kwanza (TIB Ltd) itakuwa kampuni mama (parent company), mahususi kwa kazi za benki ya maendeleo (Development Financial Institution-DFI) na ya pili ni (TIB corporate Bank subsidiary Company) itakuwa kampuni tanzu ikifanya kazi za benki za biashara lakini ikiwa mahususi kwa ajili ya wateja wa DFI. Muundo huu unalengo la kuifanya benki kutoa huduma zote za kibenki kwa wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, TIB kama benki ya maendeleo inajukumu la kuunga mkono juhudhi za serikali kutekeleza sera na mikakati yake ya kitaifa ili kuongeza kasi ya maendeleo katika kukuza viwanda, madini, kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli zingine za kiuchumi na maendeleo na hivyo kuwawezesha wananchi kuzalisha kwa wingi na kuondokana na umasikini. Benki hii imekuwa ikifanya vizuri mfano, ukaguzi wa hesabu za benki mwaka 2013 unaonyesha kwamba benki imepata faida kabla ya kodi shilingi bilioni 15.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.5 mwaka 2012. Walaka wa mizania wa benki umekuwa na kufikia shilingi bilioni 405.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 337.8 mwaka 2012. Mikopo ya aina mbalimbali imetolewa na benki na kufikia shilingi bilioni 311.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 242.9 mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na ongezeko la mtaji na utoaji wa mikopo benki bado ina mtaji mdogo sana ikizingatiwa jukumu la benki kutoa mikopo ya maendeleo, mtaji mikubwa unaiwezesha benki kuwa na uthubutu wa kutoa mikopo mikubwa itakayokuwa na athari chanya (positive impacts) kwenye uchumi. Mitaji mikubwa pia inaiwezesha benki kutoa mikopo kwa riba nafuu kwani inaipa uwezo benki kukopa kirahisi na kwa gharama za chini kwenye vyanzo vingine vya fedha, kwa kuwa wakopeshaji wanakuwa na uhakika na uwezo wa benki. Pia kutiwezesha benki kutoa mikopo mikubwa ya pamoja na taasisi zingine za fedha duniani (Loan Syndication).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuzingatia umuhimu wa benki hii katika uharakishaji wa maendeleo, uchumi na ukuaji wa sekta binafsi tulikubaliana katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano (FYDP-2010/2011-2015/2016) benki hii ipewe shilingi bilioni 500 yaani kila mwaka wa fedha shilingi bilioni 100. Lakini cha kusikitisha hadi sasa ni shilingi bilioni 110 tu zimetolewa. Ikiwa umebaki mwaka mmoja tu wa mpango kukamilika.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa serikali imeshindwa kutimiza adhima yake ya kuiongezea benki hii mtaji kama ilivyokubalika katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano hivyo Serikali ikubali ombi la TIB kuiruhusu kukopa shilingi bilioni 300 toka katika mifuko ya jamii ya PPF na NSSF na kwamba serikali ikubali kutenga fedha shilingi bilioni 30 kila mwaka, kulipa riba ya mkopo huo kwa mfululizo kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015.

4.2.3 BENKI YA POSTA TANZANIA (TPB)

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki hii imekuwa ikifanya vizuri na mtaji wake umekuwa ukikua, mfano kwa mujibu wa ukaguzi ukuaji wa faida kabla ya kodi mwaka 2007 ilikuwa shilingi bilioni 0.44 na kukua kufikia shilingi bilioni 6.9 mwaka 2013. Changamoto kubwa ya benki hii ni mtaji mdogo ikilinganishwa na ukuaji wa benki. Ili benki hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi inahitaji mtaji wa shilingi bilioni 7.5.

Maoni na Ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri serikali kuipatia benki ya TPB mtaji wa shilingi bilioni 7.5 kama walivyoomba ambapo kamati imejiridhisha na uwezo mzuri wa kiutendaji ambayo faida inaonekana waziwazi.

4.2.4 TWIGA BANCORP LIMITED

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki hii haifanyi vizuri sana, thamani ya amana imepungua kutoka shilingi bilioni 59.1 na kufikia shilingi bilioni 47.8 Desemba 31, 2013 ikiwa ni upungufu wa 19%. Taasisi ilipata hasara ya shilingi bilioni 9.8 kwa mwaka 2012 na shilingi bilioni 1.9 mwaka 2013. Hasara hii imechangiwa kwa kiwango kikubwa na wizi wa fedha taslimu shilingi bilioni 3.3 uliofanywa na baadhi ya watumishi wa benki makao makuu wakishirikiana na wafanya kazi wa benki tawi la Mlimani city na wateja. Licha ya kamati kuomba kuletewa taarifa ya hatua stahiki zilizochukuliwa na uongozi wa benki imekuwa ikiletewa taarifa nusunusu na zisizo kamilika na kipelekeea mashaka makubwa kuwa uongozi umekuwa hauna nia ya dhati ya kurejesha fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inauliza ni kwanini wizi ulioanza kufanyika mwaka 2007 uje kugundulika mwaka 2012 wakati ukaguzi umekuwa ukifanyika kila mwaka?

Kwanini hadi sasa kesi iliyopo mahakamani ni ya shilingi milioni 704 tu? Kamati haikubaliani kuwa eti wizi wa shilingi bilioni 2.596 bado unafanyiwa uchunguzi chini ya DCI, ni uchunguzi gani unaofanyiwa zaidi ya taarifa ya ukaguzi iliyobaini mpango mzima wa jinsi fedha hizo zilivyo chukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeamua kuunda kamati ndogo kufuatilia hatua mahususi zinazochukuliwa kuhusiana na wizi huu.

4.2.5 CHANGAMOTO ZINGINE ZINAZOIKABILI SEKTA YA BENKI/FEDHA NCHINI.

i. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mabadiliko ya mara kwa mara ya ubadilishaji fedha (exchange rates), mfumuko wa bei (inflation rates) na viwango vya riba (interest rates) unaathiri sana kuendesha mabenki nchini.

- ii. Mheshimiwa Naibu Spika**, Kiwango kikubwa cha lazima cha sehemu ya amana (Statutory minimum reserve-SMR) za sekta binafsi (private sector deposits) 10% na 40% kwa amana za serikali (Government deposits) ambacho ni kiasi kinachohifadhiwa na Benki Kuu ikiwa ni amana isiyo na faida yoyote wakati mabenki hulipia riba kwa kutunza fedha hizo. Kiwango hiki cha SMR ni kikubwa na kwamba utaratibu huu hauzingatii uwezo wa benki na hivyo unaathiri uwezo wa utoaji mikopo ya bei nafuu na hivyo huchangia mabenki kutoza riba kubwa.
- iii. Mheshimiwa Naibu Spika**, Benki kuu kuweka kiwango kikubwa sana cha riba inayotozwa kwa mabenki na serikali zinapokopa kutoka Benki Kuu (Treasury bill rate). Benki kuu imepandisha kiwango cha riba kutoka 7.58% hadi 12.58%. Kiwango hichi cha riba cha takribani 13% kimekuwa ni kichocheo kikubwa cha mabenki kutoza riba kubwa na kumesababisha wananchi kushindwa kukopa, kurejesha mikopo yao pia hata kufirisika kwa kushindwa kurejesha riba kubwa.
- iv. Mheshimiwa Naibu Spika**, Njia ii na iii zimekuwa zikitumiwa na Benki Kuu kama njia ya kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi lakini zina madhara makubwa sana katika uchumi wa nchi.
- v. Mheshimiwa Naibu Spika**, Kukosekana kwa sovereign rating ambayo ingesaidia mabenki na taasisi za fedha kukopa fedha kutoka katika soko la kimataifa (International market) kwa riba nafuu. Kukosekana kwa utaratibu huu ambapo serikali imekuwa ikisema iko kwenvye mchakato kwa muda wa zaidi ya miaka 10 sasa na hivyo huwa lazimu kulipa kiwango kikubwa cha kinga ya hasara (High risk premium).
- vi. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali kushindwa kulipa dhamana zake katika mabenki (Bank guarantees), vilevile serikali kuchelewesha malipo ya wazabuni na wakandarasi ambao ni wateja wa mabenki, hali hii huzizoofisha benki katika utoaji mikopo kutokana na ongezeko la mikopo isiyolipwa (Non Performing Loan-NPL), riba kuongezeka kwa wakopaji na hivyo kipelekea kufirisika. Hivi sasa deni la wakadarasi kwa serikali limefikia shilingi trilioni 1.3 kwa serikali kuu pekee.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

- Mheshimiwa Naibu Spika**, Kamati inashauri kwamba Serikali kuptitia benki kuu ipunguze kiwango cha riba kwa mabenki kutoka 12.58% hadi 7.58%, mpango wa sovereign rating ukamilike haraka, kiwango cha statutory minimum reserve kipungue kutoka 10% hadi 5% kwa sekta binafsi na kutoka 40% hadi 20% kwa amana za serikali kwa kufanya hivyo kutasaidia kuongeza uwezo wa mabenki kukopesha na kupunguza viwango vya riba vinavyotolewa na mabenki.
- Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipe dhamana zake (Government guarantees) na madeni ya wazabuni na wakandarasi ambayo yamefikia shilingi trilioni 1.3 kwa upande wa serikali kuu pia kuzitaka serikali za mitaa nazo kulipa madeni yote wanayodaiwa.

5.0 MSAJILI WA HAZINA

Mheshimiwa Naibu Spika, Msajili wa hazina anasimamia jumla ya mashirika 224 ambapo mashirika 215 ni ya uwekezaji wa ndani (*Domestic Investment*) na 9 ni kutokana na uwekezaji wa nje (*Foreign Investment*) ikiwa mashirika 70 yanamilikiwa na Serikali 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji wakuu wa mashirika (CEOs) wanao kaimu katika mashirika na taasisi za umma kwa muda mrefu wako 26 sasa na wengine wana zaidi ya miaka 5 katika nafasi hizo za ukaimu.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaagiza kwamba ifikapo Desemba 31, 2014 nafasi zote zinazokaimiwa ziwe zimejazwa.

6.0 Taasisi za mafunzo

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati ilikutana na taasisi za mafunzo zilizo chini ya wizara kama Chuo cha mipango na maendeleo vijiji (IDRP), kituo cha utaalam wa uhasibu (NBAA), Chuo cha uhasibu Arusha-(IAA), chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) chuo cha usimamizi wa fedha (IFM) na Taasisi ya uhasibu Tanzania (TIA).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kamati haikuridhishwa na ongezeko kubwa la gherama za ujenzi wa maktaba ya kisasa uliongezeka kutoka shilingi 2,898,519,144/= hadi shilingi 6,879,362,004 na kwamba sababu zilizotolewa juu ya ongezeko hilo haziridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutohana na sintofahamu hiyo kamati imeiagiza mamlaka ya usimamizi wa manunu (PPRA) kufanya ukaguzi wa mradi huu ili kujiridhisha kama ongezeko hilo ni halali na kama sheria na taratibu za ununu wa umma zilifuatwa.

7.0 Shirika Hodhi la mali za mashirika ya umma (CHC)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio namba 5/2011, azimio la Bunge la kuridhia muda wa shirika hodhi la mali za mashirika ya umma yaani "The consolidated holding corporation" Bunge liliazimia kuwa nanukuu "kwa hiyo basi, kwa madhumuni haya maalum, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ,katika mukutano wa nne kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha sheria ya Benki linaazimia kuongeza muda wa uhai wa shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, 2014 ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika kukamilisha taratibu za kuitendaji na kisheria. Ndani ya Muda huo Serikali itafanya tathmini ya kazi za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (Consolidated Holding Corporation) ili kubaini kama lionezewa tena muda au kufanyiwa uamuzi mwengine" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutekeleza Azimio hilo, wizara kwa kuzingatia sheria ya ununu wa umma ilitangaza kwenye vyombo vyaya habari kumpata mshauri mwelekezi wa kufanya tathmini ya utendaji wa CHC mwezi septemba, 2013. Chuo cha elimu ya Biashara (CBE) kimepata zabuni hiyo baada ya taratibu zote kukamilika. CBE imepewa muda wa hadi tarehe 30, Mei 2014 kuwasirisha taarifa/ripoti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashangazwa na wizara kushindwa kutekeleza Azimio la Bunge kwa miaka 3 na kutangaza kumpata mzabuni katika mwezi wa mei 2014 ikiwa ni mwezi mmoja kabla ya shirika hili kufikia ukomo. Hata hivyo kamati iliagiza wizara kuleta taarifa ya tathmini mbele ya kamati tarehe 2 Juni 2014 lakini hadi nasoma taarifa hii agizo la kamati halijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilialifiwa kuwa shughuli za CHC zitarithiwa na ofisi ya Msajiri wa Hazina ambayo hajaandalika kuweza kukabiliana na majukumu hayo ambayo yamesalia; **Moja** ufuatilaji wa madeni ya shilingi bilioni 116.88; **pili** usimamizi wa kesi 432 zenye madai ya takribani shilingi bilioni 656; **tatu** ufilisi wa mashirika 13; **nne**, ubinafsishaji wa vitengo/mashirika 32; **tano**, ufuatilaji na tathmini ya mashirika 156 yaliyobinafsishwa na zoezi hili endelevu.

Maoni na Ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa majukumu yaliyosalia ni mazito na kwa kuwa serikali imeshindwa kufanya tathmini kwa wakati kama azimio la Bunge lilivyotaka na kwamba ofisi ya msajili wa Hazina hajaandalika kikamilifu kushika majukumu haya hivyo kamati inashauri kuwa CHC iongezewe muda miaka 3 mingine.

8.0 MANUNUZI YA UMMA

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imekuwa ikitoa taarifa kuhusu manunuzi ya umma, aidha imekuwa ikibainisha jinsi wakaguliwa (Procurement Entities-PE) zinavyoikiuka manunuzi kwa makusudi, mfano kulipa zaidi ya mkataba, kulipa kazi ambayo haikufanyika, kulipa kwa bei kubwa zaidi ya bei iliyoko sokoni na miradi kutokuwa na thamani halisi (value for money), mfano mamlaka katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi oktoba 2013 ilifanya kaguzi katika PEs 120 zikiwemo wizara na idara zinazojitegemea 32, mashirika ya umma 46 na serikali za mitaa 42. Kaguzi zililhusisha mikataba 5,867 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.99. Ripoti ya ukaguzi inaonyesha wastani wa uzingatiwaji wa sheria ya ununuzi ulikuwa ni 64% tu. Endapo eneo hili litasimamiwa kikamilifu ili kila shilingi ifanye kazi yake stahili tutaokoa fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Licha ya unyeti wa suala zima la manunuzi serikali imekuwa haitili maanani katika kuiwezesha PPRA kutekeleza jukumu lake la msingi la kushauri na kufanya ukaguzi katika manunuzi. Mfano katika mwaka wa fedha 2012/2013 mamlaka iliomba kiasi cha shilingi bilioni 11.5 lakini iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.3 sawa na 11.3% tu ya mahitaji. Mamlaka hiyo katika mwaka wa fedha 2012/2013 iliweza kukagua wakaguliwa 120 kati ya wakaguliwa 454 ambao walipaswa kukaguliwa hii 30% tu. Vilevile mamlaka hii inawatumishi 50 tu wakati mahitaji ni 142.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya mwaka ya utendaji ya PPRA (the annual Performance Evaluation report), licha ya ripoti hii kubeba mambo muhimu kuhusu manunuzi ya umma lakini huwa haipewi nafasi ya kuwasirishwa na kujadiriwa bungeni kama ilivyo taarifa ya CAG. Taarifa zilizopo kwenye ripoti hiyo ni nyenzo muhimu ambayo kama itatumiwa vizuri itasaidia taasisi nunuzi kuboresha majukumu yao ya ununuzi. Aidha, inaweza kutumiwa kama nyenzo muhimu katika ngazi za maamuzi kwa lengo la kuboresha ununuzi wa umma nchini kwa kuhakikisha suala la usimamizi na udhibiti wa ununuzi linapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za ukaguzi zinazoibuliwa na PPRA hutegemea pia uchunguzi wa jeshi la Polisi na PCCB, kamati imebaini kuwa hakuna mawasiriano thabiti kati ya taasisi hizo. Na kwamba PPRA anapopeleka hoja kwa PCCB na Jeshi la polisi nyingi hupotelea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sheria ya manunuzi umma na sheria ya ubia (Public Procurement Act, 2011 and Public Partnership Act, 2010) yaliyofanywa na Bunge kupitia Finance Bill 2013 kuwezesha "Unsolicited PPP Proposals" kutohusika na utaratibu wa ushindani inabidi utazamwe upya kwa kuwa ni vigumu kujua "value for money" na pia masharti na vigezo, na hivyo inaweza kutumika vibaya (Area of abuse) na kuwa uchochoro wa ujisadi nchini. Changamoto kubwa ya mfumo huu ni jinsi ya kuoanisha/kuwianisha matakwa ya uwazi kutotoa

fursa za udanganyifu/ rushwa katika mchakato wa ununuzi (Transparency of the procurement process) najitihada za aliye buni mradi (unsolicited PPP proposals).

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati wa mikataba mikubwa ya uwekezaji wa raslimali za taifa, mfano Ardhi, Madini, mafuta, gesi, misitu n.k. kuridhiwa na Bunge, Mikataba ya kati ya manunu zi iridhiwe na kamati za kisekta na huku manunu zi mengine ya kawaida yanaweza kuishia katika ngazi ya PEs.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya manunu zi ya mwaka 2004 iliwaondoa waheshimiwa madiwani katika uidhinishaji wa zabuni kitendo kilichopelekea miradi mingi kutoku tekelezwa kikamilifu. Sheria mpya PPA, Act 2011 imewarejesha waheshimiwa madiwani kuridhia zabuni baada ya mchakato wa zabuni kukamilika.

9.0 MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII (Pension funds)

Kamati ilikutana na mashirika ya hifadhi za jamii kama PPF, LAPF, PSPF, GEPF na NSSF ili kujadili fursa na changamoto katika uwekezaji na uendelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Mashirika haya yamekuwa yakiikopesha serikali ili iweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ujenzi wa chuo kikuu cha Dodoma na ukumbi wa Bunge, lakini serikali imekuwa hailipu madeni hayo na kufanya mashirika kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Hadi kufikia Machi 2014 madeni yaliyoiva yamefikia ni shilingi bilioni 608.36 kwa mujibu wa mikataba ya mikopo iliyopo katika mchangano ufuata; PPF shilingi bilioni 11.01, LAPF shilingi bilioni 62.15, PSPF shilingi bilioni 182 na NSSF shilingi bilioni 353.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali katika ripoti yake ya Mashirika ya Umma ya 2012/2013 amebainisha kuhusu dhima ya watumishi wa Serikali kwa Mfuko wa PSPF na uharaka unaohitajika katika kulipwa kwa dhima hiyo. Taarifa hiyo imeonesha kuwa Mfuko wa PSPF una upungufu (actuarial deficit) ya shilingi trilioni 6.487 kwa mwaka unoishia tarehe 30 Juni 2010. Dhima hiyo inatokana na Serikali kutolipia michango ya nyuma ya watumishi kabla ya mwaka 1999. Kutokulipwa kwa dhima hiyo kwa wakati ni changamoto kubwa inayoikabili Mfuko wa PSPF. Hali hii inasababisha ongezeko la dhima na kuathiri uwezo wa Mfuko wa kulipa mafao jambo ambalo linaufanya Mfuko usiwe endelevu.

Ushauri na maoni ya Kamati

i. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali itenye fedha na iweke kipaumbele kulipa madeni yote ya mifuko ya jamii (Pension Funds) yaliyofikia shilingi bilioni 608.36 katika mwaka wa fedha 2014/2015. Na kama serikali itashindwa kutenga fedha hizi katika mwaka ujao wa fedha Deni hili liingizwe kwenye deni la Taifa na serikali itoe hati fungani za muda mrefu na mfupi kulipa deni hilo, vile vile serikali ilipe kwa wakati madeni yanayoiva hivi sasa.

ii. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa upande wa mfuko wa PSPF serikali iongeze kiwango cha michango kwa watumishi wanachama wa PSPF kutoka 15% hadi 20% ya mshahara wa mwanachama (hiki ni kile kiwango kinacholipwa na Serikali hivyo Mwanachama hataathirika na ongezeko la michango hiyo), vilevile serikali iendelee kulipa kiasi cha shilingi bilioni 50 kila mwaka wa fedha kunusuru mfuko huu.

11.0 MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jukumu kubwa la CMSA ni kubuni na kutekeleza hatua za makusudi ambazo zitawezesha kuanzisha na kuendeleza masoko ya mitaji endelevu, yenye ufanisi, uwazi

na yenye kutoa haki sawa kwa washiriki wote. Mamlaka hii inasimamia masoko ya mitaji na dhamana ya DSE na UTT.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwahishe mchakato wa kutunga Sheria mpya ya masoko ya mitaji na masoko ya bidhaa (capital markets and commodities Act) ili kuweza kuondoa mapungufu ya sheria ya sasa na kuendana na mpango wa Tanzania kuanzisha soko la bidhaa.

10.1 Soko la hisa la Dar es Salaam (DSE)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hadi kufikia April 2014 ni makampuni 18 tu yalikuwa yamesajiliwa katika soko la hisa la Dar es salaam kati ya hayo 12 ni makampuni ya ndani na 6 ni makampuni ya nje. Makampuni mengi yenye mchango mkubwa katika uchumi hayajasajiriwa katika soko la hisa la Dar es salaam, mfano makampuni ya madini, gesi, mabenki, simu, n.k. Hii ni tofauti na nchi zingine ambazo sheria zao zinalazimisha makampuni yote ya aina hii kusajiriwa katika soko la hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivyo namba ya wawekezaji katika soko la hisa bado ni ndogo sana kulinganisha na idadi ya watanzania, ikiwa inachangiwa na idadi ndogo ya makampuni iliyopo sokoni na uchache wa hisa za makampuni yaliyopo sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokusajiriwa kwa makampuni mengi inawanyima fursa watanzania kushiriki katika uchumi wa nchi yao na Serikali inaendelea kukosa mapato katika mauzo ya hisa.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba DSE ipewe kipaumbele katika mipango ya serikali hasa katika eneo la ukusanyaji raslimali (Resource mobilization) na pia kufikia hitimisho la utekelezaji wa sheria ya mawasiriano (Electronic and Postal Communication Act-EPOCA, 2010) na ya madini ya mwaka 2010, DSE itakuwa na uwezo wa kutimiza majukumu yake katika kukuza uchumi wan chi na hivyo kutimiza malengo yaliyooainishwa katika kuanzishwa kwake.

10.2 Dhamana ya uwekezaji Tanzania (UTT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza kitendo cha kuifanya marekebisho ya kumuundo (Restructuring) dhamana ya uwekezaji Tanzania (Unit Trust Of Tanzania), kwa lengo la kuwafikia na kuwawezesha watanzania wengi zaidi hususani wenyе kipato cha kati na chini. Makampuni hayo ni UTT-Microfinance Plc (UTT-MFI)-Taasisi inayotoa huduma za kifedha na mikopo kw wajasiliamali wa kati na chini na kuwa suluhisho la mtaji kwa wahitaji; UTT-Asset Management and Investor service plc (UTT-AMIS)-ikiwa na dhaman ya kusimamia raslimali na kutoa huduma kwa wawekezaji katika mifuko ya dhamana ya uwekezaji na UTT-Projects management and infrastructure Development Plc (UTT-PID)-Ikijishughulikia usimamizi wa mradi na maendeleo ya miundo mbinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto; katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake UTT MFI; imeshuhudia changamoto kubwa katika sekta ya huduma za kifedha na mikopo (Microfinance industry) baada ya elimu/ufahamu mdogo wa huduma za kifedha; ni kutokuwa na mfumo rasmi wa usimamizi wa sekta hii (Microfinance regulatory regime). Ambapo, kwa wakati huu

hakuna chombo mahususi kinachosimamia na kurasimisha makampuni na watoa huduma katika sekta ya Microfinance.

Maoni na ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba mfumo rasmi wa usimamizi wa sekta hii (Microfinance regulatory regime) ianzishwe ili kuweza kusimamia na kurasimisha makampuni na watoa huduma katika sekta ya microfinance.

11.0 SHERIA ZINAZOSIMAMIA FEDHA ZA UMMA

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna haja kubwa ya kuzifanya marekebisho sheria zinazosimamia fedha na raslimali za umma ili ziendane na hali halisi ilivyo sasa ambapo upotevu wa fedha za umma unazidi kuongezeka. Sheria za fedha zilizopo sasa hazina nguvu ya kutosha kuweza **kulinda, kusimamia na kudhibiti matumizi (utilization) ya raslimali za taifa**.

I. Economical and organized crime control Act, 1984

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lilifanya marekebisho Katika sheria ya uhujumu uchumi, Toleo la sheria "Act supplement No.3 la tarehe 20 march 2009; The written laws (Miscellaneous Amendments Act) part x" kifungu cha 39 kinatamka: **the First Schedule to the Principal Act is amended by deleting paragraph 1 and 2** Maana yake ni kwamba makosa ya rushwa yaliyomo kwenye jedwali la kwanza ya uhujumu Uchumi (Economic and Organized Crimes Control Act, Cap 200) yameondolewa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya ya sheria yaangaliwe upya kwa kuwa kuyaondoa makosa ya rushwa katika sheria ya uhujumu uchumi ni kuimarisha rushwa. Waasisi wa Taifa letu walipotengeneza sheria ya kuzuia rushwa mwaka 1971 waliona umuhimu wa kuyaweka makosa ya rushwa kuwa ni makosa ya uhujumu uchumi ili kuweza kutoa adhabu kali kwa wanaopatikana na hatia ya kujihusisha na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivyo basi kuyaondoa makosa ya rushwa kutoka kwenye makosa ya uhujumu uchumi ni kupunguza kasi ya kupambana na rushwa, suala linalopelekea sasa hivi Mahakama kutoa adhabu ndogo au kutoa adhabu ya kulipa faini kwa wanaopatikana na makosa ya rushwa. Adhabu ya juu kabisa ya makosa ya rushwa ni faini isiyozidi kiasi cha Tshs. 15,000,000/=. Haiingii akilini mtu aliyejipatia mabilioni kwa njia ya rushwa aishie kulipishwa faini ya Tshs. 15,000,000/=.

II. Public Finance Act 2001

Kifungu cha sheria cha 44 (1-2) cha sheria ya fedha za umma, 2001, kimeainisha adhabu ya makosa kwa mtu atakaye kiuka taratibu za fedha za umma atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya kulipa fedha, ambazo kimsingi siyo zaidi ya shillingi laki tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja. Adhabu hii ni dhaifu na imepitwa na wakati katika kuweza kudhibiti wizi na ubadhilifu wa fedha za umma na badala yake inahamasisha wizi na ufujaji.

III. Public Procurement Act, 2011

Sheria hii mpya inafuta sheria ya zamani ya PPA, 2004 imezingatia umuhimu wa waheshimiwa madiwani kuridhia mikataba inayoingiwa na hal mashauri na inatoa adhabu kali kwa wanaovunja sheria hii, Marekebisho ya sheria ya manunuzi (Public Procurement Act, 2011)

katika kifungu cha 31(4) na 60 (4) vinavyowawezesha madiwani kushiriki katika mchakato wa manunuzi na kifungu cha 104(1) kinachotoa adhabu kali ya kufidia hasara iliyosababishwa au kufirisiwa ili kufidia fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini sheria hii iko kimya kwa mikataba inayoingiwa na serikali kuu. Hivi sasa zabuni, mikataba ya miradi ya maendeleo na uwekezaji katika raslimali za umma yaani ardhi, misitu, gesi, mafuta na madini inaingiwa na watendaji wa serikali bila Bunge kuridhia hii ni hatari kubwa kwa taifa na tutaendelea kulalamika kutokana na mikataba isiyo na tija kwa taifa.

Maoni na ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati italeta marekebisho ya sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 ili mikataba yote iridhiwe na kamati za kisekta za Bunge na mikataba ya uwekezaji wa raslimali za umma yaani ardhi, misitu, mafuta, gesi na madini iridhiwe na Bunge zima.

IV. The public Audit Act, 2008

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna ucheleweshaji usiokuwa na msingi kwa wabadhilifu wa fedha za umma wanaogundiwa na CAG hata kwa makosa ambayo yako wazi, ripoti ya CAG haitumiki kama ushahidi mahakamani moja kwa moja mpaka uchunguzi zaidi wa DCI na PCCB.

Maoni na Ushauri wa kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya ukaguzi wa fedha za umma 2008, na Finace Act No.15,2010, zifanyiwe marekebisho kifungu cha 27 (2) ili kuwezesha mtuhumiwa kufikishwa mahakamani kwa ushahidi wa taarifa ya CAG kwa makosa ambayo hayahitaji uchunguzi zaidi wa Polisi na TAKUKURU.

12.0 UCHUMI WA MADINI, GESI NA MAFUTA

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ziara nchini Norway kwa nia ya kujifunza namna taifa linaweza kunufaika na uchumi wa gesi na kuongeza mapato ya serikali. Kwa ujumla Norway inafanya vizuri sana. Kamati iliamua kupitia baadhi ya mikataba ya Gesi hapa nchini ili kuweza kubaini kama mikataba hiyo inawanufaisha watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri serikali kuptitia upya mikataba yake ili kuona kama kweli maslahi ya taifa yamezingatiwa. Kwa mfano, mkataba wa nyongeza (Addendum) kwa mkataba wa uzalishaji wa kugawana uzalishai (PSA) kati ya serikali ya Tanzania (TPDC-GoT) na kampuni ya Statoil Tanzania AS (Norway) (Addendum to existing production sharing agreement between GoT and TPDC and Statoil Tanzania AS and Exxonmobil Exploration and Production Tanzania Limited Block 2).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mnamo Aprili 18, 2007 serikali ya Tanzania ikiwakilishwa na Wizara ya nishati na madini, Shirika la Maendeleo ya Mafuta (TPDC) na kampuni ya Statoil Tanzania AS ya nchini Norway, ziliingia mkataba wa kugawana uzalishaji (PSA) kwa ajili ya kutafuta na kuendeleza mafuta (crude oil) katika kitalu Namba 2. Hapo baadaye ilipoonekana kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa gesi asilia katika kitalu hicho, Serikali iliamua kuingia mkataba wa Nyongeza (Addendum) ili kujumuisha utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia katika mkataba wa kwanza wa tarehe 18 April 2007. Kampuni ya ExxonMobil Exploration and production Tanzania Ltd nayoiliingia katika mkataba wa nyongeza kama mbia wa 35% wa kampuni ya statoil.

Kamati iliona yafutayo katika mkataba huo:

i. Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa watanzania katika uchumi wa gesi (local content), katika utangulizi uliopo ukurasa wa 3 na ibara ya 8.1(n) iliyopo ukurasa wa 11 katika mkataba wa nyongeza imewekwa wazi kwamba "any gas commercialization project shall be structured either through an integrated or segmented gas value chain at the contractor's absolute discretion. Prior to making its decision the contractor shall consult with TPDC". Hii ina maana kwamba sera ya ushirikishwaji wa watanzania (Local content policy) haitakuwa na nguvu ye yote kisheria kwa sababu tayari mkataba umeshaingiwa ambao unasisitiza kuwa kampuni za nje (Statoil na Exxonmobil) zitakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusiana na minyororo ya thamani na ugavi (value and supply chains).

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali ni kwamba je sera yetu ya ushirikishwaji wa wazawa ambayo ipo katika mchakato wa kutayarishwa na wizara ya nishati na madini itakuwa na nguvu za kisheria juu ya vipengele vya mikataba ambayo imeshaingiwa huko nyuma?

ii. Mheshimiwa Naibu Spika, Mgao wa gesi ambao Tanzania itaupata kupitia TPDC, kanuni iliyowekwa katika mkataba wa nyongeza kwa ajili ya kufikia mgawanyo wa gesi zinazostahili kupata kampuni za nje na TPDC ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya gesi kuchimbwa zinafanyika hesabu kutambua kiwango cha gesi kilichopatikana, ukiondoa iliviyotumika katika uzalishaji .Hii inaitwa Adjusted gas Quantity, ikiwa ni kwa mujibu wa ibara ya 11.1 ya mkataba wa nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Adjusted gas quantity ikishajulikana kampuni za kigeni zinakuwa na haki ya kuchukua gesi kiasi kinacholingana na gharama wanazostahili kurudishiwa kimkataba (recoverable contract expenses). Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 11.1 (a),(b) na (C) iliyopo katika ukurasa za 11 na 12 katika mkataba wa nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Recoverable contract expenses zimeanzishwa katika ibara ya Annex D (f) iliyopo ukurasa wa 19 kuwa ni gharama za uendeshaji (operating expenses), gharama za utafutaji (exploration expenses) na gharama za uendeshaji (development expenses).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa ibara ya 11.1 (a) iliyopo ukurasa wa 11 katika mkataba wa nyongeza, kampuni za nje zimeruhusiwa kutumia hadi 70% ya gesi iliyozalishwa ili kujilipa gharama zilizotumika kimkataba. Hii ina maana kwamba hadi hapo watakapomiliza kujilipa kila kitu, gesi itakayobaki kwa ajili ya kugawana (profit gas) ni 30% ya gesi yote iliyozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho, gesi iliyobaki kwa ajili ya kugawana (profit gas) inagawanywa kati ya kampuni za kigeni na TPDC kwa kanuni ifuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika gesi yote inayochimbwa makampuni ya kigeni yanaanza kwa kuchukua 70% na kubakisha 30%. Katika hiyo 30% iliyobaki, TPDC na makampuni ya kigeni wanakaa na kugawana uwiano kama ulivyoainishwa kwenye jedwari hapo juu, ambapo TPDC itaanza kwa kugawiwa 30% na kampuni ya kigeni kwa kuchukua 70%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivyo basi kihalisia TPDC itakuwa inapata mgao 30% ambayo ni sawa na 10% ya gesi yote inayozalishwa, wakati makampuni ya kigeni yanapata 70% ya 70% ambayo ni sawa na 90% ya gesi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swalii la msingi la kuhoji ni kwamba zile ahadi za kwamba watanzania tutapata 70% au 65% ya gesi yote inayozalishwa ziko wapi?

iii. Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato ya Kampuni za nje, Kwa mujibu wa ibara ya 11.1 (h) iliyopo ukurasa wa 13 mkataba wa nyongeza, kampuni za nje zitaruhusiwa kuweka nje ya nchi mapato yote ambayo wanapata kwa kuuza gesi yetu. Kwa utaratibu huu je tutakuwa na ubavu wa kuwadhibiti pale tutakapoona kuwa wamekiuka makubaliano yetu? Mfano kama wataongeza gharama ama kutoa takwimu za uongo kuhusu uzalishaji. Kamati inaona kuwa ingekuwa jambo la busara kama asilimia Fulani ya mapato yange bakizwa nchini hata kama ni kwa muda mfupi.

iv. Mheshimiwa Naibu Spika, Gesi kwa matumizi ya ndani ya nchi; Kwa mujibu wa ibara ya 10 (ii) ya mkataba wa nyongeza ukurasa wa 10, kiasi cha gesi ambacho makampuni ya nje yatalazimika kutenga kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi yetu hayatazidi 10% ya uzalishaji. Hii ina maana kwamba hata kama Tanzania itakuwa inahitaji zaidi hatutaweza kuwalazimisha kupata mgao zaidi, labda tukubali kununua kutoka kwao kwa bei ya ushindani wa soko la kimataifa. Je watanzania wataweza kumudu bei hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kupitia upya mikataba inayohusiana na mikataba ya vitalu vya gesi na kukili kuwa baadhi ya mikataba hiyo ni mbovu na haina maslahi kwa taifa. Ambapo Mwezi septemba 2012, Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter Muhongo alinukuliwa akisema kwamba "baadhi ya mikataba ni ya hovyo, na inahitaji kuvunjwa" na "sitovumilia mikataba ambayo haina maslahi kwa nchi na inawanufaisha wachache". Je ni mikataba mingapi imepitiwa mpaka sasa? Na mingapi imevunjwa au kurekebishwa kwa manufaa ya umma? Mwisho, Je mkataba huu wa statoil na TPDC kwa mapungufu hayo hapo juu siyo mbovu? Mkataba huu unapatikana katika Link ifuatayo:

(<https://onedrive.live.com/view.aspx?cid=0EC42B180C06D0B8&resid=EC42B180C06D0B8%21107&app=WordPdf>)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inashauri kuwa kuwepo na kikao cha pamoja kati ya kamati ya Uchumi, viwanda na biashara na ile ya Kamati ya Nishati na madini ili kuweza kuipitia mikataba ya namna hii na kujua madhaifu yaliyofitokeza na kuweza kulishauri Bunge juu ya hatua zaidi za kuchukua. Kamati inaimani kwamba bado hatuja chelewa na tuna muda wa kuweza kufanya yale yaliyo na manufaa kwa taifa hili (**Wahenga walisema ni heri tukawie lakini tufike**).

13.0 UCHAMBUZI, USHAURI NA MAONI YA KAMATI KATIKA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

i. Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenye fedha na iweke kipaumbele kulipa madeni yote ya mifuko ya jamii (Pension Funds) yaliyofikia shilingi bilioni 608.36 katika mwaka wa fedha 2014/2015. Na kama serikali itashindwa kutenga fedha hizi katika mwaka ujao wa fedha Deni hili liingizwe kwenye deni la Taifa na serikali itoe hati fungani za muda mrefu na mfupi kulipa deni hilo, vile vile serikali ilipe kwa wakati madeni yanayoiva hivi sasa.

ii. Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa upande wa mfuko wa PSPF serikali iongeze kiwango cha michango kwa watumishi wanachama wa PSPF kutoka 15% hadi 20% ya mshahara wa mwanachama (hiki ni kile kiwango kinacholipwa na Serikali hivyo Mwanachama hata athirika na ongezeko la michango hiyo), vilevile serikali iendelee kulipa kiasi cha shilingi bilioni 50 kila mwaka wa fedha kunusuru mfuko huu.

iii. Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa serikali imeshindwa kutimiza adhma yake ya kuiongezea benki hii mtaji kama ilivyokubalika katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano hivyo Serikali ikubali ombi la TIB kuruhusu kukopa shilingi bilioni 300 toka katika mifuko ya jamii ya PPF na NSSF na kwamba serikali ikubali kutenga fedha shilingi bilioni 30 kila mwaka, kulipa riba ya mkopo huo kwa mfululizo kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015.

iv. Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri serikali kuipatia benki ya TPB mtaji wa shilingi bilioni 7.5 kama walivyoomba.

v. Mheshimiwa Naibu Spika, Muda wa kushughulikia hoja na kesi za TP hivi sasa ni miaka 3 tu muda ambao ni mfupi sana inapendekezwa muda huo uongezwe hadi miaka 6.

14.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi (MB), Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani za pekee ziende kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa kwa jinsi wanavyoniunga mkono na mimi naendelea kuwaahidi kuwa sita pumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa. Kwani ni heri Punda aumie lakini mzigo wa tajiri ufike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara na mimi mwenyekiti wenu najivunia sana kuwa na wajumbe walio mahiri waliobobea katika masuala ya uchumi biashara na fedha. Michango na ushauri wao utalisaidia taifa na nina washukuru sana, na naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, MB, - Mwenyekiti
2. Mhe. Dunstun Luka Kitandula, MB, - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Margareth Agness Mkanga, MB,- Mjumbe
4. Mhe. Aeshi Khalifan Hilary, MB, - Mjumbe
5. Mhe. Ester Lukago Minza Midimu, MB,- Mjumbe
6. Mhe. Hussein Nassor Amar, MB - Mjumbe
7. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, MB, - Mjumbe
8. Mhe. Joyce John Mukya, MB, - Mjumbe
9. Mhe. David Zakaria Kafulila, MB, - Mjumbe
10. Mhe. Shawana Bukhet Hassan, MB,- Mjumbe
11. Mhe. Said Mussa Zubeir, MB - Mjumbe
12. Mhe. Vicky Pascal Kamata, MB - Mjumbe
13. Mhe. Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, MB- Mjumbe
14. Mhe. Khatibu Said Haji, MB - Mjumbe
15. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, MB - Mjumbe

16. Mhe. Josephine Jonson Genzabuke, MB - Mjumbe
17. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, MB - Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Hamis Misanga, MB - Mjumbe
19. Mhe. Dkt. Terezya Luoga Huvisa, MB - Mjumbe

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati.

Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah. Halikadhalika, napenda kuwashukuru Ndugu James Warburg, Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

15.0 MAOMBI YA FEDHA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi:

- (i) Fungu 50 Wizara shilingi **66,239,790,000** kwa matumizi ya Kawaida na shilingi **29,803,232,000** ni matumizi ya miradi ya maendeleo.
- (ii) Fungu 21 HAZINA shilingi **1,129,792,305,000** matumizi ya Kawaida na shilingi **47,513,033,000** matumizi ya miradi.
- (iii) Fungu 22 Deni la Taifa shilingi **4,354,865,076,000** kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa.
- (iv) Fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi **82,558,735,000** kwa matumizi ya Kawaida na shilingi **7,950,000,000** kwa matumizi ya Miradi ya Maendeleo
- (v) Fungu 10 Tume ya Pamoja ya Fedha shilingi **2,355,271,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida
- (vi) Fungu 13 Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu shilingi **2,000,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **195,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya maendeleo
- (vii) Fungu 7 Ofisi ya Msajili wa Hazina shilingi **88,552,642,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **1,943,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.
MWENYEKITI
KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA
4 JUNI, 2014.**

NAIBU SPIKA: Sasa nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Fedha, Mheshimiwa James Mbatia. Mheshimiwa Mbatia, karibu tafadhali.(Makofii)

MHE. JAMES F. MBATIA – MSEMAMI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:
Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na kwanza kabisa kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, nichukue nafasi hii kutoa pole zetu dhati kwa Mheshimiwa Shida Salum, aliyekuwa Mjumbe wa Bunge la Katiba, Mwenyekiti wa Walemau Tanzania, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo na mama mzazi wa Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Pia nitoe pole kwa baba mzazi wa Mheshimiwa Deo Filikunjombe, pamoja na Mheshimiwa Martha Moses Mlata na Wabunge wote waliopotolewa na ndugu na jamaa zao hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na siha njema ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2013/2014 pamoja na Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, Mbunge kwa kunitfea mimi kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha pamoja na Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mbunge kuwa Naibu Waziri Kivuli katika Wizara hii. Aidha, shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Naibu Waziri Kivuli na viongozi wenzangu kutoka vyama vya siasa hususan CHADEMA, CUF na NCCR - Mageuzi kwa ushauri wanaonipatia katika kusimamia wizara hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2013/2014. Katika Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kuwa Serikali ifanye mambo yafuatayo ili kuleta ufanisi na tija katika utendaji wa Wizara:-

i. Kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa. Serikali haikuweza kutekeleza kwa ufanisi pendekezo hili kwani hivi sasa misamaha ya kodi ni zaidi ya asilimia tatu ya Pato la Taifa. (Makofii)

Endapo pendekezo hili lingetekeliza ipasavyo, mapato ya Serikali yangeongezeka. Pia ingesaidia kupunguza nakisi ya bajeti ya serikali kwa kutegemea misaada na mikopo ya nje pamoja na mikopo ya ndani.

ii. Kufanya uchunguzi kupitia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) kuhusu manunuzi ya mafuta ya kuendesha mitambo ya IPTL ya kuzalisha umeme.

Pendekezo hili lilitokana na matumizi yenyenye mashaka ya shilingi bilioni 1.4 kila siku kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendesha mitambo hiyo. Katika pendekezo hilo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tuliiata Serikali kuleta taarifa ya uchunguzi huo Bungeni. Mpaka sasa taarifa rasmi ya uchunguzi huo haijawahi kuleta katika Bunge hili Tukufu. Pia ikumbukwe kuwa ni kwa kipindi kirefu sasa Serikali ilitoa ahadi ya kubadilisha mitambo ya IPTL itumie gesi badala ya mafuta yenyenye gharama kubwa, lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

iii. Kudhibiti wizi wa fedha katika mabenki ya hapa nchini kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu kilichopo katika wizara ya fedha. Taarifa rasmi kuhusu hatua zilizochukuliwa kuimarisha udhibiti huo haijaletwa na Serikali katika Bunge hili Tukufu. (Makofii)

iv. Kuielekeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kama vile reli na bandari. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza pia kwamba fao la elimu lililokuwa likitolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF, liwe fao la lazima kwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Pendekezo hili linaendelea kutekelezwa na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii.

v. Kutoa taarifa za hesabu za robo mwaka za kila Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kama ilivyo katika mabenki ili wanachama waweze kupata fursa za kuona utendaji wa mifuko wanayohifadhi fedha zao.

vi. Kuhamishia mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwenye Wizara ya Kazi na Ajira ambayo kimsingi ndiyo inayohusika na Hifadhi ya Jamii (*Social Security*). Pendekezo hili lilitokana na kwamba kwa hali ilivyo sasa mifuko hii iko katika Wizara tofauti tofauti jambo ambalo linaleta ugumu katika kuidhibiti na kusimamia. Hoja hiyo mpaka sasa hajiatekelezwa. Aidha, Mamlaka ya Kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) haijaweza kudhibiti kwa ufasaha Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini. (Makof)

vii. Kutoa maelezo ya kina kuhusu uuzwaji na umiliki wa hisa za Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Pendekezo hili lilitokana na utata wa uuzwaji na umiliki wa hisa kati ya Serikali na mwekezaji katika shirika hilo. Utata huo bado umeendelea kujitokeza. Ni vema Serikali ikaheshimu na kutekeleza maazimio yaliyo pendekezwa na Kamati ya Bunge ya TAMISEMI mwaka jana na kuridhiwa na Bunge hili tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Fedha kutoa maelezo ya namna Wizara ya Fedha ilivyotekeliza mapendekezo yote yaliyotolewa mwaka 2013/2014 hapo juu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha ndiyo msimamizi mkuu wa bajeti ya Serikali na jukumu lake la msingi ni kutunga sera nzuri ya bajeti itakayowezesha utekelezaji na ufanisi wa bajeti ya Serikali. Ni lazima Serikali ije na bajeti halisi inayoendana na mapato yetu huku ikizingatia vipaumbele. Ili kuwezesha hili, ni lazima Serikali iweke wazi madeni yote ya mwisho wa mwaka na kueleza namna yatakavyopatiwa fedha kwa mwaka unaofuata, vinginevyo isipoonesha deni la mwaka uliopita utaanza mwaka na bajeti pungufu na mwishoni kutokufikia malengo ilijojiwekea. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kuijiliza hapa je, Tanzania tunayo Sheria ya Bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya wastaifu (pensheni). Mafao ya wastaifu katika nchi hii yameendelea kuzua migogoro mbalimbali na manung'uniko katika jamii. Moja ya mambo yenye karaha kwa wastaifu ni namna wanavyobaguliwa katika kupewa haki zao. Wapo wastaifu ambao wameendelea kudai mafao yao kwa miaka zaidi ya 36 sasa na hakuna majibu ya kujitosheleza, mfano ni wale wastaifu wa iliyokuwa Jumuia ya Afrika Mashariki. Aidha, kuna wastaifu waliokuwa watumishi wa umma ambao wamebaguliwa na Sheria ya Mafao kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 (*The Public Service Retirement Benefits Act, Cap. 371, R.E. 2002*).

Kwa mujibu wa sheria hiyo, pamoja na kufuta Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954 (*The Pensions Ordinance of 1954, Cap. 371 of the Laws of Tanzania*), bado ilibakiza matumizi ya sheria hiyo kwa watumishi wa umma waliokuwa wakipokea mafao yao kwa sheria na kanuni za sheria iliyofutwa. Hali hii inajidhihirisha kwenye kifungu cha 84 cha Sheria ya mwaka 1999 kama kinavyosomeka:-

"84. Employees under the Pensions Ordinance [Cap. 371 R.L.] to continue under the same notwithstanding anything to the contrary, any person or category of persons who was covered under the Pensions Ordinance or any other written laws and who is not covered under this Act, shall continue to enjoy all the rights and benefits conferred under that law as if this Act had not been enacted." (Makof)

Aidha, kifungu cha 73 cha sheria hiyo hiyo kinasomeka kama ifuatavyo:-

"73. Repeal of R.L. Cap. 371

(1) [Repeals the Pensions Ordinance *.]

(2) All persons who, immediately before the commencement date, were receiving pension, allowances, additional benefits or other retirement benefits granted under the provisions of the Pensions Ordinance* which are similar to those set out under section 20(4) of this Act, shall continue to receive those benefits as if the Pensions Ordinance * had not been repealed.

(3) All the employees who were immediately before the commencement of this Act qualified under the pension scheme shall on attainment of retirement age be entitled to receive their pension for the service they rendered in the Service before the commencement date plus the remaining portion of the pension entitlement under this Act."

Matumizi ya Sheria ya Pensheni ya mwaka 1999 yamesababisha ubaguzi na unyanyasaji mkubwa kwa watu waliowahi kutumikia Taifa hili kwa uadilifu, uaminifu na uzalendo uliotukuka. Kwa sasa asilimia kubwa ya watumishi hao wanalipwa mafao yasiyoendana na hali halisi ya maisha yao, wapo kwenye hali ngumu ya udhalilishwaji na umaskini uliopindukia. Wengi wao hupewa shilingi 20,000/= tu kwa mwezi huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na aibu kwa Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafanywe mabadiliko ya sheria zote zinazohusu mafao kwa wafanyakazi katika sekta zote za ajira nchini. Pia kipaumbele kiwekwe kwenye marekebisho ya Sheria ya Pensheni ya mwaka 1999 na kuwafanya wale wote waliokuwa wakistahili kupewa pensheni zao kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954 wanapewe pensheni hizo kwa kuzingatia viwango vipyaa vinavyokidhi mahitaji ya msingi ya binadamu na utu, siyo viwango vya mwaka 1954. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara hii imethibitisha kuwa na udhaifu mkubwa wa kuanda bajeti inayotekelzeza. Haya yanajidhihirisha katika Ripoti ya fedha ambazo hutolewa na Benki Kuu ikiwa ni moja ya taasisi zinazosimamiwa na Wizara. Katika ripoti tatu mfululizo za robo mwaka (*quarterly reports*) zilizotolewa Septemba 2013, Disemba 2013 na Machi 2014, Wizara imeshindwa kukusanya mapato yaliyokusudiwa katika bajeti. Hali hii imelisababishia Taifa kukosa mapato yanayofikia shilingi bilioni 977.2. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi zinaonesha kuwa Wizara imeshindwa kusimamia majukumu yake ya kukusanya mapato kikamilifu au iliandaa bajeti isiyotekelzeza kwa kutozingatia vigezo muhimu.

Kuhusu riba katika benki na asasi za fedha, Wizara ya Fedha kuititia Benki Kuu inayo wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sera za fedha na sheria zinazohusu mashirika ya fedha na benki. Jukumu hili huambatana na wajibu wa kudhibiti mfumuko wa bei (*inflation*). Jukumu hili Wizara imejitalidi kulitekeleza.

Hata hivyo, Wizara imeshindwa kusimamia viwango vya riba vinavyotozwa na mabenki pamoja na taasisi za fedha. Wakati mfumuko wa bei umeshuka toka asilimia 19.8 Disemba, 2011 na kufikia asilimia sita mwezi Machi, 2014, viwango vya riba katika mabenki na Asasi za fedha vimeendelea kuwa vya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba halisi (*real interest rate*) ambayo inakadirisha kama tofauti ya *nominal interest rate* na *inflation rate* hivi sasa ni asilimia 12 mpaka 18. Hakuna shughuli ya kiuchumi ya kawaida unayoweza kuifanya na kuweza kulipa riba za juu kiasi hiki. Mwananchi

wa kawaida akiweka akiba yake analipwa riba (*saving deposit rate*) ya asilimia tatu wakati mfumko wa bei wa sasa ni asilimia sita. Hata wakati mfumko wa bei ulikuwa asilimia 19.8 riba aliyolipwa mwananchi wa kawaida anayeweka akiba ilikuwa asilimia 2.9. Mabenki yetu hayampi mwananchi wa kawaida motisha wa kuweka akiba na yanambana mjasiriamali kwa kumtoza riba kubwa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, riba katika benki na asasi za fedha imeendelea kuwa juu, mojawapo ya sababu ya kiwango hiki kuwa juu ni Serikali kuwa mmoja wa wakopaji wakubwa kutoka katika mabenki na asasi za fedha za hapa nchini. Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania iliyotolewa mwezi Machi, 2014 imeanisha kuwa Serikali imekopa kutoka kwenye vyanzo vya ndani zaidi ya shilingi triliioni moja katika kipindi cha mwezi Machi, 2013 hadi Machi, 2014. Hali hii imesababisha ushindani usio wa haki baina ya Serikali na wananchi wanaokopa katika mabenki hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukopaji wa Serikali kama ulivyoelezwa hapo juu unachangia kufanya riba ziwe za juu. Riba inayolipwa na Serikali kwa *Treasury Bills* ya mwaka mmoja mpaka Disemba, 2013 ilikuwa asilimia 15.63. Kwa mabenki mengi kuwekeza kwenye hatifungani za Serikali (*treasury bills and bonds*) kuna faida kubwa ya uhakika ambapo kumkopeshwa mjasiriamali wa kawaida kuna risk kubwa ya kutolipwa. Pamoja na kuwepo na mabenki mengi mfumo wetu wa fedha haufanyi kazi ya kukusanya akiba kwa wingi na kuiwekeza kwa wajasiriamali wa ndani ili kukuza uchumi na kuongeza ajira. (*Mfumo wa riba upo kwenye Quarterly Economic Report of March 2014 ya Benki Kuu Table 3.13*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa riba za benki kutaongeza fursa za kukopa na kusaidia wananchi kukuza mitaji. Hali hii itasaidia ongezeko la ajira, kukua kwa uchumi wa Taifa, idadi ya walipa kodii itaongezeka na ustawi wa wananchi utaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya fedha za kigeni hapa nchini yaani *dollarization*. Aidha, biashara ya fedha za kigeni imeendelea kukua katika miji mikubwa pamoja na miji iliopo mipakani. Pamoja na kukua kwa biashara hiyo, kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara kutoza bidhaa na huduma kwa fedha za kigeni hususani dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imeendelea kusababisha wananchi kukosa imani na shilingi ya Tanzania na kukosa tija ya kuweka akiba (*savings*) kwa shilingi ya Tanzania. Badala yake, baadhi ya wananchi wameanza kuhifadhi akiba zao kwa kutumia dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha za kigeni kwa malipo ya ndani unafanya fedha za kigeni kuwa sehemu ya ugavi wa fedha (*money policy*) ya nchi yetu na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na matumizi ya fedha zetu. Matumizi ya fedha za kigeni kwa malipo ya ndani unarahisisha utoroshaji wa mali na mitaji nje ya nchi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa. Deni la Taifa limeendelea kukua kila mwaka. Taifa limeendelea kukopa kwa kiasi kubwa, kiasi ambacho dhamana za Serikali zinaendelea kuwekwa rehani.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira kubwa ya kuruhusu Serikali kukopa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hakuna taarifa za kuridhisha kuhusu namna ambavyo fedha zinazokopwa na zinavyotumika katika kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Deni la Taifa kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu, limeongezeka kutoka Shilingi triliioni 9.3 mwaka 2007 hadi Shilingi triliioni 22.2 mwezi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya deni lote la Taifa la ndani na la nje ya nchi ni Shilingi zaidi ya triliioni 28. Kwa hali hii, kila Mtanzania anadaiwa wastani wa Sh. 600,000/= . Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuwasilisha katika Bunge hili taarifa sahihi za namna fedha zilizokopwa na zilivyotumika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua mafanikio yaliyofikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kukusanya kodi kwa mujibu wa sheria inazosizimamia. Tunawapongeza. Hata hivyo, tatizo kubwa limebainika katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na maduhuli yaani non-tax revenues. Mfano, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imeshindwa kukusanya mapato yatokanayo na maduhuli yanayofikia Shilingi bilioni 190 kwa sababu za kimfumo (Ripoti ya Benki Kuu 2012/2013.)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza maboresho makubwa yafanyike kuongeza ufanisi wa Serikali katika kukusanya mapato hayo. Uwepo mfumo wa ufuatiliaji, usimamiaji na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Fedha za Umma. Ripoti ya mwaka 2012/2013 ya Benki Kuu ya Tanzania imebainisha katika ukurasa wa 18, kuwa Serikali ililipa Shilingi bilioni 87.6 zaidi ya ilivyokadirwa kwa ajili ya mishahara. Ripoti hiyo inaonesha pia kuwa Serikali ililipa Shilingi bilioni 173.9 zaidi ilivyokadiria ikiwa ni riba ya mikopo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa majibu sahihi kuhusu sababu za kufanya malipo yasiyo katika makadirio ya Serikali ya takribani Shilingi bilioni 261.5 kwa mwaka huo wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa miaka mitano, yaani 2011/2012 - 2015/2016 na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, yaani Big Result Now, imenorodhesha mambo mengi yenye masilahi mapana kwa Taifa na wananchi wake. Hata hivyo, bajeti na utendaji wa Serikali hauthibitishi nia hiyo inayoelekezwa kwenye nyaraka hizo muhimu kwa Taifa. Hii ni dhahiri kuwa Serikali iliyoko madarakani inayongozwa na Chama cha Mapinduzi imeshindwa kusimamia na kutekeleza kikamilifu Mipango hii ya Taifa. (Makof)

Aidha, athari za kushindwa utekelezaji wa Mipango hii kwa kiwango chenye tija, kinajidhihirisha kwa kuwa na Watanzania takribani asilimia 28.1 ambaao ni zaidi ya Watanzania milioni 12 kuendelea kuwa fukara. Hizi ni takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2012. Aidha, pengo kati ya walio nacho na wasio nacho linazidi kuongezeka. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha inaweka mifumo inayofaa na ya haraka katika kubaini na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima, malipo yasiyoendana na makadirio, upotevu wa fedha zitokanazo na maduhuli, na ufanisi katika kuandaa na kutekeleza sera za mapato na matumizi ya fedha za Serikali, yaani nidhamu ya matumizi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni msingi mkubwa wa kanuni ya demokrasia ulimwenguni kuwa sheria zote na mamlaka za kusimamia na kutoza kodi zizingatie uwakilishi wa wananchi ambaao ndio walipa kodi. Serikali yetu inaendeshwa kwa ridhaa ya Watanzania ambaao tumekubali kuchangia matumizi ya Serikali kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yetu ya uwakilishi, yaani sisi Wabunge, tunao wajibu wa pamoja kuweka masilahi ya Taifa mbele, na siyo itikadi za vyama vyetu, ili tuweze kuwatendea wananchi wote haki ya kukuza na kustawisha utu wao binafsi na utu wa Taifa letu. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuomba Bunge hili Tukufu kutokomeza tabia, hulka na matendo yote yanayoashiria ubabe wa baadhi ya viongozi wa Serikali, wanaotumia vibaya madaraka waliyopewa na kuliingiza Taifa katika hasara. Uwezo huo

tumepewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2). Tukiamua tunaweza! Kwani makosa yetu ya jana, japo yasikitisha sana, ni mafundisho yetu ya leo! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa, Serikali itazingatia maoni haya katika mwaka wa fedha 2014/2015, kwani hakuna mtu au kikundi cha watu katika nchi yetu chenye hatimiliki ya fikra. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia hekima na busara wewe Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Katibu wa Bunge kwa dhamana mliyopewa ya kulitumikia, kulisimamia na kuliongoza Bunge hili Tukufu. Nawashukuru wote walioshiriki katika kuandaa maoni ya hotuba hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Fedha.

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mustafa Mkullo na atafuatiwa na Mheshimiwa Dalali Kafumu. Wakati wakijandaa, nitangaze tangazo moja fupi kutoka kwa Mwenyekiti wetu wa Bunge Sports Club, Mheshimiwa Iddi Azzan, kwamba Waheshimiwa Wabunge mazoezi yanaendelea kwenye Uwanja wa Jamhuri kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya kirafiki. Mnaombwa wachezaji wote mfike katika mazoezi kwa wingi.

Pia wanaombwa hata wale ambao wamesajiliwa kupitia dirisha dogo, nao waweze kufika. Wachezaji ambao wamesajiliwa kupitia dirisha dogo hivi karibuni ni Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ambapo kuna pambano mwisho wa wiki kati ya Bunge Sports Club na Akiba Commercial Bank, siku ya Jumamosi; na Jumapili ni Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani wa Dodoma Mjini. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Baada ya tangazo hilo, sasa nimwite Mheshimiwa Mkullo dakika saba; Mheshimiwa Kafumu atafuatia na Mheshimiwa Khalifa Khalifa ajiandae.

MHE. MUSTAFA H. MKULO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuchangia, niliambiwa ningechangia mchana, lakini nashukuru umeamua kwamba niwe wa kwanza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijachangia siku nydingi. Sasa leo kwa sababu nimepata nafasi, naomba uniruhusu nitoe maelezo kidogo, halafu niendelee na uchangiaji wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aprili mwaka 2012 nilituhumiwa katika Bunge lako hili Tukufu wakati nikiwa Waziri wa Fedha kwa kuuza kiwanja namba kumi cha CHC. Sijawahi kupata nafasi ya kueleza, wala kujitetea. Kwa nafasi hii uliyonipa, naomba niseme kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuza kiwanja, sikuidhinisha uuzwaji wa kiwanja, wala sikushiriki mchakato wa kuuza kiwanja. Nini kilichotokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, CHC, Bodi yao waliiandikia Wizara ya Fedha kuomba ruhusa ya kuuza kiwanja namba 10 kilichopo Nyerere Road. Barua haikwenda kwa Waziri wa Fedha, ilikwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kama ilivyo kawaida ya Serikali. Msajili wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hazina akafanya uchambuzi akatoa maoni yake kwa Katibu Mkuu. Katibu Mkuu akapendekeza kwa Waziri wa Fedha nini kifanyike. Waziri wa Fedha akatoa maelekezo kwamba kulikuwa na upungufu mkubwa katika mapendekezo ya Bodi.

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha akaagiza ufanyike utaratibu wa kawaida, wafuate taratibu, wafuate kanuni kumpata mtu ambaye angweza akauziwa kiwanja hicho. Barua ikandikwa kwa CHC. Baada ya barua kuandikwa kwa CHC ikagundulika kwamba yule mtu waliyemtaka kununua kiwanja hicho, ukweli ni kwamba alishalipa nusu ya gharama za kiwanja hicho. Kwa maombi ya Bodi kwa Wizara, kwa maana nyingine ilikuwa ni ghiliba. Ni cover up kwamba walishauza kiwanja, sasa walikuwa wanatafuta Waziri aidhinishe. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuidhinisha. Nataka niseme ukweli! Mimi sikuidhinisha, Katibu Mkuu hakuidhinisha, wala Msajili wa Hazina hakuidhinisha! Waliouza kiwanja kile, alikuwa ni Mwenyezeki wa wakati huo wa Bodi na aliyekuwa Acting MD wa Bodi. Wala siyo Bodi nzima! Wanajulikana! Kwa hiyo, kiwanja kiliuzwa na wenywewe, sio Waziri aliyeuza, ni kama UDA kabisa hii! Hii ni mbaya zaidi hata ya UDA. (Kicheko/Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye nikashikiwa bango na Mbunge mwenzetu, akaanza kupeleka karatasi za uongo kwenye magazeti. Nadiriki kusema kwamba makaratasi yote yaliyopelekwa kwenye magazeti yote yalikuwa ya uongo, hakuna karatasi hata moja ili yotoka kwenye faili la Hazina, makaratasi yote yalitoka CHC. Sasa makaratasi mengine yalikopatikana, Waheshimiwa Wabunge wengine niksema niwaambie hapa, wote mnawenza mkatapika. Kwa sababu njia zilizotumika hazikuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilajaribu kuomba kupata nafasi ya kutoa utetezi wangu humu Bungeni, kwa bahati mbaya sikupata mpaka nilipoondoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mkataba wa kuuza kiwanja hicho ulitoa saini miezi mitano baada ya mimi kuondoka Hazina. Wabunge wenzangu, niliuza mimi kiwanja hicho saa ngapi? Mkataba wa kuuza kiwanja hicho sasa rasmi na kuwakabidhi hao walionunua, ulisainiwa miezi mitano baada ya mimi kuondoka Hazina. Kwa hiyo, nilitaka nieleze haya. Nimeona nieleze haya, mimi ni Muislamu, Marehemu baba yangu Sheikh, babu yangu alikuwa Chief; kwa hiyo, sikuzoea kusema uongo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuzoea kusema uongo! Nimesema haya makusudi na wote wanisikie. Nataka nije nife kwa heshima. Nisije kufa kwamba mimi nilikuwa mwizi na watu walionyesha hapa makaratasi, mwizi namba moja, Mkullo!

Mheshimiwa Naibu Spika, naangalia kwenye mtandao niko Washington, wakati ninyi mnazungumza hapa, niko kwenye Ofisi ya Benki ya Dunia mpya kwenda kumpa hongera. Natafuta pesa kwa ajili ya nchi, huku naambiwa mwizi. Sasa nimeona niseme haya. Pesa zilishapokelewa kabla sisi hatujafanya chochote, mkataba wa mauzo umesainiwa mimi nimeshaondoka Hazina. Kiwanja hicho niliuza saa ngapi? (Makofij/Kicheko)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkulo ahsante tunakushukuru sana. Muda hauko upande wako tena!

MHE. MUSTAFA H. MKULO: Dakika zimekwisha?

NAIBU SPIKA: Muda hauko upande wako, umekwisha!

MHE. MUSTAFA H. MKULO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kuniruhusu kusema hayo. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Tunakushukuru kwa maelezo yako. Huo ni ushuhuda mmojawapo wa baadhi ya mambo ambayo hutokea humu ndani.

Sasa namwita Mheshimiwa Dalaly Kafumu, na Mheshimiwa Khalifa ajiandae!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi namli niwe mchangiaji katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji katika Bunge lako Tufuku. Pili, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha pamoja na wasaidizi wake, Mawaziri vijana, tunategemea makubwa kutoka kwa vijana hao (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mambo makubwa matatu tu kwa kifupi kabisa. La kwanza, mwaka 2013 katika Bunge hili Tukufu, mimi pamoja na Wabunge wengine tuliihauri Serikali kwamba ni wakati sasa wa kuanza kutunza dhahabu kwenye hazina yetu. Naomba nirudie tena kusema jambo hili. Sisi saizi ni wazalishaji wakubwa wa dhahabu katika Afrika na hatuna sababu yoyote ya kutokuwa na dhahabu katika Hazina ya Taifa letu.

Sheria ya BOT kifungu namba 5 (1) hivi, kinaruhusu na kinasema, kazi ya BOT ni kutunza fedha za kigeni lakini pia kutunza dhahabu safi. Kuna faida kubwa sana kutunza dhahabu safi katika Hazina ya Taifa hili. Faida kubwa, nchi zote unazosikia tajiri duniani ni kwa sababu zina hazina kubwa ya dhahabu katika Hazina zake. Lakini nchi hizi zina fedha zenye nguvu. Ukiishakuwa na dhahabu kwenye Hazina yako, unakuwa na fedha yenye nguvu. Inaweza ikitalemka ukauza kidogo, fedha yako inapanda thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba tena Serikali mwaka huu turudie jambo hili. Jipangeni, liweke jambo hili kama Jambo la BRN pia ili tuweze kutunza dhahabu. Kwa nini tusiwe na dhahabu wakati sisi tunazalisha dhahabu? Mwaka 2013 tulisema Wabunge kadhaa na mimi kwamba tunaweza kuanza kuyaagiza makampuni ya madini yakatulipa kiasi kidogo cha mrabaha katika dhahabu safi, au hata mrabaha wote katika dhahabu safi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaweza tukaanzisha utaratibu wa kununua dhahabu kama tulivyofanya miaka ya nyuma. Tunanunua dhahabu safi kwa sababu dhahabu inatoka Tanzania. Pia, tunaweza tukaiagiza STAMICO nayo ikaweza kufanya miradi ambayo faida yake tukatunza katika dhahabu safi. Itatusaidia sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ukurasa wa 43 naona hakuna kilichosemwa juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Hazina ni moyo wa Taifa na ndiyo tunategemea Hazina itoe fedha kwa ajili ya kuendesha miradi kwenye Wizara, Halmashauri na miradi yote hii tunayojivunia ya BRN. Shida kubwa, Wabunge wote wanafahamu, fedha hazitoki Hazina! Mwisho wa mwaka fedha zinakuwa zimetoka asilimia 30, 40 au 20! Sasa tutaweza kuendesha kweli miradi namna hii?

Nakala ya Mlango (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Hazina, tubadilike sasa, tusifanye kazi ile ya business as usual, tubadilike! Tumebakiza mwaka mmoja tufike mwaka 2015, basi tufanye makubwa, tupeleke fedha hizi tulizoipangia. Kama hazipo, basi tusipange bajeti kubwa hivyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, nataka nizungumze kidogo kuhusu malipo mishahara ya Walimu wapya. Limetokea tatizo kule Igunga wiki iliyopita. Walimu zaidi ya 100 hawajalipwa mishahara ya mwezi wa Nne na mwezi wa Tano. Matokeo yake, Walimu hawa wameandamana, wamekwenda Ofisi ya DED na Ofisi ya DC, wamewafungia, wanataka kufanya vurugu. DC na DED wamepata taabu kweli kuwatuliza vijana hawa. Mpaka DC ameji-commit anasema, ifikapo tarehe 13 mishahara ya Walimu hawa itakuwa imelipwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Wizara ya Fedha, ninyi ndio watoa fedha. Kama hamjapeleka fedha, jamani pelekeni! Tarehe 13 tumewaambia Walimu wetu wapate mishahara yao. Vinginevyo tumeajiri Walimu, tunaishukuru sana Serikali kwa kutupa Walimu katika Wilaya ya Igunga, lakini tuwalipe mishahara na marupurupu yao. Wizara ya Fedha, pelekeni mishahara ya watumishi maana tunahitaji Walimu wawe na moyo wa kufanya kazi badala ya kushindana na Viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mambo matatu kwa kifupi, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi, na nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kwenda kuangalia Uchaguzi wa Malawi. Uchaguzi ulikuwa mzuri, tumepeata Rais na naomba kuwaambia wananchi wa Igunga, tuko pamoja, nimesharudi Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (Makof)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dalaly Kafumu ahsante sana. Kumbe ulituwakilisha huko Malawi! Sasa yule mama imekuwaje tena? (Kicheko)

Sasa namwita Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nami nipate fursa ya kusema machache kuhusu Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa sababu ni watendakazi wazuri, na ninaamini ikiwa watafanya kazi kwa nia njema kabisa na wakipata msaada wa wenzao, huenda tukaondoka hapa tulipo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, labda niseme kuwa katika hali ya kawaida, Kiongozi anatakiwa awe mtu wa mwisho yeye mwenyewe kuharibu. Wizara ya Fedha ndio Wizara Mama katika masuala ya matumizi katika nchi yetu kwa sababu wao ndio wanaolipa katika maeneo mengine. Sasa inapokuwa wao wenyewe ndio wanaolipa, lakini wao wenyewe katika Wizara ya Fedha mambo hayaendi vizuri, hilo ni jambo ambalo ni lazima liangaliwe na waliangalie kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya mwaka 2013 ya CAG iliyomalizia Juni, ukurasa wa 122 mpaka 134, kuna matatizo makubwa ambayo yamezungumzwa kutokea katika Wizara ya Fedha. Mambo haya ni vizuri yakashughulikiwa kwa sababu haiwezekani hata siku moja, ndani ya Wizara ya Fedha, utokee upungufu mkubwa wa fedha au matumizi yasiyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna matumizi ya Shilingi milioni 319 ambayo ni masurufu ambayo hayakurejeshwa.

Kuna malipo ya vifaa visivyostahili, Shilingi bilioni 2.3, kuna malipo chini ya kiwango stahiki, Shilingi milioni 68, kuna matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti, Shilingi milioni 15, kuna malipo yasiyo na stakabadhi, Shilingi bilioni 47 na mengi mengineyo, kwa ujumla ni Shilingi bilioni 86.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara kubwa kama hii ambao wao ndio wanaotoa fedha, wanashindwa kusimamia wao wenyewe fedha ndani ya Wizara yao; hili ni tatizo! Mimi nawaambia kwa nia njema kabisa, lazima kwanza, kabla hamjawalenga mawe watu wengine, basi muwe makini sana. Fagieni nyumba yenu ili muweze kuzifagia nyumba nyingine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu deni; Wizara, sasa hivi ina madeni makubwa ya ndani, Shilingi bilioni 277.7, katika ripoti hiyo ya CAG, ukurasa wa 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya ndani ni kikwazo kikubwa kwa utekelezaji wa shughuli za ndani. Wizara hizi nyingi zinazolalamikiwa na wadeni, ni kwa sababu Wizara ya Fedha wenyewe hawapeleki. Sasa ikiwa hampeleki malipo ya Wazabuni kwa mfano, malipo ya Wakandarasi, mnategemea nini? Watu hawa ndio wanaojenga Ofisi za Askari, ndio wanaolisha Askari, ndio wanaolisha Magereza. Sasa kama hamkuwalipa wanyonge hawa, ambao wengi wao wanachukua mikopo katika mabenki: Je, mnataka wafilisiwe? Wakifilisiwa, hasara inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu SPika, maana yake, hivyo ni vitu ukiviangalia labla nje utadhani ni vidogo, lakini ni vikubwa sana katika mustakabali na uendeshaji wa nchi. Nawaombeni sana, mwangalie kwa karibu mambo haya, kwa sababu mtawatia watu katika mzigo mkubwa, mwisho watasusa tu! Wakisusa, wanaweza watu wengine wakashitakiwa. Kwa sababu mtu anakwenda kukopa kwa mfano Shilingi milioni 400 kwa mtu, anakwenda kujenga Ofisi ya Polisi, au anajenga Ofisi fulani, halafu unafika muda hakupeleka fedha za watu, lakini source ilikuwa kumbe fedha hazikutolewa na Treasury kwenda kulipwa. Sasa inatia huzuni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu SPika, kuna pointi ilizungumzwa hapa na Kamati, nami naomba hii niizungumze vizuri kidogo. Ni suala la CHC. CHC kwa mujibu wa sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni, wanapaswa ku-handle over majukumu yao kwa Msajili wa Hazina ifikapo Juni, 30 mwaka huu. Kazi ya CHC mimi siamini kuwa imekwisha! Wanao upungufu wao, lakini pamoja na hayo, kazi waliyofanya ni kubwa, nami siamini kuwa ikifika Juni 30, wakitua majukumu yao kwa Msajili wa Hazina, Msajili wa Hazina ameshaandaliwa kuweza kukabiliana na kazi kubwa waliyofanya CHC.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba mambo mawili. Kwanza, Wizara ya Fedha iwe makini sana katika hili, lakini pili, naliomba Bunge ikiwezekana tu-revisit sheria hii ambayo tuliipitisha, kwa sababu tumeipitisha sheria, lakini utekelezaji wake sasa utakuwa mgumu, matokeo yake tutalaumu, lakini lawama ile mwisho inaweza ikarudi kwetu kwa sababu inawezekana tumeipitisha kitu, lakini kukitekeleza ni vigumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tui-revisit hii sheria na ikiwezekana ije katika *miscellaneous amendment* tuweze kufanya marekebisho. Kama kuna namna ya kuwaongezea muda hawa jamaa, tuwaongezee. Vinginevyo, Msajili wa Hazina tunaweza tukaipeleka, lakini tukajikuta hatukutatua tatizo, tumeongeza tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sikusikia katika maelezo yake hapa katika suala zima la mikopo, misaada na nini kimekwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. Wao wanasema wanatusaidia sana; na ni kweli wanatusadia, hebu tupe mchanganuo kidogo, tumepata nini katika bajeti ya mwaka huu na kiwango gani kimekwenda Zanzibar na kitasaidia vipi katika maendeleo ya huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa, nakushukuru kwa mchango wako. Mheshimiwa Waziri atatusaidia jioni kujua, hawa CHC kila mwaka wao ikifika wakati wa kukabidhi, tunaambiya bado mambo; kila mwaka, kazi yetu sisi kuwaongezea muda. Basi wawe wa kudumu tu sasa mwisho wake. (Kicheko/Makof)

Sasa namwita Mheshimiwa Moses Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami nichangie Wizara hii ya Fedha. Kimsingi, kwanza naomba nipongeze hotuba iliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ambayo ukiangalia kimsingi kama Serikali itakuwa iko serious, basi inaweza pengine ikichukua ushauri huu, unaweza ukawa pengine ni suluhusho la matatizo ambayo yanaikabili Serikali hii, ambayo wakati mwengine inapoteza umakini katika kushughulikia mambo mbalimbali ambayo ni ya msingi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umetolewa ushauri hapa, na niungane na Mheshimiwa Dalaly Kafumu ambaye amezungumzia kwamba ni aibu Wizara ya Fedha, mmetengewa bajeti na mwaka huu mnakuja mnatuomba bajeti. Bunge litapitisha kama kawaida, lakini kesho unakuta mnasema makusanyo ni kidogo, fedha kwenye miradi ya maendeleo haziendi kama zilivyokusudiwa. Hili ni tatizo kubwa! Kwa sababu unaona hapa tunawasulubu Mawaziri wa Maji, tumewasulubu Mawaziri wa Afya pamoja na watu wengine, lakini chimbuko la matatizo yote ni nyinyi Wizara ya Fedha. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kwa Bunge lako, wakati mwengine kujaribu kuwa serious ili kuhakikisha kwamba watu hawa, fedha ambazo tunawaihinishia, waende wakazitumie kuhakikisha kwamba malengo ambayo yamekusudiwa, basi yanafikiwa. Haya mambo ya kuja kutuambia sijui wafadhili hawaajaleta fedha; sisi hatustahili kuwaelewa kuja kutuambia kitu ambacho ninyi mlipaswa kuweza kuwajibika nacho. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hilo kwa kweli kwamba tuliangalie. Tunaweza tukawa tunajadili kila siku lakini bado mwakani watakuja tena na matatizo yale yale; na Wizara nyingine imeanza kuzipunguzia fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala hilo, pengine niungane na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusiana na suala la UDA. Kumekuwa kuna maelezo hapa ambayo kwa kiasi Fulani ni kama vile Serikali inajichanganya. Serikali katika maelezo yake na hasa kupitia kwa Naibu Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, wakati anajibu maswali ambayo yalikuwa ni ya Mheshimiwa Mdee, yaliyoulizwa na Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, alisema kwamba, Shirika la UDA linamiliikiwa na Serikali kwa asilimia 100, jambo ambalo ukiangalia kwa mujibu wa records na vielelezo ambavyo viro, siyo kweli. (Makof)

Mwanzoni inaonekana kabisa kwamba, Serikali walikuwa wana hisa 49, halafu Jiji asilimia 51 walizokuwa wamepewa na Serikali. Sasa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za

Nakala ya Mlango (Online Document)

Mitaa, ambayo ilijaribu kuweza kuchunguza suala hili, kwanza, moja ya matatizo ambayo yalibainika, ni wazi Serikali walimuuzia Simon Group hisa hizo kwa bei ya chini sana. (Makofii)

Kwa mfano, waliuza hisa moja kwa Sh.145/=, tofauti hata na ushauri ambaa ulikuwa umeshauriwa na mshauri ambaye ni KPMG, kama sijasahau, ambaye aliwaambia, kama *in case* Simon Group atanunua hisa zile, pamoja na madeni, alistahili auziwe kila hisa kwa Sh. 1,600/=. *In case* atauziwa bila ya kurithi madeni, alitakiwa auziwe hisa moja kwa Sh. 2,600/= na kidogo.

Leo tunapozungumza, Simon Group anamiliki zaidi ya hisa 76 na kidogo, Serikali kwa maana ya Msajili wa Hazina, ana hisa 23 na kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amelieleza Bunge wakati akijibu maswali yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mnyika, kwamba Serikali UDA pamoja na Jiji kwa asilimia 100.

Haya maelezo tutaomba Serikali tuweze kupata pengine ufanuzi wa suala hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirejea taarifa za Hansard, kumbukumbu za Bunge, wakati wa taarifa za Kamati zinasomwa hapa mwaka 2013, Kamati yako ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilifanya kazi mgogoro huu na kuona Serikali ni kana kwamba inamwonea huyu Simon Group. Kwa nini?

Ni Serikali hii hii ambayo imeweza kumpatia Simon Group ndani ya UDA bank clearance guarantee. Ni Serikali hii ndiyo ambayo ilikuwa inafanya mambo haya. Pia ni Serikali hii ambayo imempatia tax exemption, huyu bwana ambaye ana hisa ya asilimia 76 na kidogo, ndani ya UDA na Msajili wa Hazina asilimia 23. Ni tatizo!

Sasa Serikali hebu mtueleze, huu mkanganyiko unatokana na nini? Huyu anasema hivi, halafu mtu mwengine anazungumza yake.

TAARIFA

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali, upokee taarifa.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima zote za Bunge lako na kwa heshima ya msemaji aliyekaa; kwanza msemaji aliyekaa ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, Kamati ambayo ndiyo ilikwenda kufanya uchunguzi nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya TAMISEMI haifanyi mahesabu ya Mashirika ya Umma. Kamati ya TAMISEMI inasimamia sera. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli uliokuwepo hapa, ripoti ya CAG iliyoletwa, ina mandate zaidi ya Kamati ya TAMISEMI. Tunaomba Wajumbe humu ndani, tutetee maslahi ya public, tusije hapa tukatumika kutetea maslahi ya watu nje ya utaratibu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hiyo taarifa. Kama ataikubali au ataikataa, lakini ukweli ndiyo huo.

MBUNGE FULANI: Habari ndiyo hiyo!

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Kamati ya TAMISEMI haina mandate ya kutoa amri au ya kushauri jambo lolote kuhusiana na mahesabu Mashirika ya Umma. Kamati zinazohusika zipo na Mjumbe huyu haja-declare interest kama yeye yumo kwenye Kamati hiyo. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa wote nyinyi mnatakiwa m-declare interest, maana mambo haya yanaleta taabu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naomba niseme tu kwamba taarifa ya Mheshimiwa Zungu ina upungufu ufuatao, kwa hiyo, sikubaliani na taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa sababu nilikuwa bado naendelea kuzungumza, ni-declare interest tkwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anaposema kwamba Kamati hii ilifanya uchunguzi wa suala hili kinyume cha utaratibu, anatakiwa athibitishe kwamba ni utaratibu gani ambao ulikiukwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kamati yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, inashughulikia masuala ya kisera. Tujiulize, kwa mujibu wa kumbukumbu ya Hansard ya mwaka jana, tarehe 13 Desemba, Bunge hili, na ninakumbuka siku hiyo Bunge ulikuwa undiongoza wewe Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulisema wakati Mheshimiwa Lwanji anahitimisha hoja ya Kamati, naomba ninukuu. Kwamba, "hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nashukuru sana Mheshimiwa Lwanji kwa kuhitimisha hoja yako viziri sana na tunakupongeza sana. Sasa naomba kulihoji Bunge lako kwamba, lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na mapendekezo na maoni ambayo yamo katika taarifa yao."

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo lilikuwa addressed na Bunge lako likawa limeshauri, ni pamoja na utata uliogubika juu ya masuala ya Shirika la UDA. Sasa kama Bunge lako liliridhia na likapitisha mapendekezo ya Kamati ya Tawala za Mikoa pamoja na masuala yote, ambayo yalikuwa yanahu Shirika hili! Leo hii mtu anaposema kwamba; sijui Mheshimiwa Zungu pengine alikuwa wapi?

Hata watu wa Jiji la Dar es Salaam ambalo naamini Mheshimiwa Zungu ni Mjumbe, naye alipaswa kuwepo kwa sababu Jiji waliandikiwa na wao wote walikuwepo. Mkuu wa Mkoo wa Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Jiji na baadhi ya Wabunge wa Dar es Salaam, tumefanya kazi, Dar es Salaam pamoja na pia tumekuja Dodoma, baadhi Wabunge wa Mkoo wa Dar es Salaam, hawakushiriki kwenye suala hili. Sasa Kamati yako imeweza kulifanyia kazi suala hili, imeleta Bungeni. Kama ni kukosoa, wangeweza kukosoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja yangu ni nini? Tuitake Serikali, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ameeleza kwamba, Shirika la UDA linamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali, jambo hilo ambalo kisingi ukiliangalia kidogo, bado lina utata. Watueleze ili kusudi suala hili liweze kufikia tamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tulizonazo na kwa mujibu wa nyaraka mbalimbali ambazo zipo, ni kwamba Simon Group anamiliki asilimia 76 ya hisa za UDA. In case kuna taarifa nyiningine, basi waweze kulisaidia Bunge na pengine suala hili liweze kufikia tamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ajabu sana Bunge hili linakaa linafanya uamuji juu ya suala fulani, halafu kesho anakuja mtu mwingine, ambaye anaweza akawa na *interest* zake na haeleweki, jambo hili kwamba pengine limetokana na nini. Bunge lako litakuwa ni Bunge la ajabu! Maamuzi ya Bunge ni lazima yawe yanaheshimiwa! Hata kama yalikuwa ni mabovu, basi iweze kufanywa review na kuwe kuna hoja zenye ithibati kuweza kuangalia kwamba jambo hili limekuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushuru, mimi naishia hapa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Machali. Sasa namwita Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichanguie katika Wizara hii nyeti. Kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa timu nzuri aliyoipanga katika Wizara hii, na wengine tunategemea huenda hapo baadaye tukaona wakitusaidia katika nchi hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa tatizo ambalo mimi nalionna katika upelekaji wa fedha kwenye Wizara mbalimbali. Kumekuwepo na tatizo kubwa la fedha ambazo tunaidhinisha kama Bunge, kutotolewa kwa wakati kwenda katika Wizara mbalimbali na hatimaye kufanya kazi kama zile ambazo tumezipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ninaloliona hapa, jambo la kwanza ni kuandaa bajeti kwa kutabiri. Maana bajeti yetu tunatabiri tu kwamba mwakani tutaweza kukusanya kiasi hiki na tunabandika pale tunaaza kugawa hizo fedha, ambazo hatujawa nazo mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa, hujui una nini kwenye kapu, lakini wewe unaanza kuandaa bajeti.

Kwa hiyo, naomba, nishauri Wizara ya Fedha, ni vyema tukabadilisha utaratibu, badala ya *cash budget*, tukaanza kuwa na *capital budget*. Huwezi kuandaa kitu ambacho hujui may be kutatokea mafuriko, kutatokea majanga, lakini wewe umeandaa bajeti na unaitoa, matokeo yake haitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niongee kutokana na hili; kwa mfano Wilaya yangu ya Misenyi, imeathirika kutokana na bajeti kutotekelze. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bajeti ilikuwa imeandaa Shilingi milioni 93.6 kwa kuipeleka Wizara ya Afya na kuipeleka katika Wizara ya Afya na hatimaye ifike katika Jimbo la Nkenge, lakini matokeo yake, hatukupata hata senti tano. Fedha hizo ilikuwa Shilingi milioni 20 iende kukarabati nyumba tatu za Walimu, Shilingi milioni 40 iende kujenga nyumba za watumishi wa afya, Shilingi milioni 40 kujenga majengo mapya ya Kata ya Kagera na Mwemage na Shilingi milioni 50 kununua madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na bajeti ambayo haitekelezeki, hizi fedha hazikupelekwa hata senti tano. Matokeo yake, watu wanaugua, watu wanakufa, watu wanapoteza maisha, wanawake wanashindwa kwenda Hospitali kwa ajili ya kujifungua, wanashindwa kupata huduma nzuri za afya. Hivyo nilikuwa nashauri, ni vyema tuhame katika utaratibu wa *cash budget*, twende katika *capital budget*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niongelee kuhusu VICOBA kidogo. VICOBA maana yake ni *Village Community Bank*. Hizi ni mbinu zilibuniwa kwa ajili kusaidia watu wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe unatoka huko Dodoma ambako na mimi ndiko nilikoolewa, kule Mтанана. Unaangalia mtu wa chini hana uwezo wa kwenda kukopa Benki, hana uwezo wa kwenda kufanya lolote, lakini huu mfumo ni mzuri unaomwezesha hasa mwanamke katika kutatua matatizo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi VICOBA kwa nini visiингizwe kwenye utaratibu kama SACCOS ikatambuliwa na matokeo yake ikaweza kukopeshwa? Napenda nikueleze, katika Jimbo langu tuna VICOBA 375 na kila kimoja kimebeba watu 30. Watu 30 ukizidisha mara 375 unapata watu walioko katika mtiririko 11,250. Watu hawa wa akiba yao Sh. 985,000,000/=, lakini pesa hizi tumezipata kwa taabu mno! Tukienda kukopa tunaambiwa hatutambuliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapokuja hapa hebu njoo na utaratibu wa kuweka VICOBA katika system. Wanawake ndio waliomo katika VICOBA, na wanawake leo ndio wameshika familia, ndio wanaolea watoto, naomba tutambue VICOBA na hatimaye tuweze kumwinua mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa niongelee kidogo Benki ya Wanawake. Kwa kweli Benki ya Wanawake azma yake ilikuwa wanawake wengi wapate kunufaika na benki hii. Lakini ninachokiona kwenye hii Benki imetoka kwenye makusudio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kukopa katika Benki hii, lazima unahitaji kwenda na hati kama Kenya Commercial Bank, kama Benki ya NMB, sasa tofauti yake ni nini? Kwa nini tuwe na Benki ya Wanawake wakati haiwezi kusaidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri, tuweke dirisha katika NMB Banks zote ambalo litakwenda kutumia zile fedha zinazotoka katika Benki ya Wanawake ili wanawake walioko kule Nkenge, Kigoma na Tabora waweze kufanikiwa kupitia Benki hii. Lakini kitendo cha kunufaisha wanawake wa Dar es Salaam tu, hicho hakikubaliki. Kama haiwezekani, basi tuweke kitu kwenye Mfuko wa Maendeleo ili wanawake waweze kupata fedha za kuwasaidia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika nilichokuwa naomba zaidi kwenye Wizara hii, niongelee mapato yatokanayo na kodi. Malengo ya kukusanya kutokana na TRA yalikuwa yamekusudiwa Shilingi trillioni 10.4, na badala yake wamekusanya Shilingi trillioni 7.2 ambayo ni sawa na Asilimia 69.2. Hii imefanya bajeti yetu ishindwe kukamilika. Lakini ni nini kinachotokea TRA? Hawajaweka nguvu za kutosha katika makusanyo. Watu wengi wamekwepa kodi, na wanakwepa kodi, hakuna lolote linalotokea kwa mkwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali sasa ije na utaratibu, mtu anapokamatwa amekwepa kodi, adhabu yake ni kiwango gani? Kwa maana kama tutaweka kiwango cha kutosha...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Assumpter Mshama, nakushukuru sana...

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu, ni zamu yako kuchangia .

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba Wizara ya Fedha ina jukumu kubwa mahsusil a kusimamia uchumi wa nchi kwa ujumla. Wizara ya Fedha ndiyo inayosimamia mapato, ndiyo inayosimamia matumizi, ndiyo inayopanga au kutoa fedha ambazo zimeidhinishwa kwenda kwenye matumizi mbalimbali. Ili kutimiza majukumu yake Wizara ya Fedha inatakiwa iwe na sera maalum au Sera ya Bajeti na hivyo kuhakikisha kwamba bajeti yetu inatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikisimama hapa leo ili kuitendea haki Wizara ya Fedha na majukumu yake, inabidi niangalie maeneo ambayo Wizara ya Fedha inayosimamia kama yametekelezwa na hivyo tujue kama Wizara ya Fedha imefanikiwa ama la! Katika eneo la mapato, tunajua kwamba mwaka unakaribia kwisha na TRA hawajaweza kufikia malengo ya mapato. Japokuwa wamejitalidi lakini mapato ya kodi yatakuwa pungufu kama tulivoambiwa na taarifa mbalimbali za Wizara kwa takriban 7%. Maduhuli nayo yalikuwa yamechangiwa kwa takriban asilimia 44 tu ya matarajio hadi ilipofika mwezi Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunajiuliza, ni kwa nini matarajio ya mapato hayatekelezwi? Je, Wizara ya Fedha ina vyanzo vya kutosha vya mapato? Tunajua kwamba vyanzo vya mapato ni vingi na tumetoa ushauri mara kadhaa, lakini umekuwa haujatekelezwa. Kuna vyanzo vingi vya mapato ambavyo havijazingatiwa. Kwa mfano sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiuliza Wizara ya Fedha kwa nini hawachangishi kodi katika sekta isiyo rasmi? Wanasema kwamba sekta isiyo rasmi haijulikani iliko, wanasubiri mradi wa vitambulisho vya Taifa ili waweze kuwatambua wachangiaji wa kodi katika sekta isiyo rasmi. Lakini ukiangalia kwenye mradi wa NIDA wenyewe, hawajapewa fedha ya kutosha, na kwa hiyo, Wizara ya Fedha inajua kwamba suala la NIDA halitatekelezeka na kwa hiyo sekta isiyo rasmi itaendelea kuto kuchangia mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna mambo mengine ambayo hayahitaji kuwa na ramani ya Mitaa ndipo ukachange. Siku hizi tunajua kwamba watu wa DAWASCO kwa mfano wanatuletea bili za maji mpaka mlangoni, hivi wenyewe ramani ya walipa bili zao wanazipata wapi ambazo TRA hawawezi kuzitumia? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi imeendelea kuwa ni tatizo kubwa. Toka nimeingia Bunge hili tumeishauri Wizara ya Fedha wahakikishe kwamba misamaha ya kodi inapungua hadi kufikia asilimia moja ya pato la Taifa lakini mpaka wakati huu, miaka inazidi kwenda, bado misamaha ya kodi ni asilimia 3.1 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi ikiwa minge, inapunguza mapato ya Taifa. Matumizi yasiyofaa yakiwa mengi, yanapunguza mapato ya Taifa. Tumehoji mara nyigi suala la matumizi: Je, Serikali inatumia hela za walipa kodi katika matumizi yenye tija? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bajeti inayopitishwa inakwenda kwa matumizi yaliyolengwa? Kwa mfano, katika bajeti inayokwisha, ni matumizi mangapi yamekwenda kinyume na bajeti? Ni fedha kiasi gani zimetumika nje ya bajeti, hela ambazo zilikuwa hazijapangwa kwenye bajeti, hususan tukiangalia mfano wa fedha zilizotumika takriban Shilingi bilioni 24 kwenye Sherehe za Muungano, lakini kwenye kitabu cha bajeti cha mwaka huu unaokwisha fedha hizo hazionekani! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongelea miaka yote matumizi ya Serikali yasiyo na tija. Kwa mfano, tumeongelea suala la ununuzi wa magari ya kifahari. Katika nchi masikini kama

Tanzania, viongozi wanatumia magari mapya V8 yanayonunuliwa kwa bei ya zaidi ya Shilingi bilioni 280, hiyo ni sawa na Dispensary moja anatembea nayo kiongozi mmoja wa nchi. Je, Wizara ya Fedha ina sera gani ya kupunguza matumizi haya makubwa na yasiyo na tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa kuhusu deni la Taifa. Nimeangalia hotuba ya Kamati ya Wizara hii iliyowasilishwa leo ikieleza kwamba deni la Taifa limepanda kutoka Shilingi trilioni 21 hadi 29, na ni ongezeko la Shilingi trilioni nane tu kwa miaka saba. Sasa tunajuliza, kukopa ni sahihi, na nchi yoyote inakopa, lakini je, madeni na mikopo tunayokopa inakwenda kwenye fedha za maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwa mwaka huu miradi ya maendeleo, karibu miradi yote imepelekewa fedha chini ya asilimia 50, mbona ukuaji huu wa deni hauendani na fedha zilizokwenda kwenye matumizi ya maendeleo? Inawezekana basi tunakopa na tunaelezwa kwamba deni ni stahimilivu, lakini fedha kama haiendi kupunguza matatizo ya wananchi inakuwa haina maana ya kukopa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hazijaenda na wakati huo huo TRA tumesema kwamba wamekusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 90. Ndiyo kusema kwamba kuna reallocation na kuna fedha ambazo haziendi kwenye matumizi yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningeishauri Serikali, naona kwamba bajeti ya Serikali imekuwa haitekelezeki na siyo halisia, kwa sababu unapoanza bajeti ya mwaka bila kuonesha madeni uliyonayo unadhani kwamba madeni hayo ukija kutumia hela iliyoidhinishwa na Bunge la mwaka wa fedha unaohusika, ukazitumia kulipa madeni ya nyuma ambayo hukuyaonesha, definitely utashindwa kumaliza bajeti ya mwaka wako. Kwa hiyo, naitaka Serikali, kila tunapomaliza mwaka, kwa mfano ikifika tarehe 30 Juni Serikali itueleze ina madeni kiasi gani na madeni hayo yatazingatiwaje katika mwaka unaofuata wa fedha ili yatengewe fedha?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Tunakushukuru sana. Dakika haziko upande wetu. Sasa namwita Mheshimiwa David Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia Wizara hii muhimu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu pengine ya muda ni finyu sana, naomba niende moja kwa moja kwenye suala la mafao ya wafanyakazi wa uliokuwa mgodi wa chumvi Uvinza. Namwona Mheshimiwa Waziri anasikitika!

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wafanyakazi walistaafishwa wakati mgodi unauzwa mwaka 1998, mpaka leo hawajalipwa mafao yao. CHC walifanya uchunguzi, wakathibitisha kwamba madai yao ni genuine; wanadai takriban Shilingi milioni 340. Tangu mwaka 1998 mpaka leo wameshafariki takriban robo ya wazee wote ambao walikuwa wanadai mafao yale; na pesa yenye ni kidogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wamefanya kazi miaka 30, mafao yao ni Sh. 900,000/=, kuna watu walifanya kazi miaka 20 mafao yao ni Sh. 600,000/=, kuna watu walifanya kazi miaka 15, mafao yao ni Sh. 400,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kwa kweli ifike mahali Serikali iwe na huruma. Hawa wafanyakazi takriban 280 wanadai Shilingi milioni 340, ni kama wastani wa Shilingi milioni moja na kidogo kila mmoja. Kwa hiyo, naomba kabisa, kwa msisitizo kabisa, tuisubiri mpaka wazee wote hawa wafe ndiyo pesa hii itoke. Natambua Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake ni wapya na jambo hili wanalfahamu vizuri. Ni matarajio yangu kwamba mtalipa uzito wa kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza kwa msisitizo, ni kwamba tuna changamoto kubwa sana ya Serikali kushindwa kukusanya mapato yake. Ni maoni yangu kwamba tufike mahali sasa tuwe na mkakati mkubwa wa kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo fedha haikusanywi inakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nimetoa taarifa mara kadhaa tangu mwaka wa juzi; Mgodi wa Mwadui, wa almasi pale, tangu tupate uhuru mwaka 1961 wanasema wanapata hasara, kwa hiyo, hawalipi kodi. Kama wanapata hasara kila mwaka, kwa nini hawendi kwao? Ifike mahali walipe kodi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza mara kwa mara hapa, kwamba kuna umuhimu na kuna kila sababu ya Watanzania kushiriki kwenye uchumi wa nchi yao. Moja ya eneo ambalo linafanya Mtanzania ashiriki kwenye uchumi wa nchi yake, duniani kote huwa ni masoko ya mitaji (*stock markets*). Soko la Mitaji Tanzania (DSE) pale limeanzishwa mwaka 1996, kwa malengo ya kwamba viwanda vyote ambavyo vinauzwa takriban 336 viwe *listed* kwenye *stock market* ili kusudi Watanzania washiriki kwenye uchumi wao. Lakini kati ya viwanda 336 ambavyo vilibinafsishwa ni viwanda saba tu; ni mashirika saba peke yake ambayo yako *listed* kwenye *stock market*. Hii tafsiri yake ni kwamba tunawanyima fursa wazawa kushiriki kwenye uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Benki kwa Tanzania, leo ni sekta kubwa sana. Tanzania ni nchi inayoongoza kwa idadi kubwa ya Benki katika nchi zote za SADC, lakini bado Sekta hii ya Benki imekuwa haina manufaa kwa Taifa hili. Riba bado ziko juu na zimekuwa ni vichochoro vyta *money laundering*, ndiyo vichochoro vyta utoroshaji wa fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya njia ya kisayansi ya kuzifanya hizi benki zifanye kazi yake, ni kuzishinikiza benki hizi ziwe *listed* kwenye *stock market*. Benki hizi zikiwa *listed* kwenye *stock market* maana yake mahesabu yake yote yatakuwa wazi; maana yake tutapata uwazi wa kuhusu benki hizi. Hii ni moja ya njia ya kuifanya Serikali ipate kodi sahihi kutoka kwenye benki hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujifunze Sri Lanka, tujifunze Nigeria, *financial institution* zote ziko *listed* kwenye *stock market*. Moja ya sababu ni hiyo, tupate uwazi, tupate kodi, lakini ushiriki wa jamii hii kwenye uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nisisitize, ni makampuni ya simu na makampuni ya madini. Tangu mwaka 2010 ilipitishwa Sheria ndani ya Bunge hili kwamba migodi na kampuni za simu zinapashwa kuwa *listed* kwenye *stock market*.

Malengo ni kwamba Watanzania washiriki kwenye uwekezaji wa madini na kwenye Sekta ya Simu. Sekta ya Simu leo hii ni sekta kubwa sana. Wanatengeneza fedha nydingi, lakini

wamegoma ku-list hisa zao kwenye stock market. Madhara yake ni kwamba Serikali sasa inakosa kujua kwa uhakika kiasi ambacho Makampuni haya yanapata.

Faida ya ku-list kwenye stock market ni hiyo, kwamba yakiwa *listed* pale Serikali itajua kiasi sahihi ambacho makampuni ya simu na migodi yanapata. Mkijua kiasi sahihi ni rahisi kujua kodi yenu sahihi.

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri sana hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zambia pale wana kampuni ambayo inaitwa ZCCM. Ile kampuni ile ina takriban wananchi 1,500,000...

TAARIFA

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Mwjjage!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ulindwe!

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mdogo wangu, kwamba baada ya kuona kwamba watu wa migodi, kama uliwatolea mfano, hawalipi ushuru au kodi, kilianzishwa kitu kinaitwa *alternative tax*, na *Williamson Diamond* wamelipa Shilingi milioni 178 chini ya uongozi wa yule jamaa anayeitwa Profesa Muhongo. (Kicheko/Makofi)

NAIBU SPIKA: Unaipokea hiyo taarifa Mheshimiwa Kafulila! Kifupi!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasikitika sana kwamba hii taarifa ya ndugu yangu msomi kabisa, siwezi kuipokea kwa sababu mgodi huu una-*multi billions* of Shilings. Shilingi milioni mia moja ni kiduchu ndugu zangu!

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, Zambia kuna kampuni ambayo, kama TPDC yetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda tayari hauko upande wako Mheshimiwa Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Aaaaaah!

NAIBU SPIKA: Samahani sana, muda umwekwisha. Mkiangalia saa yetu pia, muda umekwisha.

Wale ambao nina majina yenu kwenye orodha, msiwe na wasiwasi mtapata nafasi leo jioni. Yupo Mheshimiwa Roman Selasini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Ally Keissy,

Nakala ya Mlango (Online Document)

Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Rage, Mheshimiwa Masele na wengine, jioni tuwahi tu.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna Mbunge ameokota funguo ya gari tunaomba atuleee meza kuu hapa kwa Makatibu.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba kuna orodha ya nyongeza ya shughuli za leo, imepitishwa huko. Kama hamjaipata mtaipata baadaye kidogo. Jioni tutaifanyia kazi hii nyongeza, ni kwa ajili ya kusomwa mara ya kwanza Miswada ya Serikali ambayo tutaishughulikia siku zijazo, lakini tutaifanyia kazi jioni ya leo.

Tangazo la mwisho ni taarifa ya uchaguzi, na hapa naomba mnisikilize vizuri Waheshimiwa Wabunge. Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tutakuwa na chaguzi mbalimbali hivi karibuni sana, ambapo wale ambao mtapenda kushiriki katika uchaguzi huo mnaombwa mkachukue fomu kwa Katibu wa Bunge kuanzia leo tarehe 4 Juni, na Mwisho wa kurejesha fomu hizo ni Jumapili tarehe 8 Juni, saa kumi jioni. Kuanzia leo tarehe 4 - 8 Juni kurudisha fomu kwa Katibu wa Bunge.

Nafasi ambazo zitafanyiwa chaguzi mbalimbali na category nne. Kundii la kwanza, Wajumbe wa Bodi na Mabaraza ya Vyuo Vikuu nchini. Pia atachaguliwa mwakilishi kwenye Jumuia ya Mabunge ya nchi za Kusini mwa Afrika SADC-PF. Pia patakuwa na uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge. Hii ni kuziba nafasi zile ambazo zilikuwa zimejitokeza.

Hii nafasi ya Tume ya Utumishi ni nafasi ilioachwa na Mheshimiwa Zambi, kwa hiyo, inabidi kuiziba; hii ya SADC PF nafikiri alikuwa ni Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuu, Mheshimiwa Dkt. Kamani. Vyuo Vikuu pia zime-expire muda wake. Kwa hiyo, wale ambao wana interest, tarehe 4 – 8 Juni, Jumapili saa 10.00 jioni ndiyo mwisho wa kuchukua fomu hizo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda hauko upande wetu, basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 leo jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Selasini, anaafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, niseme tu kwamba ungelinipa nafasi asubuhi, nisingesema haya ninayotaka kusema sasa. Lakini baada ya kupata nafasi ya kwenda Kanisani mchana, sasa nataka niseme haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa na ninaishangaa sana Serikali. Kwa nini Serikali kila mara imekuwa ikitengeneza mianya ya migogoro? Kwa nini Serikali kwa makusudi mazima inajitafutia nafasi za kulaumiwa, kushutumiwa na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu, suala la UDA, linatia kichefuchefu. Linatia kinyaa, kwa sababu jambo hili liko katika vinywa vyetu, tangu mwaka 2011. CAG, ametengeneza taarifa yake, yale mapendekezo ya CAG, baadhi yametekeliza,

baadhi hayajatekelezwa. Pendekezo kubwa katika Ripoti ya CAG, ni kuhusu thamani ya Hisa ambazo zilikuwepo kwa ajili ya ile Kampuni ya UDA, ambazo Simon Group, alizinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu aliunda Tume, na ile Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu, ilifikia uamuzi kwamba value za zile hisa zitazamwe upya. Ikaundwa Kampuni ya Kimataifa, KPMG, na ikaleta valuation mpya ya zile Hisa.

Nilichokigundua baada ya kutoka hapa asubuhi, ni kwamba tofauti ya thamani ya Hisa, kama zilivyopendekezwa na KMPG na CAG, illipwa na Simon Group. Sasa hoja iliyopo na mshangao ambao mimi Napata, ni kwa nini Serikali haitaki kukaa na kumaliza huu mgogoro? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovypote vile ambavyo mtu ye yeyote ataelewa, ni kwamba hapa kuna kitu! Hapa kuna harufu mbaya! Nami ndiyo maana nikasema, nilipotoka Kanisani, nimikuja na mtazamo tofauti kwa sababu harufu mbaya kwangu mimi ni dhambi. Serikali imesema hapa haitambui Kampuni ya Simon. Serikali hii hii ndiyo inayoipa udhamini mabenki kukopa, Serikali hii ndiyo iliyopia exemption ikaingiza mabasi juzi!

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Dar es Salaam wanachokitaka siyo malumbamno ya humu ndani; kati ya akina nani wanaouna mkono Kampuni ya Simon, au akina nani wanaunga mkono Serikali wala kundi lolote? Wananchi wa Dar es Salaam wanataka usafiri rahisi na wa bei nzuri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe ushauri kwa Serikali. Hili jambo haliwapi sifa yoyote. Kwa sababu mateso ambayo wanayoyapata wananchi wa Dar es Salaam kutokana na adha ya usafiri, finally yataleta lawama Serikalini.

Mimi naipa ushauri Serikali, mkae mtatue huu mgogoro; na ushauri mmeishapata wa kutosha! Tunataka mtuambie leo hapa, namna mnavyokwenda kutatua huu mgogoro. Kwa sababu kila mtu anayeangalia huu mgogoro, anaona tu kuna conflict of interest baina ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika mahali siyo kwamba Serikali mnadhalilika tu, mnatudhalilisha hata sisi Wabunge. Kwa sababu leo hii Mbunge utakayechangia kwa maslahi ya nchi, unaonekana kwamba unachangia kwa namna fulani tofauti. Kwa hiyo, ili kuondoa uzalilishaji huu, Serikali tunataka leo mtupe tamko huu mgogoro unamalizika namna gani, ili wananchi wa Dar es Salaam wapate usafiri mzuri na wa bei rahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu madeni. Tumepitisha Bajeti hapa, lakini kila Wizara ina madeni ambayo ambayo hayajazingatiwa kwenye Bajeti, na matokeo yake ni kwamba utekelezaji wa Bajeti unakuwa ni mgumu.

La pili, tumepitisha bajeti hapa. Kila Wizara imetengewa fedha kwa ajili ya Utilities; umeme maji na kadhalika. Hakuna Wizara inayolipa! Madeni mengi ukienda kwenye Mawizara ni ya umeme, Maji, na hadi sasa tunashuhudia Vituo vya Polisi vinakatiwa umeme, Magereza yanakatiwa maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa, Wizara itengeneze utaratibu wa kuwashughulisha Maafisa Masuuli. Kwa nini hizo pesa tunazipitisha hapa Bungeni katika Bajeti, lakini zikifika kwenye utekelezaji hawalipi? Kwa nini Hazina pesa hizo kama zimeshapitishwa zisipelekwe? Matokeo yake ni nini? Tunaua Mashirika mengine. Tunaua Makampuni ya Maji, TANESCO inashindwa kufanya kazi na tunaua Makampuni ya Simu.

Kwa hiyo, ifike mahali Hazina au Serikali ije na utaratibu wa kuwachukulia hatua Maafisa Masuuli ambao hawalipi hizi pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofisi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ninakushuru Mheshimiwa Joseph Selasini. Namwita Mheshimwia Dunstan Kitandula, atafutiwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuweza kutoa mchango wangu kwa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza, Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia mradi wa kutoa mikopo kwa Wajasiriamali wadogo yaani SELF. Wamefanya kazi kubwa na mradi ule unaendelea kutupa heshima katika Taasisi za Kimafaifa ambazo zimekuwa chachu ya kutoa mikopo kwa shughuli hizi za kuwasaidia Wajasiriamali. Lakini pamoja na pongezi hizo, zipo changamoto ambazo nilidhani ni vizuri niziseme ili tuondokane na matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010 Serikali iliingia makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuanzisha Awamu ya Pili ya Mradi wa SELF. Katika makubaliano yale, Benki ya Maendeleo Afrika ilikubali kutoa mkopo wa masharti nafuu wa takriban Shilingi bilioni 44. Leo hapa kwenye hotuba ya Waziri ametueleza jinsi Mradi wa SELF unavyofanya vizuri.

Katika mwaka huu tayari wamekwisha toa takriban Shilingi bilioni tisa kwenda kwa wajisilimamali. Hili ni jambo la kuwapongeza. Kwa sababu tunajua wote penetration rate ya kutoa mikopo kwa Taasisi na wananchi kule vijiji, iko chini sana. Kwa hiyo, tunapokuwa na Mradi unaofanya vizuri kama huu, ni jambo la kupongeza. Lakini tatizo lilopo hapa ni kwamba tulipoingia makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika, yapo mambo ambayo tulikubaliana yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza lilikuwa ni kwamba, kabla ya kufika mwaka 2015, mradi ule uwe umekuwa transformed, kuwa independent institution. Katika kufanya hivi, ndipo ambapo tunaweza kupata tranche ya pili ya fedha zile kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa tunapozungumza, jambo hili halijafanyika. Mwaka 2015 ni mwaka kesho tu. Nachelea kusema kwamba tunaweza kujikuta tunapoteza fedha zile, au tukaingia katika orodha ya nchi ambazo zimeshindwa kutekeleza miradi kwa wakati, jambo ambalo katika scoring ya miradi ya nchi, lina athari ya kufanikiwa katika miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naisihi sana Serikali, kwa sababu mwaka 2013, nilipouliza tuliambiwa kwamba unaandalifu waraka wa kwenda kwenye Baraza la Mawaziri ili jambo hili likamilike, lakini mpaka leo waraka ule haujaingia kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji maelezo kwamba waraka ule utaingia lini ili tuweze kulimaliza jambo hili. (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Benki Kuu ndiyo iliyokuwa inasimamia shughuli za Micro Finance, lakini takriban miaka minnem mitano iliyopita, Benki Kuu ilijitoa kwenye kusimamia Taasisi ambazo hazichukui dhamana. Maana yake ni nini? Maana yake usimamizi wa Taasisi hizo sasa hakuna anayeufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliona hili, Benki ya Maendeleo ya Afrika wakati inaingia makubaliano na Serikali, ilikubaliana na Serikali kwamba tuanzishe kitengo cha kusimamia taasisi za Kifedha pale ndani ya Wizara ya Fedha. Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikuwa tayari imekubali kugharamia uanzishwaji wa kitengo kile. Mradi unafungwa mwaka 2015, mpaka leo hatujaanzisha kitengo kile. Siyo sahihi, nadhani hatufanyi vizuri. Naiomba Serikali itupe majibu, ni lini kitengo kile kitaanzishwa kwa haraka ili tusiweze kupoteza fursa hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tunalizungumza kwa sababu tunaonu uzoefu. Huko kwenye masoko, kwenye operation huko Taasisi zinajijendea zinavyotaka. Matokeo yake wananchi wanatozwa riba kubwa na hakuna chombo kinachosimamia kuangalia kwamba wananchi hawapati matatizo. Tunataka chombo kile kianzishwe kwa haraka ndani ya Wizara ile ili kuweza ku-regulate Micro Finance Institution katika nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hili kwa sababu tunaona mifano. VICOBA imeshika kasi katika nchi yetu, lakini mpaka leo hii hakuna sheria mahsus ya kusimamia Taasisi ile. Tunacheza na fedha za wananchi, tutakuja kupata matatizo kama ya DECI, halafu tutakuja kunyooosheana vidole. Nafikiri wakati umefika tuhakikishe kwamba mifumo hii inawekwa ili kuwaepushia Watanzania matatizo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba urasimu uondoke, tuyafanye haya kwa haraka, tusije tukaingia aibu kama ile iliyotukuta kule Arusha, kwamba tumeshindwa kutoa ardhi, kwa ile East African Business Council kwa miaka 10. Matokeo yake, Taasisi ile ile imehamishiwa Rwanda. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuachane na urasimu. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Agustino Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Filikujombe.

MHE. AGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii adimu ili name niweze kutoa mchango wangu katika hii Wizara nyeti katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, nikiwa kama Mbunge wa Wilaya mpya kwenye Mkoa mpya wa Geita, Jimbo langu la Mbogwe, tunalo tatizo la Benki. Wilaya yetu hiyo ni mpya, watu wapo, wanafanya biashara, wanahitaji Taasisi za kifedha kama Benki hasa katika Miji inayokua kwa haraka kama vile Mjini wa Masumbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Masumbwe, una wafanyakishara wengi wakubwa, lakini hawana huduma ya Benki. Mji kama Lulembela ni Mji unachipua kwa haraka, nao unahitaji huduma ya Benki; na kwa wananchi wa kawaida katika maeneo mbalimbali katika Jimbo la Mbogwe tuiombe Wizara ya Fedha itufanyie wepesi ili basi wananchi wa Mbogwe waweze kupata huduma ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kwamba Wilaya yetu haina majengo ya Ofisi za kufanya kazi katika Halmashauri, hata Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hatuna. Basi tunaomba, maana katika mwaka wa fedha uliopita ambao ndiyo tunaumaliza sasa hivi, tulitaraji kwamba pengine tungepewa fedha ili tuenze ujenzi wa Ofisi hizi lakini hatukuweza kufanikiwa. Basi naomba katika mwaka huu wa fedha, Serikali ione umuhimu wa kutupatia fedha hizo ili ule mpango wa Serikali wa kusogeza huduma kwa wananchi uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie, ni utaratibu ambao kidogo unaleta matatizo katika utekelezaji wa shughuli katika Halmashauri.

Kuna kitu kinachoitwa *Exchequer Notification*, nazo hizi zinakuwa zinaleta matatizo kwamba wakati mwingine, *Exchequer Notification* inakwenda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ikieleza kwamba jamani eh, Wilaya fulani imepatiwa fedha kiasi fulani. Lakini ukienda kwenye Halmashauri husika hela hizi huzikuti. Matokeo yake kunakuwa na mkanyanyiko, hatuwezi kuelewa kwamba fedha hizi kweli zilitoka au hazikutoka; na kulitokea nini? Kunakuwa hakuna ufanuzi. Jambo kama basi wenzetu wa Hazina na Wizara ya Fedha waliangalie. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu fedha hizi hasa noti. Shilingi mia tano, Shilingi elfu moja na Shilingi elfu mbili. Ubora wake unatia mashaka kwa sababu zinachakaa kwa haraka sana. Sasa sijajua Wizara na Wataalam mbalimbali wa masuala ya fedha, wanalionaye jambo hili? Mimi naomba basi uchunguzi ufanyakike ili kuweza kujua kuna tatizo gani katika utengenezaji wa hizi noti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na masuala ya pension kwa watu ambao wamestaafu siku za nyuma, ambao kwa kweli pension zao ziliwa ni za kiwango cha chini sana, ambacho mpaka sasa hivi, hakiwezi kuwasaidia katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, unamkuta mtu anapata pension ya Sh. 20,000/= kwa mwezi. Kwa kweli, tuiombe Serikali iwatazame watu hawa ili malipo wanayoyapata yaendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni kuhusiana na hizi hati za kimila za umiliki wa ardhi. Wananchi, wakulima wa vijiji huko wamekuwa wakipewa hizi hati ili ziweze kuwasaidia pengine katika kupata mikopo ambayo ingeweza kuwasaidia kuwaboreshea maisha. Lakini inavyonekana ni kwamba Benki haizipokei hizi Hati za Kimila. Naiomba basi Serikali ione uvezekano wa kuweza kuona kile kipingamizi ambacho kinajitokeaza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. AGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Agustino Masele kwa mchango wako. Kama nilivyosema, sasa namwita Mheshimiwa Deo Filikunjombi, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi nataka kwanza nitambue kwamba katika Wizara zote tulizonazo, tuna Wizara zaidi ya 25, lakin Wizara ya Fedha ni Wizara mama, ni Wizara nyeti na ndiyo moyo wa Serikali yetu. Ndiyo maana Katibu wake Mkuu wa Wizara ya Fedha, ni Katibu Mkuu pekee ambaye ana majina mawili. Makatibu Wakuu wengine wote, wanaitwa Makatibu Wakuu; lakin Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anaitwa pia PST; vyote ni vyeo vyake Paymaster General. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nimekuwa Mbunge nimegundua kitu kimoja; sisi Wabunge tunakuwa wepesi sana kwenda kwenye kuhojji kwamba fedha ni kidogo. Kwetu sisi Bajeti imekuwa ni kugawana. Keki imekuwa ni ndogo, sungura amekuwa ni mdogo; ndiyo yamekuwa ni majibu ya Mawaziri. Lakini baadaye nimekuja kugundua kwamba kumbe Bajeti

siyo kugawana peke yake, Bajeti pia ni revenue, yaani Bajeti pia ni mapato pia. Hapa ndiyo msingi ambao nataka tuweke msisitizo. Bila kuwa na inflow kubwa, hatuwezi kuwa na outflow kubwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana pengine sasa tu mkazo uwe kwenye kukusanya mapato kwenye revenue. Sisi Wabunge tuwe sehemu kwanza ya kukusanya; tuisitiza Hazina, Wizara ya Fedha wawe na fedha na baada ya hapo ndipo tuwalaumu kwamba kwa nini fedha hizi hamleti na kwa nini fedha hizi hampeleki?

Nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale, kwanza namwonea huruma, ni mama; nataka nimshambulie, sasa... (Kicheko/Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba sisi kama Wabunge tuisaidie Serikali, tuisaidie hii Wizara ya Fedha kukusanya. Leo Ludewa tunajenga barabara ya lami ya kilomita 50, lakini barabara ya kutoka Njombe - Lulewa mpaka Mali ni kilomita 200. Nilipomfuata Katibu Mkuu na Waziri wa Ujenzi kwamba naomba mniongezee wakasema fedha haitoshi. Nikakumbuka, kumbe huu ndiyo wajibu wangu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Wabunge wenzangu kwamba naomba sana turekebishe Sheria ya VAT. Tuna misamaha mingi ya kodi bila sababu ya msingi. Tumeacha nchi hii sasa hivi, wanaolipa kodi ni watumishi wa Umma, yaani wafanyakazi peke yake. Hatuwezi kuacha Serikali ijiendeshe kwa PAYEE. Wanaolipa kodi ni wafanyabiashara wadogo, Wamachinga, ndio hao wanaosumbuliwa na wafanyakazi wa Serikali, lakini wafanyabiashara wakubwa hawalipi kodi. Sisi Wabunge tuwe sehemu ya kuisaidia Serikali ikusanye kodi. (Makof)

Mimi nina mfano mmoja mdogo, mwaka jana peke yake, watu watatu peke yake wamepewa exemption ya Shilingi bilioni 94 na bahati mbaya mmoja kati ya wafanyabiashara hao yuko humu humu ndani. (Makof)

MBUNGE FULANI: Nani huyo?

MHE. DEO. H. FILIKUNJOMBE: Sasa hebu tubane, sitaki kumtaja!

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufike mahali tuisaidie Serikali, tuisaidie hii Wizara kwanza wakusanye fedha za kutosha; haiwezekani tuwe tunasamehe Shilingi trilioni moja na nusu kama misamaha ya kodi. Asilimia tatu, tunapitiliza mno! Misamaha hii, tumeitunga sisi Wabunge, tumeipitisha sisi Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi, rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola aliomba mwongozo wa kwa nini Serikali haitaki kuleta Sheria ya Mabadiliko ya VAT? Msipoleta Muswada huu, kwa kweli na mimi nitakuwa mbaya. Msipoleta Muswada huu tutapambana! Siwezi kuwaelewa! Nitaona ninyi wahusika, Serikalini mmekuwa Mafisadi, mnashirikiana na wafanyabiashara wakubwa kuhakikisha kwamba mambo hayaendi.

Mheshimiwa Lukvi uliahidi hapa siku ile, Umma ulikuona! Ndiyo! Uliahidi hapa, uko hapo! Ule Muswada uje tuurekebishe! Hatuwezi tukawa tunasamehe! Wafanyabiashara wakubwa walipe kodi. Hatuwezi kumlaumu Waziri kila siku kwamba haleti fedha, yule Waziri wa Fedha atoe wapi? Atoe fedha yake mfukoni? Nimeona kwenye vitabu humu, ndiyoi! Kuna Wizara zimepelekewa 14% tu ya tulichopitisha. Hebu tuisaidie kwanza kwenye makusanyo, baada ya hapo ndiyo twende mbele. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma takwimu za TRA, TRA wanaonyesha kwamba wao wanakusanya *beyond target*. Lakini PAC tumekaa na TRA; hii Mheshimiwa Waziri nataka unisikilize kwa umakini sana, sijui kama unanisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA kwenye ku-set malengo, wanajiwekea malengo wao wenyewe. Hili ni tatizo! Hili ni tatizo kubwa! TRA kuwe na Bodi *independent* ya nje kabisa ya kuweka malengo. TRA kama wanaona uwezo wa kukusanya kodi ni triliioni nane, wataweka malengo triliioni saba. Kwa hiyo, kwenye kukusanya, wanapitiliza *target*, kitu ambacho siyo kweli! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa nyingi! Mimi naamini pale mmepeata DG mpya, Ndugu Kitilya ametufikisha pazuri; mahali tulipofika ni pazuri, lakini tunataka kwenda pazuri zaidi. Ndugu Rished Bade unaweza; ukifanya ya Kitilya peke yake, hutang'ara. Tunataka Rished Bade ukusanye fedha nyingi, fedha zije hapa na fursa zipo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la UDA tuliliibua sisi POAC wakati ule. Watu wamepelekana Mahakamani, yaliyojiri huko yanajulikana.

Ni bahati mbaya sana Serikali huwe haipendi kufanya maamuzi, lakini maamuzi ya Mahakamani yametoka. Mnayutana sasa hivi! Tunawaambia na tumewaandikia, Msajili wa Hazina tunapitia hesabu zake na Wizara ya Fedha tunapitia hesabu zake. Ni bahati mbaya Wabunge tunalumbana bila sababu ya msingi, tuheshimiane kama Kamati. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mimi ningependekeza ifuatavyo: Kamati pekee yenyе kuweza kupitia ubinafsishaji, *shareholding structure* na hesabu za Serikali za Mashirika ya Umma ni PAC. Naomba suala hili liende kwenye Kamati husika, hesabu zake zipitiwe, tutaleta mapendekezo kwenu, suala hili na limalizike. Haiwezekani kila siku watu tunalumbana juu ya UDA kama vile hakuna mambo mengine ya kufanya. Kila siku UDA, UDA, haiwezekani!

MBUNGE FULANI: Kamati za UKIMWI zinazungumzia UDA!

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Kamati za UKIMWI zinazungumzia UDA! Sasa sisi tunashangaa, hiki ni kitu gani? Kwa hiyo, naomba hebu tufike mahali Serikali ilimalize suala hili na kama mnashindwa, basi lije PAC tuta-review, tutaleta mapendekezo suala hili limalizike. (Kicheko/Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, rai yangu kwenu, tuisaidie Serikali kwenye mapato; tuwasaidie wenzetu, tumsaidie Waziri wa Fedha akusanye fedha nyingi. Mimi napenda kuona wanafunzi wanapata fedha za mikopo, barabara yangu ya Ludewa inajengwa mpaka inamalizika, lakini bila mapato tutamlamu Waziri wa Fedha bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba Waziri wa Fedha una Manaibu Waziri wazuri wa kukusaidia, shirkiana nao na sisi Wabunge tutakuwa pamoja na wewe.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja! (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Kama nilivyosema, sasa namwita Mheshimiwa Said Mussa Zubeir. Mheshimiwa Said Mussa Zubeir! Hayupo eh! Basi tunaendelea na Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Ally Keissy ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Deo aliyemaliza kuzungumza sasa hivi kuhusu suala la UDA. Tunaomba Serikali imalize jambo hili, itoe kauli inayojulikana. Ni mbaya sana kwa Waheshimiwa Wabunge kuanza kushutumiana humu ndani kwa sababu itaondoa hata *integrity* ya Bunge lako Tukufu na Bunge litakosa nafasi yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tukianza kurushiana maneno kwamba wewe hivi, umeletwa hivi, umefanya hivi, italeta matatizo. Tukikubali kulea migogoro jamii haiwezi kustawi. Serikali ifanye maamuzi ili hili jambo liishe na ikishindana lipelekwe kwenye Kamati ya POAC ifanye kazi yake. Kwa sababu inaonekana jambo hili lilishawahi kuletwa mpaka na Kamati ndani ya Bunge, maamuzi yakafanyika na Hansard zipo. Sasa kunakuwa na kauli za kutatanisha. Ukweli utatuweka huru! Ukweli ujulikane, haki ipatikane na heshima ya Bunge iendelee kuwepo! Tasisababishe migogoro ya kurushiana makombora wenyewe kwa wenyewe, heshima yetu itaondoka na sasa tutakosa *integrity*, tutakosa uadiliu katika jamii, tutashindwa kuisimamia Serikali kwa sababu labda na sisi tuna take upande mmoja au mwengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo sahihi kifanye kazi yake kama ni Serikali, wawekezaji na Treasury wakae ili hili jambo limalizike, uwazi ujulikane na ukweli na haki itendeke, tutakuwa tumemaliza jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge chonde chonde, tuchunge kushutumiana, hakuna kitu kibaya kama kushutumiana au hisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nizungumzie kuhusu riba. Suala la riba kwenye mabenki yetu ni kubwa sana. Ni-declare interest kwamba mimi ni Mbunge, nimekopa. Ukitoka Shilingi milioni 200 kwa *interest* ya asilimia 16 ni kwamba kwa mwaka ni Shilingi milioni 32. Sasa Mbunge labda ametoka kwenye kampeni hali ndiyo iko hivyo akaona ile Shilingi milioni 200 ina maana sana, lakini kuja kulipwa imekuwa ni maumivu makubwa sana. Ndiyo maana unakuta leo hii hata Waheshimiwa Wabunge wamechoka kwelikweli kwa sababu *interests* hizi ni kubwa sana! (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani *inflation* ishuke kutoka asilimia 19; yaani mfumuko wa bei ushuke kutoka asilimia 19.8 mpaka 6%, lakini riba bado ibaki palepale au inakwenda juu zaidi. Hii inawanyima hata nafasi wafanyakazi wa kawa, Walimu, Wajasiriamali, Wafanyabiashara wadogo wadogo wanakwendaje kukopa kwenye mabenki haya katika *interest* ambazo ziko juu kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara inasimamia Sekta hii ya Mabenki, tuangalie namna bora ya kuweza kusaidia hili tabaka la katililiweze kuwa na nafasi ya kukopa na kuwa na riba sahihi ili waweze kukuza mtaji, kuongeza ajira na kustawisha Taifa la Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wewe ni Mbunge, address yako inajulikana, Bunge hili linajulikana, lakini bado ukikopa benki inakwambia *risk* ya kurudisha huo mkopo, unapigwa *interest* ya 16%! Haya ni maumivu makubwa sana!

Kwa hiyo, utakuta katika hali ya namna hii haiwezi ikasaidia, address zinajulikana na mambo ya namna hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utakuta waliokopa Shilingi milioni 200 labda ni Wabunge, at the end of the day baada ya miaka mitano watakuwa wamelipa karibu riba ya zaidi ya Shilingi milioni 80 mpaka Shilingi milioni 100. Sasa hiyo ni biashara ya ajabu kweli kweli! Kwa hiyo, lazima hilo liangaliwe kwa umakini wa hali ya juu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la wastaafu. Ni kweli wapo wastaafu baada ya mwaka 1999, kwa mfano, Ma-general wa Jeshi. Kulikuwa na taarifa kwenye vyombo vya habari, mtu kama General Sarakikya yaani pensheni yake kwa mwezi ni Sh. 50,000/=, na huyu amelitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa. Leo hii mwangalieni Balozi Hashim Mbita, yuko kwenye hali ya masikitiko makubwa sana kutokana na pensheni anayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Marehemu Apio wakati ule alikuwa Waziri Kiongozi, lakini alitolewa kule kwenye hali ambayo ni ya kusikitisha, Mwenyezi Mungu amweke mahali pema! Jamani Wazee walitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa kiasi hicho, leo hii tunawaweka namna gani? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hai, ni-declare interest kwamba Baba Mkwe wangu, Sylvester Barongo, ndiye mwanzilishi wa Shirika la TPDC, amekuwa Mkurugenzi pale na Mwenyekiti kwa miaka 23 ameijenga TPDC tunayoisema leo hii. Leo hii miezi sita tunampa kiinua mgongo au pensheni ya Sh. 480,000/= kwa mwezi, yaani kwa siku tunampa Sh. 2,000/=. Ametumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa! Mkiizungumza TPDC, mniamzungumzia Sylvester Barongo; Mheshimiwa Mwando sya unamjua, ni rafiki yako wa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu fikiria per diem ya Mbunge ndiyo pensheni ya Sylvester Barongo kwa mwezi mzima, haki iko wapi? Inasikitisha sana! Sasa huyu alikuwa kwenye level ya Mkurugenzi; nyumba yake anashindwa kupaka rangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo tusipoyafanya kwa uadilifu, tusipotenda haki, leo tuna nafasi ya kufanya maamuzi; ni bora tukafanya maamuzi leo, tuisubiri kesho. Tukishindwa kufanya maamuzi leo, kesho tutaanza kulia kwamba laiti ningelijua, laiti ningelijua!

Mheshimiwa Waziri, tufanye maamuzi leo tuisubiri kesho! Marehemu Mama yangu aliniambia kamwe kichaka kilichokuhifadhi usikitie moto. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia. Kama figure uliyotaja ndiyo pensheni anayoipata General Sarakikya, ni hatari! Inabidi jambo hilo liangaliwe kwa kweli! Sasa namwita Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Kawawa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii siyo masikini. Tulidai uhuru ijitegemee. Hatukudai uhuru asilimia 40 kupata kwa wafadhili au kwa Wazungu. Mpaka Wizara ya Maji inapata asilimia 32, Wizara ya Afya asilimia 25; sasa ndugu zangu Wazungu wakikataa kutusaidia, ina maana wananchi watakuwa kwa magonjwa, na watakosa maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina pesa! Ni sisi wenyewe kujipanga katika namna ya ukusanyaji. Humu humu tunaomba Bungeni tu, baadhi ya harusi mpaka Shilingi milioni 70 zinachangwa, hazilipi kodi! Kadi zinapita, zinachangiwa, lakini Uingereza au Ulaya, hufanyi kitu chochote mpaka ulipe kodi. Kama una harusi yako inazidi kiwango Fulani, ni lazima ilipiwe kodi. Michango ya Shilingi milioni moja au Shilingi milioni mbili mtu anachanga za harusi humu, hazilipi kodi! Tunachecha tu! Hatuwezi kufika! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi tu hapa iliundwa Tume, uhalali wa kuchunguza posho, na yenyewe ililipwa posho kwa ajili ya kuchunguza posho, hapa hapa! Sasa hatuwezi kwenda! Nchi tajiri hii! Lazima twende na kila kitu na ni lazima tulipe kodi! Misamaha imezidi!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanzia sasa misamaha yote ifutwe. Tulizungumza kabisa kwamba hakuna cha kumsamehe mtu kodi, nchi yetu ni masikini! Wote walipe kodi! Wawekezaji wote walipe kodi, ndiyo wezi wakubwa hao! (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Mashamba!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mashamba, wanachukua mashamba, hawalipiii hata ardhi! Mwulize hata Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, kuna mashamba hayalipiwi kodi. Mtu ana kajumba kake kajenga, analipia kodi. Lakini shamba hapa na Muheza, halipi kodi! Hivi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema nchi ni masikini, tunategemea Wazungu. Mwisho, Wazungu masharti yao ni kuoana. Nani atakubali kuoana? Nanyi mnakataa! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote waliopewa mikopo kupitia dhamana ya Serikali wanaishi kama wako Peponi, sisi wengine tupo motoni. Hatupati maji, wala barabara. Lakini viongozi hawa waliwapa mabilioni ya pesa, leo hawakulima, wanakuja na ma-briefcase wamechukua mabilioni katika mabenki, dhamana ya Serikali, hawajalipa lolote na tunawachekea tu! Lazima wafuatwe, walipe!

Mheshimiwa Naibu Spika, leo muuza vitumbua au muuza nyanya analipa Sh. 200/= kwa siku. Kodi yake ukipiga hesabu ni Sh. 73,000/= kwa mwaka. Muuza nyanya! Anakuja mwekezaji, halipi hata senti tano! Mnamkamua muuza nyanya sokoni, mnapita kila siku sokoni kwa wauza nyanya! Wanalipa mpaka Sh. 72,000/= kwa mwaka, lakini hawa Mabepari wakubwa, hawalipi chochote. Mtu ana partition ya maghorofa Dar es Salaam, anapangisha kwa fedha za kigeni, lakini halipi kodi. Haki iko wapi nchi hii? Pepo itatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere alisema, ukitaka kukopa kwenye mabenki haya, labda ufanye kazi ya kuza Bangi au Madawa ya Kulevy, riba imezidi! Ndiyo maana watu wanaamua kwenda kuwinda tembo! Mabenki yamezidi riba! Wanyang'anyi, ni sawa na wavunja majumba! Nani atalipa riba ya asilimia 18 au asilimia 16?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana watu wanashindwa kufanya biashara, wanafanya biashara za magendo. Mnambana mtu mdogo wa chini, wakubwa wanachukua mahela mnawaona mchana kweupe. Inawezekana mnashirikiana! Maana yake haiwezekani nchi inanyonywa na Mabepari, ninyi mnatazama! Hawalipi kodi wananchi, ninyi mnawatazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Mawaziri hao ni wachapakazi, wametangaza na sisi tunafahamu; hakuna kumsamehe mtu kodi awe mwekezaji au mwezeshaji, wote walipe kodi! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi shule binafsi ada yake ni kubwa sana ndugu zangu, hawalipi kodi! Mwanafunzi anasoma kwa ada ya mpaka Shilingi milioni mbili kuliko kada ya Chuo Kikuu!

MJUMBE FULANI: Dola 3,000!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Wanalipa Dola 3,000! Kodi gani analipa kila mwanafunzi? Tunawaachia tu, wananeemeka, wanajenga mashule nchi nzima, na elimu yao ni ile ile, wanadanganya danganya tu!

MJUMBE FULANI: Kingereza!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Kingereza ni lugha kama lugha nyingine! Kuwanyonya! Kwa hiyo, lazima na wenyewe mwafuatilie! Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Adam Malima na Dada yangu Mheshimiwa Saada, hawa na wenyewe walipe kodi! (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna bond ya magari yanayokwenda nje; mwenye gari moja ni Shilingi milioni moja, mwenye gari mia Shilingi milioni moja; haki iko wapi? Haki iko wapi? Si ujambazi huu! Mmemezwa na matajiri wakubwa ili matajiri wadogo waende kuwa wadogo zaidi! Mwenye gari moja Shilingi milioni moja, na mwenye gari mia Shilingi milioni moja! Haki iko wapi? Jaman! Hii Serikali inatupeleka wapi?

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee UDA. Wanazungumza sana UDA na kazungumza sana Mheshimiwa Filikunjombe. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya POAC ndugu zangu, yaleteni tuyamalize kule sisi. Hata Mgololo walimuuzia Dola moja tu, kiwanda kizima kwa sababu ni Mzungu. Dola moja, sijui Dola moja, eh, Dola moja tu walimuuzia. Tunaipeleka wapi? kiwanda miti imejazana, kwa Dola moja tu! Leo mnashangaa ya Musa, mwisho mtashangaa ya Firauni nchi hii! (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Dar es Salaam wanataka usafiri, hawataki malumbano, leteni tuyamalize! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tender, mnatoa tender Serikali yangu, mtu ajenge nyumba ya Serikali au barabara hamna hela. Hamna hela! Anabaki Mchina anakula tozo, ana hasara gani? Barabara ya Shilingi milioni 80 kuja kufikia mwisho ni Shilingi milioni 120, hata bajeti yake hacieleweki! Huwezi kuwa na Shilingi milioni 100, unakwenda kujenga misingi ya nyumba 30, unashikilia viwanja 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wa miaka mitano, huna nyumba hata moja, una misingi tu! Sasa wale mafundi wanakutoza tozo. Hakuna barabara hata moja ndugu zangu ya Shilingi milioni 80, tukalipa Shilingi milioni 80. Ile Shilingi milioni 40 inayozidi, inatoka wapi? Si ni kodi ya wananchi?

Sasa ndugu yangu angalia sana Mheshimiwa Saada, matumizi yenu ya Serikali yamekuwa makubwa sana! Ni uongo, hakuna gari ya Shilingi milioni 280. Agizeni magari Japan moja kwa moja! Hakuna Shangingi la Shilingi milioni 280, nilishawaambia miaka na miaka hapa, na invoice ninazo. Lakini kwa sababu mnakula rushwa, ndiyo maana mnakazania Shilingi milioni 280. Hakuna gari la Shilingi milioni 280 nchi hii! Lakini kwa sababu na ninyi mna pasu yenu pale, ndiyo sababu mnaachia Serikali inunue magari kwa bei inayotaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy, ahsante sana, dakika saba zimekwisha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa nimalize mambo mengi. (Kicheko/Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, dakika hazitoshi Mheshimiwa tunashukuru sana. (Kicheko)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Ninaunga mkono hoja, lakini ninasema hivi, msamaha wa kodi ukija siungi mkono hoja. Mkisamehe kodi siungi mkono hoja na wenyе mashamba walipe kodi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa hoja zako za umakini sana. Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa unyenyekevu mkubwa, nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kutokana na imani kubwa ambayo Rais ameijenga juu yao. Ni matumaini yangu kwamba, watachapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa hoja yangu unahuus uhai wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na nitajikita hasa kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF). Kwa kuwa mimi ni Mwanachama wa Mfuko huu, ninaomba uniruhu nitumie Kanuni ya 61(1), ku-declare interest. Vilevile nitayazungumza haya kwa sababu ninawawakilisha wafanyakazi na haya masuala yanawahuus wafanyakazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhai wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unatokana na michango ya Wanachama. Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma ulianza mwaka 1999 mwezi Julai. Ulipewa grace period ya miaka mitano ili uweze kukusanya michango ya Wanachama (Wafanyakazi) na ilipofika mwaka 2004 ukaanza kulipa mafao kwa Wafanyakazi. Serikali iliji-commit kwamba, kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 1999 kwenda nyuma, Serikali ilipaswa kulipa michango ya Wanachama wake. Sasa wapo Wanachama Wafanyakazi 190,000, ambaa Serikali mpaka leo hajjalipa michango yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha uliopita, Rais alitoa ahadi kwamba, kila mwaka Serikali itakuwa inalipa shilingi bilioni 60. Cha kushangaza ni kwamba, Serikali ililipa shilingi bilioni 30 tu. Mwaka huu wa fedha tunaoujadili leo, Serikali hajjalipa hata thumni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha unaokuja, kutakuwa na Wafanyakazi wanaostaafu siyo chini ya 6,000 na Mfuko huu utatakiwa kulipa siyo chini ya shilingi bilioni 650. Sijaona kwenye Kitabu hiki cha Hotuba ya Bajeti, PSPF imekusanya kiasi gani. Kwa kuwa mimi ni mdau ninafahamu kwamba, kuna bomu linakuja. Kama Serikali haitolipa deni hili la shilingi bilioni 250 kwa PSPF, mwakani Mfuko huu utaanza kulipa kwa hasara. (Makofi)

Kumbukeni hii ni michango yetu, tunachangia tunakatwa fedha kwenye mishahara yetu. Ningeweza kutumia mshashara wangu kwa kufanya mambo mengine tu, lakini nimeamua kuiwekeea akiba kwenye huu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Sasa ninaamua kuzungumza kwa upole kwa sababu tu ni Mawaziri wapya, isingelikuwa hivyo, leo nilisema siungi mkono hoja, kwa sababu ni dhahiri kabisa sijaona dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba, inalipa hili deni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maneno maneno yanasemwaa kwamba, huu Mfuko utakufa kwa sababu formula ile inalipa mafao mengi kuliko Mifuko mingine. Ninawaambieni kwa uzoefu wangu hilo siyo la kweli. Anayesema hivyo ni kwa sababu ya lugha ya kiushindani,

kwa sababu mifuko sasa hivi inashindania Wanachama. Hili deni la shilingi bilioni 270 kama lingelipwa tangu wakati huo mwaka 1999, hizo fedha zingewekezwa na zingeweza kuendelea kulipa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe Serikali bado inadaiwa madeni mengine. Mlichukua fedha kwenda kujenga UDOM mpaka leo hamjalipa. Mlichukua fedha kuwakopesha Wanafunzi wa Elimu ya Juu mpaka leo hamjalipa. Ukiwauliza watu wa Hazina wanakwambia aah, unajua wale Bodi ya Mikopo hatuwezi kusema kwamba, tutalipa sisi kwa sababu wao watazembea kulipa, lakini ninyi ndiyo mliowadhamini; so what? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uende ukawalipe wale halafu hamtaki kunirudishia, nikistaafu nitalipwa nini? Mnatengeneza bomu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Zainab Kawawa. Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtemvu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuipongeza Manispaa ya Iringa hasa Mkurugenzi na Watendaji wote, kwa kushika nafasi ya kwanza katika Manispaa kuwa wasafi, tumeongoza baada ya Moshi. Jamani si mnipigie walau makofi mbona mmenuna? (Kicheko/Makofi)

Jambo la usafi ni la muhimu katika Manispaa yetu na mimi mwenyewe nimekuwa nikiongoza katika kufanya usafi katika Manispaa ya Iringa. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mama Mahongo, kwa kazi kubwa na Watendaji wote wa Manispaa ya Iringa. Mungu awabariki sana, mnafanya kazi nzuri sana mkishirikiana na Mbunge wenu na niko hapa sitawaangusha. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niende kwenye Wizara hii nyeti kama ambavyo wenzangu wamezungumza. Niwapongeze sana waliotangulia Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Selasini, kwani wamezungumza mambo ya msingi sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, mimi nina imani kubwa na wewe, umetulia, uko focused, kwa hiyo, ningeomba hii Wizara hebu tulete mapinduzi sasa, kwa miaka mingi tumeona imekuwa business as usual. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara inapozembea, tunategemea inaandaa policy ambazo tunategemea zitatengeneza mazingira ya kukusanya kodi, ambayo itakwenda kutatua matatizo makubwa ambayo Wananchi wetu tunaowatetea wanayo. Mnapokuwa mnazembea, wana-cause shida nyingi sana kwenye Majimbo yetu na hasa kwa Mwananchi wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza kwamba, hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wa chini ndiyo wanaopata tabu kwa sababu hao ni rahisi kuwapata na ndiyo wanakuwa waaminifu kulipa kodi, lakini hamuwatendei haki. Wizara hii imekuwa ikitumia nguvu nyingi sana kukusanya kodi bila weledi, lakini hakuna nidhamu ya matumizi ya fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara hii iwe na nidhamu ya matumizi ya fedha. Takwimu zinaonesha kwamba, Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, Tanzania ni nchi inayoongoza kwa kuwa na matumizi *luxurious*. Hatuna vipaumbele, tunatumia fedha katika matumizi ambayo siyo *priorities!* Kwa mfano, kama una njaa huwezi kuweka sherehe nyumbani. Tunazungumza hakuna mtu anayetaka sherehe, lakini kutumia fedha nyingi wakati watu

wanaodai (wadeni wa ndani) hamuwalipi; kwa mfano, Wazabuni hamuwalipi, mkatumia mabilioni ya fedha kuonesha vifaru pale, *that is unfair, hatuwatendei haki kabisa.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye JIMBO langu la Iringa Mjini kuna wapiga kura wangu wana matatizo makubwa sana, kwa sababu Wizara hii haijaweka priority. Kuna Wazabuni wame-supply vyakula kwenye Shule za Msingi na kwenye Magereza, wanadai Serikali hajjalipa, halafu tunakwenda pale kupiga kwata tu. Kwa tuliosoma historia, hizi ni tabia za Dola za Kirumi na Nchi za Kisovieti kutaka kujionesha wakati ndani kuna njaa. (Makofi)

Hawa watu kwa mfano; Shule ya Iringa Girls inadai shilingi milioni mia mbili na kitu, Lugalo shilingi milioni 73, ukienda Tosamaganga ambayo Mawaziri wengi mmesoma, ndiyo inaongoza kuidai Serikali mpaka wale wapiga kura wangu wanashindwa sasa na wengine wanataka kuuziwa nyumba, tena wengine ni Wanachama wazuri na wanai-support CCM. Magereza kwa mfano, kuna mfanyakiaresha anaitwa Malekela mpaka anataka kuuziwa nyumba, wamepeleka fedha nyingi sana, ni kwa sababu hamjaweka vipaumbele katika kuangalia ni yapi yatangulie. Tunatumia matumizi makubwa, wamezungumza wenzangu hapa kununua magari ya kifahari. Mawaziri kwa nini magari yenu yasiwe ya binafsi kama ya Wabunge ili yanapokwenda gereji muumie kama tunavyoumia sisi Wabunge? Maeneo hayo ni sehemu ya wizi, kwa nini Wizara isitengeneze policy?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa sababu hili ni Jimbo langu na hawa watu wameniomba nizungumze, wana matatizo makubwa mpaka nyumba zao zinauzwa kwa sababu ya uzembe. Huu ni mfano tu kwa Iringa, lakini najua maeneo mengi na Manispaa nyingi Wazabuni wengi wana matatizo. Sasa na Wabunge watasema ya kwao, lakini kwa mfano Iringa, kuna Mzee Ngwada, Malekela, Sekilovo, Mgina, Sakafu, Mlowe, Ng'owo, Sembigiri, Patrick na Ndekidemi, wanadai fedha nyingi sana, wana hali ngumu. Ninaomba hizo fedha mzipeleke mapema muweke vipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, tunaweka bajeti hapa, kule kwenye Manispaa yetu tunajipanga, fedha za maendeleo, lakini hazifiki kwa wakati na wakati mwingine hazifiki kabisa. Kwa hiyo, mipango ambayo tumeponga inakuwa haifanyiki. Kwa nini tunawadanganya watendaji wetu wanapata wakati mgumu na tunawaaminisha Watendaji wetu na Wananchi kwa ujumla kwa vitu ambavyo havipo? Kwa nini tusiwe realistic tukaleta kitu ambacho kiko wazi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalofanyika hapa, hakuna priority. Mwanafalsafa Masman Row anasema; “The greatest mistake in life is being busy but not effective”. Hii Serikali iko busy sana lakini haiko effective. Mnafanya mambo mengi sana huku na huku, hamna target! (Kicheko/Makofi)

MBUNGE FULANI: Hawalali.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Hamlali. Naomba muwe effective, hebu tuwe na priority tunaka ku-achieve nini? Amezungumza Mheshimiwa Keissy hapa ninamuunga mkono, tuna misingi mingi sana imejengwa, mingine ilijengwa toka wakati wa Mwalimu Nyerere haijaisha mpaka leo. We are not effective, priority yetu ni ipi na tunataka ku-achieve nini? Mnatuambia hapa tukiondoka hapa tunarudi na vitabu vikubwa vikubwa tunaenda Majimboni kwamba, tunaenda kutekeleza moja, mbili, tatu, nne, hakuna fedha. (Makofi)

Tunaanza kulaumiana kwenye vikao hakuna fedha. Tunaomba mtengeneze policy nzuri. Kwa mfano, fedha nyingi sana inapotea kwenye property tax, kuna majengo mengi Dar es Salaam kodi haikusanywi, kwa sababu hamjatengeneza utaratibu mzuri. Kuna majengo mengi

kwenye Halmashauri kodi haikusanywi, lakini bado wafanyabiashara wakubwa hamuwakamati. Tunakuwa na wasiwasi na Serikali yetu ambayo inashindwa kukusanya kodi. (Makof)

Ndugu zangu uzalendo siyo kuvalaa skafu, kuonekana kwamba tumevalaa Bendera ya Taifa, uzalendo ni kuwa na vipaumbele, kuwajali Wananchi na kuhakikisha fedha tunazopata zinaenda kwa walengwa na tutumie vizuri. Kwa hiyo, uzalendo siyo kuonekana kwa macho, ni kwa vitendo. Tunaomba hizi fedha. (Makof)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Achana na hiyo namba wewe.

WABUNGE FULANI: Wewe endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui huu ndiyo utaratibu!

NAIBU SPIKA: Walikuwa wanakukumbusha tu. Mheshimiwa Mchungaji, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ulitukataza tusiwashe microphone.

MBUNGE FULANI: Kuwasha microphone ni ruhusa eeh?

MBUNGE FULANI: Anapendelea.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulie, nafasi ni ya Mchungaji Msigwa, ninawaomba sana. Tafadhalii Mchungaji endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na muda wangu ulindwe dakika mbili zimeibowi. Niseme tu kwamba, hii nchi ni ya sisi sote, kama kweli tunalitendea haki Taifa letu, lina utajiri mwangi sana; nenda kwenye maliasili, madini na kila aina ya vitu ambavyo Mungu ametupa, tunaweza tukaweka vipaumbele vizuri tukahakikisha hizi fedha zinatosha na zikaenea kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza juzi, wengi tunatoka kwenye Majimbo ambayo Wananchi wetu wana hali mbaya sana. Katika suala hili la kuikosoa hii Wizara tunapaswa Wabunge wote tuungane kwa sababu walau sisi tunaotoka kwenye Majimbo ya mijini tuna nafuu. Wengi humu ndani barabara haziko zimetengezwa na ng'ombe, ndiyo Majimbo yenu. Sasa tunatakiwa tuibane hii Serikali ili hii Wizara ikusanye fedha za kutosha, maji yapatikane maeneo yote, barabara ziwepo katika nchi, tuwatendee haki Watanzania ambao wametupa dhamana ya kuwaongoza, tuache haya malumbano ambayo hayana maana.

Wakati mwingine tunaingia kwenye malumbano ya kivyama ambayo hayatusaidii, uhalisia tunakotoka kwenye Majimbo kuna hali mbaya sana. Hii Wizara mama ni lazima iwe na nidhamu, tengenezeni policy ili tukusanye fedha nyngi. Kuna maduhuli mengi, asubuhi kwenye Kambi ya Upinzani hayajazungumzwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tena...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, muda hauko upande wako nakushukuru sana.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kwenye kitabu chake Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu Volume I, hamjatupa Volume I ili tujuu mnapataje fedha ili tuwakague. Bunge gani hili tunajua matumizi tu mapato hatuui? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi niende kwenye hoja ya UDA moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mdau wa UDA; ni kijana niliyezaliwa Dar es Salaam, nimepanda UDA nikiwa mdogo, kwa hiyo, ninaijua vizuri UDA toka ikiwa BMT. Mimi sikupuki tu nikaongelea suala la UDA bila kujua chanzo chake, lakini ni Mbunge wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe Wabunge waangalie Ripoti ya CAG ya mwaka huu, Ukurasa wa 33, kifungu cha 3.5, angalieni wengi wenu taarifa hii itawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam hatujapinga hata mara moja Shirika la UDA kubin afsishwa, lakini tunataka uhalali na haki itumike. Kwanza, mimi ni sema kitu kimoja kibaya sana, humu ndani tuna Mjumbe wa Bodi ya UDA na amekuwa akizunguka sana Mkurugenzi wa Bodi ya UDA humu ndani, hiki si kitendo kizuri. Hiki ni kitendo ...

WABUNGE FULANI: Nani?

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Kapuya. (Makofii)

Amekuwa akizunguka akiwaona watu, ni kitendo ambacho si kizuri. Labda niwaambie, naona hawajui history! Mnaongea mwekezaji kanunua UDA, mngetuambia kalipa shilingi ngapi ndiyo mngetusaidia sana. Mwekezaji huyo mnayemwongelea hapa, mnamwongelea usiku na mchana, amelipa shilingi milioni 280; ndiyo hadhi ya UDA hiyo? Hiyo ndiyo hadhi ya UDA? (Makofii)

UDA kakabidhiwa na nani? Hakukabidhiwa na vikao halali vya Dar es Salaam. UDA alikabidhiwa na Meya wa Jiji la Dar es Salaam. Baada ya kumkabidhi na yeye (Massaburi) akafanya lobbying ili Wajumbe waridhie wapitishe, lakini kwanza yeye ndiye alimkabidhi. Kwa hiyo, tunapoongea, tusianglie sambusa za Dodoma Hoteli, tuangalie uasilia wa jambo. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwasaidie, hivi tunauza mali ya Serikali bila Baraza la Mawaziri! Tunauza mali ya Serikali bila Baraza la Mawaziri? Tunaweza kuuza mali ya Serikali kutumia Kamati ya TAMISEMI ambayo Mwenyekiti wake anafanya biashara ya pamba ana mahusiano na Simon Group? (Makofii)

Kwa hiyo, tutafute ukweli, tutafute haki, tuisitake kutafuta dhuluma. Niwaambie zaidi, huyo Simon Group uwezo hana. (Makofii)

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Taarifa nani? Aah Mheshimiwa Kapuya!

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Taarifa ninazozitoa ni kama ifuatavyo:-

Moja, isiwe haramu kwa Mbunge kuonekana ni mwekezaji; sera inaruhusu Wabunge kushiriki katika shughuli za uchumi. (Makofi)

La pili kwamba, Kapuya anazunguka huku kuona watu. Afadhalii mimi kama nimefanya hiyo kazi ya kuzunguka kuona watu kuliko anayezunguka kwa niaba ya kurudisha *imprest*. Wako watu wamezunguka humu usiku na mchana ili wakidhi matakwa ya wale ambao wamewatuma kuwapa *imprest*. Wamo humu tunawajua.

WABUNGE FULANI: Nani hao?

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Na aliyezungumza ni mmojawapo. Huyo ndiye kafanya kazi kubwa hapa. Anatumwa na watu kuja kuzunguka humu, kubadilisha mawazo ya Wabunge hapa. (Makofi)

La tatu, hakuna mali ya Serikali iliyouzwa bila ya Baraza la Mawaziri, zilizouzwa ni hisa za Jiji, ambapo yeye alikuwemo katika vikao. Huyo, ameshiriki vikao vyote na posho amelipwa, ameshindwa kuzuia kule analeta hapa mgogoro wa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hisa za Serikali ziko salama mpaka sasa.

NAIBU SPIKA: Naomba ili tuokoe muda, Mheshimiwa Mtemvu endelea.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake siipokei na anaposema Mtemvu anazunguka, maana yake kuna dhana inayosemwa sijui Mu-Asia, kuna mtu ambaye si raia. Hapa tunaongelea Ripoti ya CAG, haikutaja kwamba, hawa wanahangaika ili wampe mtu ambaye siyo. Sisi tunaongelea Ripoti ya CAG ndiyo imeeleza madudu.

Sasa nataka kuwaambia kitu kingine, wewe ultumia Uwaziri wako kuchukua mali za Wana-Dar es Salaam na Wana-Dar es Salaam watakuhukumu. Unasimama hapa mtu mzima unaongea maneno yasiyofanana na wewe!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtemvu, naomba turudi kwenye mada, tusishambuliane tafadhalii.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Yeye ametumia Uwaziri wake kupata mali kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo UDA tunayoigombea hapa haipo, wamekopa fedha Benki, UDA imeuzwa tarehe 24 Februari, kwa shilingi bilioni 12; mmewaambia hao wanaozunguka, mmewaambia na walionunua siyo hao mnaowasema, wamenunua Kampuni ya Al-Jazeera. Hilo mmewaambia hao kama UDA imeuzwa kwa mnada?

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna hadithi yoyote, tunataka UDA mali ya Dar es Salaam imeuzwa kwa dhuluma, imeuzwa bila ya utaratibu, hatukushirikishwa hakuna kikao tulichoshirikishwa. Meya wa Jiji la Dar es Salaam, alichukua akamkabidhi Saimon Group, hakuna Hazina hakuna Jiji. Huo ndiyo ukweli, ndiyo maana unatuona hatuzunguki sisi tumetulia kwa sababu tunatetea haki yetu. Wewe unazunguka, unaita watu wa Dodoma Hoteli, habari zote tunazo au unataka tukupe camera? (Kicheko/Makofi)

Acheni, mmeifanya Dar es Salaam ni ya kuchuma. Hivi unapoongea hapa ndani Mbunge usiyekuwa wa Dar es Salaam unajua vizuri Dar es Salaam? Sisi tuje tuongee mambo yenu; lini tumeongea mambo yenu? Watu wa Dar es Salaam tunaongea mambo yetu na ninyi ongeeni mambo yenu. (Makof)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mtemvu. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Wizara ya Fedha ni kukusanya kodi, kusimamia matumizi, lakini jukumu mahususi ni la kukuza uchumi. Ningombam jambo hili walifanyie kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kodi, mimi naomba niongelee kodi moja ya Property Tax. Naiomba Serikali isimamie watu wote nchini tulipe kodi ya majengo. Ili tuweze kulipa kodi ya majengo, Serikali ihakikishe kila mwenye nyumba na kila mwenye shamba ana hatimiliki. Tukifika hapo tutaweza kukusanya kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la PPP. Tumetunga Sheria ya PPP kwenye Bunge hili. Mpaka leo tunaongea habari ya PPP, lakini hakuna hata Mradi mmoja wa PPP. Hatuwezi kuendesha bajeti ya nchi kama hatuwezi kwenda kwenye PPP na matokeo yake ndio maana leo reli tunataka tufanye sisi, bandari tufanye sisi, viwanja vya ndege tufanye sisi, barabara tufanye sisi, irrigation tufanye sisi; haiwezekani. (Makof)

Nchi zilizoendelea miaka ya 1960; Malaysia, Singapore hata China ni PPP; hata hili hatuwezi kujifunza? Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri, kijana mwenzangu, badilisha mfumo wa kuendesha uchumi wa nchi hii. Hatuwezi kuendeleza uchumi wa nchi hii wakati ambapo leo fedha zote mtapeleka kwenye barabara, mtapeleka kwenye reli, tutalia hapa hakuna maji, hakuna shule, hakuna madawa, hakuna umeme. Leo hii fedha tunazotumia kwenye mafuta ya umeme ni nyingi sana, lakini hewala. Nawaombeni tubadilisha mfumo wa kuendesha uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, asset management; nchi hii ina assets nyingi sana, mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu tuangalie, unajua hata kwenye level ya familia, mtoto akiwa hawezikwenda shule unaiza kondoo wako, unaiza kuku wako, unakata ndizi yako ili watoto waende shule.

Sasa leo tuna deficit ya bajeti, tuna vi-share vidogo vidogo kwenye makampuni hatuvitumii; tunaviacha vya nini? Tulikuwa na share NBC tunaambiwa hatuwezi kuwa diluted kwa sababu hatuwekezi. Tuna share sijui IROV, tuna share NMB, tuna share ya NBC, tuna share PUMA, tuna share ndogo ndogo nyingi za nini? Tuna share Airtel asilimia 40 tunaziacha za nini kama hazileti dividend?

Mimi naombe Serikali ikae kwenye asset management ili asset zetu zituletee fedha za kuongeza kwenye bajeti yetu. Kwa kweli tukifanya hivyo, tutabadilisha uchumi wa nchi yetu. Jamani lazima tubadili namna tunavyoenda. Tumeendesha nchi hii kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni private sector, tunasema private sector ndio engine ya growth, lakini hapa ndani ndio tunaongoza kupiga vita private sector, mtu akifanya biashara huyo mbaya; jamani hii ni nchi gani hii! Hatuwezi kuendeleza nchi hii bila private sector ku-participate na matokeo yake watakuja Wazungu watatengeneza fedha wataondoka. Kwa sababu ni Wazungu hamna atakayewanyoshea kidole humu ndani.

Watakuja Wa-Asia watatengeneza fedha wataondoka, kwa sababu siyo rangi nyeusi, hakuna atakayewanyooshea kidogo humu ndani. Mimi naomba suala hili tulisimamie kuhakikisha private sector inashiriki kwenye uchumi wa nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, jambo lolote likija Bungeni, msitegemee Wabunge watanyamaza. Kama liko jambo mnataka Wabunge wengine wasiliongee, msililetu kwenye Bunge hili. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkilileta suala la UDA humu ndani tutaongea, mkilileta tutasema, kama hamtaki tulijadili, jadilini huko kwenu Dar es Salaam, msililetu humu ndani. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nimwambie Attorney General, Attorney General wa nchi hii uko hapa, nakuomba uingilie suala hili. Serikali kaeni, lifanyieni kazi, haki itendeke, lakini mnatuacha Wabunge hapa tunakuja kunyoosheana vidole bila ya sababu. Ukanza kujuliza tunanyoosheana vidole kwa sababu ni wazalendo sana, tuwe wakweli hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema lipo tatizo, Serikali miltatue. Ripoti za CAG kila mwaka zipo; kuna mwaka fulani tulifukuza Mawaziri hapa kwa Ripoti ya CAG, baadaye mambo yenye tukakuta tumewaonea watu wa watu. Ripoti ya CAG, Accountant yeoyote ambaye amesoma Uhaisibu, unapoenda kukagua hata usipokuta mkataba unapiga query, kesho ukija ukioneshwa unaiondoa ile query unless hujui auditing. Tusiletewe tukadhani Ripoti ya CAG ndiyo mwarobaini, tatizo lipo nendeni mkalitatue Serikali. Naomba Attorney General simamia jambo hili ukweli ujulikane, nendeni kwenye Baraza la Mawaziri mtatue mgogoro huu wengine tumeuchoka. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nisiseme kuhusu umuhimu wa Wizara maana umeshasemwa. Jambo kubwa kabisa, leo kwa mara ya kwanza hili jambo lilishamalizwa kabisa na Mheshimiwa Mbatia. Kama tunafuata na tunasoma Hansard, Mheshimiwa Mbatia alishatoa ushauri mzuri sana juu ya hili jambo tunalolizungumza humu ndani. Shida yetu Wabunge ni kwamba, kila kinachosemwa na wewe unataka useme ili utoe jazba yako na pengine labda wapiga kura wakuone.

Jambo la msingi hapa ni kwamba, Wizara hii ni Wizara muhimu sana. Amezungumza Mchungaji Msigwa na mimi leo namuunga mkono kwa mara ya pili tena, maana kuna siku moja nilimuunga mkono na leo namuunga mkono; pesa zisipokusanywa, ndugu zangu kwenye Majimbo nilimwagiza Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Mtera, apige picha majengo yote ambayo hayajakamilika, nije nimkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa. Nitataja na mwaka, hili lilianza mwaka fulani mpaka mwaka fulani. Kwenye Majimbo kuna magofu tupu. Nyumba ya Mwalimu haijaisha unaanzisha nyumba ya Mwalimu Mkuu wa Sekondari, haijaisha unaanzisha nyumba ya Mganga, haijaisha unaanzisha josho halijaisha; haiwezekani, hivi hata Maafisa Mipango wanapanga nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara ya Fedha ikusanye fedha ya kukamilisha yale mambo ambayo hayajaisha. Tuna viporo, Ofisi ya Mbunge haijaisha, kwa hiyo hata ukisimama unachokisema wala hakuna mtu atakayekuelewa unasema kitu gani. Lazima tuwe na nidhamu ya kukusanya kodi na tunaposema kukusanya kodi, tukusanye halafu tuzilinde, maana unaweza kukusanya halafu ukaweka kwenye mfuko uliotoboka haina maana. Kwa hiyo, lazima

tukusanye na mifuko tuzibe isitoboke, tunapigizana kelele bure, hizo Wizara zote zilizotajwa bila ya Wizara ya Fedha hazina faida yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwa uchungu sana, tukisema tuangalie makundi ya watu gani hawakusanyi kodi, ni kweli kabisa amesema Mheshimiwa Ali Kessy hapa, wafanyakibashara wakubwa hawakusanyi kodi, wafanyakibashara wadogo wengine hawakusanyi kodi, lakini wanaonyanyasika ni watu wasiojua hata Sheria ya Fedha. Hivi mnajua kwamba NGOs nyingi zinapata manufaa makubwa na watu wanajenga majengo lakini hawalipii kodi? Wengine wameanzisha upatu, kuna wanakijiji mpaka wanafungwa jela, mtu anakopesha shilingi laki moja alipwe shilingi laki mbili, halipii kodi. Mnaelewa na anampeleka Mahakamani mtu anamfunga!

Hatuwezi kuendesha namna hii. Mashule watu wanalipa ada chungu nzima, kwa miezi mitatu shilingi milioni mbili, ndyo term ya shule shilingi milioni mbili, lakini mhusika analipa kiasi gani, hata uwekezaji lazima tuangalie. Tuna imani na Waheshimiwa Mawaziri, tunawaamini sana lakini tunaomba kuwe na nidhamu, tumejifunza wenzetu wa China wana vitu vitatu tu; wana uwajibikaji, nidhamu na uadilifu basi, ndyo wanaendesa nchi. Kama nchi haina uwajibikaji, mimi mwenyewe kuna kipindi kabla sijaanza kubadilisha mfumo wa maisha yangu, niliwahi kuyatazama kama TV, nikagundua kumbe adui wa maisha yangu ni mimi mwenyewe. Unaweza kuangalia matumizi unayotumia na fedha unazopata, kama uwezo wako siyo wa kunywa heineken ukinywa heineken adui wa maisha yako ni wewe wala siyo mtu mwengine. Huwezi ukapita unamlamu mtu uwezo wako siyo wa kulala Dodoma Hoteli, ukilala Dodoma Hoteli adui wa maisha yako ni wewe. Kwa hiyo, lazima Serikali yetu ijifunze inaongoza nchi gani na uchumi wetu ukaje kabla hatujakwenda kwenye jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka niwasih sana Waheshimiwa Wabunge, najua kweli kila mtu ana jazba ya kuongelea mambo ya Dar es Salaam, mambo ya Dodoma na kadhalika. Leo tunaomba mwongozo wako utusaidie, kama kuanzia leo Wabunge wanatakiwa wajadili jambo la kwao tu ieleweke hapa, asije mtu hapa akazungumzia zabibu, asije mtu hapa akazungumzia Iringa. Kwa hiyo, wa Dar es Salaam wazungumzie Dar es Salaam, Dodoma wazungumzie Dodoma, Moshi wazungumzie mlima, haiwezekani itakuwa Bunge gani hilo. Tusiamue vitu kwa jazba, tusikilize hoja.

Unajua jambo hili nimelisikiliza, kwa uelewa wangu mdogo, tusipolimaliza, Serikali msipochukua ushauri wa Mheshimiwa Mbatia, Bunge litagawanyika mara mbili. Wako watu wanaomunga mkono aliyenunua, wako watu wanamuunga mkono anayetaka kununua. Katika mazingira kama hayo, hatuwezi kutenda haki. Bora mlimalize hili jambo kwa kufuata ushauri wa Wabunge wetu. Wabunge wanaelekeza kaeni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waiteni muangalie wapi mmetereza wapi mnarekebisha, lakini mkitaka tuendelee kuchangia kwa kuvutana hivi, itaonekana ukikaa na mtu fulani umenunuliwa, ukikaa na mtu fulani umenunuliwa; hivi mtu anapangiwa mtu wa kukaa naye! Tangu lini huo utaratibu umeanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nisih, mimi narudi kwenye ushauri ule ule uliotolewa na Mheshimiwa James Mbatia, hakuna uhusiano wa suala la Dar es Salaam. Dar es Salaam mimi mwenyewe nimekaa miaka 20 pale bila kuhama na nilikaa eneo moja tu linaitwa Kawe. Kwa hiyo, ukifika Kawe ukimwuliza mtu yejote hata mtoto mdogo, hata ukimwuliza kuku ukiona anaenda tu mfuate atafika nilipokuwa nakaa zamani. Kwa hiyo, wote tumeishi wala hakuna mtu atakayeweza kutuambia hatujakaa, tumekaa maeneo mengi. (Kicheko)

Hili jambo litatuletea mzozo kwa sababu tumegawanyika mara mbili; kuna wengine wanaamini kwamba, kila kitu kizuri ni cha Mzungu, Mwfrika hana kitu kizuri, wengine hata Mwfrika akikosea hatutaki kukosoa. Kwa hiyo, nataka nishauri, Watu wa Dar es Salaam

wanataka usafiri wa uhakika na wa bei rahisi, ndicho watu wanachokitaka. Haya malumbano yetu Serikali msipoyamaliza, mwakani hili jambo litakuwa bayo zaidi kuliko mnavyoliona sasa. Kwa hiyo, tunawashi chukueni ushauri wa Wabunge wameshauri, kaeni angalieni mmejikwaa wapi, msiangalie mikodondokea, angalieni mlilikwaa sehemu gani katika jambo hili linalohusu UDA. Jambo limechokwa, kila tukikutana hapa UDA, UDA, wakati kwetu huko hata usafiri hawana ninyi kutulazimisha. Kwa hiyo, tunataka tuzungumze hapa, msitulete hoja ambazo mnajua hatupaswi kuchangia, kama mnazileta hapa tupeni ruhusa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Mheshimiwa Aden Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikushukuru na mimi niungane na Wabunge wote, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, ambao kwenye mpira naweza kusema, Waziri ni centre forward Naibu Waziri wote wawili ni *inside left* na *inside right*. Kwa hiyo, ni striker wazuri na ninaamini kabisa mwakani CCM tutapeta kama kawaida. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchukua nafasi hii, kwa mara ya kwanza, nimpongeze Waziri Kivuli, Mheshimiwa James Francis Mbatia. Ametoa Hotuba yake nzuri sana, yenye hekima, wala haina matusi, ilikuwa ina mshiko mzuri. Ninachowaomba tu Wizara ya Fedha, wazingatie ushauri ambao Mheshimiwa Mbatia ameutoa hasa kuhusiana na *interest rate*. *Interest rate* kwa kwetu hapa iko juu sana. Kwa Wachumi wanakwambia *inflation* inapokuwa low, haiwezekani *interest rate* ikawa hai tena, lazima *interest rate* ishuke. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona sasa kuna Mabenki yameingia kama utitiri, kuna taasisi za watu binafsi za kukopesha na watu wanaoumia ni Wananchi wa kawaida, kwa maana watumishi pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Mabenki yamekuwa yanawanyonya Wananchi hawa wadogo. Wanapo-deposit fedha zao aidha iwe kwenye *fixed deposit* au *current account* au *saving account*, *interest rate* benki inayotoa ni kati ya *three percent* mpaka *the highest* ni *six percent*. Sasa wao wanapata uhalali huu wapi wa ku-charge *18 percent* mpaka *24 percent*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, iko haja ya kuomba Bank of Tanzania, ndiyo kazi yake kisheria, yeye ndiyo ana-monitor hizi *interest rate* na ana mamlaka ya kisheria ambayo sisi tumemkabidhi ya ku-determine leo iwe kiasi gani au kesho iwe kiasi gani. Bank of Tanzania vilevile kuna makosa mengine wameyafanya, wamepandisha kiwango cha Wananchi wanapotaka, kwa mfano, Tabora sisi ndito tunaongoza kwa zao la tumbaku. Tukitaka kufungua benki yetu we can do it now, imepanda kutoka shilingi milioni 250 mpaka bilioni mbili. Kwa hiyo, hii ni hatari sana. Mngetupa na sisi nafasi mkaweza kuangalia katika watu kama Mkoa wa Tabora au Kilimanjaro, wakulima wanataka kufungua benki yao, hebu jamani muweke amount ya kufungulia iwe ndogo, isiwe kama hawa watu ambao wanakuja kutoka nje huko na fedha zao za ajabu ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona watu wengi wanaongea juu ya UDA, lakini kuna bomu lingine Dar es Salaam linakuja. Mheshimiwa Waziri, hebu kama lina ukweli nitaomba wakati unajibu unihakikishie; kuna haya mabasi ya mwendo kasi (*DRT*), nasikia kwamba, wametoa proposal kwenye Serikali, kutoka Kimara mpaka City Centre watakuwa wana-charge shilingi 2,500. Halafu Serikali ita-subsidize shilingi 1,500. Kwa hiyo, Mwananchi ndiyo atalipa shilingi 1,000; sijui kama huu ni kweli au vipi lakini kwenye mitandao ipo na imetokea. Kwa hiyo,

naomba tuangalie kama ni kweli, I don't know Serikali itatoa fedha wapi, kwa sababu mtawajibika kulipa siyo chini ya shilingi bilioni 30 mpaka bilioni 45 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuungana na Makamu Mwenyekiti wangu wa PAC, hili suala la UDA ili kuwepo na harmony ndani ya Bunge na kuweka heshima ya Bunge hili, kama Serikali mnaona mnapata kigugumizi kidogo, hebu tuleteeni kwenye PAC kwa mujibu wa Kanuni za Bunge sisi ndiyo wenye dhamana ya kuangalia mahesabu ya Mashirika ya Umma na Serikali.

Ninasema hivyo kwa sababu nina taarifa hapa ya *the Treasury Registrar, Statement for the year ended 30th June, page two*, maneno aliyoyasema Mheshimiwa Malima wakati anajibu maswali ndiyo yaliyoandikwa humu ndani. Kwa hiyo, mlipomshambulia Naibu Waziri, haikuwa sahihi hata kidogo. Hapa imeandikwa kwamba, *City Council* wana-own 51% na Serikali ina-own 49%. Sasa hii ndiyo confusion inayotokea humu ndani ya Bunge kwa muda mrefu. Sasa hii ni Taarifa ya Serikali, *the latest one*. Ambayo ni tarehe 30 Juni, 2013. (Makofij)

Siku ile Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali hakusema kwamba, hamtambui Saimon na wala hakusema kuwa, 100% yote imechukuliwa na Serikali. Yeye alisema, share za Serikali kama Waziri wa Fedha ana uhakika 49% na ndiyo iko hapa hata kwenye vitabu hivi vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hajakataa kama Saimon ana 51% au *City Cancel, whatever it is*. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, suala hili kidogo limekuwa linaleta mzozo ambao unatudhalilisha Waheshimiwa Wabunge na unaidhalilisha Serikali yangu, ni vyema sasa ukweli ukaeleweka hata kama ikibidi kuunda Tume ya Wabunge.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Baada ya kusema hayo, ninaunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rage. Mheshimiwa Masoud, mchangiaji wetu wa mwisho, halafu Naibu Waziri jiandae.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninataka nianze kwa kusema kwamba, ili Serikali ipate fedha ni vyema iondokane na udhaifu katika suala zima la ukusanyaji wa kodi katika mashirika makubwa, makampuni ya migodi na madini na zaidi katika makampuni ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni miezi michache iliyopita, Waziri wa Biashara na Viwanda na ninampongeza sana, alisema wakati Dar es salaam na Bagamoyo kuna Bandari Bubu zipatazo 32, ambazo zinaonekana zinakwepa kulipa kodi, ni eneo ambalo linahitaji kupewa nafasi yake liangaliwe ili basi hata kama wafanyabiashara hawa ni wadogowadogo, ionekane ni wajibu nao walipe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, mmeleta mashine ya EFGD, lakini kuna malalamiko makubwa kwamba, haikutolewa elimu ya kutosha kwa wafanyabiashara. Malalamiko mengine ni bei ambayo hata Mwenyekiti wa Kamati, naye alisema kuwa ni kati ya shilingi laki sita, laki saba, laki nane na upo uwezekano wa unafuu wa kupatikana kwa bei nafuu za mashine za EFD. Ninyi ndiyo mnajua zaidi ni utaratibu gani Serikali mnaojua juu ya tatizo hili. Kigezo gani kilichotumika kuwatambua wafanyabiashara wanaotakiwa kutumia EFD?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni manung'uniko makubwa. Suala zima la mtaji wa shilingi milioni kumi na nne kwa watumiaji wa mashine hii, liangalie sana Waziri manung'uniko ni makubwa sana, kuna tamko la hivi karibuni wanasema kwamba, Mawakili wapya, Serikali imekataa kuwasajili lakini kila mwaka nao kuna mawakili wapya mnawasajili je na wao inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kuna udhaifu huo, lakini kuna matatizo, Serikali haiko makini katika udhibiti wa fedha. CAG Report zimetoa melezo mengi; 2011/12 amesema kuna bilioni kumi na tatu zimechukuliwa na maeneo ameteja. Ninyi hapo hakuna lolote, hakuna mtu aliyejambo na hakuna mtu aliyejibishwa. Mwaka 2012/13 bilioni kumi na tatu pointi mbili, ukiangalia miaka saba iliyopita, karibu bilioni hamsini na nne, tangu 2006 hadi leo.

Serikali imepanga mikakati ipi kuwaadhibu hawa? Ni wale wale tu wanaoiba kuku na mbuzi ndiyo mnawafunga magerezani. Tatizo hili halivumiliki. Tunashuhudia mama ntilie kule Dar es Salaam wanavyohangaishwa na mgambo, tunashuhudia wamachinga wanavyohangaishwa kule Kariakoo na maeneo mengine, lakini kuna misamaha ya kodi ya trilioni moja point tano! Haya ni matatizo makubwa, ni vyema tujipange tuangalie ni utaratibu gani ulio mzuri.

Mimi ninataka nielezee jambo langu kubwa tu kuhusu Wastaafu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mbatia, nakuunga mkono. Wastaafu wetu hali zao ni mbaya sana na hata Taarifa ya Kamati imesema, pensheni zao za kila muda wa miezi mitatu wakati mwingine muda unaongezeka. Kiungo chao cha pensheni hadi leo wapo wanaopata shilingi hamsini elfu, mia moja na arobaini sawa na shilingi elfu moja mia saba na ishirini.

Mheshimiwa Waziri, hili ni tatizo kubwa, lazima liangaliwe sana. Kubwa zaidi, mafao ya wastaafu wanapostaafu, wakati wanatakiwa wapate kiwango chao wanachostahili, hawapati na sababu kubwa mnasema hamna wataalamu wa kutosha, mna tatizo la kukokotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kutoa mfano mmoja tu, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonesha kwa mwaka 2009/2010 kati ya majalada elfu nne mia tisa na sitini yaliyokaguliwa, majalada mia moja thelathini na saba yamelipa pungufu shilingi milioni mia moja na sitini na saba na suala ni lilelile mnasema kwamba mnakokotoa isivyo vizuri, hakuna wataalamu wa kutosha.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/11, kati ya majalada elfu nne mia saba na themanini na nane yaliyokaguliwa, majalada mia mbili themanini na mbili yangelipa pungufu shilingi milioni mia tano thelathini na tisa. Mambo haya miaka yote kila Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapoletwa, basi kunakuwa na tatizo la kukokotoa; hivi kweli hamna wataalamu wa kutosha mbona hamuwaongezei fedha hawa wastaafu wakaondokana na umaskini? Waongezeeni, tusije tukakokotoa isivyo halali tatizo. Kama mnakokotoa vizuri basi na mimi ningekuwa ninaruhusiwa, ningewaambia Hazina, wakati wa mwisho wa kumalizia kipindi chetu cha Ubunge, wakokotoe kidogo wakosee wamlipe isivyo halali Mheshimiwa Waziri Saada Mkuya, Mheshimiwa Naibu Waziri Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Malima. Wakokotoe isivyo halali nao waone.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo na wastaafu wetu wamekuwa wakilisema muda mrefu. Hili ni eneo ambalo hata umaskini walio nao wastaafu wetu kumbe tatizo ni Serikali. Tumesema muda mrefu hapa Bungeni, tatizo la kukokotoa jamani ni lini litapatiwa ufumbuzi? Ni kwa nini tuwapunje na kwa nini tusiwaongezee fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la matumizi makubwa ya Serikali. Waziri Mkoo alisema hapa kwamba, sasa tunaacha kabisa utaratibu wa kununua magari ya kifahari, lakini tunaona magari bado yanaendelea kununuliwa. Waziri Mkoo alisema hapa kwamba, semina na warsha zitapunguzwa; tuelezeni ni kweli zimepungua? Magari ya kifahari yameacha kununuliwa? Mwenye macho haambiwi tazama, mambo bado yanaendelea vilevile, nalo ni tatizo, ni vyema mambo haya mnapoyasema basi ni vyema myatekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake na Watendaji wa Ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoifanya, ila nawapa pole kwa jukumu zito walilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA bado mapato yanavuja sana na ndiyo maana tunashindwa kukusanya mapato stahiki kutokana na wafanyakazi kutokuwa waadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana usimamizi wa mapato TRA uangaliwe kwa makini sana, vinginevyo tutaendelea kupoteza mabilioni kwa kuingia mifukoni mwa wajanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado suala la wafanyakazi hewa linaendelea kushamiri siku hadi siku badala ya kupungua. Kila Wizara ina wafanyakazi hewa. Ukiangalia ripoti ya Mkaguzi Mkoo wa Hesabu za Serikali za kila Halmashauri au kila sekta utakuta kuna malipo hewa ya wafanyakazi, na sasa hata kwenye Mfuko wa Bima limejitokeza. Tunaomba uhakiki wa kina ufanywe ili kubaini udhaifu huu wa watumishi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vipyta ya mapato, kama sikosei nakumbuka Kamati ya Mheshimiwa Chenge, Kamati ya Bajeti imebuni vyanzo vya mapato. Je, vyanzo vile vimetiwa kapuni au vimeonekana havifai? Kama havifai, ina maana Kamati hii imekosa uwezo? Hivyo basi, ni afadhalii ivunjwe, iundwe nytingine.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kutoka maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa bajeti ya Serikali imekuwa haifikii malengo yake ilijoipangia. Kumekuwa na kilio kikubwa kwa Wizara zote kutokupewa fedha zilizopangiwa kwenye bajeti yake kwa wakati na wakati mwagine kama ilivyotokea mwaka huu unaoisha wa fedha, bado kuna mafungu makubwa sana ya fedha hayajapelekwa na mwaka unaoisha. Sababu kubwa inayopelekea Serikali kutokufikia malengo ni matumizi makubwa yasiyo na tija na mengine yaliyo nje ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi yasiyo na tija ni kama vile maadhisho mbalimbali ya sherehe za kitaifa ambazo hata hazikupangiwa mafungu ya bajeti. Sherehe za Muungano (miaka 50) zimegharimu jumla ya Shilingi bilioni 27 ambazo kwa uhakika hazikuwa kwenye bajeti. Kama Serikali itadai fedha hizi zilipangiwa bajeti, itueleze leo ni fungu gani lilielekeza hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nytingine ni safari za nje za Viongozi Wakuu akiwepo Mheshimiwa Rais ambazo kwa kweli wakati mwagine hazihitaji Mheshimiwa Rais kwenda. Hii

imepelekea bajeti iliyotengwa kwa safari za Mheshimiwa Rais kwisha katika robo ya kwanza tu baada ya bajeti. Swali la kujiuliza, Mheshimiwa Rais anapata wapi fedha nyingine za safari wakati bajeti yake ilikwisha? Siyo kweli kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ndiyo zinatumika kwa safari hizi na kusababisha miradi mingi ya maendeleo kukwama? Serikali iwe na discipline ya matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa sana kwa nchi ambayo ina kila rasilimali, kuendelea kukopa bila tija na kupelekea nchi kuwa na mzigo mkubwa wa madeni. Mwaka 2013, Juni, deni la Taifa lilikuwa Shilingi milioni 21.2. Cha kushangaza, kwa miezi saba tu, deni la Taifa limefikia Shilingi milioni 29.477 Januari, 2014. Siyo dhambi nchi kukopa, lakini mkopo unapotumika bila tija, ndipo inaleta mgogoro. Kama nchi ingekuwa inakopa kwa shughuli za maendeleo na ujenzi wa miundombinu ya uchumi, kusingekuwepo na malalamiko mengi maana ni dhahiri kwamba shughuli hizi zingeleta tija kwa muda mfupi na mrefu na hivyo deni kulipika kwa urahisi. Hivyo basi, utetezi wa Waziri na Serikali kwamba bado nchi inakopesheka, haina mshiko kwa sasa, bali maelezo ya kina ya kihalsia. Siyo ajabu fedha zinazokopwa zinatumika kifisadi na wajanja wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vichache vyatya mapato mpaka sasa kwa miongo mingi; Serikali imeshindwa kabisa kuongeza wigo wa kodi na badala yake inategemea kodi kutoka kwenye bidhaa kama vile bia, sigara, soda, maji na vingine vidogo vidogo. Ni kwa nini Serikali isipanue wigo hasa kodi mfano kutoka katika maeneo yafuatayo:-

- Mapato yatokanayo na sekta isiyo rasmi;
- Mapato yasiyo ya kweli mfano property tax (kodi ya majengo);
- Ardhi kubwa ambayo haijapimwa na minara ya simu; na
- Sekta ya Ardhi kupoteza mapato makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Serikali imekuwa ikishauriwa kuanza kukusanya mapato/kodi katika sekta hizi lakini imeziba masikio. Ni kwanini Serikali inasuasua kuchukua hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya Kodi isiyo ya lazima, ifike mahali sasa Serikali ifute misamaha yote ya kodi isiyo na tija wala na ukinzani katika nchi yetu. Kwa kuwa tumejulishwa kwamba Muswada wa Sheria kuhusu misamaha ya kodi utaletwa hapa Bungeni mapema kabla ya kumaliza Bunge hili. Nadhani Serikali itakuwa imezingatia maeneo ambayo yatafutiwa misamaha ili kodi iweze kukusanya na kuliletea maendeleo Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Wizara hata moja ambayo miradi yake ya maendeleo inategemea fedha za ndani kwa zaidi ya asilimia 50. Fedha za miradi mingi ya maendeleo mfano afya, elimu, maji na kadhalika imekuwa ikitegemea wafadhili kwa kiwango cha juu. Matokeo yake nchi inashindwa kufikia malengo yake pale ambapo wahisani wanapochelewa kutoa fedha au kutokutoa kabisa au kutoa kwa kiwango kidogo kuliko ambavyo waliahidi. Ni kwa nini nchi iliyopata uhuru zaidi ya miaka 50 bado haioni umuhimu kuwa na bajeti halisi inayozingatia vipaumbele vyatya nchi kwa kutegemea mapato yetu ya ndani na badala yake tunategemea wahisani ambao nao wana mambo yao muhimu ya kufanya katika nchi zao? Mbaya zaidi hata hiki kidogo ambacho Serikali inakitenga kwa shughuli za maendeleo hakitolewi kwa wakati na hata kikitolewa hakitolewi chote, hivyo kuharibuu utaratibu mzima wa miradi. Mfano, majengo mengi yamekaa muda mrefu bila kumalizwa na kuharibika, kitu ambacho kitahitaji bajeti nyingine ya ziada kuyamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ichukue maamuzi magumu ya kuanza kujitegemea kibajeti na siyo kufanya zimamoto hasa unapokaribia mwaka wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 13 kuhusu ulipaji wa deni la Taifa, kipengele cha 24 kinaonyesha kwamba hadi kufikia Aprili, 2014, malipo ya deni la ndani yalifikia Shilingi bilioni 1,694.53, ambapo kati ya malipo hayo riba ilikuwa ni Shilingi bilioni 581.20 na deni la nje limelipwa kwa kiasi cha Shilingi bilioni 340.22. Kati ya kiasi hicho, malipo ya riba yalikuwa ni Shilingi bilioni 201.52 na deni halisi yaani *principal* ikiwa ni Shilingi bilioni 138.70.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kiasi kilichokopwa na riba zinazolipwa haviendani. Kwa mfano, riba iliyolipwa kwa pesa za nje ilikuwa *almost* mara 0.5 ya pesa zilizokopwa, riba ni Shilingi bilioni 201.52 na mkopo ni Shilingi bilioni 138.70; ni kwanini? Mbona hayaingii akilini mahesabu haya? Pesa zilizokopwa zinakuwa ndogo kuliko riba, ni vipi? Naomba kupata majibu ya hiki kinachoonekana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika page 23, kuhusu mpango wa *Millennium Challenge Account Tanzania (MCA-T)* awamu ya pili unazungumzia miradi itakayofadhiliwa ya umeme na barabara za vijijini, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mpango huu, awamu ya kwanza tumeona miradi ya barabara na umeme vijijini, tunategemea sasa katika awamu hii ya pili tuone miradi mingi na ya kutosha ya barabara vijijini itakayogawiwa kwa watanzania wote kwa usawa kama ilivyo miradi ya umeme ya REA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Page 41, kuhusu mashine za ki-electronic; madhumuni ya kuwataka wafanyabiashara kutumia mashine hizi, ni kuongeza makusanyo ya kodi yasiyo na utata. Kama inaonekana mashine hizi zinaweza kusaidia sana kuongeza makusanyo ya kodi, ni kwa nini wafanyabiashara hawa wasigawiwe mashine hizo moja kwa moja na TRA bila malipo? Ikumbukwe kwamba mita za maji ni mali ya DAWASA, DUWASA na kadhalika. Mita za umeme ni za TANESCO; ni vyema mashine hizi za ki-electronic za kukusanya kodi zibaki kuwa za TRA. Lakini swali la kuijiliza; ni nani mwenye mradi huu wa kuumiza Watanzania? Ni kwa nini lazima kununua mashine hizo kwa huyo? Je, ikiharibika mtu huyo huyo anaenda tena kununua mashine nydingine mpya kwa mara ya pili? Ni kwa nini wafanyabiahsara wanalazimishwa ni lazima wakanunue mashine hizo kwa mtu huyo? Ushauri wangu ni kwamba, zigaweni mashine hizo bure na *impact* yake mtaiona juu ya ukusanyaji wa kodi. Wengi watakuwa na mashine hizo na kodi itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa mapato kulikosababishwa na tozo za kadi za simu (*SIM card levy*) kadirio la kodi kutokana na kadi za simu (*SIM card levy*) halikuwa sahihi hata kidogo! Naona suala hili lili-underwork.

Mheshimiwa Naibu Spika, *sim card* zilizonunuliwa au kwa kifupi naweza kusema kwamba kumekuwepo na ongezeko la kadi za simu; kwa mahesabu ya haraka, ni kwamba tozo la *SIM card* lingewezekana tu iwapo kama *SIM card* zote zilizonunuliwa au zinazomilikiwa zingekuwa zinatumika vizuri na angalau kuwekewa muda wa maongezi vizuri kila mwezi. Kwa hali ya Watanzania wengi uwezo wa kuweka angalau Sh. 2,000/= kwa mwezi, haiwezi kuwa rahisi hata kidogo kutokana na mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi SIM card levy hii ilikuwa itozweje? Kama sim card hizo zipo tu na haziwekewi fedha na maeneo mengine hakuna mitandao, watu wanatembea na SIM cards zao mifukoni mpaka afike mijini ndipo aazime simu atumie tena kwa message tu na kurudisha mfukoni, hivi kodi hii ilikadirwaje? Nashauri kwamba Ushauri: mwaka huu iondoke, tusikifanye tena kuwa chanzo cha mapato, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, GSPA - Government Procurement Services Agency; Kitengo hiki cha GSPA, nafikiri kiko Wizara ya Fedha; na madhumuni ya Kitengo hiki yalikuwa ni kusimamia taratibu za manunuzi kwenye Institutions za Serikali na hivyo kupunguza ukiukwaji mkubwa wa taratibu za manunuzi zinazoendelea ndani ya vyombo vya Serikali na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea sana kwamba kuanzishwa kwa kitengo hiki kungeisaidia sana Serikali ku-save pesa zinazopotea bure kutokana na mifumo mibaya ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala yake GSPA imekuwa au imeiongezea hasara nyingi sana na kubwa Serikali kinyume na matarajio. Tulitegemea wanaochaguliwa ku-supply au kutoa huduma katika vyombo mbalimbali vya Serikali, bei zao ziwe za chini na huduma zao bora zaidi kuliko walioko huko Mitaani ambao hawajaomba kuwa wazabuni Serikalini kupitia GPSA.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya GPSA ni nini? Mbona gharama zimeongezeka zaidi? Kwa mfano, ukienda madukani *maximum price* ya ream za makaratasi ni Sh. 10,000/= lakini kupitia GPSA ream hiyo hiyo inakwenda mpaka Sh. 20,000/= na zaidi, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano huu uko katika maeneo mengi, anayotenda, kwa mfano *Hospital bed* moja ni Sh. 200,000/=, wa Sh. 300,000/= anapewa, Sh. 600,000/= naye anakuwa Mzabuni, wote wanachaguliwa kuwa Wazabuni. Huyu wa Sh. 600,000/= anapeleka kitanda kile kile kwa Sh. 600,000/= kitanda cha Sh. 200,000/. Faida ya GSPA ni ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba GPSA ifutwe, haina msaada zaidi ya kuliongezea Taifa madeni na hasara. Kama haiwezekani kufutwa, ifanyiwe marekebisho makubwa, zitungwe sheria na miongozo mizuri ya kusimamia agency hii ili iweze kufanya kinachotakiwa kufanywa. Tenda zote zilizoidhinishwa sasa (2014 - 2017) ambazo ni za muda wa miaka mitatu zifutwe, wakati taratibu nyingine mpya na nzuri zikifanyiwa kazi. Wazabuni wameshachaguliwa kuwa Wazabuni kwa muda wa miaka mitatu hadi mwaka 2017, hii ni hasara.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake wote wawili kwa jitihada. Pia nampongeza kwa dhati Katibu Mkuu wa Fedha, Naibu wake na timu yote ya Wizara hii kwa kazi hiyo ngumu inayohusisha ugawaji wa fedha. Mchango wangu ni mfupi, lakini muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya ndani ya Mkoa ni kidogo mno. Mkoa Rukwa ni mionganini mwa Mikoa ambayo kwa muda mrefu ilisahaulika, inategemea Kilimo tu, Kilimo Kwanza, lakini Serikali inaidhinisha kuwa Kilimo siyo tija kwa kuzikatisha Halmashauri tamaa kutokuzilipa fedha za ushuru wa mahindi kupitia NFRA. Mikoa wa Rukwa unadai takribani Shilingi

biliioni 1.6, siyo vyema. Enyi wagawaji wa fedha, mwonee Mkoa huu huruma. Hayo ndiyo mapato yao ya ndani, shughuli nyingi zinakwama, na mwisho hata fedha za ufuutiliaji wa kilimo umekwama. Hiyo ni pamoja na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Mkaguzi Mkuu wa Serikali mbona kesi yake imesimama? Tunategemea mwezi wa Kumi kuwe na kongamano la uwekezaji, Mheshimiwa Rais ndiye Mgeni Rasmi; kama mtaona inafaa, basi shughuli za ujenzi ziendelee ili liwekewe jiwe la msingi au kuzinduliwa kama mtakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ya kongamano tunaomba tusaidiwe fedha za maendeleo za mwaka 2013/2014 – Rukwa zilizobaki. Pia tupewe mapema mwaka 2014/2015 ili tukamilishe shughuli hizo za ukarabati. Tafadhalii sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee kwa support mnayotupa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ceiling* ya Wilaya ya Nyasa ilipunguzwa ghafla, tatizo ni nini? Wilaya ile ni mpya na ina matatizo mengi, pamoja na TAMISEMI tunaomba suala hilo liangaliwe upya na irudishwe kama ilivyokuwa awali. Malalamiko ni makubwa, kwani mipango ya maendeleo itashindwa kufikiwa.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri wetu watatu na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ngumu, pia kuwasilisha ripoti hapa Bungeni ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo ningependa kupatiwa ufanuzi na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo makubwa sana katika Halmashauri zote nchini Serikali kuchelewesha pesa za miradi ya maendeleo na kusababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati au kuongezeka kwa thamani. Naomba kupata ufanuzi, tatizo hasa ni nini na ni vigezo gani huwa vinatumika katika kugawa pesa hizo za miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu, ikiwepo Halmashauri zilizopo katika Mkoa wa Iringa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuishauri Serikali kutegemea zaidi mapato ya ndani ya nchi yetu kuliko kutegemea pesa za wahisani. Tumeona miradi mingi mikubwa inategemea pesa za wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa ki-electronic, mashine za EFD, kumekuwepo na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa kuanza kutumia mashine hizo. Mfumo huu ni mzuri sana na nina imani kama wananchi watapatiwa elimu ya kutosha utasaidia sana kwa sababu ndiyo unatumia na nchi nyingi. Lakini ni vyema baadhi ya mambo yangeangaliwa.

- (i) Bei ya mashine hizo ingeangaliwa upya kwa sababu katika nchi za jirani, yaani Kenya, mashine hizo zinauzwa USD 100 na Dubai ili kila mfanyakishara aweze kununua bila tatizo na kuathiri mtaji wake.
- (ii) Ni vema pia mashine hizi zingemilikiwa na TRA wenye.
- (iii) Gharama pia za matengenezo ni kubwa mno na wafanyakazi wengi wandalalamikia gharama hizo. Hili lingeangaliwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya wafanyakazi 430 ya Sh. 649,719,150/= zilizokuwa za wafanyakazi wa Kiwanda cha TANCUT ALMASI IRINGA, naomba Serikali inipatie ufanuzi wa deni la mafao ya kuachishwa kazi kwa wafanyakazi wa kilichokuwa kiwanda cha Almasi cha Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni hilo ni la muda mrefu sana toka mwaka 1995 mpaka leo. Nilileta swalii hapa Bungeni sikuridhishwa na majibu ya Serikali yaliyotolewa. Naomba leo nipiatiwe ufanuzi wa kina wa jambo hili. Kiwanda hiki kilikuwa na mali ambazo ziliuzwa na Serikali, ni kwanini wafanyakazi hawakulipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ni vema Serikali ingeweka utaratibu mzuri wa kulipa mafao ya wastaafu hao kwa sababu kuna malalamiko ya muda mrefu ya ucheleweshaji wa malipo ya mafao kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya watumishi hao wako katika hali ngumu sana ya maisha, kiwango kilichopangwa kwa wakati huo ni vyema kingebadilishwa kutokana na hali halisi ya maisha ya sasa hivi. Ni lini sheria itabadilishwa ili mafao haya yaweze kumsaidia mstaafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni riba katika mabenki na taasisi za fedha. Ni vema sasa Wizara ya Fedha kuititia BOT ikasimamia utekelezaji wa sera ya fedha na sheria zinazohusu mashirika ya fedha na benki. Wananchi wanapata umasikini mkubwa sana wanapokwenda kukopa katika mabenki na taasisi za fedha. Viwango vya riba ni vikubwa mno vinawadhalilisha wananchi. Vilevile, kupungua kwa riba za benki kutaongeza fursa za kukopa na kusaidia wananchi kukuza mitaji yao, pia kukua kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Katika ukurasa wa 59 naipongeza sana Bodi hii kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa kwa kila mwaka, tumeona imekuwa ikiongeza pato katika mfuko wa Mkuu wa Serikali. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja iwapo nitapata maelezo ya hoja nitakayoeleza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe maelezo, katika bajeti hii ni wapi Serikali imetenga Shilingi bilioni tano ambazo NFRA inadaiwa na Halmashauri za Wilaya nchini ili Halmashauri zetu ziweze kulipwa fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha hizo na Halmashauri yangu ya Sumbawanga inaidai NFRA Shilingi milioni 400. Kutokulipa Halmashauri hizo ni kukwamisha mipango ya maendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini Serikali haitoi fedha katika Halmashauri zetu kama zilivyopangwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014? Kwani tumebakwa na mwaka mmoja na miradi ya maendeleo iliyopangwa ilishasimama. Serikali inazidi kusababisha viporo vingi vya miradi isiyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Serikali kutotoa fedha za watumishi wanazodai; fedha za likizo, fedha za kupanda kwa madaraja, fedha za uhamisho na fedha za ongezeko la mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watumishi waliokufa, Serikali huchelewa kulipa fedha zao kwa ndugu na familia zao hata kama vigezo vyote vimekamilika.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Pensheni imekuwa ikilipwa shilingi elfu hamsini kwa muda mrefu bila kupandishwa hata kama mishahara imekuwa ikipanda kila wakati. Thamani ya Sh. 50,000 ya miaka 10 iliyopita ilikuwa kubwa ukilinganisha na mwaka huu. Pensheni ipande kulingana na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingi ATM katika Benki zimekuwa haziangaliwi kama zimeharibika au la, hivyo kusababisha wateja kupata usumbufo. ATM ziwe na pesa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea watu hulipa kodi kwa asilimia mia moja, hata mtu anayechoma nyama hulipa kodi, lakini hapa suala la kodi au VAT ni hiari. Unakwenda dukani unaulizwa unataka bila VAT au na VAT.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili liangaliwe kwa umakini.

MHE. NASSIB S. OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tiketi za kielektroniki hivi karibuni tulifanyiwa semina na benki ya CRDB kuhusu mradi wa tiketi za electronic za mpira wa miguu. Wajumbe wa Kamati zote waliridhika kuwa mradi huu utaweza kudhibiti wizi wote unaofanyika pamoja na kuongeza mapato ya Serikali na mgawanyo wa fedha kwa vilabu na TFF. Hivyo tunaiomba Wizara hii ichukue hatua za haraka mradi huu uruhusiwe kuanza mara moja ili kuokoa fedha nyingi zinazoibowiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine za risiti *EFD* kuna malalamiko mengi sana kuhusiana na mashine hizi. Baadhi ya malalamiko hayo ni:-

- (i) Mashine hizi zinauzwa kwa bei kubwa sana, wakati bei halisi za mashine hizi ni ndogo.
- (ii) Mashine hizi huzima mara kwa mara na hivyo huleta usumbufo kwa wafanyabiashara na hivyo *TRA* huwapiga faini wafanyabiashara kwa kosa ambalo si lao.
- (iii) Mashine ikiharibika inabidi ipelekwe kwa wakala aliyeuza hiyo mashine. Kuna mifano mingi inayoonesha kuwa mfanyabiashara anakaa mbali na wakala, hivyo husababisha usumbufo mkubwa mashine inapoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua za dharura kurekebisha dosari hizi. Ikiwezekana mashine hizi zimilikiwe na Wizara ya Fedha kama mita za umeme zinavyoshughulikiwa na Shirika la Umeme.

MHE. LOLEIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia niwapongeze Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ndiyo Wizara mama ambapo bila ya Wizara hii kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa wakati hakuna jambo lolote litakalofanyika katika Wizara nyiningine. Mfano, TAMISEMI ambapo ndiko miradi mingi inakotekelawa, inahitaji sana ushirikiano kutoka Wizara ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba fedha za miradi zipelekwe kwa wakati. Mara nydingi fedha hupelekwa kwenye Halmashauri zetu mwishoni mwa mwaka wa fedha kiasi kwamba miradi haitekelezwi kwa wakati. Nashauri Serikali ipeleke fedha za miradi kwenye Halmashauri kwa wakati, hii itaboresha ufanisi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya wastaifu yamekuwa na changamoto kubwa sana. Wastaifu walio wengi hasa walio vijijini wanasumbuka sana wakati wa kufuatilia haki zao. Wengine wana miaka 10 wanadai pensheni zao bila mafanikio. Hivyo naiomba Wizara iendelee kuboresha utaratibu wa utoaji mafao ili kurahisisha upatikanaji wa pensheni kwa wastaifu hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunaiomba Serikali iweke utaratibu wa kutoa pensheni kwa wazee wetu ambao hawakuwa wafanyakazi wa kuajiriwa yaani wakulima ambao nao wametoa mchango wao mkubwa katika pato la Taifa. Naomba nipate maelezo wakati wa majumuisho ni namna gani Serikali imejipanga kuwalipa pensheni wazee hawa ambao hawapo kwenye utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya ndani katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema kuwa mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kulipa madeni ya ndani na nje. Nazidi kutoa msisitizo mkubwa kwa Wizara kulipa madeni ya watumishi mbalimbali wakiwemo Walimu na watumishi katika sekta ya afya kwani madeni ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Geita madeni ni makubwa sana. Sekta ya afya pekee (Geita) inadai kiasi cha millioni mia nne. Ili watumishi wafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa ni vema Serikali iangalie namna ya kumaliza madeni ya watumishi. Naomba nipate ufanuzi ni namna gani Wizara ya Fedha imejipanga kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na madai ya watumisshi wapo wazabuni wanaozidai Halmashauri kwa kutoa huduma. Wengine wana miaka mitatu wanadai bila kulipwa. Hii ni kuwarudisha nyuma wafanyabiashara wazawa kwa kushikilia mitaji yao kwa muda mrefu. Naomba hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo, naomba ufanuzi wa kina na naunga mkono hoja.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini suala la matumizi ya dola badala ya shilingi linazidi kupamba moto. Fedha yetu inadharauliwa hasa na Waasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi katika biashara zao, kama vile ununuzi na uuzaji wa tiketi za ndege, abiria huchajiwa kwa dola. Aidha, nyumba nyingi za kupangisha zinatoza wapangaji kwa dola. Tuheshimu fedha yetu na hivyo tuitumie katika shughuli zote za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wastaafu waliotumikia Taifa hili kwa jasho lingi na kwa uzalendo mkubwa, lakini kupewa mafao yao inakuwa kero kubwa hasa wastaafu wa lilokuba Shirika la Afrika ya Mashariki lililovunjika mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana endapo Serikali itashindwa kuwapa wastaafu hao wa Afrika ya Mashariki mafao yao. Machozi ya hao wazee na manungu'niko yao huenda ndio sababu ya matatizo mengi yasiyokwisha katika jamii yetu, hayo ni mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wastaafu waliotumikia idara mbalimbali za Serikali wanazungushwa sana kupata fedha zao. Kwa taarifa niliyopata yeye hupewa fedha zake kila baada ya miezi mitatu mitatu. Kiwango chenyewe anachopewa hakijapanda kwa muda mrefu. Serikali ipitie upya viwango vyta wastaafu wa muda mrefu na viwango hivyo vipandishwe na walipwe kila mwezi ili kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kutoa elimu ya matumizi ya mashine za EFDs, bado wafanyabiashara wengi na hasa Dar es Salaam hawapendi kutumia mashine hizo, aidha bei yake ishushwe ili wengi wasiendelee kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA ihakikishe kodi inalipwa ipasavyo. Wapo wengi wenye Super Markets, unaponunua bidhaa unaulizwa kama unataka risiti. Ni aibu sana kuona kwamba kodi haillipwi ipasavyo. Aidha, haikusanywi ipasavyo. Pasipo kukusanya kodi kwa ukamilifu ni kazi bure, wajanja wataendelea kuinyonya nchi hii kwa kutolipa kodi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuitia maandishi nichangie Wizara ya Fedha. Hii ni Wizara inayohusika na kusimamia Taasisi zote muhimu zinazohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Ili kuleta maendeleo na ustawi wa nchi hii basi ni dhahiri kuwa Wizara hii inapaswa kuimarishwa pamoja na Taasisi husika ili tukusanye kodi na ushuru kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA walitegemea mwaka huu kukusanya milioni 10.395 mpaka mwisho wa Aprili wamekusanya milioni 7.772. Kwa kasi hii ni wazi kufikia mwisho wa mwaka, katu hawatafikia lengo, watafikia milioni 9.33 tu. Nimepitia sababu zilizotolewa na Serikali juu ya upungufu au udhaifu katika ukusanyaji, nakubaliana nazo, lakini kuna fursa hazikutumika ambapo kimsingi zingeweza kupunguza pengo au hata kuziba pengo hilo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA ni moja kati ya Port Community. Utendaji wa TRA katika upitishaji wa mizigo bandarini umekuwa kikwazo kwa wadau wengine watumiao bandari, watumiqaji wa bandari wamekuwa wakiongezewa mizigo wa gharama na kutohana na utendaji wa TRA – utendaji wa asasi hii unapelekea mizigo kukaa muda mrefu bandarini hatimaye gharama za kuhifadhi mizigo ambazo ni kubwa. Hii hupunguza faida ya mfanyabiashara kama si kuua biashara kabisa. Moja ya chanzo cha kupungua kwa mapato toka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo TRA ina fursa ya kuongeza mapato ni kuchangamsha shughuli. Sekta ambayo kama Taifa tumeshindwa kuitumia ni mahali tulipo –

Location Advantage, nchi jirani kwa kiasi kikubwa zinategemea kusafirisha mizigo yao kwenda na kutoka ughaibuni kupitia Tanzania. Ni ushauri wangu kuwa kama TRA kwa niaba ya Serikali wangetengeneza mazingira stahiki, sekta hii ingeweza kuingiza pato kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukulia usafirishaji wa mafuta jamii ya petrol kwenda nchi jirani kama mfano, bidhaa hii inaingizia kipato Serikali pato lisilokuwa la moja kwa moja ni biashara kwa wauzaji wa magari, vipuri na garage, wote hawa wakiwa na biashara kubwa na wakidhibitiwa ni wazi watatoa mchango kwa TRA. Mizigo yote inayopita bandarini hulipa ushuru/tozo – wharfage charges. Hili ni pato kwa TPA na makampuni husika ambayo hatimaye hulipa ushuru/kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta yashukayo Dar es Salaam asilimia zaidi ya 40 ni mafuta yaendayo nchi za nje. Kwa mazingira stahiki nchi jirani wako tayari kupitisha mafuta yao nchini kiasi ambacho ni mara tatu ya shehena ipitayo hapa hivi sasa. Kwa kila lori lipitalo Dar es Salaam huchangia fuel levy na tozo ya REA kiasi cha takribani sh. 700,000 tripu zaidi ya elfu sabini hufanyika kuondoa lita bilioni takriban mbili zinazokwenda nchi jirani kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo cha mizigo zaidi wa mafuta usipite hapa ni muda wa mafuta yaendayo jirani kukaa nchini. Mafuta yaendayo nchi jirani yanatakiwa kukaa nchini si zaidi ya siku 30. Muda huu unaifanya njia ya Dar es Salaam ikose faida ya kiushindani kwa bandari za Beire na zile za Afrika Kusini. Bandari shindani hutoa muda wa siku 180 na 120 kama ziliviyotajwa. Muda huu hupunguza gharama za usafirishaji kwani magari machache yale huzunguka zaidi, lakini pia wateja wa mwisho wanakuwa na uhakika wa kupata mizigo wao kwani hakuna *localization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kupitia TRA waongeze muda mpaka siku 90 ili tuvutie shehena hii kupita nchini na tuivutie fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na nawatakia kila la heri katika majukumu yenu ya kila siku katika mustakabali wa nchi yetu. Ombi langu kwa Wizara msioope changamoto, changamoto ziwe fursa kwenu. Mjitume ili muweze kutuvusha msioope maneno makali na hata yale ya upole lakini yenye hisia kali, chapeni kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo. Hili la changamoto kuwa fursa ni pia kwa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo Makubwa Sasa (BRN) hatuwezi kuyafikia endapo ninyi tulio wapa dhamana ya kusimamia vyombo, taasisi au mashirika haya hamtakuwa wabunifu, kuweni wabunifu muwe na mawazo mapya yanayoendana na hali ya sasa ya sayansi na teknolojia, mkiamua nchi hii itasonga mbele na kwa pamoja tukiamua nchi itasonga mbele tusifanye kazi kwa mazoea tubadilike Serikali inatukanwa inakosolewa mpaka sisi tunaoipenda tunaona aibu, fanyeni kazi zenu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niyapongeze Mashirika yaliyo chini ya Wizara yako: GBT Shirika hili linafanya kazi zake vizuri sana, hata 10% ya gawio Serikali linalipa kila mwaka na hii ni kujituma na kuwa wabunifu kuendana na mahitaji ya wateja, endeleeni hivyo, lakini ni lini GBT katika kiwanja chenu kilichoko eneo la Victoria DSM ujenzi utaanza? Nataka kujua ni lini ujenzi utaanza, ujenzi huo na jengo likikamilika GBT itakuwa imepata chanzo kipyga cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, PPF naipongeza sana kwa kazi nzuri sana inayoifanya, inafanya kazi yake kwa weledi mkubwa, naomba PPF punguzeni malalamiko ya wateja wenu. Nawapongeza kwa kusaidia kutoa misaada katika maeneo mbalimbali katika huduma za jamii, msioope wala msitishike, fungu la kusaidia jamii lipo na halijawekwa leo, hivyo msipotoa misaada kwa jamii katika kusaidia shule, zahanati, maafa na kadhalika, zaidi ya hapo mtasaidia wapi? Simamieni mambo yenu ili mradi mnafuata sheria, kanuni na taratibu za PPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza TRA kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato ya nchi yetu, najua mnapambana na changamoto nyingi kutokana na hali halisi ya sasa. Nyie TRA ndiyo moyo wa nchi hii, mkiteleza basi nchi nzima itapata kiharusi, angalieni pato penye mianya ya ukwepaji kodi pazibwe haraka ili mapato na malengo yenu yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Twiga Bancop, hii inafanya kazi katika mazingira magumu hasa kutokana na mtaji wake kuwa mdogo lakini pia niwaombe Serikali ifanye haraka kuimarisha uongozi ili kuondoa kasoro ndogo ndogo zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yafuatayo yafanyike:-

Kwanza, vikundi vya hisa chini ya utaratibu wa Village Savings and Loan Association (VSLA) pamoja na vikundi vya VICOBA vitambulike rasmi na kuwekwa katika utaratibu unaotambulika wa kupata mikopo na fursa mbalimbali kutoka Benki Kuu.

Pili, kuhakikisha usimamizi mzuri wa mapato na utoaji wa fedha kwa Halmashauri na Taasisi mbalimbali za Serikali ili bajeti inayokusudiwa iweze kutekelezwa.

Tatu, kusimamia vizuri matumizi ya dola hapa nchini ili kulinda thamani ya fedha yetu. Nne, kubuni mbinu mpya za kukusanya mapato ya Serikali.

Tano, kuweka mikakati kabambe ya kuziba upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe pongezi zangu kwako wewe Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Katibu Mkuu na Manaibu wake, watendaji wote wa Wizara, Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa utendaji mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inafanya kazi vizuri lakini inakabiliwa na changamoto nyingi sana hadi kupoolekea kuchelewa kwa fedha ambazo zimeombwa na Wizara mbalimbali ili ziweze kutekelezza majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wiki tatu tu tunamaliza mwaka wa fedha wa 2013/2014, lakini tatizo fedha ambazo Bunge liliidhinisha kwenye Wizara hazijatolewa, je, ni vipi utekelezaji wa kazi hizo utafanyika? Naomba nipatiwe majibu ni vipi Wizara hizo zitafikia malengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na makusanyo ya fedha ya kutosha, marekebisho ya Sheria ya Kodi Muswada wake uletwe haraka sana Bungeni ili tuujadili. Hapa naipongeza Serikali kwani vyanzo vya mapato vitaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kupitia Mashirika ya Hifadhi ya Jamii ya PPF, NSSF, PSPF na LAPF. Mashirika haya yamekuwa yakifanya kazi zake kwa kiwango cha hali ya juu katika kutekeleza majukumu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) hiyo yote ni kutokana na usimamizi makini chini ya Waziri na Naibu Mawaziri mliopo, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, mimi nakuja moja kwa moja kwenye changamoto ambayo nikutopata fedha kwa wakati ambazo ni fedha za maendeleo ambazo fedha hizi zinatoka kwa wafadhili au mikopo kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kila mwaka hali hii inajitokeza kwa hiyo hivi sasa ni lazima tuitafutie dawa. Dawa ninayojua ni kuachana na bajeti tegemezi. Tuvitumie vyanzo vya mapato vipya ambavyo vimependekezwa na Kamati ya Bajeti ambayo na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka huwa tunategemea vyanzo hivyo hivyo (vinywaji), bila kuongeza vyanzo vya mapato ili kuondokana na utegemeki itakuwa ni ndoto. Tujipange tuweze kutumia matumizi ya kawaida na angalau katika fedha za maendeleo tuchangie nusu yake kutoka mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tunayoendelea nayo fedha za maendeleo kuna Halmashauri nyiningine zimepata asilimia 25 kati ya fedha zilizopangiwa na imebaki miezi miwili tu na ni vigumu kupatikana hizi fedha za ndani na za nje, kuna miradi mingi hivi sasa ambayo imesimama kutokana na kupatikana kwa fedha kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa TRA bado si waadilifu, bado mapato yanavuja, ni vyema Serikali ikazidi kuwafuatilia hawa wafanyakazi na wasiwaache muda mrefu kukaa sehemu moja kila baada ya miaka mitatu wapate uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wamefikia wapi kuhusu mashine ya EFD?

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri wake wote wawili wamethhubutu, wameweza iyobaki wasonge mbele.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, watendaji walio Wizarani na wanaohudumu katika taasisi zinazosimamiwa na Wizara. Mnafanya kazi nzuri katika mazingira magumu sana. Naamini mngependa malalamiko yote yaishe ila udogo wa keki na wingi wa midomo inayotamani keki hiyo ndogo ndivyo vitu vinavyosababisha malalamiko yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, kwa kuzingatia kuwa benki za wananchi duniani kote ndizo zinatumika kuwaingiza raia wa ngazi (kipato) ya chini katika uchumi wa fedha (monetized economy) na kuzingatia kuwa benki nyingi za wananchi hapa Tanzania zimekuwa na rekodi nzuri, ni sababu gani imefanya Benki Kuu kuweka masharti mazito kwa wananchi wa kawaida kuanzisha benki zao?

Je, Wizara na BOT hamuoni kuwa benki za wananchi zikisaidiwa kuanza na zikasaidiwa kukua ndizo zitakuwa benki za biashara zinazomilikiwa na Watanzania? Wizara na BOT hamuoni kuwa kuweka masharti magumu ni kuendelea kuwawekea mazingira mazuri wageni kumiliki

sekta ya fedha (na kwa maana hiyo, uchumi mkuu) huku wazawa wakibakia na biashara za vitumbua, juisi au kwa wenyewe bahati SACCOS?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni mkakati gani mlionao wa kulegeza masharti ili wananchi waweze kuanzisha benki zao na kunufaika na uchumi wa fedha wa Tanzania?

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hotuba ya Wizara ya Fedha ila naomba maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la riba ya mabenki, kuna utitiri wa mabenki mengi hapa Tanzania na hii inathibitisha ya kuwa biashara ya benki imekuwa haraka na faida kubwa wanapata. Je, Serikali kwa kupitia BOT ni lini mtadhibiti riba katika benki zetu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo suala la risk hakuna siku hizi. Kuna bima na dhamana ya mishahara hasa kwa Wabunge/wafanyakazi wa Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu DRT (mabasi ya kwenda kasi), kwanza niwapongeze kwa mradi huu ila kuna tetesi ya kuwa nauli za mabasi hayo itakuwa ni ya juu na Serikali itachangia kwa watumiaji. Kuna uvumi umeenea nauli ya kutoka Kimara/Kigamboni itakuwa shilingi 2,500/= na abiria atalipa shilingi 1,500/=, je, kuna ukweli katika taarifa hii ambayo ipo kwenye mitandao?

Mheshimiwa Spika, mwisho Mheshimiwa Waziri tufahamishe hatua ya UDA kwani kuna taarifa mbalimbali zinazotolewa Serikalini hasa juu ya uhahali wa hisa. Kwani kuna taarifa ya kuwa Serikali hisa zake ni asilimia 49 na Jiji ni asilimai 51, je, ukweli ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, taarifa za Kamati za Bunge kuhusu UDA, Serikali inasemaje kwani mnatuchanganya humu ndani ya Bunge?

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndio inayokisia mapato na matumizi ya Serikali kwa kila mwaka katika kupanga na matumizi ya Wizara mbalimbali, ni Wizara hii pia ndio inayoweka kikomo (ceiling) kwa matumizi ya huko Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kuwa karibu inavyozidi zaidi ya miaka minne sasa makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali hayawiani hususan kwenye fedha za maendeleo za Wizara. Fedha inayoidhinishwa na Bunge hasa kwa fedha ya maendeleo kwa Wizara karibu zote huwa upatikanaji wake ni wa kiwango cha chini kinyume na fedha iliyotegemewa na Wizara wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai wa makisio wa fedha pungufu za maendeleo tuangalie bajeti ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012 ambapo fedha iliyoidhinishwa na Bunge sio fedha halisi iliyotolewa na Serikali kwa Wizara zinazounda Serikali wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa maendeleo ni shilingi trilioni 3.75 lakini zilizotolewa na Wizara ni shilingi trilioni 2.22; hapa palikuwa na upungufu wa fedha za maendeleo shilingi trilioni 1.52 ambayo ni sawa na asilimia 41. Mwaka 2011/2012 fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi trilioni 4.31 na zilizotolewa na Wizara ni shilingi bilioni 3.38 hapa kuna upungufu wa shilingi bilioni 926.57 sawa na asilimia 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndio halisi ya fedha ya maendeleo zinavyokisiwa na fedha zinavyotolewa. Je, hali hiyo inasababishwa na nini? Mbona hali hiyo inajirudia kila mwaka? Je, makisio ya mapato ni ya juu sana ili kujifurahisha kuwa kila mwaka kuna ongezeko la mapato. Nadhani imefika wakati sasa Wizara kufikiria upya namna wanavyokisia mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya fedha za maendeleo zinavyotolewa inatisha sana hata kwa mwaka 2013/2014. Mfano hai umeonekana Ikuu, fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge shilingi bilioni 59.58 zilizotolewa ni shilingi 40.90 sawa na asilimia 69. Bunge fedha ya maendeleo nusu shilingi bilioni 8.88, na fedha iliyotolewa mpaka Machi ni shilingi bilioni 2.95 sawa na asilimia 36 na Mahakama fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge shilingi bilioni 42.71 na fedha ambayo imeshatolewa mpaka Machi, 2014 ni shilingi bilioni 5.50 sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni ushahidi mwagine kuonesha kuwa makisio yetu ya mapato sio sahihi au yapo malengo yanafanywa nje na makasio ya mapato na matumizi. Ahsante.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie riba ya mabenki ni kubwa sana kiasi kwamba inakuwa ni mzigo kwa waliokopa. Hivyo nashauri riba hizi ziangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaifu wa zamani wanalipwa kidogo sana kiasi kwamba hawawezi kumudu hata kununua chakula kwa mwezi. Nashauri Wizara iangalie kuongeza kiwango kutegemea na kupanuka kwa thamani ya shilingi, pia kulingana na gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika ukusanyaji wa kodi ni muhimu kuangalia vyanzo vingine vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wazabuni yanatakiwa kulipwa ikiwemo madeni ya maji ya Bodi ya IRUWASA ambayo taasisi za Serikali zinadaiwa ikiwemo Magereza na Polisi. Wizara isaidie kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopangwa wakati wa bajeti zipelekwe kutekeleza miradi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuwa katika Wizara hii na pia kwa uchapaji kazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, dollarization hili ni tatizo kwa nchi yetu yaani inasikitisha sana tunavyotumia dola kama vile tupo Marekani. Jambo hili linayumbisha sana fedha yetu na kuidhalilisha. Tunaiomba Serikali iliangular suala hili na kulichukulia hatua tafadhalii, hakuna kisichowezekana. Leo Zambia wamefanikiwa huwezi kununua chochote au kufanya malipo yoyote kwa kutumia dola lazima ubadilishe fedha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, EFD ni utaratibu mzuri sana wa kukusanya kodi. Tatizo kubwa la mashine hizi ni bei kwa kweli wafanyabiashara, malalamiko yao makubwa ni bei kuwa kubwa kwani watu wanasaferi huko nje na wanazona mashine hizo hivyo bei zake zinajulikana. Sasa kwa nini huyo wakala anaiza bei kubwa? Lakini pia baada ya wakala huyo kuwauzia kwa cash ni vyema wakapewa halafu wakakatwa kidogo kidogo hiyo ingewashawishi wafanyabiashara wote.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, naiomba sana Serikali itoe kipaumbele katika kulipa madeni yote ya Mifuko ya Jamii kwani fedha hizi ni za Watanzania, kutokuilipa Mifuko hii ni kuidhoofisha Mifuko.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kuwa mahali hapa ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha ya Mwaka 2014/2015. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuandaa bajeti nzuri kwa masilahi ya Maendeleo ya Taifa letu. Vilevile nichukue fursa hii pia, kuipongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na Wataalamu kwa ujumla wao, kwa kuandaa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Taifa letu linavyokwenda, Serikali haina budi kuandaa bajeti yenye kukidhi mahitaji kwa mustakabali wa hatima ya Taifa letu. Bajeti yetu kila mwaka imekuwa hajijitoshelezi, kwa namna moja ama nyininge tumekuwa tukitegemea misaada kutoka nje ili kuweza kufikia lengo la Bajeti ya Serikali. Hali hii ndiyo inayosababisha kutokufikia malengo katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo kutokana na kuwa na bajeti finyu, kutokuwa na vyanzo vya kutosha vya kujipatia fedha zetu wenyewe za ndani, hakuna njia mbadala zaidi ya Serikali kurekebisha sheria mbalimbali ambazo zitasaidia kuongeza pato la ndani ili kuondokana na utumwa tuliokuwa nao wa deni letu la nje ya nchi kukua na kutokuweza kama Taifa kujitosheleza hata nusu ya bajeti zetu.

Lazima sasa Serikali ije na mikakati endelevu ya kuliwezesha Taifa kujitegemea katika bajeti zake na si kuwa tegemezi kutoka kwa nchi hisani. Lazima tukubaliane kubadilisha baadhi ya sheria ambazo zimekuwa zikisababisha upotevu wa fedha nydingi ambazo zingelipwa kodi Serikali na hivyo kusaidia kwenda kufanya shughuli za kimaendeleo ambazo kwa asilimia kubwa zimesimama na hivyo Wananchi kuendelea kuishi katika mazingira magumu. Kuna wajibu pia wa Serikali kuangalia hali ya Mtanzania anayeishi kwa wastani wa dola moja. Dunia ya leo binadamu kuishi kwa dola moja ni jambo la ajabu sana na linaloshangaza. Hapa kwetu Wananchi wamekuwa katika hali hiyo kwa muda mrefu sasa, ni wajibu sasa wa Serikali kuchukua hatua za haraka kuwaondoa katika hali hiyo, kwani Taifa letu limejaaliwa rasilimali mbalimbali ambazo haziwanufaishi watu wetu, bali zinawanufaisha watu wachache na hivyo kupelekea watu wetu kuendelea kuishi katika mazingira duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima izingatie uboreshaji wa bajeti katika Wizara zinazogusa moja kwa moja jamii, hususan Wizara ya Kilimo na Mifugo. Wizara hii imekuwa ikilalamika kutengewa fedha kidogo ilhali kuna matatizo mengi yanazozikabili Sekta za Mifugo na Kilimo. Lazima Serikali ikumbuke kuwa, Wananchi walio wengi wako vijijini, ambao ni

wafugaji na wakulima. Tusipowaboreshea wafugaji na wakulima hali zao, kuwapatia pembejeo za kutosha, mbolea nzuri na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwapa elimu juu ya ufugaji bora na kilimo cha kisasa, basi tutakuwa hatujafanya kitu, ni lazima kuonesha nia zaidi kwa jamii hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni 19.7 katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, tofauti na shilingi trilioni 18.2 ya mwaka huu wa fedha unaoishia Juni 30. Katika fedha hizo, matumizi ya kawaida yamepangwa kuwa shilingi trilioni 14.2, ambapo kati ya hizo, shilingi trilioni 5.1 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Serikali, Taasisi na Wakala wake. Aidha, shilingi trilioni 4.4 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi trilioni 4.4 kwa ajili ya matumizi mengine.

Kwa upande wa matumizi mengine ya maendeleo, asilimia 63 inagharimiwa na fedha za ndani. Hali hii inatudanganya kujiona sasa kama tunaweza kujitosheleza wakati bado hatujafikia kiwango cha kujitosheleza katika bajeti ya nchi. Katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), bajeti ya mwaka huu imeainisha itajielekeza katika maeneo sita ya Kitaifa ambayo ni kilimo, elimu, maji, utafutaji rasilimali fedha, nishati na uchukuzi na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara. Hizi zimekuwa ni kauli za kila mwaka kwa Serikali kutamka kuwa itajikita katika maeneo fulani lakini baadaye kutotekeleza azimio lake.

Naishauri Serikali sasa katika vipaumbele vyake ilivyovitaja hapo awali, ihakikishe inavifanya kazi kwani uwekezaji katika kilimo unahitajika kwa nguvu zote. Lazima ifike mahali sasa nchi zilizoendelea ziwe zinakuja kununua chakula hapa kwetu. Hakuna sekta ambayo itamtoa Mtanzania katika hali ya umasikini kama kilimo, endapo tu Serikali itawekeza na kuwawezesha wakulima wetu kufanya kilimo chenye tija. Vilevile naiomba Serikali ituletee Muswada wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ili ifanyiwe marekebisho ambayo yatasaidia kuongeza pato kwa Serikali katika kupata kodi. Ifike mahali sasa tujivunie na rasilimali tulizonazo na kuacha kutoa misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa. Misamaha hii inatufanya tuonekane kama vile tunayabembeleza makampuni haya ilhali wao ndiyo wanaotakiwa kutubembeleza kwa kuwa sisi tuna rasilimali ya kutosha. Muswada huo utaongeza wigo wa kodi kwa kuimarisha vyanzo viliyopo na kuainisha vyanzo vipyaa pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi, ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchumi Mkuu (*Microeconomics*) ni elimu juu ya picha kamili ya uchumi, yaani njia ambayo utajiri unapatikana na unagawanywa. Inaweza kuwa elimu kuhusu nchi maaluma au dunia nzima na jinsi tofauti zinavyoingizwa katika picha nzima ya dunia. Kuna majadiliano yanayoendelea hapa nchini kama ya matajiri wanazidi kutajirika na maskini wanazidi kuwa maskini zaidi, tufanye nini kuhusu jambo hili? Serikali ijiingize kiasi gani katika uendeshaji wa soko huru? Kwa kuzingatia uharibifu wa mazingira; je, ukuaji wa uchumi usiodhibitiwa unatakiwa? Haya ni mambo tunayotakiwa kujuliza kwani tukipata majibu yake yataleta tija kubwa sana.

Kuna jambo lingine la uchumi kuwa imara (*Microeconomic Stability*); haya ni matokeo ya kuwa na kodi ya Hazina, Sera za Fedha na kiwango cha kubadilishana fedha inayokusudiwa kufikia malengo ya uchumi mkuu kama vile ukuaji wa uchumi, kupanda kwa gharama za maisha, madeni ya nje na akiba halisi ya Kimataifa. Suala hili ni lazima Serikali iliangularie ili kuleta mapinduzi. Vilevile kuna uchumi mdogo (*Microeconomics*), hii ni elimu kuhusu jinsi vivanda, sekta fulani, biashara au kaya zinazofanya kazi. Mambo haya ni lazima yafanyiwe utekelezaji ili kuondoa hili wimbi la umaskini kwa watu wetu.

Jumla ya Pato la Taifa (Gross Domestic Product – GDP) ni kipimo cha jumla cha pato la utajiri ambalo linapatikana nchini katika muda maalum. Kwa maneno mengine, Pato la Taifa ni tathmini ya bidhaa zote na huduma ambazo zinaundwa na zinabadilishwa kwa fedha. Kwa mfano, kama jumla ya thamani ya bidhaa na huduma mwaka huu ni asilimia moja zaidi kuliko ya mwaka jana, basi ukuaji wa pato la utajiri ni asilimia moja. Jumla ya Pato la Taifa (GDP), huacha kazi zingine za thamani ambazo zingeweza kujumuishwa; kwa mfano, uendeshaji wa kaya na familia kwa kupata nishati rahisi na maji na pia watu kujenga nyumba zao kwa kutumia vifaa vya asilia na ustawishaji wa vyakula kwa ajili ya matumizi yao. Jumla ya Pato la Utajiri (GNP) ni sawa na jumla ya Pato la Taifa, lakini unaongezea biashara ya ndani na biashara ya nje. Ukuaji halisi (*Real Growth*); kwa vipengele vyote viwili jumla ya pato la utajiri (GDP) na ukuaji wa pato la utajiri (GNP), kama ukuaji ni asilimia saba kwa mwaka, lakini mfumko wa bei umekua asilimia tano, basi ukuaji halisi ungekuwa asilimia mbili tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kuliangalia ni mfumko wa bei (*Inflation*). Kipimo cha kupanda kwa bei kati ya mwaka mmoja na mwaka unaofuata hasa ukizingatia wazo la kupata vifaa vya madukani au sokoni (i) mtaji wa jamii (*Social Capital*) ni kama gundi inayounganisha pamoja familia, makundi na jumuiya. Inahusisha imani, desturi na tabia za jamii ambazo husaidia kufanya kazi pamoja kwa uthabiti katika makundi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi. (ii) Vyama vya Jumuiya (*Civil Society Organisation*), inahusisha vyama rasmi ambavyo vimesajiliwa na Serikali na vile visivyo rasmi. Vyama hivyo ni pamoja na vile vya hisani, dini, vya shughuli maalum, kundi shawishi, kitaaluma na vyama vya makundi maalum kama vile Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Wanafunzi. Vyama visivyo rasmi ni pamoja na upatu, vyama vya makabila, mpira wa miguu ambavyo vinaundwa na vijana wa kiume na netiboli vinavyoundwa na vijana wa kike.

(iii) Matayarisho ya bajeti inayozingatia maskini (*Pro-poor Budgeting*) na usimamizi wa matumizi (*and expenditure monitoring*). Fedha zinatengwa katika bajeti kwa ajili ya programu zinazowalenga watu maskini, lakini fedha hizi zinapaswa kupitia Hazina, Wizara inayohusika, Serikali za Mikoa na Halmashauri za Wilaya au Miji na Kitengo cha Huduma (kama Shule au Hospitali), kabla ya mtu maskini kupata faida. Kwa usimamizi thabitii, fedha hizi zinaweza kutumika vizuri na kuwa na tija kwa Wananchi. (iv) Bajeti za Serikali (*Government Budget*), Serikali ni kama familia ambayo inapaswa kuweka uwiano kati ya fedha zinazoingia na fedha zitumikazo. Kama hakuna fedha zinazoingia Serikali inapaswa kuamua itumie kiasi gani na isitumie kiasi gani.

Utaratibu wa kukusanya taarifa hii na kufanya uamuzi ndiyo huitwa bajeti ambayo ni lazima tuijishe hapa Bungeni na bajeti hiyo ni lazima iwe na vipaumbele vinavyoteklezeka kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hivyo basi, kuna haja ya Serikali kuzingatia vipaumbele hivyo ili kuleta tija kwa Taifa.

Kuungeza kodi ni jambo lisilopendwa na baadhi ya kodi nyingine ni mzigo mkubwa kwa watu maskini kuliko watu matajiri. Mikopo ni mizuri kuziba mapengo ya muda mfupi na kuanzisha biashara mpya, lakini lazima mikopo hiyo ilipwe. Misaada inakaribishwa bali hatuwezi kupata misaada wakati wote, hivyo kama nchi tusitegemee misaada zaidi kuliko kutafuta njia zetu wenyewe za vyanzo vya mapato. Vilevile fedha za umma ni sehemu ya uchumi ambayo hushughulika na ubunifu wa bajeti ya mapato na matumizi ya kitengo cha sekta ya umma.

Mada hii hushughulikia masuala kama vile malipo ya ushuru, ni nani hasa analipa ushuru Fulani, uchambuzi wa gharama na faida ya mipango ya Serikali, athari juu ya ufanisi wa kiuchumi na ugavi wa mapato katika aina tofauti za matumizi na ushuru na siasa za kifedha. Jambo hili la mwisho, ambalo ni kipengele cha nadharia ya chaguo la umma, hubuni tabia ya

sekta ya umma kama mfano wa uchumi wa kiwango cha chini, unaohusisha maingiliano ya wapiga kura wanaojali masilahi yao wenyewe, wanasiwa na Wafanyakazi wa Serikali au Mashirika mengine.

Wingi wa uchumi ni wa manufaa, kwani hutafuta kueleza na kutabiri matukio ya kiuchumi. Uchumi wa kuamua thamani (*normative economics*), hujihusisha na kubaini liliilo zuri au baya kiuchumi. Uchumi wa ustawi ni tawi la uchumi wa kuamua thamani, unaotumia ustadi wa uchumi wa kiwango cha chini ili kubainisha kwa wakati huohuo ufanisi wa ugavi katika uchumi na ugavi wa mapato unaohusishwa nao. Huwa unajaribu kupima ustawi wa jamii kwa kuchunguza shughuli za kiuchumi za watu wanaobuni jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ni vyema baada ya bajeti kupita, basi kuidhinisha fedha hivyo mapema katika Mawizara ili utekelezaji wa Miradi mbalimbali uanze kazi mara moja. Kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa fedha na hivyo kufanya Miradi mingi kutokukamilika kwa wakati na mingine kuchukua muda mrefu kuisha. Tunaamini kuwa, Serikali ni moja hivyo basi ni vyema kufanya kazi kwa ushirikiano unaotakiwa. Kwa mfano, kuna baadhi ya Taasisi za Serikali haziwezi kukopesheka bila kuwa na udhamini wa asilimia mia moja kutoka Serikalini hasa Wizara ya Fedha.

Kumeonekana kuna baadhi ya maendeleo yanazoroteshwa na Wizara kutokubali moja kwa moja kuwa wadhamini wa taasisi hizo na hivyo kuziwezesha kupatiwa mikopo hiyo kwa Wizara ya Fedha kutoa udhamini wa asilimia chache. Hali hii imekuwa ikijitokeza kwa baadhi ya taasisi hizo za Serikali na hivyo kurudisha juhudini nzima za maendeleo. Lazima sasa Serikali ikubali kufanya kazi kwa kushirikiana na ikizingatiwa Wizara hii ndiyo Wizara Mama; hivyo, haina budi kutoa ushirikiano wa kutosha pindi inapotokea hali kama hiyo ili kuleta ufanisi katika Miradi mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilete Azimio au Tamko kuhusu kizungumkuti cha Shirika la UDA.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali juu ya ukusanyaji kodi. Nchi itaendeshwa kwa kodi hivyo ili kukusanya kodi bila shuruti, kwanza, Serikali ipunguze bei ya mashine za risiti kwa wafanyabiashara wadogo. Pili, ije na mpango kabambe wa kuwashirikisha Wananchi kuwepo na mrejesho wa fedha kwa watakaofikisha kiwango fulani cha matumizi yenye risiti aliyotumia Mwananchi mmoja mmoja. Kuwekwe viwango vya Madaraja I, II, na III kulingana na maeneo ya nchi. Hii itafanya kila Mwananchi addai risiti kwenye bidhaa anayonunua akitegemea kurejeshewa gawiyo la mwezi. Hivyo, itawalazimu wenyewe kuuza bidhaa kuona umuhimu wa kuwa na mashine za risiti, la sivyo hatapata wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni ushauri wangu.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kushika nafasi muhimu ya kuongoza Wizara ya Fedha mkiwa vijana, kwa maana ya wewe Waziri na Manaibu wako wawili. Maoni yangu ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua dhamira ya Waziri na Manaibu wake kuhusu masilahi ya Watumishi wa Umma. Naomba Mheshimiwa Waziri, awakumbuke Wafanyakazi 284 wa uliokuwa Mgodi wa Chumvi Uvinza, ambao jumla wanadai shilingi milioni 340. Hiki ni kiasi

kidogo cha mafao ya kila mstaafu na mpaka sasa zaidi ya robo ya wastaafu wamefariki. Namshukuru Waziri aliyetangulia, Mheshimiwa Mgimwa, kwa hatua alizochukua kuhakikisha CHC wanahakiki madeni na deni au mafao hayo. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amalize kwa kuwa uwezo na dhamira anayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mlipuko wa idadi ya mabenki bila tija; Tanzania inajumla ya benki 51. Hiki ni kiasi cha juu kuliko nchi yoyote ndani ya SADC, lakini mikopo na riba bado viro juu. Hakuna tija ya idadi. Nashauri tujifunze mifano ya nchi za Nigeria na Sri-Lanka, ambapo Taasisi zote za Fedha zimekuwa *listed stock market*. Uamuzi huu utasaidia uwazi wa mabenki na kodi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya ku-list Makampuni ya Simu na Madini kwenye DSE, ilipitishwa na Bunge tangu 2010 kwa lengo la kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika uchumi wao wa madini na kampuni za simu ambazo zinakua kwa kiasi kikubwa. Naomba kauli ya Serikali kwa nini miaka yote tunashindwa kutekeleza hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Mwadui haulipi kodi tangu 1961. Hawa jamaa walikuwa na uwekezaji Lessoto, miaka kumi ilipokwisha bila faida waliondoka. Kwa nini Tanzania wameendelea kuwekeza na kudai wanapata hasara na hivyo hawalipi kodi? Tunaomba maelezo kwa nini Mgodi huu usilipe kodi kwa kutangaza hasara miaka yote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ndiyo nchi inayoongoza kwa kutoza kodi wafanyakazi (*PAYE*), kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Ripoti ya *Global Tax Comparison* ya 2014, iliyofanya na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na kampuni ya nne duniani kwa ukaguzi – Price Water Coopers ilionesa kuwa PAYE kwa wastani wa dunia ni 16% wakati Tanzania ni 18%. Imekwenda mbali zaidi na kuonesha katika Afrika ya Mashariki *PAYE*: Kenya 6.8%, Uganda 11%, Burundi 10.3% na Ruanda 5.6%. Nashauri tupunguze kodi hii mpaka *single digit*. Nashauri haya kwa sababu Chama Tawala (CCM) ni Chama cha Wafanyakazi kwa asili yake. Haiwezekani Chama cha Wafanyakazi kitoze kodi kubwa kuliko Vyama vya Kibebari vya Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa madini na gesi ni suala la uchumi. Nashauri tujifunze Zambia ambako Kampuni ya Umma ya ZCCM Holding Mining Company kwa kuwa *listed* kwenye Stock Market, kiasi cha raia milioni 1.5 wamenunua hisa kwenye kampuni hiyo ambayo ni mfano wa STAMICO kwetu. Nashauri STAMICO iwe *listed* kiasi cha share zake ili Wananchi wamiliki madini. Pia TPDC share zake za gesi ziwe *listed* DSE ili wazawa wamiliki uchumi wa gesi kwa kununua share hizo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ninakusuhukuru Mheshimiwa Masoud. Sasa kama tulivyojipanga, Naibu Waziri dakika ishirini.

Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, karibu sana. Unaweza kuendelea Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba nitolee ufanuzi na kutoa majibu ya baadhi ya hoja; nitatoa moja moja lakini zingine kwa sababu zimejirudia, nitaziunganisha.

Nikianza na moja ambayo ilikuwa inajitegemea ya Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mbunge wa Igunga, aliyekuwa anaulizia ni kwa nini Benki Kuu isirejee utaratibu wa kununua dhahabu na kuweka akiba kwa dhahabu. Utaratibu wa kitaalamu; kwanza, kutunza akiba kwa dhahabu siyo

tatizo sana na kuna maeneo ambayo hutunza akiba kwa namna hiyo. Uamuzi wa kufanya hivyo huwa unafikiwa kufuatana na uchambuzi wa stability ya uamuzi huo, yaani volatility ya kuamua kutunza kwa foreign currency au kutunza kwa dhahabu.

Historia inaonesha kwamba, kuna hasara ambazo unaweza kupata ukitunza dhahabu, lakini kuna faida ambazo unaweza kupata punde ukitunza dhahabu. Moja ya hasara ambazo unaweza kuzipata ukitunza akiba kwa dhahabu, inabidi utegemee zaidi chumi za nchi zilizoendelea zinayumba hapo ndipo utapata faida, lakini kama chumi za nchi zinazoendelea zitakuwa zina-perform vizuri, kwa maana nyingine huku katika nchi zinazoendelea utakuwea katika hatihati ya kupata hasara punde dhahabu itakaposhuka bei.

Jambo lingine ambalo ni la kitaalamu, ukitunza dhahabu au ukitumia Benki Kuu kununua dhahabu, ni sawa na *ku-print* pesa. Kwa hiyo, lile lengo la kuzuia mfumko wa bei litakuwa katika hatihati ya kuweza kutimia. Kingine ni Benki zinapotunza akiba kwa fedha za kigeni huwa ni sawa na uwekezaji, kwa hiyo, kuna riba; hivyo, ukiweka kwa kutumia dhahabu utakuwa umeshaondokana na uwezekano wa kupata riba.

Jambo lingine ambalo lilisemwa na Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya Kamati ya Uchumi na nimpongeze ndugu yangu, kaka yangu wa kutoka kwetu Simiyu, Mheshimiwa Mpina, ni Deni la Taifa. Nawaomba Wabunge tuelewane vizuri, utaratibu mzuri wa kuangalia Deni la Taifa ni kuangalia baada ya kuwa umeshafanya *discounting*. Tuishangaike sana na nomino, ukienda kwenye nomino value ya kuangalia namba ya Deni la Taifa, utakuta hata Marekani ama Japani, deni lao ni zaidi ya 100%. Wako juu kuliko hata sisi. Hata ukienda Kenya nako wapo juu zaidi ya sisi, lakini tunaangalia deni kulingana na kwamba, tumeshafanya *discounting*, kwa hiyo, tunaangalia kwa sasa, tunasema present value.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo kuna Mbunge mwingine alilisemea ninadhani Mheshimiwa Lissu kwamba, kuna mazingira Serikali iseme kama fedha hizi zinaenda kwenye matumizi mengineyo. Yeye alitolea mfano wa safari, warsha na vinginevyo. Niliihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, fedha za mikopo ambazo zinaleta madeni zinatumika kwa shughuli za maendeleo. Kutumika kwa shughuli za maendeleo ni kwa sababu bajeti yetu ni cash budget na miradi ya maendeleo ni mikubwa; kwa hiyo, ukiamua kila unachokusanya ndicho ukipeleke kwenye kutekeleza Mradi, maana yake ule Mradi utakamilika baada ya muda mrefu sana. Kwa hiyo, kwa faida ya Bunge lako Tukufu, ukiona vyema, Wizara yangu tunaweza tukawapa nakala za fedha ambazo zilipatikana kwa mkopo na Miradi iliyotekeliza ili tuweze kuondokana na wasiwasi kuwa huenda fedha fulani zilitumika katika mambo ambayo siyo ya maendeleo.

Mfano tu tuna miradi mingi ambayo imetumika kwa fedha za mkopo; kwa mfano, Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Kiwanja cha Ndege Zanzibar, Kigoma, Kagera na Miradi ya Maji ya Ruvu Chini, Miradi ya Zanzibar, State University Zanzibar, Barabara za Vijijini Zanzibar, Programu ya Kuzuia Vifo kwa Akina Mama na Watoto pamoja na Miradi mingine ya Umeme. Kwa hiyo, tunaweza kutoa hiyo orodha inayoonesha fedha zilizokopwa na zilikopwa kutoka wapi, kiasi gani na zilenda katika Mradi gani.

Kuhusu uhimilivu wa deni, siyo kila mara deni litakuwa linakua. Sasa deni linakua kwa sababu ya Miradi tunayotekeliza. Kwa hiyo, kadiri tunavyoendelea kulipa na Miradi tunaendelea kuunganisha, tunaunganisha barabara kama ni barabara, tunaunganisha kama ni umeme; kwa mfano, bomba la gesi nalo ni mkopo, siyo kila mwaka tutakuwa na bomba la gesi kutoka Mtwara. Kwa namna hiyo, ina maana kuna kipindi Deni la Taifa nalo halitakuwa fishio na litaendelea kushuka. Ukienda kwenye tathmini za kitaalamu, zinaonesha come to 2023 na kuendelea, Deni la Taifa linaweza likawa limeshakuwa ni chini ya 15%.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wabunge wot, ambao wameongelea kuhusu mapato. Nami nimekuwa nikisema mara nyingi sana hapa kuhusu mapato. Ni vyema sana kama Wabunge tutakuwa chanzo cha kuhamasisha masuala ya mapato na siyo chanzo cha kupinga jithada za Serikali za kuweza kupata mapato. Limekuja suala hili la *EFD*; mimi nimezunguka na nimekutana na wafanyabiashara, nao walisema waziwazi, tulikuwa tukijifungia wanasema waziwazi. Kulikuwepo na hoja za msingi ambazo tulizichukua Serikali na nyingine zilishachukuliwa hatua. Moja, wamesema mashine zile ziliwuwa zinaongea Lugha ya Kiingereza tu; tulisharekebisha kwa sasa na mashine zile zina Lugha ya Kiswahili.

Lilikuwepo suala la bei, tulisharekebisha tukashusha na hata sasa tulisema tutaondoa VAT na tulishapeleka mapendeleko ya ushuru wa forodha ili kuweza kushusha zaidi bei. Limekuja swali kwamba ni kwa nini mashine zile zisikopeshwe au ni kwa nini zisiuzwe na TRA?

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nilisema wakati ninajibu swalii na leo hii ninasema, tulisema Serikali ikiamaa kununua zile mashine, tungeweza kuacha sekta zingine na kununua zile mashine. Tukasema maadamu yeoyote atakayenunu mashine ile, kama amenunu kwa laki sita na kodi yake ni laki tatu, maana yake atakapoenda kupigiwa hesabu ya kodi, ataondoa kwanza fedha aliyonunulia mashine; na kama ilikuwa ni zaidi ya ile kodi yake, maana yake na mwaka unaofuata ataondoa fedha aliyonunulia mashine. Kwa hiyo, ni kitu kilekile, mimi niliwauliza wafanyabiashara kwani mwaka huu hamkujipanga kulipa kodi? Wakasema tulijipanga, kwa hiyo, ni kile ikile kwamba, kodi ambayo ungelipa unatanguliza kwenye mashine. Unakuwa umefanya kazi mojawapo kwa Taifa lako, kwa hiyo, hilo ilikuwa hivyo.

Hofu moja ambayo wafanyabiashara wengi walikuwa wanasema waziwazi, walisema tukianza mambo haya ya mashine tutafilisika kwa sababu pato halisi la kwetu litajulikana na baada ya muda fulani tutaingia kwenye VAT. Nawaomba ndugu zangu wafanyabiashara wadogowadogo, Serikali inawajali sana. Hili suala la kupata hofu kwamba, tukishaingia kwenye mashine muda siyo mrefu tutaingia kwenye milioni arobaini, kwenye marekebisho tunayopendekeza tunaangalia uwezekano wa kupandisha hicho kima ili mfanyabiashara mdogo awe mdogo kwelikweli, wala msiwe na hofu kwamba hiyo milioni arobaini itafikiwa mapema.

Jambo lingine ambalo niliona nilisemee na lilisema sana hapa ni hili la misamaha ya kodi. Nilisema siku ninaapishwa kwamba, nimeongea nikiwa Mbunge na tumeenda kwenye Wizara kwenye timu yetu, tumekubaliana tukasema tutaleta Muswada na ninadhani tayari tumeshaweka mezani. Kwa hiyo, kwenye hili mimi ninachoomba mtuunge mkono tu wala fusigombane tena, tutaleta na tuboreshe na tuorodheshe vyote. Maamuzi ya kitu gani kisamehewe kimsingi kinatokana na Bunge. Mimi nitashangaa kama kuna Mbunge atakwenda kinyume na pendekezo la kupunguza ama kufuta hii misamaha ya kodi ambayo inatusababishia tukose fedha za kwenda kwenye huduma za maendeleo.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo sote tunatakiwa tukubaliane tuweze kufuta. Kwa kweli kuna vitu ambavyo kwa Mtanzania wa kawaida vinakuwa vigumu sana kuvielewa na sisi ndivyo tulivoona kama Wizara, ni vyema tukalishughulikia. Ushauri wa kitaalamu unaonesha hivyo hivyo kwamba, utaratibu ambao tulikuwa tunautumia katika kusamehe kodi, unapingana na utaratibu wa kitaalamu wa namna ya kuweza kuendesha taratibu hizi za kodi. Kwa hiyo, hili limezingatiwa na hatutaishia tu kwenye kufuta misamaha, tunaleta pia Sheria, kama nafasi itakavyoruhusu, ambayo itahusu usimamizi wa kodi. Kwenye hili tunalenga pia kupunguza mianya ya kukwepa kodi na kuweka utaratibu mzuri, kuna kodi zingine zinakera watu kwa utaratibu wake wa uendeshaji ama utawala na hiyo inasababisha mianya mingi au kushawishi watu kuweza kukwepa kodi.

Niliwaambia Mawakala wa Forodha au Makampuni yanayoshirikiana na Mamlaka ya Mapato kuwa, tutawasaidia kwenye taratibu zao za kazi. Tukawaambia wao pamoja na Mamlaka ya Mapato, tushirikiane katika suala hili ili tuweze kukomesha tatizo la ukwepaji wa kulipa kodi kwa watu wasio waaminifu.

Mheshimiwa Niabu Spika, kwanza niwapongeze Mawakala ambao wanafanya kazi kwa uaminifu. Niliwaambia pia kuanzia sasa Sheria zilishawekwa, lakini utaratibu wa kufutiwa leseni peke yake siyo adhabu. Ninalirudia tena hili waelewe hivyo, kwamba, yelete atakayekosea, kufutiwa leseni peke yake haitakuwa adhabu. Kwa hiyo, tutakuwa na hatua zingine kali zaidi na hata tutafikiria kama Sheria ina upungufu au adhabu ni ndogo, tuweze kuweka adhabu kali.

Waheshimiwa Wabunge huwa tukileta mapendekezo ya adhabu kali hapa mnaanza kuwahurumia watu kama vile watu wamejiandaa kukosa. Tutakapoleta hili nitaomba tukubaliane. Hivyo hivyo hata kwa Watumishi, nilishaiagiza Mamlaka ya Mapato na sasa hivi ninarudia tena, ninaagiza kuwa, kuhamishwa Kituo baada ya kukosea siyo adhabu, tutaenda hatua kubwa zaidi. Kwa wale wanaohusika na bidhaa, taratibu zinasema akgundulika hesabu zitapigwa upya. Hesabu ikipigwa upya maana yake tumepata tulichostahili tu, hiyo siyo adhabu. Kwa hiyo, nayo tutaenda hatua kubwa zaidi na naomba maeneo mengine ambayo sisi tutaona tutahitaji kuimarisha zaidi, kwa sababu tutaleta na Sheria inayohusu usimamizi wa mali ya umma, tuweze kama Bunge kushirikiana. (Makof)

Wabunge tushirikiane pia na mtu yelete, raia mwema, anayetambua hilo tushirikiane. Hakuna mtu ambaye anaweza akagusa mali ya umma halafu yeye asiguswe. Naomba kwenye hilo tushirikiane, tutaweza kukomesha na kupiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha.

Jambo lingine ambalo limeongelewa ambalo ningeomba niliseme ni kuhusu kuongeza uwezo wa usimamizi wa Makampuni ya Kitifa ili kudhibiti uhamasishaji wa faida kupitia bei, yaani *transfer pricing arrangement*. Tunakubaliana na Maoni ya Kamati ya Uchumi wa Viwanda na Biashara kuwa, Makampuni yenye mitandao ya Kimataifa, yaani *Multinational Enterprises*, yaana wigo mkubwa wa mianya mikubwa ya kuhamisha faida kwa njia ya bei, yaani *transfer pricing arrangement*. Kwa kutambua hilo, Serikali tayari imeshachukua hatua zifuatazo:-

Mamlaka ya Mapato imekwishakuanzisha Kitengo Maalum ambacho kinashughulikia Kodi za Kimataifa, ikijumiisha Makampuni ya Kimataifa. Pia Serikali imetoe Kanuni ya Kushughulikia *Transfer Pricing*, yaani *Income Tax Transfer Pricing Regulation 2013*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, TRA pia inaandaa mwongozo ambao utakuwa rasmi kwa ajili ya *transfer pricing* na hii yote ili kuweza kuhakikisha kwamba, tunaendana na mazingira hayo kadiri ambavyo tumeweza kubainisha. Vilevile Mamlaka ya Mapato kwa kushirikiana na NTA, inaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi, kuwawezesha kushughulikia na masuala ya kodi na Kodi za Kimataifa.

Jambo lingine ambalo lilijitokeza hapa ni lile ambalo liliikuwa linahusu kuorodhesha makampuni. Nikupongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge, kijana mwenzangu, Kafulila. Wizara yangu inakubaliana na hoja yako kwamba, kama tutaorodhesha makampuni, tutaongeza uwazi, utawala, uwajibikiaji na kupitia hayo Serikali itaweza kupata mapato.

Mpaka sasa makampuni saba yaliyoorodhesha sokoni ni miongoni mwa makampuni ambayo yanaongoza katika kulipa kodi kwa hapa nchini. Kwa hiyo, hoja hiyo ina mantiki. Sisi kama Serikali wazo hilo tunalichukua na mimi niseme tu kupitia nafasi hii, niagize kwanza Msajili

wa Hazina, Soko la Hisa la Dar es Salaam na Mamlaka ya Mtaji na Dhamana, kwanza, wafanyie kazi makampuni ambayo Serikali ina hisa na waweke mapendekezo ambayo yanatakiwa kuorodheshwa tuweze kuanza na hilo na hii nitataka wanipe taarifa baada ya kuwa wamekamilisha na sisi tumeshamaliza hapa.

zipo Sheria ambazo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tayari wameshaanza kuwa na Sheria ambazo zinaelekeza hivi. Kwa hiyo, sehemu zingine tutaelekeza kwa namna ya kisera, namna ya kikodi, kuyawezesha makampuni haya, tuyawekee mazingira lakini tuyawekee ya mazingira ya kikodi ambayo yatawawezesha kuorodheshwa ili tuweze kuweka uwazi na kuwezesha kupata mapato sisi kama Taifa na kupeleka katika mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine limesemwa la kuhusu TRA na kufanya asilimia 70 haijatumia nguvu za kutosha kudhibiti hili. Hili jambo ni la wote, Mamlaka ya Mapato, inatumia utaratibu ule ule wa kuwa na kioo cha kuangalia kama makadirio ama malengo waliyoweka yanastahili. Ukiangalia mwenendo utaona wanapoweka lengo, mwaka unaofuata wanaenda zaidi na hii inaendana na viashiria na malengo yaliyowekwa. Kwa mfano, sasa hivi wana mpango ambao wameshafikia sasa tunaenda hata hizi ambazo wanaweka, hizi *initiative*, ni kwa ajili ya kuendelea na mpango ambao ni wa kuboresha mapato ili kuweza kuwa na lengo kubwa zaidi.

Kwa sasa lengo letu na uwiano bado hatujafikia kiwango ambacho hata mamlaka yenyewe inataka. Kwa hiyo, tukiunga mkono jitihada za aina hii ni dhahiri kwamba, tutaweza kupiga hatua. Mimi naamini kabisa kwamba, kwa timu mpya na malengo yetu, twendeni tu, tunaomba mtupe ushirikiano na Taasisi zetu, tutaweza kupiga hatua na hilo litatuwezesha kupiga hatua zaidi.

Kuna mambo mengine ambayo yameongelewa kama suala la umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa. Hili ni jambo la msingi sana, nchi yetu kwa ukanda huu, tunaongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya uwiano wa sekta rasmi kwa Pato la Taifa. Pamoja na kwamba, kuna utaratibu wa Vitambulisho vya Taifa, lakin Mamlaka ya Mapato tayari imeweka Mpango Maalum ambao utawataka wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi, kuwekwa katika wigo maalum wa kodi kulingana na mapato ambayo hii itaweza kuongeza upana wa wigo wa walipa kodi.

Jambo la msingi kama wote ambavyo tulisema, ni kweli kabisa kwamba, hatujaweza kubainisha, bado kuna mashaka ya ukweli wa makampuni makubwa na kiwango kinacholipwa. Kwa hiyo, jitihada hizi zote zinazofanyika ni za kutaka kuwezesha kila mlipa kodi aliye kodi anayostahili ili tuweze kuondokana na mzigo aliousema ndugu yangu Filikunjombe, wa wafanyakazi ambao wao hawana namna ya kukwepa kodi na wafanyabiashara wadogo wadogo kuwa ndiyo ambao wanaendesa nchi hii.

Tutakapokuwa tumeweza kufikia hatua ya kila anayestahili kulipa kodi aliye kodi anayostahili, ni dhahiri mapato yetu yataongezeka na kama alivyosema Lusinde, tutadhibiti na upande wa matumizi. Suala hili tumeshaliandalia utaratibu ili kuweza kuhakikisha kwamba, tunaweza kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Niseme lile ambalo nimelisema, si kwamba, fedha zinakuwepo Wizarani na haiendi kwenye Miradi. Hili linatokana na kwamba, tunakuwa tunagawa kile ambacho kinapatikana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha

kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, bahati mbaya muda umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri Fedha. Tunajua muda hautoshi, lakini tunashukuru sana kwa hatua hiyo.

Sasa nimwalike Naibu Waziri Fedha, Mheshimiwa Adam Malima na yeye aweze kupitia katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa. Mheshimiwa Adam pia una dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Subhanahu Wata'ala aza wajaha, kwa kunijalia kwa afya na uzima na baraka zake kwa hapa niliposimama. Naomba niishukuru familia yangu na mke wangu na wapiga kura wangu wa Mkuranga. Ninawashukuru kwa namna ya kipekee kabisa, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ambao tunafanya nao kazi hizi za usimamizi wa maendeleo ya jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, kwa namna ya kipekee kabisa, naomba nitambue maneno mazuri aliyoyasema Waziri wa Fedha Kivuli. Mimi katika kukaa kwangu katika miaka mitatu, minne hapa, sijawahi kuona maneno mazuri kama yale. *That is the essence of Opposition. Umezungumza ulikusudia kujenga.* Kwa hiyo, umetolewa ushauri hapa kwamba, tuyachukue yale maneno tukayafanye kazi, maneno yake mengi ni mazuri yanafanyiwa kazi na naomba pia nimpongeze Naibu Waziri Kivuli, Mheshimiwa Christina Lissu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Livingstone Lusinde Kibajaji, aliyesema kwamba na yeye kwa mara ya kwanza ameunga maneno mazuri yaliyosemwa na mjomba wangu Mnyalukolo, Mchungaji Msigwa. Amesema *we must stretch our hands, tufike sehemu ambayo expenditure kwenye Serikali lazima iendane na uwezo wetu.* Sasa ndugu zangu, mimi naomba tuseme, *I can speak to this Parliament, I can speak to this House as an Economist,* naweza kuzungumza kama Mchumi au kama Mwanasiasa.

Nikisema tuzungumze kama Mchumi, lazima ifike mahali tuambiane ukweli. Ukweli ni kwamba, lazima tufike sehemu tukubaliane kwamba tunapokaa hapa tunazungumzia *Financial Management*, usimamizi wa kifedha wa nchi hii na kuna mambo ambayo lazima tuamue hapa. Hatuwezi tukakubali kwamba, tukae hapa, *we demand for expansion that we cannot afford.* Kwa hiyo, hapa lazima tukae tukubaliane, kuna mambo mengine ambayo tunaweza tukayafanya na kuna mambo mengine hatuwezi kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Bajeti ya Wizara, bado wiki ijayo tunakuja kukaa hapa kwenye ngoma kubwa, hiyo yenye. Labda niseme tu kwamba, mwaka jana mimi nikiwa kilimo na Waziri wangu pale Chiza ananiona, niliwhali kumwambia kuwa hapa Wabunge tulikuja mwishoni tuka-demand budgetary expansion ya 538 billion from 17 point something, tukaenda mpaka 18.25. Hatukufikia, *we had not plan for it.*

Kwa maana ya kwamba, tulikuwa hatujaifanya mikakati kwenye upande wa makusanyo ya kodi, lakini tulifika sehemu tukasema aah Mradi wangu huu ukikosekana itakuwa balaa nitasema nini Jimboni! Lazima tukubaliane kwamba, tukitaka kwenda hapa sambamba, huko mbele tunapokwenda *this must be a partnership.* Lazima tuwe na ubia baina yetu sisi, kuna mambo tunaweza tukayafanya na kuna mambo hatuwezi kuyafanya na lazima

tuambizane ukweli. Tukisema tutanue tu tutafika sehemu halafu kila mwaka tutafika tutajikuta tuna malengo ambayo hatujaweza kuyafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge na ninaomba nirejee kwenye kauli ya Mheshimiwa Mjomba Msigwa na wengine, kuna mambo ya msingi ameyasema Mheshimiwa Kibajaji, tuna masuala ya *financial discipline in public management* tuna masuala ya *budget ceilings*, wataalamu wanapokuja tunasema tuna hiki na hiki. Tuna mambo ya msingi ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyasema na lazima Serikali tukayafanyie kazi. Ninashukuru Mheshimiwa Saada, atakuja kuyasemea na tutaenda kuyafanyia kazi.

Masuala ya *expenditure constrains*. Kama kuna mambo mengine ambayo tunaweza kusema hiki kipungue ama hiki kiongezeke, kwa sababu inawezekana kabisa kwamba, labda katika kupanga matumizi tunajielekeza kule kule kwenye mfumo wa kutumia ule ule wa miaka yote. Kwa hiyo, hilo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeliona na kwenye upande huu wa *expenditure constrains* lingine ni manunuzi ya umma, *Public Procurement*. *Public Procurement* tusikae tukaongopeana, kila mwaka tunasema na bingwa wa *Public Procurement* yumo humu ndani nadhani Mheshimiwa Mwambalaswa, kila mwaka analisema. Anasema *that is our enemy number one*.

Tumeleta *Public Procurement Act* ina miaka kumi lakini bado inabidi twende tukaifumue ile Sheria. Kwa sababu haiwezekani mnatengeneza Sheria ambayo tunashindwa kufanya *impact assessment*, Sheria hiyo inatukwaza kwenye masuala ya maendeleo. Lazima kuwe na mambo ambayo lazima tukubaliane, lazima tuwe na *Prudent Financial Management*. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia masuala ya baadhi ya Taasisi zetu na namna zinavyojoindesha. Ni kweli kabisa kwamba, kwenye usimamizi wa uchumi, usimamizi wenyewe una gharama. Kwa hiyo, mwaka huu utaona kuna vipengele vya makusudi kabisa ambavyo vimeombewa hela ili kuongeza uwezo wa kusimamia. Sasa usipokuwa na uwezo wa kusimamia ndiyo unakuta watu wanajifanyia mambo ya ajabu, tunapokuja hapa tunalumbana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, hilo la kuongeza gharama kwa ajili ya kuboresha umamizi, lakini napo lazima Taasisi hizi na Serikali inabidi turudi humu Bungeni na tuseme kwa zile pesa tulizoongeza kwa ajili ya usimamizi, hiki ndiyo tulichofanikiwa kuokoa. Sasa kama utatumia *ten billion* kwa ajili ya kuwa na *Financial Expenditure Tracking Unit*, ambayo inaweza ikamvamia mtu wakati wowote, saa yoyote, lakini ikaokoa bilioni 200, *that is okay*. Umetumia bilioni kumi lakini unaokoa bilioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA*; *TRA* imekusanya asilimia 75 hadi miezi kumi hii iliyopita. Tumekusanya kama bilioni 7.8 hivi kwa malengo ya bilioni 8.5. Tumesema kuna mikakati ambayo inafanya ukusanyaji wa kodi uwe na matatizo; kuficha mauzo halisi na kutokutoa risiti wakati wa mauzo. Sasa *TRA* wenyewe wamejipangia mikakati ya namna ya kuboresha makusanyo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru Wabunge, wamefika sehemu wamezungumza hata masuala ya *Property Tax*, ambayo siyo ya *TRA*, lakini yatakusanya mapato makubwa hasa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa kabisa ambalo nadhani *TRA* wanakuja nalo ni hili la *Block Management System*, kukusanya kodi kwa Mfumo wa Vitalu. Sasa hapo ni wote. Kuna siku moja Mheshimiwa Mangungu alisimama hapa Bungeni, yeye ameishi Marekani, kule Marekani kutokulipa kodi, ikifika tarehe 1 Aprili hujalipa kodi unatafutwa, wewe mwenyewe

unaanza kujitafuta, yaani kule kuwajibika kulipa kodi ni at all levels na kutokulipa kodi kuna adhabu kubwa kweli.

Sasa katika misingi hiyo, Serikali pia itakuja na mapendelekezo humu Bungeni. Tunakuja na Sheria ya maboresho ya VAT na kadhalika, lakini pia lazima kuwe na mabadiliko ndani yetu sisi wenyewe. Sisi wenyewe Wabunge tutoke twende tukawaambie Watanzania kulipa kodi ni wajibu. Asishabikiwe mtu kwa kutokulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezunguka amesema Mheshimiwa Mwigulu, yeye amezunguka Kusini mimi nimekwenda Kaskazini. Unakuta watu wanashabikiwa na vyombo vya habari kwamba kwa nini ninyi hamkulipa kodi, maandamano yale watu wanashangilia! How? And then it is this same system ambayo inabidi igharimie non-productive sectors kama Majeshi, Walimu, Afya na kadhalika. Wale wote wanaghariwi na hiyo kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo ambalo tunatakiwa tujenge kwa Watanzania ni kwamba, tunapolipa kodi tudai, ule uwajibikaji katika ile kodi tuliyolipa. Wabunge tuseme kwamba kuna kodi, kwa mfano, kwenye bajeti ya bilioni 19 itakayotokana na mapato ya ndani ni kama bilioni 12 ama 13, mdai utendaji na uwajibikaji kwenye kodi ile!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tuambizane maneno makali hapa, hili jambo tunalolitafuta lazima lianze na uwajibikaji na kubadilisha mifumo humu humu ndani. Jambo hili la Block Management System uzuri wake ni kwamba, litakwenda kwa wakubwa na wadogo. Tusizingumzie tu kodi inayokwepwa na wafanyabiashara wakubwa. Wafanyabiashara wadogo nchi hii hawalipi kodi, kwa sababu *it is part of the informal sector* haijarasimishwa. Sasa usiporasimisha hukusanyi kodi.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba, tunakusanya trillioni 12, we can collect more, yes! Lazima sisi wenyewe tutengeneze mifumo ambayo ina gharama kubwa, lakini pia kwenye mifumo ya nidhamu ambayo tunatarajia tuje nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, linalofuata ambalo niliomba nilizungumzie ni hili la *interest rate*, riba kwenye Mabenki. Riba ni mahusiano baina ya yule anayekopa na anayekopeshwa, is a standard format. Mimi nilikuwa Benki Kuu, nimefanya kazi Benki Kuu, mwaka 1991 nikiwa Benki Kuu pale, tulileta Sheria ya kwanza ilikuwa *The Banking and Financial Institutions Act*, ambayo ndio ilikuja kuanza kutengeneza mfumo wa kuiondoa ile Benki ya zamani ya NBC ile kuwa na Mabenki mengi zaidi. Immediately tukaja na *Foreign Exchange Act*, 1992. Mimi nilikuwa Naibu Katibu wa Kamati ile ndogo iliyofanya utafiti wa Kamati ile. Mwanasheria wetu ambaye tulikuwa tunafanya reference wakati huo alikuwa Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge.

Sheria ile ilikuja kwa makusudi kabisa kwamba, wakati ule mtanisaidia, Mheshimiwa Selasini unajua, ulikuwa ukishuka na ndege pale ukiambiwa sasa approaching Dares Salaam unaweka dola zako kwenye soksi. Ukitamatwa na dola mia ndani. Leo tukitafutana hapa mzee hata wewe Selasini hata Mbatia nitakuta una mambo yako labda mazuri mazuri na kuna dollar accounts kwenye akaunti zetu hizi. Sasa *The Foreign Exchange Act* ya 1992, ililenga kuondoa hili. Kulikuwa kuna Watanzania walikuwa wana dola nyingi unakwenda nyumbani kwao unabadiishiwa huko.

Lilikuwa lengo pia la kuwafanya wale watu ambao wanaishi kwenye Diaspora warudi na zile pesa wawekeze Tanzania. Usiwe na tabu kuwa na dola yako. Sasa tuna miaka 20 tangu FEA, mimi nadhani ile Sheria ilikuja kwa makusudi lakini ikaja kuboreshwa na Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 1995, ambayo iliboreshwa na Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 2006.

Benki Kuu ina dhamana ya kusimamia masuala ya msingi katika *monetary* na *fiscal policy* za nchi yetu, tunagawana majukumu sisi na Benki Kuu. Hili suala la kufanya kazi masuala ya riba yapo kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *management* ya *interest rate* inatokana na kwamba, kwenye mifano ya nchi za wenzetu kama Marekani na kote kuna mifano ambako kusimamia *interest rate* kumefanywa miaka mingi. Kuna baadhi ya nchi ambazo ukicheza na *interest rate* nchi nzima ina-collapse. Sisi as a developing nation, *interest rate* tuna-peg kwenye mambo mawili makubwa; tuna-peg kwenye economic growth na kwenye inflation.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi hapa, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mpina, amezungumzia suala la kwamba, bank rate ilikuwa 7.58 imekwenda kwenye 12; true, lakini *it is based on indicators*. Sasa kwamba, banking system ya Tanzania is perfect siyo kweli. Mimi nawaambia wanabenki wenzangu kila siku kwamba, hii second generation financial reform, ambayo imeanza ina miaka minne, mitano sijui, we can do better. Huwezi kuwa na financial system kwenye nchi kama ya Tanzania ambayo haijielekezi kwenye matatizo ya kukopa ya mfanyakishara mdogo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyote mnajua kwamba, small and medium enterprises, anapokwenda benki kukopa anaambiwa bwana wewe ondoka, soga soga, anapokwenda mkulima soga soga. Sasa hawa ni zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, asipoweza kukopa nchi hii inatoka vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana kwamba, lazima twende tukajifungie na Benki Kuu, tuangalie hii second generation financial reform inakwenda katika misingi gani. Ninaomba niwahakikishie Watanzania kwamba, lazima tufike sehemu tukubaliane, haiwezi ikawa haya Mabenki wanafanya biashara, mambo yao mazuri, lakini kuna ile core element ya Mtanzania ambayo haifikiwi, something is wrong. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, mimi ni ex-BoT, Mwigulu ni ex-BoT, tuna ex-BoT wengine wengi humu ndani, tutaenda kukaa nao. Mheshimiwa Kitwanga yupo, tutaenda kukaa na wenzetu tuwaambie as Bank of Tanzania, sheria inakuruhusuni kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba, hizi taasisi zingine zinakuwa na masilahi kwa mkulima mdogo. Tafuta namna tu, sasa inawezekana labda ule ushindani wa mabenki is so comfortable kwao kwamba, wanahakikisha wanacheza tu na treasury bills na kadhalika, mambo yao mazuri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yote naomba niseme kwamba, tutaenda kuangalia namna ambavyo Sekta ya Fedha nchi hii na Sekta ya Benki zitakidhi mahitaji. Hatuwezi kuwa na Sekta ya Fedha isiyotambua kwamba, asilimia 70 ya Watanzania ni Watanzania maskini. Hiyo tunayoizungumzia *interest rate* na nini; hakuna watu wanawekeza, savings haikui. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukua kwa Deni la Taifa, naomba niseme tu kwa haraka haraka. Deni la Taifa limekua kwa sababu ya Miradi kama ya DART, Songwe Airport, Zanzibar Airport, Miradi ya Maji, Mtambo wa 60 Megawatts wa Nyakato ambao ulikuja kwa makusudi kabisa kwa ajili ya kuleta balance kwenye Grid System, Ubungo Megawatts 100 na kadhalika. Hii ni Miradi ambayo ni productive.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro tuliokuwa nao pia ni kwamba, kwenye element ya Deni la Taifa, ambalo tunatoka nalo zamani, baadhi ya Miradi haikuchangia kwenye Uchumi

wa Taifa. Kwa hiyo, ndiyo yale ambayo Wabunge wamesema na mimi ninawaunga mkono, katika kuzuia hatua hiyo miaka kama miwili iliyopita Serikali imesema *no more government guarantees*. Kwa sababu Serikali imedhamini Miradi ambayo wenyewe walikuwa hawana uwezo wa kuilipa. Kwa hiyo, nayo imeingia kwenye madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine limezungumzwa kuhusu Mifuko kuwekeza kwenye productive areas na madeni yanayozungumzwa mimi nakubaliana na Wabunge kwamba, hilo ni jambo ambalo lazima tulifikirie kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine limezungumzwa na Wabunge kuhusu kufanya mabadiliko ya sheria ili sheria hizi ziendane na menejimenti ya kiuchumi ile ambayo tutawafikishia Watanzania. Kuna jambo moja ambalo naomba niliseme, tumekubaliana anaweza kuja kusema Waziri mwenyewe na Wabunge tumezungumzia kwamba jambo hili tutakuja kulisemea kwa Azimio, nalo ni suala la UDA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kizaaza chote nimeanzisha mimi. Nimeulizwa, Serikali ina asilimia ngapi kwenye UDA. Sasa leo Mheshimiwa Machali amezungumza anasema Malima alisema Serikali ina asilimia 100. Naogopa kusema ninayotaka kuyasema moyoni kwa sababu hii *microphone* nchi nzima inanitazama; lakini Mheshimiwa Machali, sisi kama Wabunge kuna kitu kinaitwa *Hansard*, nilichosema siku ile ni kwamba, Serikali kuitia Wizara ya Fedha ina asilimia 49 na Jiji lina asilimia 51. (*Kicheko/Makofij*)

Maana yangu nilichosema nini? Kama kuna aina yoyote ya jambo lilitokea pale, sisi Serikali hatuna taarifa. Sisi Serikali tunapouza hisa zetu kwa namna moja au nyininge ni lazima lipitie kwenye utaratibu wa kuridhiwa na Baraza la Mawaziri. Nilipotafuta ridhaa ya Baraza la Mawaziri sikuliona! (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelisema kwa sababu nimezungumza, kwa taarifa yako tu; maana huyu bwana analetewa utaratibu wa kuonekana anaonewa sana. Juzi Jumatatu tumemwita ofisini tumekaa naye mpaka saa sita usiku; tumemwambia lete maelezo yoyote yanayoonesha kwamba wewe una uhalali wa hisa zako, sisi tunachotaka ni kwamba Dar es Salaam ipate Mwekezaji wa kuendesha usafiri wa Dar es Salaam, lakini upite njia zile za halali. Hii ya kusema uje hapa tena, Wabunge wakusemee, uende kwenye Kamati inatokana na nini? Wewe lete hisa zako kwamba nilikwenda Jiji nikanunua hizi, nikaenda kwa Msajili wa Hazina nikamlipa hizi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yenu, tulipomwuuliza tumemwambia wewe una hisa za nani akasema mimi nina hisa za Serikali. Nikamwambia mimi sina popote ambapo najua wewe umenunua hisa za Serikali; wapi umenunua hisa za Serikali? Hisa za Serikali hazitolewi kama sambusa, unakwenda unazichukua. Tunazungumza masuala ya rangi, masuala ya nini. Mimi nasema hivi; mimi hapa Adam Kigoma Malima, nataka Dar es Salaam ipate Mwekezaji wa Usafiri wa UDA ambaye atalingana na hadhi ya Dar es Salaam. Sasa kama huyu Bwana atakidhi vigezo mpeni, lakini ipitie kwenye utaratibu wa Serikali. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza humu Bungeni tumesema, mali ambazo zimebinafsishwa na zimebinafsishwa zimekwenda kule, wenyewe waliopewa hawakuzifanyia haki tuzirejeshe. Kwa hiyo, tumeanza ku-question hizi taratibu za privatization muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hapa, nilisema siku ile na ninarejea kusema kauli ile, kama yapo maelezo yanayosema mimi nimenunua UDA na kadhalika na nini, tumemwambia ayaleta ofisini, hakuna mgogoro hakuna ugomvi. Kama tabu ayaweke hapa Mezani. Habari hii ya leo mara Kigwangalla kazungumza mpaka povu linamtoka, mara leo

Nakala ya Mlando (Online Document)

Machali, ya nini! Tunadhalilishana Wabunge humu, huyu kachukua, huyu hakuchukua, aweke hapa karatasi Mezani au apeleke ofisini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru na ninaomba niseme kwamba, katika utekelezaji wa majukumu ya Hazina, Wabunge ni Wadau wakubwa. Naomba niseme kwa niaba ya wenzangu kwamba, hatutarajii kupata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yetu, isipokuwa utekelezaji huo utakuwa na ushirikiano wa karibu sana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno hayo, naomba nitamke kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Fedha. Kabla sijamwita Waziri, nitoe tangazo moja angalau kidogo wakati Waziri anajiandaa kuja na ni kutambua wageni.

Naomba niwatambue wanafunzo 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma pale mlipo; ahsante sana karibuni sana. UDOM ni Chuo ambacho tunajivunia sana katika nchi yetu na mpo hapa mjini. Karibuni sana vijana wetu kwenye Bunge lenu na mijifunze namna ambavyo mambo yanaendeshwa.

Waheshimiwa Wabunge, pia naomba niwatambue wageni wetu ambaa ni Wabunge 35 kutoka Bunge la County ya Vihiga Nchini Kenya. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Vihiga. Hili ni Bunge la County; sijui County Kiswahili chake ni nini?

WABUNGE FULANI: Mkoa.

NAIBU SPIKA: Siyo lazima sana iwe Mkoa, ni kitu kama Mkoa hivi lakini siyo Mkoa as such, inabidi Kiswahili kitafute neno la County.

Wabunge hawa wanaongozwa na Spika wao, Mheshimiwa Daniel Chitwa, karibu sana. Pia yupo na Naibu Spika, Richard Muigai, karibu sana. Wameambatana pia na Watumishi wa Bunge hilo 15 wakiongozwa na Katibu wa Bunge hilo Ndugu Josephat Msambai. Karibuni sana, mnaweza sasa mkakaa. Wageni hawa wanatoka Vihiga; sijui Vihiga ni Province ipi kule?

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimkaribishe Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na tumepata faraja mimi pamoja na wenzangu, kuona karibu Bunge zima leo tumekuwa pamoja. Bunge hili siku ya leo, Jumatano tarehe 4 Juni, kwa mara ya kwanza, Wabunge wote waliosimama wametoa ushauri mzuri sana katika kupeleka mbele nchi yetu; tunapata faraja sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, nakushukuru kwa kuendesha mjadala huu na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Nimekuwa katika Bunge karibu miaka miwili, kwa mara ya kwanza leo, Ripoti ya Waziri Kivuli wa Fedha, ni ripoti ambayo tunaweza tukasema kama tungekuwa tunafanya assessment ya miaka miwili na marking iko hundred, leo ningempa 95 na yeche ndiyo angekuwa ame-score. Padogo tu lakini tunakupongeza na tutafuata ushauri. Tunashukuru na vilevile namshukuru Naibu Waziri Kivuli, japo juzi kidogo alikuwa ... lakini naona leo tumekwenda vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Naibu Mawaziri kwa kufafanua baadhi ya hoja, lakini najua muda siyo rafiki sana, tunaahidi kwamba tutaziweka hoja zote katika maandishi na tutazileta kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilikuwa nyingi kusema kweli, kubwa zaidi kuna Mheshimiwa aliuliza kuhusiana na kuharakisha *Sovereign Credit Rating*, ilikuwa kwenye Kamati. Ile process ya nchi yetu sasa kuwa rated, kuthaminishwa. Hili ni zoezi muhimu na ni zoezi ambalo nchi nyingi Duniani, lakini nchi nyingi sana Afrika zimeshakuwa katika zoezi hilo kwa miaka kumi.

Sisi ndiyo tuko kwenye hatua ya kuelekea huko. Tunalipa zoezi hili umuhimu wa kipekee kabisa, kwa sababu kama tutakamilisha zoezi hili, basi nchi hii itakuwa ina uwezo wa kukopa katika masoko ya fedha ya Dunia, lakini kwa rate ya chini sana. Si kama sasa hivi tunapokwenda tunakopa kwenye rate za kibashara ambazo bado ni kubwa. Tunahitaji fedha, lakini tunahitaji tuzipate kwa unafuu zaidi ili tuweze kuhimili na ili tuweze kuwekeza kwa fedha kubwa au nyingi ambayo tunapata. Kwa hiyo, hili tunalifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi tumepeata *raters* wawili ambao ni Fiche na Mudis. Tulikuwa tumalize mwaka jana, lakini walipokuwa wale na zile fomu zao za kujaza, kuna vipengele vingi ambavyo vilikuwa vimeingizwa mle, ambavyo havijaendana na matakwa yetu. Kwa hiyo, wakati tunataka tulifanye haraka zoezi hili, tunataka vilevile kuhakikisha kwamba, taratibu za nchi katika kuwachagua hawa *raters* kutokana na miongozo yetu tunafuata. Kwa hiyo, imebidi turejeshe lakini sasa hivi tumerudi tena tumelewana na kabla ya mwisho wa mwaka huu wa kalenda, yaani Disemba, 2014, nina hakika kwamba, Tanzania tutakuwa tumefikia mahali pazuri katika kuwa rated.

Tuombe Mungu, tukishakuwa rated hata makampuni yetu ya ndani yanaweza kwenda kukopa nje, kwa sababu ile sura halisi ya Tanzania kutokana na rasilimali zake sasa itakuwa inajulikana na *investors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, sehemu pekee ambapo hawa wakopeshaji wanaweza kupata confidence ya sura ya nchi kwenye uwekezaji ni IMF, Mpango wetu wa *Policy Support Instrument (PSI)*. Tukienda kwenye *Sovereign Credit Rating*, sasa tutakuwa tuna eneo pana zaidi la wawekezadi kutoka Duniani kuja kuwekeza Tanzania na Serikali kupata mapato kwa ajili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ambayo kila Mbunge takribani ameizungumzia kuhusiana na mapato. Tunakokwenda ama hapa tulipo na pengine toka tumeanza bajeti hii, kumekuwa kuna changamoto kubwa sana ya utolewaji wa fedha. Wengi tulikuwa tukijadili kwamba, Hazina haitoi fedha. Ningetamani Hazina lile Jengo lote au Jengo hili la Bunge lingekuwa ndiyo fedha ambazo tunazipeleka kila pahali kwa wakati. Tukiondoka hapa, tukipitisha bajeti hapa, Hazina sasa kwa kushirikiana na Taasisi nyingine, maana na wao kila Taasisi inayokuja hapa, ina wajibu wa kupeleka fedha Hazina kwa mpango ule wa maduhuli. Kila Taasisi iliyokuja imesimama hapa. Kwa hiyo, siyo jambo la kuwa wao wanda-demand ama tunasema tupeleke fedha maji, no na wao wana wajibu wa kuleta fedha pale. Tukiondoka hapa tunakwenda kufanya taratibu zote za kukusanya mapato ikiwemo maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza, wengi wanashangaa kuona TRA inakusanya mpaka asilimia 90! Ndiyo, Bajeti yetu chazo chake siyo TRA peke yake. Sasa tuweze kukusanya TRA kwa asilimia mia moja na ishirini, kutokana na bajeti yetu ilivyo hatutaweza mapato ya asilimia 120 ya TRA kupeleka kila sehemu. Kama Saada, kama mwanamke, nisingependa kumwona mama anakufa kwa sababu ya ukosefu wa dawa hospitali, nisingependa kumwona

mama anakosa muda wa kufanyakazi, wa kumpeleka mtoto wake shule, kwa sababu ya kwenda kutafuta maji. Nadhani hilo ni suala la msingi na sote tunajua lakini tutafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo nimeliona hapa na Wabunge wamekuwa na motisha zaidi ya kulizungumzia ni kuhusiana na masuala ya kodi. Kila mtu ana wajibu wa kulipa kodi. Sote tuna wajibu wa kulipa kodi. Kodi ina vipengele vingi, tunaweza siku tukaleta hapa mapendekezo jamani hapa na pale twende kwenye kodi, watatoka wengine watatupinga lakini lengo letu tupate fedha.

Jambo la msingi, sina uhakika humu ndani, lakini tunapokwenda kunua vitu dukani sijui kati yetu sisi ni nani anaweza kusimama kwa ujasiri aka-demand risiti ya kile anachonunua; maana uki-demand ile risiti ndiyo unahakikisha sasa ile fedha yako ulioitoa pale, kodi unayokatwa, inakwenda kwenye core functions za Serikalini na baadaye inakwenda kulipia huduma za maji kijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu sote, siyo Hazina tu, ni wajibu wetu sote hususan wa kwanza tunaopata kupata tabu ya kusimama tukatetea. Waheshimiwa Wabunge nyote mnasimama kwa nguvu zenu nyote mnatetea, lakini tunafanyaje kwenye hili?

Naomba leo tukiondoka hapa, ukienda kununua soda, ukienda kununua mkate, dai risiti yako. Ndiyo, lazima tuwajibike sote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nimepata tabu sana kila Wizara nasimama. Mheshimiwa Waziri Mkuu kila Wizara lazima asimame, atoe maelekezo, atoe nini, vyanzo vyetu vya mapato tumeviweka, lakini suala la ulipaji wa kodi bado linakuwa gumu nchi hii, linakuwa gumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote zilizoendelea, kweli hatuwezi kutegemea misaada na mikopo kwa sababu wao wanawatoza kodi watu wao, wanatuletea sisi. Haiwezekani wenzetu wakalipe kodi sisi tuje hapa tutegemee wao, sisi tusilipe kodi. Tutafika miaka 200, 300 tuko katika hali kama hii, wajibu wa kulipa kodi unaanza kwetu sisi sote, Waheshimiwa Wabunge naomba tuungane kwenye hili, tuungane kwenye hili, lazima kodi ilipwe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wanakatwa kodi automatic hakuna ku-negotiate. Mfanyakazi huko huko aliko anakatwa kodi, pay as you earn, wanakatwa, *Income Tax* anakatwa, lakini wafanyakazi wakubwa hawalipi kodi, *it is true*, wafanyakazi wakubwa ndiyo wanakuja ku-compromise kutaka ku-negotiate na Serikali katika ulipaji wa kodi. *That is just not fair*, siyo *fair* hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wafanyakazi wanalipa kodi bila ya ku-negotiate na Serikali, huko huko watu wanakatwa, lazima ufike wakati tuweke misingi imara sote na Wabunge mna wajibu wa hili kwa sababu sasa hivi wako wengi hapa na lobbying yao kubwa ni aidha kupunguziwa kodi ama kutokulipa kodi. Tukilifanya hili hatuwezi kwenda. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala lingine la Mheshimiwa Faith Mitambo nadhani alikuwa na wasiwasi kuhusiana na ulipaji wa deni la Taifa. Alikuwa tu ana concern kwamba malipo ya mikopo ya nje ni shilingi bilioni 138, lakini malipo ya riba ni bilioni 200.52. Kwa nini malipo ya pesa zilizokopwa ni ndogo kuliko malipo ya riba. Concern yake iko valid lakini ina maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wakati tunapokwenda kukopa components nyingi za mikopo kunakuwa kuna eneo ambalo tunaita Grace Period yaani kama kabla ya kulipa ule mtaji wenyewe uliokuwa umekopa kuna kipindi cha mapumziko mikopo ambayo ni ya kawaida siyo commercial, siyo mikopo ya kibashara, nazungumzia mikopo ya concession kwamba kuna kipindi cha Grace Period. Sasa Grace Period zinaweza zikawa miaka 10, lakini kuna kipengele cha kulipia riba ambacho ukishakopa unaweza kuanza kulipa hata mwezi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo utaona kwamba sasa ile riba tunalipa nyingi ama tunaanza kulipa haraka zaidi, lakini ile principle yenye tutalipa baada ya kuanzia miaka 10 huko tunakokwenda. Kwa hiyo, ndiyo maana utaona katika mchanganuo wetu kwamba riba inakuwa kubwa kuliko ile principle yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nadhani liende sambamba na uelewa wetu sote ni kwamba, ripoti imetolewa kwamba sasa hivi kila Mtanzania anadaiwa sijui laki sita whatsoever. Mikopo hiyo mingine sasa ndiyo hicho ninachokieleza kwamba, wakati tumeanza kukopa, kuna mikopo mingine leo ndiyo tunaanza kulipa principle. Kwa hiyo, utaona leo deni la Taifa limekuwa kwa sababu kuna mikopo ya miaka 40 nyuma ndiyo tunaanza kulipa leo. Mbali ya kuwa tunaendelea kukopa, lakini kuna mikopo ambayo ilishakopwa zamani, kwa hivyo leo hii ndiyo tunalipa ile principle yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo itakwenda sambamba na sisi vile vile kama Serikali tuchukue wajibu wetu wa kuhakikisha kwamba sehemu tunazokopa ni sehemu ambazo zinatoa mikopo ya masharti ya nafuu, lakini vile vile tunahakikisha kwamba mikopo tunayokopa inawekezwa katika miundombinu ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuhakikishe tunakopa kwa Sheria na mikakati. Tunahakikisha kwamba hatuendi nje ya Sheria zetu za kukopa. Kwa hiyo, tutakopa maana hilo hatuwezi kuli-deny, kama hapa tunahamasisha benki zitoe mikopo ili mwananchi aweze kukopa ni sawasawa na Serikali sasa ni lazima na yeye akope. Kwa sababu njia moja ya financial inclusion pamoja na kupata hiyo mikopo. Kwa hiyo, tutakopa lakini tutahakikisha kwamba mkopo tunaokopa ni wenye masharti nafuu, lakini tunakopa kutokana na vigezo vyetu vya uhimilivu wa deni. Vile vile tuhakikishe kwamba tunakopa lakini mikopo yote inakwenda katika miundombinu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kulikuwa na hoja ya CHC. Tumezungumzia sana. Kweli tulitoa miadi kwa Kamati yetu ya Uchumi na nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, anafanya kazi nzuri sana pamoja na Wajumbe wa Kamati. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitoa miadi kwamba tutawasilisha tathmini ile CHC. Utaratibu tuliufanya na tuliwapata wenzetu wa Chuo cha CBE wakafanya tathmini. Naomba tu kutoa taarifa kwamba tathmini hiyo final imewasilishwa Mezani kwangu leo. Kwa hiyo, tutafanya utaratibu wa kuiwasilisha kwa Kamati kama vile ambavyo tumeahidi. Leo ndiyo imewasili na kwa sababu ilipowasili draft, tulitoa comment zetu tukairejesha na leo wamekamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na tathmini hiyo, ndiyo Serikali tutaweza kufanya decision uamuzi wa kuamua whether CHC iendelee or isiendelee. La msingi tulipofanya uamuzi wa kusema kwamba majukumu ya CHC yamalizike tarehe 30 Juni, 2014 au kuna concern nyingine inasema labda TR hajatayarishwa? Nataka kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge, TR ametayarishwa ametayarishwa kupokea majukumu ya CHC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yataendelea kwa sababu wale Watendaji amba walikuwa wako CHC wana uzoefu mkubwa sana. Tutaendelea nao kwenye Treasury Registrar

yetu, hatutawachukua wafanyakazi wapya. Majukumu yataendelea yatakuwa yanafanywa na wafanyakazi wale wale. Kwa hivyo, lengo letu hapa ni kuwa tusiwe na Taasisi mbili ambazo kimsingi majukumu yake yanafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni katika kwanza, kupunguza hizi gharama. Tutakuwa na chombo kimoja chenye nguvu, ambacho kitafanya kazi za CHC. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tuna nia njema tu na hili jambo kwamba tuna-harmonize vyombo hivi viwili ili kiwe chombo kimoja chini ya Msajili wa Hazina na zifanye kazi. Hata hivyo, tutawasilisha kwa Kamati ripoti ile na tutakuwa tunashauriana kadri tunavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika,, suala la PPP, concept ya PPP naweza nikasema kwamba siyo mpya hapa kwetu, isipokuwa tulikuwa hatuna Sheria ya PPP. Kuna miradi inafanyika ya PPP, leo ukienda Airport pale tutaona Swiss Port wanafanya kazi zao. Mfano kama ule ni PPP, lakini umeingiwa kwa utaratibu ambao ni utaratibu halali, lakini sasa tunataka tuweke Sheria ambapo taratibu zote za kuingia mikataba ya PPP ndizo zitakazofuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii PPP siyo kama hatuna miradi. Miradi ipo isipokuwa miradi ambayo itakuwa chini ya Sheria ambayo tunataka kuianzisha ndiyo kwa sasa, kwanza tunaanza na mradi DART. Actually DART ni pure PPP na miradi mingine ambayo bado tunakwenda kufanya assessment.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa hapa mbali na Sheria, Serikali ilikuwa haina Mfuko wa kuwezesha feasibility studies kufanya. Kwa hiyo, mwekezaji anapokuja anataka kufanya PPP anakwenda anagharamika kufanya stadi, lakini baadaye stadi kama anaiona kwamba mradi ule hauko viable kwake yeye, anaondoka. Kwa hiyo, tunataka tu-facilitate PPP vile vile na katika bajeti ya mwaka unaokuja tutahakikisha kwamba tunaweka Mfuko huu wa PPP Facilitation Fund, ili kuhakikisha kwamba tunafanya sisi wenyewe hizo feasibility study na mwekezaji anapokuja anaiona feasibility study iko viable yeye anawekeza fedha zake kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, PPP ipo, lakini siyo katika utaratibu ule wa kisheria ambayo tunataka tuweke hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Serukamba alizungumzia eneo lingine la asset management. Nadhani totalichukua hili kwenda kufikiria shares zetu ambazo hazileti tija na hizi tunaweza tukazuza ili kupata finance, lakini kuna shares ambazo zinafanya vizuri. Nachukua fursa hii sasa kuwapongeza NMB wanafanya kazi nzuri sana na wengineo ambao vile vile kama Serikali tunapata dividend zetu kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kuhusu DART Mheshimiwa Rage, Serikali kama itatoa subsidy sisi hatuna taarifa. Sisi hatuna taarifa kwamba tuta-subsidize nauli na the way tunavyoona kwamba kama hivyo ndiyo ilivyo basi hii itakuwa siyo sustainable. Isipokuwa ninachosema kwamba sisi hatuna taarifa. Kwa hiyo na hiyo taarifa kama proposal ikiletwa basi tutaifanya kazi tuone sustainability yake, lakini mpaka sasa be comfort kwamba Serikali haina taarifa hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameelezwa kuhusiana na riba, nadhani mwenzangu Naibu Waziri amelielezea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna issue hii ya UDA. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akitiba kesho yake, magazeti yote yakamwandika Naibu Waziri wa Fedha amepata wapi ujasiri wa kuelezea maelezo yale. Yeye alijibu kwa niaba ya Waziri wa Fedha, lakini tu nadhani tufunge mjadala huu labda kwa statement inayofuata kwamba, Serikali chini ya Msajili

wa Hazina tuna-own tunamiliki asilimia 49 za Allotted Shares. Kwa sababu ikiwa tumeuza, mimi kama Waziri wa Fedha sina taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia kumbukumbu hakuna taarifa za kuuzwa hizi na utaratibu wetu wa Kiserikali unajulikana. Kwa hiyo, Baraza la Mawaziri halijapokea taarifa ya uuzwaji wa Shares hizi na TR wangu ndiyo anakamilisha pendekazo hilo kwa ajili ya kupelekwa Baraza la Mawaziri. Kama ufahamu wetu uko sahihi basi zile Unallotted Shares yaani bado zile shares ambazo hazijagawanya. Tunachokifahamu sisi kama Hazina zinabakia 7,880,303/= kama zilivyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo msimamo wa Serikali mpaka sasa hivi, asilimia 49 ya shares zetu. Kwa hiyo, hakuwa Mheshimiwa Malima lakini ulikuwa ni msimamo wa Serikali. Kuna mapendekazo ya kupelekwa, nadhani tutayachukua mapendekazo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na tutayaafanya kazi, lakini huu ndiyo msimamo wa Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Sheria ya Bajeti, mpaka sasa hatuna Sheria ya Bajeti, lakini ni *intention* yetu kama Hazina kukamilisha Sheria hii ya Bajeti. Tumeshaanza na tutaendelea nayo mbele kwa sababu hata sisi kama Serikali hatupati *comfort* na yanayoendelea, fedha hazipo, lakini zile zilizokuwepo kunakuwa na matumizi mengine mengine, hata huko tunakozipeleka. Waheshimiwa Wabunge tunaomba tu *support* yenu wakati tutakapoleta hii Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zainab Kawawa ingawa alisema, leo hasemi kwa ukali, lakini nau-feel ule uchungu wake aliokuwa anauelezea kuhusiana na PSPF. Nataka kumpa *comfort*, alikuwa na uhakika kwamba Serikali haijalipa hata sumni, lakini tumesha-allocate bilioni 50 (*Fifty billion*), tayari tumeshazi-allocate na tutakwenda kuzilipa PSPF kabla ya Juni 2014. Tunajua kweli kwamba kama hatutalipa PSPF itapata hasara na sasa tutaipa kipaumbele kuhusiana na malipo kwenye PSPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi holela wa gari, limesemwa nalo katika nia njema ya kupunguza matumizi. Hata maelekezo ya Mheshimiwa Rais mwenyewe ameshatupa lazima magari yanunuliwe kutokana na yule mtengenezaji. Maana ukiingia huu msururu wa katikati hapa ndipo unaposikia gari limenunuliwa shilingi milioni 250. Kwa hiyo, sisi kwa sababu ndiyo tunaosimamia manunuzi tumeshaandaa Waraka na tunaapeleka Baraza la Mapinduzi, samahani Baraza la Mawaziri kwa ajili ya, *the sleep of the tongue*. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapeleka Baraza la Mawaziri, nadhani mmenielewa, tunapeleka Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuridhiwa. Hii isiwe hoja, mmenielewa. Kwa hiyo, hilo tunalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna-encourage sana Taasisi, Mawizara pale ambapo hakuna umuhimu wa kufanya semina nje, nadhani kila Wizara karibu zote zina Kumbi za Mikutano. Tufanyeni ndani, hata si-encourage Kamati za Bunge ziende Bagamoyo, mimi mwenyewe si-encourage. Wabunge tunazo Kumbi kule, njooni tutumie. Hii ndiyo tuna-save, we are saving the money kwa ajili ya kupeleka kwa wananchi kwenye maji, kwenye umeme. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa hata nyinyi mkiwa mna Semina tuambieni sisi. Kama mna Semina Dodoma tuna Kumbi tutakupeni kule. Tusikodi kumbi, si kama tunataka tusiwape biashara, lakini pale ambapo tunahisi sisi wenyewe tunaweza tukaji-accommodate vizuri sisi wenyewe, tukawa comfortable ambapo ni sehemu tutaweza kufanya

semina vizuri. Tufanye, kwa sasa mnatuambia sisi tupunguze magari, ununuzi wa samani na nini, I hope nimeelewaka, lakini tuanze na sisi vile vile kama Waheshimiwa tuonyeshe mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifurahishwa sana safari hii tumekaa na Kamati ya Bajeti ukumbi wetu wa pale *Foreign Affairs Mwalimu Nyerere*. Yaani comfortably kabisa, tumekaa vizuri yaani vitu kama hivyo ndivyo ambavyo, hii nidhamu ya matumizi iwe kwetu sote siyo tu kwa Serikali kwetu sote na sisi Waheshimiwa Wabunge. Uwe unakwaraza kote kote msumeno. Kwetu na kwenu, sote tuonyeshe kwamba yale ambayo tunayozungumza tunayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuwe sote tunajitahidi, sisi kama Serikali tutajitahidi, upande wa magari na upande wa ununuzi wa samani. Tuliletu mwaka jana tamko na mambo mengine mengine tutahakikisha kwamba tunapunguza matumizi kwa njia hizo ili fedha zinazopatikana ziende kwenye maji na umeme, kweli vijijiini tunakokwenda hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nikimsikia Mheshimiwa Haroub anataka hata watoto pia walelewe na Serikali, lakini sasa fedha yenyewe ndiyo hivyo. Kwa hiyo, hili tulatifanya kazi kwa upande wetu, lakini vile vile kwa upande wenu tulifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika,, kulikuwa kuna hoja nyininge ya *dollarization*, tatizo according to statement iliyotolewa hapa ni kwamba, kubwa. Wakati ilipokuwa ikitolewa hoja hii mwaka jana ama mwaka juzi, sisi Wizara kuitia Benki Kuu tulifanya research ili kuona kwamba hili tatizo lina ukubwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya research yetu kwa mikoa karibu sita na tukachukua watoa huduma 3,945. Mikoa tuliyofanya ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma pamoja na Morogoro. Sasa basi labda tu naweza nikawapa matokeo ya utafiti wenyewe, ni kwamba, pengine inawezekana matokeo ya utafiti wetu usiende na dhana nzima ya wanaofikiria kwamba tatizo hili bado ni kubwa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, asimilia 3.2 tu ya wafanyabiashara na watoa huduma wanankuu bei kwa fedha za kigeni, lakini biashara kama hii ambayo inakuwa quoted kwa fedha za kigeni, kuna baadhi ya maeneo, kwa mfano, Dar es Salaam maeneo kama Oysterbay, Masaki, Mikocheni, Upanga. Wao wanankuu biashara zao kwa dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matumizi hayo ya fedha za kigeni katika kunukuu bei, yanalinga zaidi baadhi ya huduma pamoja na bidhaa, nyumba za kupanga, shule binafsi international school, kuna malipo ya ving'amuzi kama DSTV na baadhi ya vitu vikubwa kama vile magari na kompyuta, lakini walengwa ni wateja maalum hasa wageni kutoka nje ya nchi ambao wanatembelea na wanaoishi nchini kwa muda, kama vile Mabalozi, wafanyakazi na Mashirika ya Kimataifa, wanaweza kulipa kwa shilingi vile vile, lakini haya ni matokeo ya tafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna proposal ambazo zimetolewa kuhusiana na Bureau De Changes, kuhusiana na suala la kuwa, hawatoi risiti. Kwa kushirkiana kwa pamoja, hili tunaweza tukalitatua. Unapokwenda kubadilisha fedha zako dai risiti na akupe risiti, lakini vilevile kuitia Benki Kuu tutahakikisha kwamba, sasa hata hizo Bureau De Change, maana hii kutoa na kudai risiti iwe ni wajibu wa kila mtu. Hata hizo Bureau De Change nazo zinatoa risiti kwa lengo la kuhakikisha kwamba, hii Dolarisation tunaweza ku-maintain, lakini vilevile tuhakikishe kwamba, hata biashara inayofanyika ni biashara halali. Mwenzangu alielezea kwa kina kuhusiana na hii na jinsi gani ilivyokuwa hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukasema tufunge moja kwa moja matumizi ya dola, haiwezekani. Tanzania ni nchi inayoendelea, Wawekezaji, hususan wawekezaji wetu wa ndani

bado wana-demand hata dola kwa ajili ya kwenda kununua vitu na kuleta ndani. Kwa hivyo, kusema kwamba, tunalifunga hili haliwezekani na kiwango cha sasa cha *Dolarisation* hapa ni 30%, ambacho ni kiwango cha wastani katika nchi za Afrika. Wenzetu wako juu zaidi, lakini kwa 30% bado ni kiwango cha wastani, lakini tutachukua mapendekezo yenu Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kutusaidia na hili jambo likatulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa David Kafulila, alizungumzia kuhusiana na mafao ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Mgodi Uvinza. Nadhani tumelichukua na tutaliangalia, maana madeni yapo mengi sana, tunayaafanyia assessment, lakini tutalichukua kwa umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna moja kubwa na la umuhimu ambalo limeelezewa, hususan madeni yanayozikabili Taasisi za Serikali. Kwetu sisi wakati tunapotoa fedha ndani yake kunakuwa kuna component ya kulipa madeni, lakini tumeona hii trend ya kuwa suppliers hawalipwi kama inavyotakiwa, hawalipwi kabisa. Kweli hawa suppliers ndio wanao-supply vitu Mawizarani, Serikalini na kadhalika.

Sasa basi, kuanzia mwaka 2014/2015, tumeanza kulifanya hili zoezi sasa hivi; Hazina itachukua jukumu la kulipa madai moja kwa moja. Yaani sisi sasa Hazina tutakuwa tunalipa madai ya Wakandarasi, tutakuwa tunalipa madai ya Wazabuni wengine moja kwa moja, maana tumeona kwamba, tukiziingiza hizi fedha na kwa sababu fedha zenyewe zinakuwa kidogo, kweli priority hapewi yule Supplier, lakini sisi tutalichukua, tumeanza ingawa zoezi liliikuwa gumu, lakini tumesema tumeweza. Kwa hiyo, hili tutalichukua na nimeona concern hii pia ya Wabunge wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa kuhusiana na Taasisi za Kifedha, hususan VICOBA. Mheshimiwa Assumper Mshama alilisemea hili vizuri na sisi tunataka kutoa tu taarifa kwamba, tulikuwa tumepeleka muundo wetu wa Wizara kwa ajili ya ku-accommodate Idara ambayo itasimamia hizi *micro finance*, ikiwemo VICOBA na SACCOS. Tumeputa approval ya kuanzisha Idara hiyo na tutaanzisha, tutaanzisha Sera na Sheria, ili kuhakikisha kwamba, sasa VICOBA inakuwa sehemu ya *Financial Institution* kama zilivyo hizo nytingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele imelia, naomba kutoa hoja, lakini kabla hawajasimama napenda tu kusema kwamba, kuna Mwanafalsafa mmoja alisema kwamba, "Even if you fall on your head", hata kama utaanguka mbele, lakini ukafikia kichwa, you are still moving forward, bado utakuwa umesogea kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa tulitafakari hili, kuna changamoto nydingi, lakini tuzi-recognise efforts ambazo zinafanywa na Wataalam wetu. Wizara ya Fedha, wanajitahidi, kuna wengine kweli, wana upungufu, lakini wengi wao wanafanya kazi kwa jitihada kubwa sana, tutashirkiana pamoja katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya kwa kujaribu kupitia Hoja za Waheshimiwa Wabunge; nafahamu muda ulikuwa hautoshi, lakini umejitahidi kupitia hoja nydingi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu, tuendelee!

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 7 – MSAJILI WA HAZINA

Kif. 1001 - Administration and Human Resources Management... ... Sh. 1,225,759,600/=
Kif. 1002 - Finance and Accounting Sh. 281,494,800/=
Kif. 1003 - Planning Unit Sh. 631,390,000/=
Kif. 1004 - Legal Services Unit Sh. 79,156,000/=
Kif. 1005 - Procurement Management Unit Sh. 316,648,000/=
Kif. 1006 - Information and Comm. Technology Sh. 260,546,000/=
Kif. 1007 - Information, Education and Comm. Unit... Sh. 56,500,000/=
Kif. 1008 - Internal Audit Unit Sh. 169,423,000/=
Kif. 2001 - Public Investment MGT Division Sh. 84,560,140,000/=
Kif. 3001 - Privatization and Monitoring... Sh. 403,539,000/=
Kif. 4001 - Management Service Division Sh. 470,681,600/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Sasa Katibu, ili kuokoa muda twende kwanza kwenye Fungu la Mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ndio tutarudi kwenye haya mengine. Fungu Namba 50.

FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA

Kif. 1001 - Administration and Human Resources Management Sh. 10,318,596,000/=

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Chami.

MHE. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri anaeleza jinsi ambavyo Wizara imeweka taratibu nzuri za kuwafanya wananchi waweze kunufaika na sekta ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia na nimemwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuwasiliana na Benki Kuu na atupe majibu hapa kuhusu sababu ambazo zimeifanya Benki Kuu ikaongeza kiwango cha kuanzisha Benki za Wananchi kutoka shilingi milioni 250 mpaka bilioni mbili. Nikasema kwamba, ni vigumu sana kwa wananchi wa Tanzania kuweza kuanzisha Benki kama kiwango kinakuwa kikubwa namna hiyo cha shilingi bilioni mbili, ukizingatia kwamba, Watanzania walio wengi ni wakulima vijijini. (Makofî)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi Moshi Vijijini tulikwenda Benki Kuu tukaambiya milioni 250; tunaanza kukusanya fedha tumekwenda Benki Kuu tukaambiya zimeongezeka imekuwa bilioni moja. Tumekusanya tena *commitments* tumekwenda Benki Kuu tukaambiya bilioni mbili, wananchi wamekata tamaa, hawakuchanga tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri awasiliane na Mheshimiwa Gavana wa Benki Kuu, ambaye alinisaidia sana ili angalau wakati tunapeleka Sheria ya Kurekebisha mambo kama Mheshimiwa Malima alivyoahidi hapa, angalau kwa upande wa Moshi Vijijini ambako wananchi wameshatoa fedha zao *tupewe exception*, ili tuweze kuanza Benki hiyo kwa sababu, ziko benki nydingi hapa Tanzania za wananchi ambazo zinafanya vizuri, lakini mitaji yao ni milioni 500, milioni 400. Sasa kwa nini Moshi Vijijini tulazimike kuweka bilioni mbili ndio tuanze Benki hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana; naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri. (Makofii)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM K. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Chami kwamba, kuna mabadiliko kidogo kwenye Capitalisation ya hizi Benki. Kinachosababisha *ku-raise* ile Capitalisation ni kwamba, wakati vile viwango vya awali vinawekwa miaka hiyo iliyopita na uwezo wa wale depositors nao ulikuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachoendelea sasa hivi ni kwamba, tunatarajia kama nilivyosema wakati nachangia pale kwamba, hivi vibenki vidogovidogo vifanuke zaidi na viwe na uwezo wa kuhimili zaidi hata misukosuko ndani ya benki, lakini pia tunataka hata wale wanao-deposit hela zao wawe na uhakika kwamba, wakiweka hela zao wakija wakizihitaji watazikuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii deposit ya milioni 250, nakumbuka, nadhani ilikuwepo hata mimi nilipokuwepo karibu miaka 18 iliyopita. Ni *ka-deposit* kadogo, kwa hiyo, as the economy as evolved wame-raise ile to two billion.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, kitu kingine ambacho tunajaribu kuhamasisha kwenye hizi Benki ndogo ndogo ni kwamba, mbali ya ile Capitalisation inayotokana na michango ya wale wanaochanganya, lakini pia watafute ubia na hizi Benki zingine. Ndio lile nililokuwa nasema kwamba, kuna mabenki ambayo kama ni NMB, CRDB na nani, yanaweza yakawa na ubia na hivi vibenki vidogo vidogo, ili kuwapa sustainability kubwa zaidi na kuwapa backup ile benki just in case kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni katika yale ambayo tumesema tunakwenda kuongea na Benki Kuu, ili waweze kujenga mtandao ambao unahimili kuhamasisha ukuaji wa hizi benki ndogo ndogo, biashara ndogo ndogo na wakulima pia wadogo wadogo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuiliza hiki Kifungu cha Waziri. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya pamoja na wasaidizi wake; nina imani kwamba, mwanzamke mwenzetu hatatuangusha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata ufanuzi kuhusiana na malipo ya wafanyakazi wa Kiwanda kilichokuwa cha Almasi, wafanyakazi 430, shilingi milioni 649. Toka mwaka 1995 kimefungwa kiwanda hiki cha Tancut

Almasi, lakini mpaka leo hii karibu miaka 20 wafanyakazi wale bado hawajalipwa mafao yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kuleta swalii hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri nafikiri alinijibu, japokuwa bado mpaka sasa hivi hatujajua hatima yao kwa sababu, nimekuwa nikiitwa sana kwenye vikao vyao kwa sababu unajua wafanyakazi 430 sio watu wachache; wana familia zinazowahusu na kuna wengine ambao tayari wameshapoteza hata maisha, kuna wengine wameshaathirika hata kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba, hata Sheria ya Muflisi inasema kwamba, kiwanda au shirika likifilisiwa na Serikali, watu wanaopewa kipaumbele ni wale wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi pamoja na madeni. Tunajua kwamba, kiwanda hiki kilikuwa kina mali za kiwanda ambazo ziliuwepo na tunajua kwamba ziliuzwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba leo hii pengine Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ambayo kwa kweli, imekuwa ikifanya vizuri sana na nashukuru hata Mheshimiwa Msigwa amekubali kwa sababu, usafi pale unafanyika vizuri sana na kwa sababu, Madiwani wengi ni wa CCM na ndio maana amekuwa akifanikiwa sana mambo yake katika lile Jimbo. Ningeomba kwa kweli, msiniangushe wafanyakazi hawa wapewe sasa jibu ambalo litawasaidia. Na ninajua kwamba... (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nitatoa shilingi kama sitapata majibu mazuri. (Makof)

MWENYEKITI: Umeshachelewa Mheshimiwa Rita.

Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MWIGULU L. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rita Kabati kwa kufuatilia sana maslahi ya Watanzania na haki zao. Niseme tu kwa niaba ya Waziri wa Fedha, jambo hili la madeni tofautitofauti, likiwemo hili alilolisemea, tulishaanza kulifanyia kazi na tunafanya kwanza uhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ni mengi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alisema, kwa Iringa kuna hilo, kwa Njombe kuna watu wa Mgololo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunalifanyia kazi kama ambavyo Waziri alishalitolea maelekezo kwa Wataalam kuweza kuhakiki na kwa kuwa, bado tupo na timu kwa kweli, imedhamiria kubana matumizi ili kuweza kuhakikisha kwamba, watu ambao wanadai haki zao waweze kupata haki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpongeze tena Mheshimiwa Ritta kwa kuwa mzalendo. Uzalendo sio kuwashambulia watu waliovaa scuff ni kuwasemea wanyonge. (Kicheko/Makof)

MWENYEKITI: Huo ndio msemo wa leo huo. (Kicheko)

Mheshimiwa James Mbatia!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye maoni yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tuliulizia suala la kuwa na Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Sheria ya Bajeti kwa sababu, licha ya maelezo mazuri waliyotoa Waheshimiwa Mawaziri hapa, suala la nidhamu ya matumizi ni matatizo makubwa. Re-allocations zinafanya bila utaratibu, performance ya bajeti inakuwa ni matatizo, hasa bajeti ya maendeleo, sehemu nyine inakuwa na 30%, kwingine 20%, kwingine 40% na nyine bajeti ya matumizi inakuwa zaidi au fedha za maendeleo zinakwenda kwenye matumizi, yaani ule utaratibu mzima wa kibajeti unakuwa hauna nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka tupate *commitment* ya Serikali, ni zaidi ya miaka miwili sasa wanatoa ahadi ya Sheria ya Bajeti kuletwa ndani ya Bunge hili ili haya tunayopitisha tuweze tukahakikisha yanatekelezwa ipasavyo na Bunge liwe na nafasi ya kuisimamia vizuri Serikali na hata bajeti ya mwaka huu tunayomalizia sasa ina upungufu mkubwa sana wa mapato na matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali *iji-commit* hapa kwenye Bunge lijalo ihakikishe Sheria ya Bajeti inakuja kwenye Bunge hili ili tuhakikishe kwamba masuala yote ya kuisimamia Serikali, yanakwenda sawasawa. Sasa nataka *commitment* ya Serikali, je, Sheria hiyo italetwa mwaka huu yaani kwenye Bunge lijalo? Kama sitapata majibu ya kuridhisha nakusudia kutoa shilingi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. MWIGULU L. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama ambavyo alisema Mheshimiwa Waziri kwamba sisi kama Serikali tunakubaliana mia kwa mia kuhusu umuhimu wa Sheria ya Bajeti na umuhimu wa Kamati yenewe ya Bajeti. Kama utakavyoona Kamati hii imeendelea kuwa ya msaada sana kwa Serikali na sisi tunataka isitusaidie tu kwenye zimamoto ya wakati wa bajeti, tunataka kadiri tunavyopitisha tu bajeti tuanze hapo hapo kuhakikisha kwamba bajeti inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lilipo tu nikienda kwenye swalı lake, sisi kama Wizara tumeshakamilisha concept paper ya mapendekezo, lilipo tunatakiwa tupitishe kwenye utaratibu, iende kwenye Cabinet Secretariat, ifuate hatua zote, halafu na kuhusu kupangiwa nako itarudi kwenye kitu chako kama utakavyokumbuka kwamba tuna Miswada kadhaa ambayo tumeshasema kwenye Bunge linaloshughulika na Miswada tutaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wake na mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Bajeti nimhakikishie Mheshimiwa Mbatia kwamba jambo hili litapewa uzito unaostahili na nimwombe tu wala hata asitoe shilingi kwa sababu bajeti ikitekelezwa vizuri, kwetu sisi ni mafanikio makubwa sana ya hii timu na Serikali na sisi hiyo ndio nia yetu. Kwa hiyo, hili wala halina ugomvi, wala hatutachelewa hata sekunde baada ya kuwa tumeshakamilisha hili.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kusudio langu la kutoa shilingi sasa nalitamka kwamba natoa shilingi. Nasema hivyo kwa sababu zaidi ya miaka miwili sasa, tumeona hii Sheria au Muswada wa VAT unakuja kwa haraka, hii ni sehemu ya kupata mapato. Sasa kuna upande mwengine wa pili wa kuisimamia matumizi, Serikali hapa inasema bado ipo kwenye mchakato. Sasa hizi lugha za mchakato, mchakato, mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji ni kwamba Sheria ya Bajeti ije kwenye Bunge lijalo, wafanye kazi usiku na mchana ili kama mapato yakipatikana huku, matumizi nayo vile vile yasimamiwe, tuondoke kwenye haya mambo ambayo ni zimamoto, patapotea. Nakubaliana kabisa kama alivyoeleza, lakini tunachohitaji kwa Serikali ituambie ni lini Sheria ya bajeti italetwa ndani ya Bunge lako Tukufu? Nimesema natoa shilingi ili wenzangu nao wawezekuchangia suala hili.

MWENYEKITI: Hili jambo la lini kabla ya kuchangia hatuwezi kupata angalau hints kidogo labda kutoka kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, kwa sabbau suala ni lini kwa kweli.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, haya anayosema Waziri ni kweli na sina hakika kama ni Bunge lijalo kwa sababu Bunge lijalo linawezekana kuwa mwezi Julai kwa sababu hili jambo linatakiwa umakini wa uandishi. Nilipokuwa kwenye Kamati nikibembeleza bajeti yangu iongezwe niliwaambia kwamba kwa sababu ya transparency ya bajeti process na matumizi tunahitaji Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jambo ambalo hata mimi mwenyewe nalikubali na tuhakikishe kwamba kabla ya mwezi Disemba tutakuwa tumeleta hapa Rasimu hiyo kwa kupitia hizo ngazi zote ambazo amesema Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunaomba urudishe tu shilingi yako kaka yangu Mbatia.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa James naona kama mnaongea lugha moja tafadhalii Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwanasheria Mkoo amesema kabla ya mwezi Disemba yaani Bunge la Novemba mwaka huu kama nilivyomwelewa kwa kuwa kusudio hilo amelisema, narudisha shilingi nimekubaliana naye. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge niliwaambia wakati ule kwamba, tulipitisha order paper ya ziada ambayo baadaye Makatibu leo leo watasoma baadhi ya Miswada ambayo itasomwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kikao kitakachofuata baada ya hiki. Mheshimiwa Zungu!

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katiba imetambua idara au vyombo ambavyo vinatakiwa vifanye kazi kuisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake; kuna chombo cha CAG, Attorney General, Chief Justice ni vyombo ambavyo vina heshima ya juu na hakuna kuvi-question kwa sababu vimeaminiwa na watu wanaopewa vyombo hivi wanaaminiwa na Katiba inawaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua tu, inapotoka kauli kuwa ripoti za CAG ni ripoti tu, hata mwaka jana tulifukuza Mawaziri Hazina, nataka kujua tu kwa Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa Wizara yake ambaye pia anafanya kazi zero distance na CAG. Serikali inasemaje kuhusu credibility, are we questioning CAG katika Bunge hili na ukitazama CAG wala hafukuzwi kazi na kama anatuhuma inachukua Majaji matatu wa Kimataifa kuja kuchunguza na kum-relieve duties zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie, sina shida ya kutoa shilingi ila nataka anisaidie credibility ya chombo hiki cha CAG na vitabu hivi ambavyo anavitengeneza kila mwaka, tunamsifia na kwa kazi nzuri anajenga hoja kuiweka Serikali in line na kutusaidia sisi Wabunge kujua upungufu ambaio unatokana na utendaji. Nataka anisaidie tu Mheshimiwa Waziri, how does she hold Ofisi ya CAG kwenye ripoti zake ambazo zinakuja Bungeni na zinakwenda katika maeneo mbalimbali ya nchi.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunamtambua CAG na CAG ametambuliwa katika Katiba. Kwa hiyo, kwanza credibility yake iko hapo kwamba ni chombo

ama ni mtu ambaye anatambuliwa kwenye Katiba. CAG ana utaratibu wake wa kufanya kazi na katika Bunge hususan hili Bunge la bajeti nadhani ripoti za CAG ndizo zinazo-*hold* hapa, sote wengi wetu tumekuwa tuki-quote vifungu vingi kwenye ripoti ya CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Waziri sina *doubt* kabisa na ripoti ambazo zinatolewa na CAG. CAG anafanya kazi kwa utaratibu, CAG anapoingia kwenye taasisi anakuwa na *entry meeting* anafanya kazi yake akiondoka ana *exit meeting*. Tunapewa nafasi sisi kama Watendaji kuanza kushughulikia ripoti za CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ripoti za CAG zipo *credible*, tunazithamini na ndizo ripoti ambazo zinatoa mwelekeo wa aidha *fault* zilizotoka au aidha kama yako mambo ambayo hatujatekeleza. Kuna mambo mengi ambayo CAG amekuwa akitoa ripoti na tumeyatekeleza sisi, tunaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna *doubt* na ripoti hizi za CAG. Mimi kama na yumo humu namwombea fedha zake, kwa hiyo sina tatizo naye na nadhani ripoti zake ziko *valid*. Utekelezaji wa ripoti za CAG ndiyo hatua nyingine, lakini utoaji wa ripoti zake nadhani hakuna *doubt* na sote nadhani tunakubaliana na hilo.

MWENYEKITI: Labda tu kidogo katika hili kwa maana ya uendeshaji wa Bunge, Bunge kama taasisi, CAG ana ripoti kadhaa, ana ripoti za kazi maalum anazopewa na Serikali anapeleka moja kwa moja na kadhalika, lakini zile *standard* ripoti za kawaida ambazo zinakuwa *laid* hapa, baada ya hapo zinakwenda kwenye Kamati zetu zile za fedha.

Kamati za fedha zinazipitia zile ripoti na Kamati zile zinatengeneza ripoti kufuatia ripoti ile, ripoti zile zinakuwa *tabled* hapa. Ni vizuri sana Wabunge tukatumia ripoti za Kamati kuliko kuchukua ile ripoti ile ya kwanza ambayo ni raw, tayari tunalipeleka Taifa kuliaminisha vitu ambavyo bado viko kwenye mchakato, havijafika mwisho. (Makofii)

Kwa hiyo, niwatake tu hasa wajumbe wale wa Kamati zetu zile kufanya kazi yao kwa wakati, kwa haraka, kutuletea ripoti ili tufanye kazi kwa ripoti zile kuliko kila wakati inakuwa CAG kasema mabilioni fulani yamefanya hivi baadaye ripoti ikija ya Kamati inazungumza vitu viwili tofauti. Kwa hiyo hilo ni la kuliweka sawasawa kwa sababu baadhi ya watu wanapenda sana kurukia ripoti ya CAG ambayo bado ipo kwenye process ili tuweze kwenda wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Chomboh twende Zanzibar kidogo!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushika mshahara wa ndugu yangu leo hapa. Kuna tatizo moja ambalo nataka Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi. Katika Kitabu chake moja katika matatizo amesema kwamba kuna upungufu au ukosefu wa mapato, ni ushuru wa bidhaa ambazo kuna bandari au njia za panya zinazopita bidhaa mbalimbali katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja liliokuwepo ni kwamba TRA haijaweka au haina misingi ya kuwafanya walipa kodi kuona kwamba ni lazima walipe kodi, hawawawekei mazingira rafiki, wanawawekea vitu ambavyo vinawafanya wafanyabiashara wawakimbia TRA na baadaye watafute njia za panya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mmoja, Zanzibar kuna containers au kuna meli ambazo zinatakiwa kwenda kuteremsha mzigo Zanzibar, kuna baadhi ya meli hazifiki Zanzibar kwa sababu ya ukubwa wake na container zile *port of destination* ni Zanzibar zinafika Dar es

Salaam, Dar es Salaam zinakuwa destuffed zinakwenda Zanzibar kwa ajili ya kulipia kodi then kwenda kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatokea mfanyakibashara yuko Dar es Salaam *in address*, lakini soko lake liko Zanzibar akateremsha mzigo wake *destination* Zanzibar, lakini TRA wakazuia containers ambazo zinatakiwa ziende Zanzibar kwa sababu tu *address* ya mwenye mzigo ameandika ni Dar es Salaam, lakini *port of destination* ni Zanzibar, Kisheria kontena lile lifike Zanzibar, kuna TRA, lifanye *verification* lilipiwe ushuru kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sasa limeshalipwa kontena Zanzibar, *verification* inafanywa Dar es Salaam, *this is unfair*. Unamfanya mfanyakibashara atafute njia nyingine makusudi kwa *interest* ya mtu tu, hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake zaidi ni kwamba sasa hivi wafanyakibashara wanafikiria sasa kontena wasizilete Dar es Salaam zikateremshiwe Mombasa. Sasa matokeo yake bandari ya Dar es Salaam itakosa kazi, yatateremshwa Mombasa yaje Zanzibar, then Zanzibar yawe verified.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Umeelewaka. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani analolisema Mheshimiwa Chomboh hapa ni jambo ambalo specific lilitokea mwezi mmoja karibu nyuma na mimi binafsi nimelishughulikia. Nimekwenda Zanzibar, nimekutana na wengine baadhi ya wafanyakibashara, lakini lilipelekwa lenyewe kwa Wizara ya Fedha, Zanzibar na wakati tumekutana pamoja na Waziri mwenzangu wa Fedha Zanzibar tukalzungumza suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ile action ya TRA, tumeona hapa kwamba wengi wanailaumu TRA, baadhi yao wanaisifu kwa sababu wanakusanya, lakini wengi wanailaumu TRA kwa kuwa labda kuna wafanyakazi ambao siyo waadilifu. Sasa wale kama *institution*, kama staff wanachukua kila *precaution* ya kuhakikisha kwamba kama kuna kitu tu kinatiliwa mashaka si utaratibu wa kawaida ndiyo wana-hold.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili lilitokea kwenye makontena haya ni kwamba, addressee yaani yule mtu ambaye anapelekewa ule mzigo *address* yake ilikuwa ya Dar es Salaam, lakini *port of destination* ilikuwa ni Zanzibar. Katika utaratibu kama huo TRA walichukulia kwamba hapana isije kuwa kwamba huu mzigo unapelekwa Zanzibar, halafu utarudi Dar es Salaam yaani ioneokane kwamba ushuru umelipwa kule, kule pengine ushuru haukulipwa yaani, utakwenda Zanzibar halafu utarudi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kilichotokea TRA kweli walizua hili na wakasema lazima tufanye *verification* walifanya *verification* na kwa makubaliano ya wafanyakibashara wenyewe, wakasema kweli hili tumekosea lakini mzigo kweli *destination* ulikuwa unakwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo walifanya *verification* na wakaamua kwamba sasa kwa sababu mzigo unakwenda Zanzibar, hiyo *verification* acha ifanyike, lakini mzigo utakwenda kushuka Zanzibar. Kwa hiyo, hiyo ilikuwa ni *unique case otherwise tunajitahidi* kama TRA kutatua migogoro kama hii hususan kwa sababu migogoro kama hii ndiyo inayochipua hata hizo kero tunazozita kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajitahidi kwamba kuweka utaratibu, lakini vile vile tusitiliwe mashaka kwamba, kwa sababu kodi lazima wafanyabiashara walipe kodi stahiki whether TRA Makao Makuu or TRA Zanzibar kwa sababu hata ukikwepa kodi kule maana yake unaikoseshaa mapato Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, tutajitahidi kuweka utaratibu, lakini tunataka compliance ya wafanyabiashara iwe katika hali ya juu ili kuepuwa usumbufu wa aina kama hii. Kwa hiyo, hili nimelichukua, tumekwenda tumelifanya kazi na nadhani kesi sasa hivi imeshakuwa solved.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chomboh umeridhika?

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

MWENYEKITI: Alikuwa ametoa mwanzo kabisa kwa wale ambao mlimsikiliza, alitoa alianza kabisa na kutoa mwanzoni kabisa na akasema natoa shilingi kwa dada yangu. Nasikiliza vizuri jamani na natenda haki.

Twende Pemba sasa Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kufika Pemba kwenye marashi ya karafuu. Katika mchango wangu niligusia suala zima la hali mbaya ya maisha ya wastaifu na kabla ya kutoa maelezo ambayo yatafuata baadaye kama sikupata majibu ya kuridhisha naondoa shilingi, naendelea na mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa kwamba hali za maisha ya wastaifu wetu ni mbaya sana na ikaonekana pensheni za wastaifu kwa muda mrefu na hasa wale wa kima cha chini hazijarekeblishwa na mara nyingi kabisa Serikali imekuwa ikitoa maelezo mbalimbali lakini hadi sasa hakuna ongezeko la pensheni za wastaifu wetu waliofanya kazi kwenye hali ngumu, maisha yamepanda na inaonekana bado wapo wengine wanalipwa kila miezi mitatu shilingi laki moja na hamsini elfu sawa na shilingi hamsini elfu kwa mwezi, sawa na shilingi 1720 kwa siku, hata chai ya asubuhi haitmii. Tatizo kubwa Serikali imewatupa, imewatelekeza, inawaonea, mnawahujumu maisha yao na familia zao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa commitment ya Serikali itueleze hapa mna mpango gani sasa wa kuweza kuongeza angalau kima cha shilingi laki moja hamsini elfu kwa miezi mitatu, angalau hadi shilingi laki nne na hamsini elfu. Kama sikupata majibu yaliyo sahihi kabisa kama maeneo mengine, shilingi naichukua mapema sana. Nashukuru sana. (Makofii)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM K. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimsihi rafiki yangu Masoud asiondoe shilingi ya Waziri, lakini tukubaliane tu kwamba Masoud pensheni ni function ya kuchangia, unavyochangia unakatwa kwenye ile sehemu ya mapato yako ili ukifika kule mbele ukachukue kile ambacho ulikuwa unakatwa huku nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ni mtiririko wa kawaida tu kwamba kwa mfano ulikuwa unachangia kule na unaweza kukuta kwa mfano mdogo, kuna watu wawili kwa kazi moja waliofanya na kwa kipindi kimoja miaka ishirini, lakini kama walizifanya nyakati tofauti, mmoja kafanya mwaka 1965 mpaka 1985, mwingine 1985 mpaka 2005 kwa sababu viwango vyta kuchangia vilikuwa tofauti utakuta huyu mtu kwenye pensheni analipwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna utaratibu ambao nchi nyingi zimefanya na Tanzania tumejaribu kufanya na tunajaribu kuliangalia la kuhuisha pensheni. Hili unalozungumza

Mheshimiwa Masoud ni kuhuisha pensheni ambayo Wabunge wengi wamelizungumzia, ni jambo ambalo kusema kweli labda niseme tu hapa nakumbuka kwamba Baba wa Taifa mwenyewe wakati ameondoka pensheni yake ilikuwa shilingi 10,250/= kwa mwezi, maana yangu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni kwamba, ule utaratibu wa kuhuisha mpaka mwaka 1999 na ngapi ulikuwa bado haujafanyika na hata sasa hivi unaposema kwa mfano, kwamba pensheni ya laki moja iende kila mwezi mtu apewe pensheni laki nne na nusu, *theoretically*, kwa nadharia ni jambo zuri kabisa, wote tunakubaliana nalo, lakini ile laki tatu inayoongezewa lazima itoke kwa mtu na kama itatoka kwenye pensheni itoke kwenye pensheni ya mtu mwininge ama isitoke kwenye pensheni ya mtu mwininge itoke kwenye kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, lazima uchumi huo uwe umefikia kiwango fulani cha uwezo mkubwa zaidi ili ile nyongeza kuhuisha pension itoke kwenye Mfuko mwininge. Sasa hili jambo taasisi, kwa maana ya Hifadhi za Jamii wao wenyewe wanaangalia namna ya kuboresha pension zao kwa wachangiaji wa zamani. Lakini kwa sisi ambao tuko Serikalini, ambao tayari tuna mgogoro wa PSPF na vyombo vingine ambavyo ni vytaa za umma, lazima kulihuisha tulifanyie analysis na hesabu zake kwa sababu hii nyongeza ambayo tunataka tuwape, lazima itoke sehemu, haiwezi kutoka hewani, lazima itoke sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Masoud aridhie kwamba, zoezi hili la kusema ni kiwango gani cha pension kinachoweza kuhuishwa na kinatoka wapi na gharama yake itakuwaje linaendelea. Atupe nafasi tulifanyie kazi na kulinga na uwezo huo, Serikali itakuja Bungeni na kusema tumelifanyia kazi, hiki ndiyo kiwango tunachoweza kuhuishwa na kwa kipindi gani na kadhalika kwa wastaafu wanaoazia muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna mchakato kidogo ambao ni wa kina na inabidi uhusishe taasisi nyininge. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Masoud aridhie kwamba ni zoezi gumu kidogo lakini tunachukua commitment ya kulifanya.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa shilingi, mwaka jana mlisema tuwape nafasi, nafasi tumewapa na kama Serikali inawajali kwa umakini wastaafu wake na leo wastaafu mnaona jinsi hali ilivyo ni ombaomba na jinsi ambavyo walivyoitumikia nchi hii katika hali ngumu za maisha, lakini mwaka jana mkaesema tuwape nafasi, leo mmekuja na majibu haya haya. Mara hii mnasema tuwape nafasi, kesho kutwa ni uchaguzi 2015 mnasema tuwape nafasi, nafasi ipi tena mnayotaka nyie, mimi siioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwa wastaafu ni kundi kubwa lina idadi kubwa ya watu walioko nyuma yao na hali zao za maisha tunazijua na jinsi wanavyotabika tunaelewa. Kwa nini tusijifunze hata nchi nyininge jinsi wanavyoweza kuwatunza na kuenzi wastaafu. Leo ukienda India utakuta kwamba wastaafu wameandaliwa mazingira mazuri kabisa hawawi ombaomba, leo unaambiwa hata wastaafu wale wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanafanya kazi ambazo hazistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu hata kwa vikosi vyetu vytaa ulinzi na usalama waliostaafu wanafanya kazi kwenye maeneo ambayo hayastahili. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono, jambo hili ni kubwa na zito, linahitaji Serikali itoe majibu ya kina, tena leo hapa pasiwe na itikadi ya aina yoyote tuwasaidie wenzetu wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba Waheshimiwa Wabunge tuchangie.

MWENYEKITI: Wale ambao hawakuchangia asubuhi, jamani mnatosha wengi mno, orodha niliyonayo inanitosha, wengi mno tayari, orodha niliyonayo inanitosha, tuanze na Mheshimiwa Jafo, kifupi kifupi dakika mbili mbili.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyozungumzwa na ndugu yangu Masoud ni hoja ya msingi sana na namwomba tu Mheshimiwa Masoud kwamba jambo hili nadhani lina ukubwa wake na jambo hili ukija kuangalia nadhani SSRA sasa hivi inataka kuwa katika mchakato mkubwa sana wa kuhakikisha jinsi gani wanafanya ili kuona ni jinsi gani watasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tumezungumza sana humu ndani kuhusu jinsi gani ya kusaidia watu wetu kwa kuhusisha Mifuko ya Jamii, watafanyaje ku-reflect hali halisi ya watu wa kada mbalimbali za pension kuweza kuwasaidia. Ndiyo maana nimesema ni hoja ya msingi, lakini nadhani tungewapa nafasi hasa SSRA wafanye kazi na unapoletwa ule Muswada wao wa Sheria ya harmonization ya Mifuko na jambo hili litakuwa limefanyiwa kazi. Nadhani litaleta mantiki sana kwa Taifa hili kwa maslahi ya nchi yetu. Ahsante sana.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hili suala la wastaifu ni kweli kama nilivyochangia hapa linatia uchungu na fedheha kubwa kwa Taifa letu. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri namna gani ya kuhuisha, *logic* yake ni msingi sana. Sasa Serikali haioni busara kuhakikisha kwamba angalau basi, kwa sababu hawa, hasa wale ambao tunawasema hapa watu kama akina Mzee Ruhuza ambao wana miaka 90 ambao tangu mwaka 2000 hata kulipwa hawapwi tena mmewasau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *individual cases*, watu kama akina Brig. Hashim Mbita, hali zao siyo nzuri. Sasa Serikali ingeji-commitment japo imesema itachukua muda, ni muda gani huo, liandaliwe hata fungu maalum kwa ajili ya wazee hawa ili watoe busara hata wakiondoka hapa duniani tuendelee kuneemeka vizuri watuachie Baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ione busara namna gani inaji-commitment kwa muda gani ili tuweze kuwasaidia wazee wetu hawa wakati process nyingine ya haya makubwa zaidi ikiendelea, lakini kuna kikundi cha wazee wako kwenye hali ambayo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud, naomba appointment ya muda.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba hii hoja ina mashiko na ni hoja nzito na ni hoja ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Naiunga mkono nikiwa na sababu moja kubwa, lazima tukubali kwamba hii Mifuko inafanya biashara na faida wanapata. Kwa nini faida yao wawe wanajua na hesabu za kila mwaka za faida wanazijua kutookana na michango ile ile ambayo imetokana na wale waliokuwa wafanyakazi ambao sasa hivi ni wastaifu. Leo waendelee kuomba muda kwa ajili ya kufanya michakato ya kujua kitu gani cha kuwalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namuunga mkono Mheshimiwa Masoud kwa asilimia mia. Hii Mifuko inapata faida na faida wanajua na kwa nini mchakato huu uchukue muda mwingi watuambie ni lini sasa hao watu watafdiwa. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi sana na nasema baba yangu pia ni mstaafu wa Jeshi, lakini tukubaliane Wabunge wenzangu tunajua umuhimu wa wastaafu jinsi wanavyotabika na hicho kiwango ambacho wanakipata. Kweli leo sisi tunaweza kupanga kiwango katika hii Kamati ya Matumizi ndiyo itakuwa solution. Kwa hiyo, kuna mambo msingi lazima tujadili kama viongozi. Nadhani ni vyema tukatoa nafasi kwa Serikali wakafanya tathmini ya kutosha ya kuona ni jinsi gani tunaweza kulitatua jambo hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa angalizo, kuna mambo hapa ambayo tulisema hapa Sera ya Afya kwamba matibabu ya wazee, watoto yaye bure, lakini tunaona sasa hivi reaction yake ikoje kule site. Sasa kuna mambo ya msingi tunatakiwa tuyatafakari kwa kina, tutoe nafasi kwa Serikali ione ni jinsi gani italic fanya kazi, maana tunaweza tukasema hapa kiasi fulani na isifanikiwe. Hoja ni ya msingi, lakini lazima tutoe fursa ya kufanya tathmini ya kina jinsi gani ambavyo tunaweza tuka-handle hii issue. (Makof)

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud kwa asilimia mia moja, kwa sababu katika maisha ya kawaida unamlipa mstaafu 1,720 kwa siku, hapati hata mkate wa mtoto mmoja, hivi kweli hatuoni kama tunawaonea? Mifuko hii inafanya biashara, wanajenga majumba sijui wanafanyakie, kwa nini Serikali haiwabani basi angalau pakawa na ongezeko hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliyejita anasema kama ye ye baba yake ni mstaafu wa Jeshi, ndiyo wewe ni Mbunge una uwezo wa kumsaidia baba yako, lakini je, yule mzee ambaye ye ye mtoto wake siyo Mbunge? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nadhani ifike mahali tuone, Waswahili wanasema mgeni wa leo mwenyeji wa kesho. Humu wengi wetu Wabunge walikuwa ni wafanyakazi huko katika Mawizara Fulani, fedha ya Mbunge tukitoka humu ndani ndiyo imekwisha hapa hapa. Tukitoka hapa unakwenda kulipwa 50,000 kwa mwezi, 1,750 kwa siku itakufikisha wapi, kwa sababu wengine wamefanya kazi humu, wengine ndiyo hatuna, tutakwenda huko tukafie kwetu, lakini wengine je, nadhani ni hoja ya msingi, ni lazima Serikali itafutie ni ufumbuzi gani namna ya kuwasaidia wastaafu.

TAARIFA

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachanganya mambo, tusiongelee mambo ya Mifuko, kinachoongelewa ni Government pension hasa ya wale watu ambaao walistaafu before 1998, baada ya 1999 tulipoanzisha PSPF, watu wameendelea kuchangia, hili siyo tatizo. Tunachoongelea hapa ni wazee waliostaafu before 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo suala la kuhuisha Mifuko, kuhuisha ni kuhuisha kwa ajili ya kuleta formula hapa kinachoongelewa ni wale waliostaafu before 1998 ambaao wakati ule Serikali ilikuwa haina Mfuko wake, ilikuwa kitengo kidogo pale Hazina kinacho-deal na pension. Kwa hiyo, ukimaliza wanakupa tu kidogo, kwa mfano, namfahamu mtu mmoja aliyejewa IGP Mgaya anapewa 20,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule walikuwa hawachangii, ndiyo maana Serikali ulikuwa ukimaliza wanakupa. Sasa tunasema Serikali inafikiriaje wale wazee wa nyuma kama kuna namna na ambayo nadhani Serikali inafikiria vizuri, lakini tusilichanganye na suala la Mifuko. (Makof)

MWENYEKITI: Nashukuru sana umetuwekeea...

TAARIFA

MWENYEKITI: Nani? Kwa kifupi sana Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji wa mwisho kwamba taarifa aliyoitoa siyo msingi wa kile ambacho mtoha hoja au mtoha shilingi amekieleza. Mtoha shilingi amezungumzia hoja ya mafao, amezungumzia hoja ya pension ambayo mtumishi baada ya kustaafu analipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa na ni kubwa kwa sababu mfumo wetu wa mafao wenyewe una tatizo. Chukua mfano, Waziri Mkuu hapa Mheshimiwa Pinda, akiacha Uwaziri Mkuu leo atalipwa asilimia 80 ya mshahara wa Waziri Mkuu ambaye yuko madarakani au Rais akistaafu leo, atalipwa mshahara wa Rais ambaye yuko madarakani mpaka atakapokufa. Sasa huo mfumo kwa vigogo ni mzuri sana kwa sababu una-maintain value ya kile ambacho analipwa, lakini ule huo kwa watumishi wa kawaida bado kuna tatizo ni mbaya. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusikwepe hoja, hoja ni kwamba Mifuko hii ya Hifadhi...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kafulila hiyo taarifa imekuwa ndefu sana, sasa tumsikilize Mheshimiwa Waziri. Ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. MWIGULU L. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba Bunge lako Tukufu lielewe kwamba hatupingani kuhusu msingi wa hoja, kila mmoja anaridhia kwamba hii ni hoja ya msingi na kila mmoja anajua maisha ya watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokuwa tunasema sisi kama Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri pacha wangu ameleezea vizuri kwamba kama tunasema tunatoa fedha hii na kama haikuwa imechangiwa maana yake inatakiwa itoke mahali. Sisi kama Serikali tunaposema tupewe muda, tunaangalia namna ambayo tunatakiwa tupige hesabu ya viwango tofauti na implication yake kwenye bajeti na sisi kama timu ambayo ndiyo inaanza tunahamasisha sana suala la mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutafanikiwa kwenye utaratibu wetu huu ambaao tuna matumaini makubwa tutafanikiwa wa kuongeza mapato, tunaahidi kitu ambacho ni sahihi, si jambo nzuri sana kubishania takwimu tu na tukapitisha, halafu tuje kufanya kitu ambacho hakitekelezi kwa watu ambaao walifanya kazi nzuri kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utazingatia si tu wastaafu, mtakumbuka hapa hapa tumeongelea hata watu walioko kazini, tuna Polisi hivi tukimaliza kikao hiki tunakwenda kuangalia allowances zao, tuna Wanajeshi, tuna Wizara hizi, kuna mambo ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunaposema tupewe muda *actually* si kwenda tu kupitisha bajeti, ni kwenda kucheza na hesabu tuone *implication* yake, kwa sababu kwa sasa hivi tukiwaambieni tu kwamba tutafanya hivyo ndugu yangu Masoud, katika fedha ya bilioni

800 zinazopatikana kila mwezi, mia nne zinakwenda kwenye mishahara, mia mbili zinakwenda kwenye mambo ya maendeleo, tuna mia moja zinakwenda kwenye *rationing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vinginevyo tunaweza tukataja hapa, halafu fedha yote ya ndani ikawa imeishia kwenye migao ya aina hii tukakosa hata ya ruzuku ama ya mitihani ama ya madawa ama vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba tupewe fursa, sisi tunasema tutaongeza mambo ya mapato na baada ya mapato, hivi vitu ambavyo Wabunge wanavitoa hapa na sote tunakubali kwamba ni vya msingi, tutavipa kipaumbele na ndugu yangu Masoud wala usitoe shilingi, tuko serious kwa sababu ndiyo kwanza tunaanza hii kazi na sisi tunaipenda hii kazi na tunaiweza. Kwa hiyo, lazima tufanye kwa uaminifu na kwa uadilifu na kwa vitendo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud na mimi niongezee kidogo kukuomba uwarudishie shilingi kama walivyoji-commit wao wenyewe kwamba watafanya kazi jambo hili kwa sababu moja ya matatizo makubwa katika nchi yetu ya ufisadi hata rushwa yanatokana na tendency hizo.

Kijana anapoajiriwa na anaona baba yake anapata 1,700 sijui 30,000 kama ndiyo pension ina-send message kwake kwamba nisipochangamka sasa hivi na mimi nitakuwa sina hatima kama huyu mzee. Kwa hiyo mambo haya kwa vyovyyote vile, huwezi kuondoa rushwa katika mazingira ya namna hiyo, kama vijana wanaangalia hawaoni matumaini watakuwa na behavior fulani, unamfanya yule kijana automatically awe na behavior fulani hivi. Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi na Mheshimiwa Naibu Waziri pale, rafiki yangu Mwigulu Lameck Mchemba, kuwa atacheza na hesabu hizo atakazozicheza yeye na wenzake wawili mbele yake hapo jumla watatu, wanacheza vizuri tu. Amesema suala la muda, sasa huo muda hasa hakusema, anasema tu tupeni muda, lakini muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakwenda kucheza, wanaweza wakacheza kwa muda gani siku kumi, mwezi mmoja na nyie mko watatu, sasa waseme muda gani wacheze na hesabu hiyo, ili jambo hili kulipatia ufumbuzi watueleze ili baadaye process nyingine ziendelee, lakini nyie mnasema muda tu, mnataka kucheza na hesabu. Chezeni tunawaruhusu lakini sasa mtuambie muda wa kucheza muda gani ili process nyingine ziendelee, vinginevyo bado nitabakia pale pale twende kwenye kura. Watuambie muda wa kucheza cheza kwao ni muda gani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aliko Kibona, nimekuona unashindwa kukaa chini hebu pumua kidogo Mheshimiwa.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa bahati nzuri mtoha hoja vilevile na mimi ni rafiki yangu. Nataka nimjulishe na niungane na Serikali kwa kawaida, kwa utaratibu suala la ku-calculate pension kwa watumishi, Serikali inaposema inaomba muda kuna wataalam wanaita wanatoa taarifa inakuwa inaitwa *actuarial report, calculation za pension ili Mifuko* hii isije ikafa ambapo inatakiwa tuwe na uhakika, tukianza kutoa kiasi fulani cha pesa je, Mifuko inaweza ika-sustain inaweza ikawa hai mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niungane na Serikali na nimshawishi mwenzangu, kwamba ni vizuri tukatoa nafasi ma-acturial scientist, waweze kupatikana, wafanye mahesabu ili siku zijazo mbele Mifuko yetu isije ikageuka kuwa balaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutoa taarifa hiyo. (Makofij)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ilikuwa nyongeza tu kidogo, taarifa zote nazikataa, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja ya Masoud ni valid, sisi hatuna dispute na hilo ni valid kabisa. Mnionia leo am very young, lakini ni mistaafu ambaye nitakuja, isipokuwa kama sijafanya kazi sasa hivi kuwaweka vizuri hawa waliopo nadhani tutakuwa hatujafanya wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge, kucheza kwetu sisi si kama kucheza kama anavyoitafsiri wewe kucheza kwetu ni kazi, tunafanya kazi. Hili ni jambo la muhimu, tumemwambia kwamba tunalichukua, tutaleta, tutakuwa tunakwenda pamoja na Kamati ili kutoa progress ya hili zoezi linavyokwenda. *Intention* yetu ya kuweka viwango ambavyo, sidhani kama tutakuwa tunampa pensioner bilioni moja kwa mwezi kama itakuwa inamtosha kutohana na hali ilivyo. Kwa hiyo, angalau tuweke katika kwango kinachoendana na hali ya mapato yetu yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, focus yangu kubwa ni kwa wale wastaafu ambao tunawalipa sisi Hazina, hao ndio wanaolipwa kiwango cha chini cha sh. 50,000/= kiwango ambacho kilihuishwa kimetokana na kuhuishwa 2009. Kwa hiyo, tupe muda siwezi nikakwambia kwamba hii kazi tunaji-commit tutafanya miezi mitatu. Hapana, kuna mambo mengi hapa yametokea. Tutakuwa tunatoa progress report the way tunavyokwenda na Kamati na Bunge mtajua jinsi kazi hii itakavyokuwa inakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalichukua kwa umuhimu wa pekee, tunakwenda kulifanyia kazi. Usitoe mshahara maana tukiwa hatujapata mshahara kazi itakuwaje.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud nakuomba sana tuvuke, orodha yangu ni ndefu hapa.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na Mheshimiwa Waziri na wale Wajumbe wa Kamati namba kumi na moja wa Bunge la Katiba, wale pale wawili nao shilingi yao nairudisha.

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Hii inaonesha picha jinsi gani Waheshimiwa Wabunge mnavyopigania maslahi ya wananchi wenu, ukilia maanani kwamba kwa wananchi ambao hawafahamu, Mbunge akishamaliza kipindi chake ye ye hana pension, lakini bado anapigania wafanyakazi wengine kupata pension. Mheshimiwa Majiyatanga Mzindakaya, alikaa hapa Bungeni kati ya miaka 35 au 40 hivi, miaka 40 amekaa Bungeni, alikuwa ameingia kijana mdogo, amekaa 40 years hapa, ametoka hapa hana pension. Kwa hiyo, haya ni mambo vilevile ya kuangaliwa na Waheshimiwa hawa kuona jinsi gani ya kufanya kesho na kesho kutwa.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Wakati nachangia niliongea namna gani tunashindwa kukamilisha bajeti yetu na nikasema utaratibu mzuri kama ushauri, naona ni vyema sasa wakati umefika tukaanza kutumia capital bajeti, bahati nzuri tulikwenda training, Waingereza ndio walitufundisha, wakasema hata sisi tulianza na cash bajeti lakini tuliona inatueletea matatizo, hivyo tukamuua kuanza polepole mpaka tukafika kwenye capital budget.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, haoni kama ni vyema kwenda katika system hiyo ili tuondokane na deficit kubwa inayotupata katika budget.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. MWIGULU L. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana mama Mshama kwa concern yake hii nzuri na kimsingi kusudi lake hili linatokana na kiu yake ya kutaka fedha za maendeleo ziende kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mara nyingi akiyapigania haya na niseme tu kwamba kwa bahati nzuri yeye ni mjambe wa Kamati ya Bajeti na tulikuwa naye kwenye *think tank* ya kwanza ambayo tulikuwa tunashughulikia kubainisha vyanzo vya mapato na sisi Serikali tunakusudia kwa kweli kushirikiana vizuri sana na *think tank* kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii tutaibeba na tutaifanyia kazi na jambo lolote ambalo litaleta manufaa kwa Watanzania, kwa kweli si la mjadala ni la kulifanyia kazi tu kwa kuwa tunataka tuweze kupiga hatua. Kwa hiyo, nimpongeze sana mama Mshama kwa kujali sana mambo ya maendeleo ya akinamama VICOBA na juzi kapigania *ambulance* mpaka ikapatikana kwenye Jimbo lake.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Sanga!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ambayo nataka kusema, wenzangu wengi wamesema, ilikuwa ni hii inayohusiana na mambo ya pension, lakini kwa sababu wengi wameshasema sina hoja tena.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Peter Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu nimezungumzia jinsi ambavyo kuna maeneo mengi wazabuni hawajalipwa hela zao kwa muda mrefu. Kutolipwa pesa zao kumeleta umaskini sana kwa wafanyabiashara hasa wazawa wa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nili-cite maeneo ya Iringa nikawataja wafanyabiashara lakini hawa ni cutting across na nakusudia kutoa shilingi kama sitapata majibu ya kutosha, lakini hii haiathiri tu masuala ya wazabuni, inaathari kwa Wizara hii kutokuleta pesa za maendeleo kule kwenye Halmashauri zetu, tunashindwa kupanga mambo yetu vizuri, miradi mingi haiendelei. Nataka njue ni kwa kiwango gani kwa sababu muda umebakira kidogo sasa hivi tunaelekeea mwisho na pesa nyingi za maendeleo hazijaja kwenye Majimbo yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa sasa unisaide kwa sababu utaratibu wetu hoja ni moja, je, ni ile ya Wazabuni au ni hizi fedha za maendeleo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Wazabuni nimeweka kama mfano, lakini hoja ya msingi kwa sababu hata hizo fedha zitakuwa ni za ndani, zitakwenda pamoja na Wazabuni watalipwa, zote kwa pamoja. Kwa hiyo, ninachozungumzia ni fedha za maendeleo kwa sababu zinacheleweshwa na sasa hivi tunakwenda mwishoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa kiasi gani Wizara hii inaji-commit sasa, wiki chache zimebaki kwenda mwishoni. Ni namna gani wanatuletea kwenye Halmashauri yetu hii pesa ili tuendelee na shughuli za maendeleo katika Manispaa yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama sitapata majibu ya kuridhisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli kama Serikali, tunayo hii concern kwamba maeneo mengi ikiwemo Iringa bado fedha hazijakwenda na sasa tumebakwa na wiki tu chache kumaliza mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kueleza, ni gumu nataka tu kueleza kwamba, tunapo jitahidi kufanya haraka sasa hivi ndipo ambapo tunapokwenda katika kutekeleza yale ambayo hatujayakamilisha, lakini Mheshimiwa Mchungaji tumesema hapa bajeti yetu mpaka sasa hivi ni asilimia 75, tunaendelea kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho tukijaliwa tutakuwa na mukutano na Washirika wa Maendeleo hapa hapa Dodoma. Ijumaa tarehe 13 tutakuwa na mukutano na Washirika ea Maendeleo hapa hapa Dodoma, kuhakikisha kwamba ile commitment yao waliyokuwa hawajakamilisha ambayo ndiyo tunayo-mobilize kupeleka kwenye sehemu kubwa ya maendeleo, wana kamilisha kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia World Bank sasa hivi tumeshasaini na nadhani tumeshakamilisha; Japan tunasaini tarehe 16 na wengineo. Kwa hiyo, hiyo ni commitment, tunamobilize kwa ajili ya kupeleka fedha ambazo hazijakamilika. Sikupi guarantee kwamba tutapeleka a hundred percent.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwe mkweli na nategemea mtanifahamu, lakini tunajitahidi kwa kiasi kikubwa, yale mafungu ambayo hayajapata fedha basi angalau tunayapa fedha hususan za maendeleo. Tumeji-commit hapa pesa za REA, tumeji-commit fedha za maji na ny inginezo tutakuwa tunaendelea kutoa. Mchungaji tunajitahidi hili na naamini hutatoa shilingi maana naamini kwamba utakuwa umenifahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mchungaji nakupa kifupi hutakuwa na muda wa kuendeleza sana, lakini hebu windup kwa sababu muda hauniruhusu kabisa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi shilingi naitoa unisamehe tu Mheshimiwa Waziri, natoa shilingi kwa sababu moja. Wizara hii ninyi sio watu wa kulalamika hapa kama Wizara ny ingine zote ambao wanaomba hela, ninyi ni watu wa kutafuta hela. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, umesikika na umesema wewe ni first class economist, tunategemea tupate mazao hayo, mnatafuta vyanzo vya hela, siyo mna complain hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema, vyanzo vingi vya mapato katika Manispaa na Halmashauri ny ingi zimechukuliwa na TRA, vinginevyo tungkuwa tunakusanya wenyewe kwenye Halmashauri tungeweza kuleta maendeleo. Sasa mmekabidhiwa ninyi mnavichukua, tunashindwa kufanya maendeleo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wabunge wenzangu muniuunge mkono, hili suala tulijadili kwa pamoja ni namna gani hizi pesa za maendeleo kwenye Halmashauri zetu zitakuja na bajeti hii inakwenda mwisho ili watu wanaoidai Serikali na maendeleo ambayo hatujayafanya yaweze kutatuliwa. Kwa hiyo, nawaomba wenzangu kwamba tuunge mkono tujadili hili suala kwa sababu ninyi si watu wa ku-complain hapa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, angetamani Ofisi yake iwe na pesa, yeye anatakiwa a-deliver atuambie vyanzo vya kupata hela vitatoka wapi na siyo sisi.

Kwa hiyo, naomba wananchi, samahani Wabunge wenzangu mniunge mkono. (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa anaomba wananchi wa Tanangozi waingilie kati.

Waheshimiwa tuwe tunaangalia na muda, muda hauko upande wetu, zimebaki dakika kumi muda kwisha. Kwa hiyo, ni guillotine, Makatibu naomba tuendelee.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts... ... Sh. 1,236,715,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning... ... Sh. 34,070,205,000/=

Kif. 1004 - Legal Services... ... Sh. 1,276,748,000/=

Kif. 1005 - Government Communication

Unit... ... Sh. 1,438,138,000/=

Kif. 1006 - Internal Audit Unit... ... Sh. 471,587,000/=

Kif. 1007 - MCC Tanzania... ... Sh. 1,700,000,000/=

Kif. 1008 - Procurement Management

Unit... ... Sh. 706,089,000/=

Kif. 1009 - Public Procurement Policy

Unit (PPU) Sh. 0/=

Kif. 1010 - Information and Communication

Technology... ... Sh. 1,270,000,000/=

Kif. 2003 - Treasury Registrar... ... Sh. 0/=

Kif. 3001 - Internal Auditor General... ... Sh. 4,034,761,000/=

Kif. 5001 - Government Asset Management

Division... ... Sh. 6,803,551,000/=

Kif. 6001 - Financial Management Information

Systems Division... ... Sh. 2,913,400,000/=

Kif. 6002 - Tax Revenue Appeals Board... ... Sh. 0/=

Kif. 6004 - Tax Revenue Appeals Tribunal... ... Sh. 0/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA

Kif. 1001 – Administration and Human

Resource Management... ... Sh. 1,520,571,000/=

Kif. 1002 - Internal Audit Unit... ... Sh. 104,370,000/=

Kif. 2001 - Technical Department... ... Sh. 589,220,000/=

Kif. 2002 - Zanzibar Office... ... Sh. 104,500,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 13 – KITENGO CHA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU

Kif. 1001 - Administration and Human Resource
Management Unit... Sh. 1,286,135,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit... Sh. 43,455,000/=
Kif. 1003 – Internal Audit Unit... Sh. 11,980,000/=
Kif. 1004 – Monitoring Unit... Sh. 267,170,000/=
Kif. 1005 – Inspection Unit... Sh. 163,230,000/=
Kif. 1006 – Procurement Management
Unit... Sh. 22,470,000/=
Kif. 1007 – Legal Services Unit... Sh. 13,710,000/=
Kif. 1008 - Management Information Systems
Unit... Sh. 191,850,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 21 – HAZINA

Kif. 1002 – Finance and Accounts... Sh. 1,231,815,000/=
Kif. 1009 – Public Procurement Policy
Unit (PPU) Sh. 1,776,162,000/=
Kif. 2001 - Government Budget
Division... Sh. 556,807,370,000/=
Kif. 2002 - Policy Analysis Division... ... Sh. 211,314,119,000/=
Kif. 4001 – External Finance Division... ... Sh. 14,712,377,000/=
Kif. 4002 – Public Private Partnership
Unit... Sh. 1,368,959,000/=
Kif. 7001 – Poverty Eradication and
Empowerment... Sh. 3,114,414,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 22 – DENI LA TAIFA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ... Sh. 4,354,865,076,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 45 - OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Kif. 1001 –Administration and Human
Resource Management... ... Sh. 26,628,386,000/=
Kif. 1002 – Finance and Accounts
Unit... Sh. 1,548,017,000/=
Kif. 1003 – Internal Audit Unit... Sh. 572,186,000/=
Kif. 1004 - Ministerial Audit Division... ... Sh. 8,052,360,000/=
Kif. 1005 - Regional and Local Government

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Audit Division... Sh. 13,926,075,000/=
Kif. 1006 – Value for Money Audit
Division... Sh. 2,772,608,000/=
Kif. 1007 – Treasury Audit Division... Sh. 4,524,335,000/=
Kif. 1008 – Technical Support, Research
and Consultancy... Sh. 5,516,903,000/=
Kif. 1009 – Public Authorities Audit
Division... Sh. 1,115,572,000/=
Kif. 1010 - Planning Unit... Sh. 2,081,208,000/=
Kif. 1011 – Procurement Management
Unit... Sh. 615,360,000/=
Kif. 1012 – Information Technology
Unit... Sh. 2,490,815,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 7 – MSAJILI WA HAZINA

Kif. 1001- Administration and Human
Resources Management... Sh. 107,690,000/=
Kif. 1003 – Planning Unit... Sh. 270,300,000/=
Kif. 1004 - Legal Services Unit... Sh. 190,000,000/=
Kif. 1006 - Information and Comm.
Technology... Sh. 243,950,000/=
Kif. 1007 – Information, Education and
Comm. Unit... Sh. 237,900,000/=
Kif. 2001 – Public Investment Management
Division... Sh. 118,800,000/=
Kif. 3001 – Privatization and Monitoring... ... Sh. 398,060,000/=
Kif. 4001 - Management Service Division... Sh. 376,300,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 13 - KITENGO CHA UDHIBITI FEDHA HARAMU

Kif. 1001 – Administration and Human
Resource Management... Sh. 195,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 21 – HAZINA

Kif. 1009 – Public Procurement Policy
Unit (PPU) Sh. 1,698,200,000/=
Kif. 2001 – Government Budget
Division... Sh. 2,914,283,000/=

Nakala ya Mlando (Online Document)

Kif. 2002 – Policy Analysis Division... ... Sh. 36,499,584,000/=

Kif. 4001 - External Finance Division... ... Sh. 3,954,948,000/=

Kif. 4002 – Public Private Partnership

Unit... Sh. 10,000,000,000/=

Kif. 7001- Poverty Eradication and

Empowerment... Sh. 2,350,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 23 - IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Kif. 3003 – Financial Management... ... Sh. 6,597,000,000/=

Kif. 3004 – Financial Systems... Sh. 923,000,000/=

Kif. 4001 – Local Government

Finances... Sh. 430,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Kif. 1001 – Administration and Human

Resource Management... ... Sh. 8,000,000,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts

Unit... Sh. 816,100,000/=

Kif. 1010 – Planning Unit... Sh. 4,195,332,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA

Kif. 1001- Administration and Human

Resource Management... ... Sh. 10,320,000,000/=

Kif. 1003 – Policy and Planning... ... Sh. 10,878,685,000/=

Kif. 1005 – Government Communication

Unit... Sh. 1,074,300,000/=

Kif. 1007 – MCC Tanzania... Sh. 0/=

Kif. 1009 – Public Procurement Policy Unit (PPU) Sh. 0/=

Kif. 2003 – Treasury Registrar... Sh. 0/=

Kif. 3001 – Internal Auditor General... ... Sh. 3,045,777,000/=

Kif. 3002 - Government Asset Management

Division... Sh. 2,384,470,000/=

Kif. 3003 - Financial Management Inform.

Systems Division... Sh. 2,100,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilrudia)

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 Yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Manaibu wote wawili; Katibu Mkuu Dkt. Likwelile;, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha.

Kwa niaba ya Bunge zima niwape hongera kwa kazi mnayofanya kwa niaba ya Taifa letu, tunawatia moyo, mwendelee kufanya kazi hiyo kwa ubora zaidi na sisi tutakuwa pamoja nanyi na mzingatie ushauri wote ule ambaa mmeputa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, muufanye kazi ili tutakapokutana kwa wakati mwingine mambo yawe ni mengine tusiongelee yaleyale tena kila wakati. Kwa hiyo, tunawatachia kila la kheri na ahsanteni sana. Katibu!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa Mwaka 2014 (*The Tax Administration Bill, 2014*)

Muswada wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani wa Mwaka 2014 (*The Value Added Tax Bill, 2014*)

Muswada wa Marekebisho katika Sheria ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2014
(*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2014*)

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2014 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2014*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hizo ndiyo sheria zetu zinazosomwa mara ya kwanza, natumaini mmeshapata nakala hii inayoonyesha kuna Sheria nne ambazo tumesoma mara ya kwanza.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mwongozo muda hauko sana upande wangu, labda kwa dakika moja moja sana. Ni Waheshimiwa Wangapi? Watatu wote Opposition? Tuanze na Mheshimiwa Christina!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa kifungu cha 68(7) sitakisoma kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati unatoa ufanuzi wewe mwenyewe kuhusu utaratibu mzuri wa namna ripoti ya CAG inavyotumiwa na Bunge, ulieleza kwamba, ripoti ya CAG ikileta hapa isitumiwe *direct* jinsi ilivyo bali ipelekwe kwenye Kamati, Kamati ikaichambue ndiyo kuanzia hapo Wabunge wataanza kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba CAG *aki-table report* yake hapa Bungeni inakuwa ready for public use. Sasa kwa maelezo yako inabidi kwanza Kamati ikachambue ndiyo Wabunge waje waitumie. Sasa sielewi ni Kamati gani hiyo ambayo ina majukumu ya kuchambua ripoti ya CAG, maana tunajua CAG anafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Naomba Mwongozo wako kuhusu ni wakati gani hasa tunatakiwa kutumia ripoti ya CAG.

NAIBU SPIKA: Nieleweke vizuri, sikupiga marufuku matumizi ya taarifa yoyote ile ya CAG. Taarifa yoyote ile ya CAG au ya mtu mwingine yeyote inapowekwa hapa mezani maana yake is a public document, lakini hata kama ni public document haimaanishi kwamba it's the end in itself. Maana yangu ni kwamba, katika utaratibu wa Kibunge, mchakato wake unaendelea na tunazo Kamati tatu na Kamati hizo zinaongozwa na ninyi Wapinzani. Safari hii ni mbili. Tunazo Kamati mbili ambazo zinapitia moja wapo Mwenyekiti wake ni jirani yako hapo. Mnaptia hoja kwa hoja, kila kitu, kila kitu mnatuandikia ripoti, ripoti inatuweka mahali pazuri kama Bunge, kuweza kuelewa ni nini hasa ambacho kimetokea na mahali gani.

Hatukukataza habari ya kutumia ripoti, tunasema itumie lakini consciously!

Tuendelee kwa sababu ya muda, Mheshimiwa...

TAARIFA

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012, baada ya ripoti ya CAG kuleta hapa Bungeni kulitokea mambo mazito na sintofahamu ya kutosha, kuna baadhi ya Mawaziri wakapoteza nafasi zao.

Baada ya pale ikaletwa miscellaneous hapa ndani ambapo kwenye ile sheria tukabadilisha katika ile miscellaneous kwamba ripoti za CAG zikija kabla hazijajadiliwa ziende kwanza kwenye Kamati, then wakishakwenda kwenye Kamati ndiyo yale mapendekoz yao tuyachukue tuyafanyie kazi. Tuliamua wenyewe through miscellaneous.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana kwa kunikumbusha, kwa kweli huo ndiyo utaratibu na ndiyo Sheria tuliyonayo. Mheshimiwa Wenje kwa kifupi!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Leo asubuhi wakati akijibu swalii la Mheshimiwa Kafulila alipoomba Mwongozo kwako, Mheshimiwa Mary Nagu alisema kwamba, kutohana na taarifa iliyotolewa Bungeni na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Masele na akaungwa mkono na Waziri wake pamoja na Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mary Nagu alitoa ufanuzi kwamba taarifa inayosimama ni taarifa iliyotolewa na lkulu kuukana msimamo uliotolewa humu ndani ya Bunge na Mheshimiwa Massele iliyoungwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa kwa kuwa Serikali imekana taarifa zilizotolewa ndani ya Bunge, maana yake ni kwamba taarifa zilizotolewa ndani ya Bunge si za kweli na kwa kiasi fulani walipotoka.

Sasa nataka kujua Mwongozo wako, kama msimamo wa Serikali ni ule uliotoka nje kule lkulu, hawa waliofanya haya makosa ndani ya Bunge wanachukuliwa hatua gani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekia Wenje unachofanya unamtetetea Balozi...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwepo siku hiyo ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anatoa ufanuzi wa masuala haya. Kama *hansard* itamnukuu sahihi, alisema tumesikia aliyyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri, haya yote tutayapeleka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inayohusika na Mahusiano na Mabalozi. Kama unaichukulia hiyo kama kumuunga mkono au kutomuunga mkono, basi ningemwomba Mheshimiwa Wenje atafsiri.

NAIBU SPIKA: Nashukuru sana Profesa Mwandoza, Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wangu mimi nimeuondoa, ila tu nilikuwa na dogo niliseme kuhusiana na taarifa ya CAG kwa sababu na mimi ni mhusika katika hilo.

Ukweli ni kwamba CAG baada ya kuwasilisha ripoti zake hapa Bungeni na kuwakabidhi Wenyeviti wa Kamati zile mbili zinazohusika na hesabu, ni wajibu wetu taarifa zile kuziacha kwa Serikali kwa kipindi cha mwezi mmoja ili Serikali wazipatia majibu zile taarifa na hapo ndiyo Kamati zinaweza kuanza kuzifanya kazi. Ni hilo tu! (Makofii)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana kwa sababu umetueleza masuala ya utaratibu na huo ndiyo utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru mno kwa ushirikiano ambao tumepeana siku ya leo tumefanya kazi yetu vizuri, tumechambua toka tulivyoanza Wizara zote mpaka tumemaliza na Wizara ya Fedha. Tutaendelea na utaratibu kadiri ambavyo Kamati ya Uongozi imepanga. Kwa kuwa tumefika mwisho wa shughuli zetu sasa, naomba kwa heshima na taadhima niahirishhe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 2.05 Usiku, Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 5 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)